VOLUME 1, NUMBER 1, MARCH 2022 ISSN 2820-2775

INITIUM SAPIENTIAE TIMOR DOMINI

TUMA JOURNAL OF SOCIAL SCIENCES

A JOURNAL OF TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA
FACULTY OF EDUCATION, HUMANITIES, ANDSCIENCE

EDITOR-IN-CHIEF
Dr. Perida Mgecha

ASSISTANT TO EDITOR-IN-CHIEF
Mr. Dickson Mlowezi
Mr. Thaddeus Lekule

VOLUME 1, NUMBER 1, MARCH 2022 ISSN 2820-2775

TUMA JOURNAL OF SOCIAL SCIENCES

A JOURNAL OF TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA
FACULTY OF EDUCATION, HUMANITIES, ANDSCIENCE

EDITOR-IN-CHIEF
Dr. Perida Mgecha

ASSISTANT TO EDITOR-IN-CHIEF
Mr. Dickson Mlowezi
Mr. Thaddeus Lekule

EDITORIAL TEAM

EDITOR-IN-CHIEF
Dr. Perida Mgecha

ASSISTANT TO EDITOR-IN-CHIEF
Mr. Dickson Mlowezi
Mr. Thaddeus Lekule

CONSULTING EDITORS
Prof. Faustin Mahali
Prof. Deogratias Ngonyani
Prof. Fikeni E.M.K Senkoro
Prof. Kokel Melubo
Dr. Joachim Kisanji

ASSOCIATE EDITORS

SPECIALIZED STUDY FIELDS

Dr. Perida Mgecha	*Tumaini University Makumira*
Dr. Neema Mturo	*Tumaini University Makumira*
Dr. Leonard Flavian Ilomo	*University of Dar es Salaam*
Dr. Elither Kindole	*University of Dar es Salaam*
Dr. Joachim Kisanji	*Ms-TCDC*
Dr. Cyril K. Komba	*Moshi Co-operative University*
Dr. Roberto Gaudiaso	*Napoli University, Italy*
Dr. Adrian Fuluge	*Mzumbe University*
Dr. Arnold Gawasike Msigwa	*University of Dar es Salaam*
Dr. Kijakazi Makame	*State University of Zanzibar*
Dr. Samwel Mhajida	*Dar es Salaam University College of Education*
Mr. Said Omary	*Ms-TCDC*
Mr. Dickson Mlowezi	*Tumaini University Makumira*
Mr. Simon Masatu	*Tumaini University Makumira*
Mr. Joachim Kawiche	*Tumaini University Makumira*
Ms. Gestuta Tilia	*Tumaini University Makumira*

PRINTING, MARKETING, & DISTRIBUTION
Ms. Gestuta Tilia
Ms. Grace Samwel
Ms. Vumilia Rugakingira

FORMATTING & COMPILING
Mr. Dickson Mlowezi
Mr. Hagai Maanga
Ms. Grace Mkawe

EDITORIAL BOARD

CHAIRPERSON: PROF. ISMAEL MBISE

MEMBERS

DR. ROSE MUNISI
Dean, FEHS, TUMA

PROF. KIMMO JOKINEN
Univ. of Jyvaskyula, Finland

PROF. FAUSTIN MAHALI
Faculty of Theology, TUMA

DR. NEEMA MTURO
Head of Depertment, DSS, TUMA

DR. PERIDA MGECHA
Dept. of Education, TUMA

DR. DOWARD KILASI
Dept. of Science

MR. MOSES MASAGO
Dept. of Education, TUMA

MS. MARTHA SHIO
Dept. of Education, TUMA

DR. APOLO MUGYENYI
Dept. of Education, TUMA

DR. SOPHIA LAIZER
Dept. of Humanities, TUMA

MS. GESTUTA TILIA
Dept. of Humanities, TUMA

DR. JOACHIM KISANJI
MS-TCDC, Arusha

MR. DICKSON MLOWEZI
Dept. of Humanities, TUMA

MS. KATRI NIIRANEN-KILASI
Dept. of Humanities, TUMA

DR. PARIT OLE SARUNI
MNMA, DSM

Mr. THADDEUS LEKULE
Dept. of Humanities, TUMA

DR. ROBERTO GAUDIASO
Napoli University, Italy

Advertisements

TJSS welcomes advertisements and rates will be quoted on request. Enquiries should be emailed to Editor-in- Chief and can be followed up via +255 765006622 .

Subscription rates

The journal is published twice a year in April and November. The price per issue excluding postage is 10,000Tshs in Tanzania and 15 US Dollars outside Tanzania, payable through CRDB account number 01J1035922100 (Tumaini University Makumira)

A free copy of an issue will be posted to authors whose articles appear in that issue and to successful peer- reviewers of articles in the issue.

Orders should be sent to:

The Editor-in-Chief, Faculty of Education, Humanities and Science, Tumaini University Makumira, P.o Box 55, Usa-River, Arusha, Tanzania; or send via email: **tjss@makumira.ac.tz** and copy to -Editor in Chief- **peridaalfred@gmail.com**

© Tumaini University
Makumira All rights
reserved

TUMA Journal of Social Sciences is registered with the Tanzania Library Services (TLS)

Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Mission and vision

TUMA Journal of Social Sciences (TJSS) is a biannual peer-reviewed research journal published by Tumaini University Makumira. Its mission is to serve researchers in social sciences, and affiliated professionals around the world by publishing and disseminating significant research articles, novel ideas, and reviews in any subfield of social sciences. Its vision is to become a leading East African research journal, with notable and insightful contribution to social sciences field.

General Guidelines for Contributors

a) TJSS publishes original, novel, and thought-provoking peer-reviewed research and non-research articles in any subfield of social sciences. Manuscripts relevant to the needs of the Tanzanian society are given top priority. All manuscripts should be emailed to the Editor-in-Chief via **tjss@makumira.ac.tz** or copy to **peridaalfred@gmail.com**

b) Manuscripts should be in MS Word format (preferably MS Word 2007 and above) and should be submitted as email attachments. File names should begin with the journal's name (TJSS) followed by the surname (or second name) of the author (if the manuscript is authored by one author) or by the lead author (if the manuscript is written by two or more authors), for example, TJSS_Mlowezi.doc

c) The maximum length of an article should not exceed 8000 words (including diagrams and/or other visual illustrations). Book reviews should not exceed 1000 words. Abstracts should not be more than 200 words. Articles and reviewed papers published in TJSS are those that are not published or intended for publication in another journal. All manuscripts should be written in either English or Swahili Language and should be in the APA formatting style.

d) TJSS retains the right to edit the content and style of submitted and accepted manuscripts.

e) Final proofs of research articles and reviews will be emailed to authors for correction. Authors should respond to the Editor-in-Chief at most five days after receiving the proofs.

f) Specific quality guides and policy of TJSS will be posted to authors and peer-reviewers when needed

TABLE CONTENTS

TATHMINI YA MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA KISWAHILI IKIWA NI LUGHA YA KIGENI KWA KUTUMIA NADHARIATETE YA INGIZO...1

Vinold John na Perida Mgecha

UBUNIFU WA VIJANA WA KITANZANIA WANAVYOTUMIA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA KUBAINISHA UTAMBULISHO WAO...20

Dickson Jonas Mlowezi

MBINU WANAZOTUMIA RAFIKI WA LUGHA KATIKA UKUZAJI WA STADI YA MAZUNGUMZO KWA WAJIFUNZAJI WA KISWAHILI IKIWA NI LUGHA YA KIGENI...34

Elivira Jovinus na Perida Mgecha

TATHIMINI YA ATHARI ZA MABADILIKO YA KIFANI NA KIMAUDHUI KATIKA USHAIRI WA BONGO FLEVA KATIKA JAMII...46

Getruda Modest Ngakoka na Neema George Mturo

UNYAMBULISHAJI WA VITENZI KATIKA LUGHA YA KIMASAI-IRKISONGO...61

Editha Siphael Mollely na Perida Mgecha

SABABU ZA UTOAJI WA MAJINA YA KOO KATIKA JAMII YA WAMERU...82

Joyce Henock Nyiti na Perida Mgecha

NAFASI YA MWANAMKE NA MWANAUME KATIKA TAMTHILIYA YA KISWAHILI YA *KIVULI KINAISHI* NA *KITANZI* WAKATI WA UTANDAWAZI...97

Benjamin Gambaloya na Neema George Mturo

TAHARIRI

Jarida la 'Tuma Journal of Social Sciences' ambalo kifupisho chake ni TJSS ni jarida jipya lililoanzishwa mwaka 2022 katika kitivo cha Elimu, Humanitia, na Sayansi - Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Jarida hili limejikita katika kutoa maarifa ya lugha, na sayansi za jamii. Jarida linamilikiwa na Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kinachopatikana Arusha-Tanzania. Chuo hiki kinaongozwa na mihimili mitatu ambayo ni utafiti, ufundishaji na utoaji huduma kwa jamii. Hivyo jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mihimili hiyo.

Jarida la TJSS linapokea makala kutoka sehemu mbalimbali, ndani na nje ya Tanzania zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza. Toleo hili la kwanza 2022 lina jumla ya makala saba. Kwa sasa makala hizi zimejikita kwenye tasnia ya lugha hasa isimu na fasihi. Maarifa yaliyomo kwenye makala hizi yanaendana sana na wakati tuliopo, na changamoto zilizopo kwenye jamii. Kama inavyofahamika Kiswahili ni lugha inayokua kwa kasi sana, na sasa imetengewa siku rasmi ya maadhimisho ambayo ni tarehe 7/7 kila mwaka kimataifa. Pia kutokana na mwingiliano mkubwa kimataifa katika nyanja za elimu, utalii, utabibu, sayansi na teknolojia kwa kutaja machache, kunahitajika wataalamu wengi wa kufundisha, kufanya tafiti, kutafsiri, kutunga vitabu na kamusi kwaajili ya kukuza na kuendeleza lugha adhimu ya Kiswahili katika nchi mbalimbali ulimwenguni.

Kutokana na uhitaji huo, jarida la TJSS lina makala zinazotoa maarifa kuhusu ufundishaji wa Kiswahili ikiwa lugha ya Kigeni ambapo maarifa mbalimbali yametolewa yakiwemo mbinu zitumikazo kufundishia, changamoto zake na namna ya kuzitatua. Pia masuala ya lugha ya Kiswahili na utambulisho wa vijana yamechambuliwa kwa weledi. Aidha, maarifa kuhusu mabadiliko ya muziki wa kisasa, nafasi ya mwanamke na mwanaume katika jamii kwa sasa ikoje, na maana za majina ya koo (hasa za Kibantu) yamechambuliwa. Sambamba na hayo, maarifa ya isimu ya lugha za Kinailotiki yamebainishwa kwa uwazi hasa katika unyambulishaji wa vitenzi vya Kimasai.

Hivyo ndugu msomaji hakikisha unapata nakala ya jarida hili la toleo la kwanza 2022. Pamoja na hayo unakaribishwa kutuma makala ili kuchangia maarifa katika nyanja mbalimbali kama vile za lugha, fasihi, jiografia, historia, elimu ya uraia, na vipengele vingine vya sayansi za jamii.

Dkt Perida Mgecha

Mhariri Mkuu-TJSS

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Tathmini ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa Kutumia Nadhariatete ya Ingizo

Vinold John
vinoldjohn@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Perida Mgecha
peridamgecha@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii

IKISIRI
Makala hii imejikita katika kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo. Malengo mahususi yakiwa kwanza kubaini mbinu za Nadhariatete ya Ingizo zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, pili kutathmini matumizi ya mbinu hizo kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo. Data zilikusanywa kwa njia ya ushuhudiaji kutoka kwa walimu wanaofundisha Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya walimu wanatumia mbinu za Nadhariatete ya Ingizo lakini matumizi yake hayazingatii kwa kiwango kikubwa mwongozo wa Nadhariatete inayohusika. Pia matokeo yanaonesha kuwa kiwango cha maarifa mapya wanachopewa wajifunzaji kinaathiriwa na mbinu, weledi wa walimu, utayari wa mjifunzaji, na mazingira ya kujifunzia. Hivyo, ni vyema walimu wapewe mafunzo ya ufundishaji kulingana na utofauti wa mahitaji ya wanafunzi ili kuweza kuwa na ujuzi wa kukadiria kiwango cha ingizo wanachopaswa kuwapa wajifunzaji.

MANENO YA MSINGI:
Tathmini, Nadhariatete ya Ingizo, Lugha ya Kigeni

1.0 UTANGULIZI

Mwingiliano baina ya watu ulimwenguni umeanza kutoka karne nyingi zilizopita, katika Bara la Afrika. Mwingiliano huo unarejeshwa hadi karne ya 15 ambapo wageni mbalimbali walianza kutembelea Bara la Afrika kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni kwa lengo la kufanya biashara. Mwingiliano huu ulikuja na mahitaji mbalimbali miongoni mwake ni mawasiliano. Wafanyabiashara wa sehemu mbalimbali ulimwenguni walihitaji kuwasiliana na wafanyabiashara katika Bara la Afrika hususani katika sehemu za mwambao wa Pwani. Mwingiliano huu umeendelea hadi hivi leo na kusababisha kuwepo kwa haja kubwa ya kuibuka taaluma ya ufundishaji wa baadhi ya lugha za wazawa kwa wageni, hasa lugha zenye mawanda mapana kimawasiliano Kiswahili kikiwemo.

Wageni wengi waliotembelea maeneo mbalimbali ya Afrika walihitaji kujifunza lugha na tamaduni za wazawa kwa malengo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, masomo, utalii na shughuli kadha wa kadha za kikazi (Mtesigwa, 2009). Katika ukanda wa Afrika ya Mashariki lugha ya Kiswahili iliwavutia wageni wengi kujifunza kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu wanaoizungumza na msambao wa eneo ambalo lugha ya Kiswahili inatumika. Inakadiriwa, idadi ya watu milioni themanini katika Afrika Mashariki na kwingineko barani Afrika wanazungumza Kiswahili hususani katika nchi kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Somalia, Msumbiji, Malawi, Rwanda, Burundi, Zambia na Kongo (zamani Zaire) (Ojiambo, 2014).

Katika Tanzania, ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni umekuwa ukifanywa katika taasisi mbalimbali pamoja na watu binafsi; baadhi ya taasisi

hizo ni Alliance Française Arusha, Morden Lingustic and African Culture (MOLAC)-Arusha, MS Training Centre for Development Co-operation (MS TCDC)-Arusha, na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) -Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo kubwa la ufundishaji huo ni kuhakikisha mjifunzaji anapata maarifa yanayofaa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili katika stadi zote za lugha yaani kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. Mchakato wa ujifunzaji Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na namna ya kutumia ya mbinu za ufundishaji wa lugha hiyo.

Kutokana na uhitaji mkumbwa, ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni au Lugha ya Pili, tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii. Gawasike (2014) anajadili mbinu mbadala ambazo zinaweza kutumika kufundishia Lugha ya Kigeni au Lugha ya Pili ili kuondokana na tatizo la usukuku kwa jamii ya Wakinga ambao wanajifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Gawasike (keshatajwa) anapendekeza kufanyika kwa usasanyuzi wa mahitaji ya wajifunzaji wa lugha, pafanyike upimaji uwezo wa wajifunzaji, pawe na ukuzaji wa mtazamo chanya juu ya lugha lengwa wanayojifunza, kupandikiza mbinu mahususi za ujifunzaji na kuendeleza umilisi wa lugha na mkakati wa kipragmatiki miongoni mwa wajifunzaji.

Naye Saidi (2018) alitafiti kuhusu mbinu ya kutumia magazeti katika kufundisha stadi ya kusoma. Matokeo ya utafiti wake yanabainisha wazi umuhimu wa kutumia magazeti katika kufundisha stadi ya kusoma ambao ni kuwawezesha wajifunzaji kujua namna neno linavyoandikwa, kuelewa maneno yanavyotumika katika miktadha mbalimbali, kuwajengea wajifunzaji uwezo wa kusoma na kusikiliza. Halikadhalika Mkomwa (2019) alichunguza dosari za kimofosintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Utafiti wake ulikuwa mahususi katika kuchambua dosari za Kimofosintaksia na mbinu zinazoweza kupunguza dosari hizo. Mkomwa (keshatajwa) anapendekeza matumizi ya mbinu ya ingizo ambalo ni sahihi ili kumpa muda mjifunzaji wa kukumbuka.

Ijapokuwa kuna maelezo yaliyo wazi ya namna ya kutumia Nadhariatete ya Ingizo iliyoasisiwa na Stephen Krashen katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni, bado pamekuwepo na malalamiko ya aina mbili kutoka kwa wajifunzaji ambayo ni kuwepo kwa taarifa nyingi darasani wakati wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, wengine hasa katika madarasa ya hatua ya pili na ya tatu kuona kuwa taarifa azipatazo mjifunzaji darasani hazimpi changamoto ya kutosha kupata maarifa mapya wakati wa ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Kauli hizi mbili zimekuwa ni sehemu ya mazungumzo ya wajifunzaji katikati ya tathmini mbalimbali zinazofanywa wakati wa ujifunzaji na hata mwisho wa kozi au programu husika ya ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Hivyo, makala hii inatathmini ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo ili kubaini mbinu za Nadhariatete ya Ingizo zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, na kutathmini matumizi ya mbinu hizo kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo. Kwa kufanya hivyo kunasaidia kuona namna ya kuwasaidia walimu kutumia mbinu hizo kwa namna itakayompa mjifunzaji ingizo kulingana na kiwango chake cha uelewa.

1.1 DHANA YA NADHARIATETE YA INGIZO

Kwa mujibu wa Gass na Mackey (2015), ingizo ni lugha ambayo mwanafunzi hukutana nayo katika uga au muktadha wa kimawasiliano kwa njia ya kusikiliza, kusoma, na kutazama ishara mbalimbali ikiwa ni lugha ya ishara.Kwa maneno mengine ingizo hujumuisha taarifa za kiisimu na za kimatumizi azipatazo mjifunzaji wa Lugha ya Pili au ya Kigeni ambazo zinaweza kuwa katika mfumo wa maandishi, mazungumzo, au ishara. Nadhariatete ya Ingizo iliasisiwa na Krashen mwaka 1982. Nadhariatete hii inasisitiza kuwa ingizo hutokea pale ambapo wajifunzaji wanaipata lugha na kuielewa, na kuweza kuitumia katika

muktadha wa matumizi halisi, na si kujua namna lugha ilivyo tu. Kulingana na Krashen hili ndilo anaona kuwa ni ingizo faafu.

Krashen na Terrel (1983) wanafafanua Nadhariatete ya Ingizo kuwa mwanafunzi anaweza kutoka katika hatua *i* (ambapo *i* ni kiwango cha umilisi alichonacho mwanafunzi wa Lugha ya Kigeni) hadi *i + 1* (ambapo*i + 1* ni hatua ambayo inafuata tu baada ya *i* katika mpangilio asili) endapo tu ataelewa lugha *i + 1*. Wataalamu hawa wanaona kuwa, kama mwanafunzi atakuwa hana uelewa wowote na Lugha ya Kigeni basi mwanafunzi huyo yupo katika ngazi ya *i*; na mara anapoanza kuielewa lugha hiyo basi anakuwa katika ngazi ya *i + 1*.

Katika hatua nyingine ya matumizi ya Nadhariatete ya Ingizo inapaswa iwe na *i + 1* ili mwanafunzi aweze kujifunza Lugha ya Kigeni. Hii ni sawa na kusema kuwa kama mawasiliano yanafanikiwa basi *i + 1* inapatikana katika kile ambacho mwanafunzi anakisikia. Katika Nadhariatete ya Ingizo katika ufundishaji wa Lugha ya Kigeni, Ellis (1985) anaona kuwa ingizo halipaswi kuwa gumu sana wala rahisi sana bali linapaswa kuwa katikati ya ugumu na urahisi. Hivyo nadhariatete ya ingizo imeweka bayana namna ya kumfindisha mwanafunzi kwa kumpa ingizo analoweza kumudu.

Pia kuna mbinu kadha zinazobainishwa na Nadhariatete ya Ingizo ambazo hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni ambazo ni: daiolojia, maswali na majibu, utoaji wa taarifa, uigizaji dhima, matumizi ya vitendo, michezo ya lugha, kwa kutaja chache. Kwa mujibu wa Nathariatete hii kila mbinu ina kanuni zake za kuzingatiwa na mwalimu anapotumia darasani ili kumpa mwanafunzi ingizo lililo sahihi (Krashen na Terrel, 1983). Hivyo makala hii inatathmini mbinu zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo.

2.0 MBINU ZA UTAFITI

Uchanganuzi kifani ni usanifu ambao uliwezesha makala hii kuteua mahali na vitu ambavyo vilishughulikiwa katika mchakato mzima wa utafutaji taarifa. Makala iliteua vyuo vitatu ambavyo ni MS TCDC-Arusha, MOLAC-Arushana Alliance Française Arusha. Makala hii ilitumia mkabala wa kitaamuli ambapo data ziliwasilishwa, na kuchanganuliwa kwa maelezo. Sambamba na mkabala huo, takwimu elezi pia zilitumika katika uchanganuzi wa data. Aidha, usampulishaji lengwa ulitumika katika uchaguzi wa vyuo na taasisi zenye uzoefu wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Pia usampulishaji lengwa ulitumika katika kuwapata walimu 9 wanaofundisha Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Mbinu hii ilitumika kwa sababu walimu katika uga wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni ni wachache.

Data zilikusanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya makala. Katika ukusanyaji wa data hizi, ulifanyika ushuhudiaji kwa mwalimu mmoja mmoja darasani ili kubaini, na kutathmini mbinu wanazotumia katika ufundishaji Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kuongozwa na Nadhariatete ya Ingizo. Ushuhudiaji ulifanyika kwa ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu.

Uchanganuzi wa data ulitumia mbinu ya kimuktadha, mbinu hii ilionekana kufaa zaidi kuchanganulia data zilizokusanywa kwa mkabala wa kitaamuli. Hii ni kwa sababu mbinu hizi huzipa nafasi hata data-ibuka ambazo hazikupangwa na mtafiti kuchanganuliwa kufanyiwa kazi. Aidha, majedwali maalumu pia yalitumika katika mchakato wa uwasilishaji, na uchanganuzi wa data za ushuhudiaji.

3.0 MATOKEO YA UTAFITI

Katika sehemu hii matokeo yamewasilishwa na kuchambuliwa kama yalivyopatikana uwandani. Uwasilishaji wa data kuhusu ubainishaji wa mbinu za Nadhariatete ya Ingizo zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, na tathmini ya matumizi ya mbinu hizo katika kufundishia na kujifunzia Kiswahili ikiwa ni

Lugha ya Kigeni umeoneshwa kwa muhtasari katika jedwali namba 1 ambalo linaonesha data za ushuhudiaji uliofanyika katika awamu mbili tofauti kwa kila mwalimu kwa madarasa matatu ya lugha ya Kiswahili yaani darasa la ngazi ya kwanza, la ngazi ya pili na ngazi ya tatu kama ifuatavyo;

Jedwali 1: Tathmini ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo

Na.	**Utumikaji wa Mbinu ya...**	**Awamu za Ushuhudiaji**									
		Awamu ya Kwanza					**Awamu ya Pili**				
		1	**2**	**3**	**4**	**5**	**1**	**2**	**3**	**4**	**5**
	Daiolojia yenye mada mtambuka	5	1	3			6	3			1
	Maswali na majibu yenye kuzingatia viwango vya wanafunzi		5	4			5	3	1		
	Utoaji taarifa wenye kuzingatia viwango vya wanafunzi	4	2	3			5	4			
	Uigizaji dhima wenye kuzingatia utayari wa mwanafunzi	6	3				7	2			
	Utumizi wa vitendo wenye kuibua maana			7	2			5	4		
	Michezo ya Lugha yenye kuzingatia utayari na viwango vya wanafunzi		9					7	3		
	Majadiliano yenye kuzingatia mada mtambuka na utayari wa mjifunzaji	7	2				6	2			1
	Nyimbo			4	4	1				9	

Ufunguo: **1**= Anatumia kwa kutozingatia kabisa NtI[1]
2= Anatumia kwa kuzingatia NtI kwa Nadra sana
3= Anatumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati
4= Anatumia kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi
5= Anaitumia kwa kuzingatia NtI kwa muda wote

Jedwali la 1 linaonesha mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia NtI zilizojitokeza katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika vituo ambavyo vilihusika katika ukusanyaji wa data hii kwa njia ya ushuhudiaji, na tathmini ya mbinu hizo. Mbinu za kumpa mjifunzaji ingizo zilizojitokeza na zilizotathminiwa ni: daiolojia yenye kuzingatia mada mtambuka, maswali na majibu yenye kuzingatia viwango vya wanafunzi, utoaji wa taarifa wenye kuzingatia viwango vya wanafunzi kwa maana ya tungo wanazoweza kutoa na uwezo wao wa kuzungumza kulingana na kiwango cha maarifa walichonacho.

Halikadhalika, uigizaji dhima wenye kuzingatia utayari wa mjifunzaji, matumizi ya vitendo vyenye kuibua maana bila kuchanganya lugha katika kuelezea au kufafanua dhana,

[1] Nadhariatete ya Ingizo

majadiliano yenye kuzingatia mada mtambuka na utayari wa mwanafunzi; pia mbinu ya nyimbo ingawa haijajitokeza waziwazi katika NtI inayohusu ufundishaji wa Kiswahili ikiwa Lugha ya Kigeni lakini ilionekana kutumika darasani wakati watafiti walipokuwa wanashuhudia ili kutathmini matumizi ya mbinu hizo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbinu sita zilitumika katika ngazi zote tatu lakini matumizi ya kila mbinu yalitofautiana kimaudhui kati ya kiwango kimoja na kingine wakati mbinu ya utoaji taarifa na majadiliano zilitumika katika ngazi ya pili na na ya tatu. Ufuatao ni uwasilishaji wa data za tathmini ya matumizi ya mbinu hizi kwa kutumia NtI katika ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni LGK[2].Hapa mbinu moja moja imetathiminiwa.

3.1 MBINU YA DAIOLOJIA YENYE MADA MTAMBUKA

Mbinu ya daiolojia inahusisha wanafunzi kupata wasaa wa kujadiliana juu ya kile walichojifunza darasani. Kwa mujibu wa NtI matumizi ya mbinu hii humtaka mwalimu kuwaongoza na kuwashawishi wanafunzi kujibizana kwa kuzingatia uwezo wao wa lugha walionao. Jedwali la 2 linaonesha awamu mbili za ushuhudiaji na idadi ya namba ya walimu na asilimia zake.

Jedwali 2: Tathmini ya Mbinu ya Daiolojia Ngazi ya I-III

Mbinu	Ushuhudiaji Awamu ya Kwanza	Ushuhudiaji Awamu ya Pili
Daiolojia	5 (55.6%) wanatumia kwa kutozingatia kabisa NtI 1 (11.1%) anatumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana 3 (33.3%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati 0 (00.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote	6 (66.7%) wanatumia kwa kutozingatia kabisa NtI 2 (22.2%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana 0 (00.0%) inatumika kwa baadhi ya wakati 1 (11.1%) anatumia kwa kuzingatia NtI kwa muda wote

Katika data za jedwali la 2, inaonesha kuwa mbinu ya daiolojia yenye kuzingatia mada mtambuka katika awamu ya kwanza ya ushuhudiaji haikutumiwa kabisa kwa kuzingatia NtI na walimu 5 ambao ni sawa na 55.6% walioshuhudiwa wakifundisha lakini mwalimu 1 sawa na 11.1% alitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana wakati walimu 3 sawa na 33.3% walitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati katika ufundishaji.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji, walimu 6 sawa na 66.7% walitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana wakati walimu 3 sawa na 33.3% walitumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati ingawa mwalimu 1 sawa na 11.1% alitumia mbinu hii jinsi inavyopendekezwa na NtI katika ufundishaji wake kwa wakati wote. NtI inaelekeza kuwepo na utayari wa mwanafunzi kushiriki katika shughuli mbalimbali katika darasa. Wanafunzi walionekana kuwa tayari kushiriki katika daiolojia kama ilivyoelekezwa na mwalimu.

Hii ina maana kuwa 11.1% tu kati ya walimu wote waliweza kutumia mbinu ya daiolojia kwa kuzingatia NtI. Hivyo ni idadi ndogo sana ya walimu wanatumia mbinu ya daiolojia kama ilivyowekewa mwongozo na NtI katika ngazi zote tatu.

3.2 MASWALI NA MAJIBU

Mbinu ya maswali na majibu pia ilibainishwa na walimu kuwa ni moja ya mbinu wanazotumia katika kufundisha Kiswahili ikiwa ni LGK. Katika mbinu hii maswali na

[2]Lugha ya Kigeni

majibu hutawala baina ya mwalimu na mjifunzaji. Mwalimu anaweza kuuliza swali kwa mjifunzaji ili ajibu, na kinyume chake. Data zifuatazo katika jedwali la 3 zinaonesha tathmini kwa muhtasari wa namna mbinu hii inavyotumika kama vile NtI inavyoelekeza.

Jedwali 3: Tathmini ya Mbinu ya Maswali na Majibu Ngazi ya I-III

Mbinu	Ushuhudiaji Awamu ya Kwanza	
Maswali na majibu	0 (0.00%) inatumika kwa kutozingatia kabisa NtI. 5 (55.6%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 4 (44.4%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (00.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0(00.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.	5 (55.6%) wanatumia kwa kutozingatia kabisa NtI 3 (33.3%)atia NtI kwa nadra sana. 1 (11.1%) atia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (00.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0(00.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote

Data za awamu ya kwanza katika jedwali la 3 zinaonesha kuwa hakuna mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya maswali na majibu kwa kutozingatia kabisa NtI lakini walimu 5 sawa na 55.6% walitumia mbinu hii ya maswali na majibu kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana na walimu 4 sawa na 44.4% walitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI. Data inaonesha hapakuwepo na mwalimu yeyote aliyetumia mbinu ya maswali na majibu kwa kuzingatia NtI kwa wakati mwingi wala aliyetumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji, data inadhihirisha kuwa walimu 5 sawa na 55.6% walitumia mbinu ya maswali na majibu kwa kutozingatia kabisa NtI. Walimu 3 sawa na 33.3% walitumia mbinu ya maswali na majibu kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana wakati mwalimu 1 sawa na 11.1% alitumia mbinu ya maswali na majibu kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. Pia data inaonesha kuwa hapakuwepo na mwalimu yeyote katika awamu ya pili aliyetumia mbinu hii ya maswali na majibu kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala kwa muda wote.

Data hii ina maana kuwa yapo matumizi ya mbinu hii ya maswali na majibu katika ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni LGK. Walimu wachache sana ambao wanatumia mbinu hii kwa ufanisi hata hivyo matumizi hayo yanajidhihirisha kwa kiwango cha nadra na kwa kiwango cha baadhi ya wakati tu. Hivyo mbinu hii inaonekana muda mwingi kutokutumika kwa kuzingatia mwongozo wa NtI.

3.3 MBINU YA UTOAJI TAARIFA

Mbinu hii ilijitokeza katika baadhi ya madarasa hasa darasa la ngazi ya pili na ya tatu ambapo wajifunzaji wanapewa zoezi la kwenda kudadisi juu ya jambo fulani na kisha kutoa taarifa darasani kama sehemu ya kujifunza lugha kupitia jambo hilo walilolidadisi au kulitafiti. Kwa mujibu wa NtI mbinu ya utoaji taarifa inapaswa kuendeshwa kulingana na kiwango cha lugha na utayari wa mwanafunzi na hivyo hushauriwa kutumika katika ngazi ya pili na ya tatu ya ujifunzaji wa lugha. Data za utekelezaji wa tathmini ya mbinu hii kwa kutumia NtI zinawasilishwa katika jedwali la 4 kwa muhtasari kama ifuatavyo.

Jedwali 4: Tathmini ya Mbinu ya Utoaji Taarifa Ngazi ya II-III

Mbinu	**Awamu ya Kwanza ya Ushuhudiaji**	Awamu ya Pili ya Ushuhudiaji
Utoaji Taarifa	4 (44.4%) walitumia kwa kutozingatia kabisa NtI. 2 (22.2%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 3 (33.3%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati.	5 (55.6%) walitumia kwa kutozingatia kabisa NtI. 4 (44.4%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 0 (0.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati.

Jedwali la 4 linadhihirisha data zinazohusu tathmini ya mbinu ya utoaji wa taarifa ambayo ilishuhudiwa kwa awamu mbili katika vituo husika. Katika awamu ya kwanza ya ushuhudiaji data zinadhihirisha kuwa walimu 4 sawa na 44.4% walitumia mbinu ya utoaji wa taarifa kwa kutozingatia kabisa NtI, walimu 2 sawa na 22.2% walitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Pia, data zinabainisha kuwa walimu 3 sawa na 33.3% walitumia mbinu ya utoaji taarifa kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. Hata hivyo katika awamu ya kwanza hapakuwepo na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala kwa wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni LGK.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji, data zinadhihirisha kuwa walimu 5 sawa na 55.6% walitumia mbinu ya utoaji taarifa kwa kutozingatia kabisa NtI wakati walimu 4 sawa na 44.4% walitumia mbinu ya utoaji taarifa kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Katika awamu hii ya pili data zinaonesha kuwa hapakuwepo na mwalimu yeyote aliyetumia mbinu ya utoaji taarifa kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala kutumia mbinu ya utoaji taarifa kwa kuzingatia NtI kwa wakati wote.

Data hii inadhihirisha kuwa idadi kubwa ya walimu wanatumia mbinu hii bila kuyazingatia masuala kama vile aina ya tungo ambayo wanafunzi wanaweza kuitoa na aina ya mambo ambayo wanafunzi wanaweza kuyazungumzia kulingana na kiwango chao cha lugha kwa wakati huo. Hata hivyo wanaotumia mbinu hii darasani kwa kuzingatia NtI kuna wakati wanazingatia matumizi sahihi lakini ni wachache. Jambo hili huenda linaweza kuathiri tathmini za wanafunzi kuhusu mwalimu na hata kozi ya lugha wanayojifunza.

3.4 MBINU YA UIGIZAJI DHIMA

Mbinu ya uigizaji dhima imejitokeza sana katika ushuhudiaji uwandani. Mbinu hii inamtaka mjifunzaji kuvaa uhusika fulani na kuzungumza kuendana na uhusika aliouvaa. Uhusika huo huweza kuwa ni uhusika wa daktari, mwalimu, mkandarasi kwa kutaja kwa uchache. Mbinu hii ilijitokeza kutumiwa katika ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu, na imetathminiwa kwa muhtasari katika jedwali la 5 kama ifuatavyo.

Jedwali 5: Mbinu ya Uigizaji Dhima Ngazi ya I-III

Mbinu	**Awamu ya kwanza ya Ushuhudiaji**	**Awamu ya pili ya Ushuhudiaji**
Uigizaji dhima	6 (66.7%) walitumia kwa kutozingatia kabisa NtI. 3 (33.3%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 0 (0.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) inatumika kwa kuzingatia	7 (77.8%) ngatia kabisa NtI. 2 (22.2%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 0 (0.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.0%) atia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

	NtI kwa muda wote.	

Data kwenye jedwali la 5 katika ushuhudiaji wa awamu ya kwanza inadhihirisha kuwa walimu 6 sawa na 66.7% walitumia mbinu ya uigizaji dhima kwa kutozingatia kabisa NtI, walimu 3 sawa na 33.3% walifundisha kwa kutumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Katika awamu ya kwanza hapakuwepo na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu hii ya uigizaji dhima kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala aliyetumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji data inadhihirisha kuwa walimu 7 hawakuzingatia kabisa NtI wakati walimu 2 sawa na 22.2% ya walimu wote walitumia mbinu hii ya uigizaji dhima kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Data pia inabainisha kuwa hapakuwepo na mwalimu yeyote ambaye alitumia mbinu hii ya uigizaji dhima kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, kwa muda mwingi wala kwa kuzingatia NtI kwa wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni LGK.

Utafiti unaonesha kuwa licha ya kuwa mbinu hii inatumika katika madarasa ya ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu ya ufundishaji wa Kiswahili, ni wazi kwamba haitumiki ipasavyo ili kuleta tija katika ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. NtI katika mbinu hii inaeleza kuzingatia masuala ya utayari wa mjifunzaji kuweza kuigiza, kiwango cha msamiati alicho nacho mjifunzaji, na aina za tungo ambazo mjifunzaji anaweza kuzitoa wakati wa kuigiza. Masuala haya yote kwa kiasi kikubwa hayakuzingatiwa na idadi kubwa ya walimu wanaofundisha Kiswahili ikiwa kama LGK hali inayoifanya mbinu hii kutokuwa na ufanisi wa kutosha katika kumpatia mjifunzaji ingizo stahiki.

3.5 MBINU YA UTUMIZI WA VITENDO

Katika mbinu hii, mwalimu hutumia vitendo ili kuweza kueleza dhana au maana ya neno. Lengo ni kuepuka uchanganyaji wa lugha wakati wa ufundishaji wake. Mbinu hii inamtaka mwalimu atumie njia yoyote ile kueleza au kufafanua dhana kwa viungo au mijongeo ya mwili. Mbinu hii ilitumika katika madarasa yote matatu (ngazi ya kwanza, ya pili, na ya tatu). Data za mbinu ya vitendo zimewasilishwa katika jedwali la 6 kwa muhtasari kama ifuatavyo.

Jedwali 6: Mbinu ya Utumizi wa Vitendo Ngazi ya I-III

Mbinu	Ushuhudiaji Awamu ya Kwanza	Ushuhudiaji Awamu ya Pili
Vitendo	0 (0.0%) inatumika kwa kutozingatia kabisa NtI. 0 (0.0%) inatumika kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 7 (77.8%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 2 (22.2%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.	0 (0.0%) ilitumika kwa kutozingatia kabisa NtI. 5 (55.6%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 4 (44.4%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

Data za awamu ya kwanza ya ushuhudiaji katika Jedwali la 6 zinabainisha kuwa hapakuwa na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya vitendo kwa kutozingatia NtI kabisa wala waliotumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Walimu 7 sawa na 77.8% walitumia mbinu hii kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, na 2 sawa na

22.2% walitumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi katika ufundishaji lakini hakuna mwalimu aliyetumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa muda wote wa ufundishaji.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji data zinadhihirisha kuwa hapakuwepo na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya vitendo kwa kutozingatika kabisa NtI lakini walimu 5 sawa na 55.6% walitumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana; na walimu 4 sawa na 44.4% walitumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. Hata hivyo data inadhihirisha kutokuwepo kwa mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala kwa wakati wote wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Hii ina maana kuwa hapakuwepo na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu hii ya vitendo kwa kuzingatia NtI kwa muda wote alipoitumia. Walimu wengine walitumia mbinu hii kwa kuchanganya na lugha ya Kiingereza pale waliposhindwa kueleza dhana kwa kutumia matendo ikiwa ni kinyume na NtI. NtI inasisitiza kutotumia lugha nyingine yoyote kinyume na lugha lengwa ambayo katika muktadha huu ni lugha ya Kiswahili.

3.6 MBINU YA MICHEZO YA LUGHA

Mbinu ya michezo ya lugha ni miongoni mwa mbinu iliyobainika kutumiwa na walimu darasani katika ngazi zote ambazo ni ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Mbinu hii ni moja kati ya mbinu za kimawasiliano zinazotumika katika ufundishaji wa LGK. Katika NtI mbinu hii inashauriwa kutumiwa katika darasa ambapo wanafunzi wapo tayari, na michezo hiyo izingatie kiwango cha mwanafunzi alichonacho katika kutumia lugha lengwa. Katika jedwali la 7 mbinu hii imewasilishwa kwa muhtasari kama ifuatavyo.

Jedwali 7: Mbinu ya Michezo ya Lugha Ngazi ya I-III

Mbinu	Ushuhudiaji Awamu ya Kwanza	Ushuhudiaji Awamu ya Pili
Michezo ya Lugha	0 (0.0%) ilitumika kwa kutozingatia kabisa NtI 9 (100%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.	0 (0.0%) ilitumika kwa kutozingatia kabisa NtI. 6 (66.6%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 3 (33.3%) wanatumia kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi. 0 (0.00%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

Jedwali la 7 katika ushuhudiaji wa awamu ya kwanza, data zinadhihirisha kuwa hakuna mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya michezo ya lugha kwa kutozingatia kabisa NtI. Walimu 9 sawa na 100% waliotumia mbinu hii ya michezo ya lugha waliitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Katika awamu hii hapakuwa na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya michezo ya lugha kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, kutumia kwa muda mwingi wala kutumia kwa muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa LGK.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji, data zinadhihirisha kuwa hapakuwepo pia na mwalimu hata mmoja aliyetumia mbinu hii kwa kutozingatia kabisa NtI. Walimu 6 sawa na 66.7% walitumia mbinu ya michezo ya lugha kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana wakati walimu 3 sawa na 33.3% walitumia mbinu ya michezo ya lugha kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. Data hizi zinadhihirisha pia hakuwepo mwalimu hata mmoja aliyetumia

mbinu hii ya michezo ya lugha kwa kuzingatia NtI kwa muda mwingi wala kwa muda wote wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni LGK.

Data inaweka wazi kuwa mbinu ya michezo ya lugha ilitumiwa na walimu wote katika vituo vilivyohusika katika utafiti huu lakini utumizi wake haukidhi vigezo vile anavyobainisha Krasheni katika NtI. Miongoni mwa vigezo ambavyo havifuatwi nawalimu wakati wa utumiaji wake ni pamoja na uwezo wa mjifunzaji kuendana na kasi ya mchezo, kiwango cha msamiati alichonacho mjifunzaji na utayari wa mwanafunzi kushiriki katika mchezo husika. Vigezo hivi vilizingatiwa kwa kiwango cha nadra sana au baadhi ya wakati tu hali inayoleta mushkeli katika ufanisi wake.

3.7 MBINU YA MAJADILIANO

Mbinu ya majadiliano inahusisha wajifunzaji kupata fursa ya kufanya mdahalo kutokana na kile walichojifunza au mada husika. Katika mbinu hii mwalimu huchokoza mada na wajifunzaji huendeleza mada hiyo ili kukazia wanachokifahamu na kupata maarifa mapya. Kwa mujibu wa NtI mbinu ya majadiliano itumike kwa kuzingatia masuala kama hisia, utayari na uwezo wa mjifunzaji kutoa tungo zitakazomwezesha kudumu katika mjadala. Masuala haya yasipozingatiwa ujifunzaji hauwezi kufanikiwa ipasavyo. Mbinu ya mjadala ilionekana kutumika zaidi katika madarasa ya ngazi ya pili na ya tatu. Data katika kipengele hiki zinawasilishwa kwa muhtasari katika jedwali la 8.

Jedwali 8: Tathmini ya Mbinu ya Majadiliano Ngazi ya II-III

Mbinu	Ushuhudiaji Awamu ya Kwanza	Ushuhudiaji Awamu ya Pili
Majadiliano	7 (77.8%) walitumia kwa kutozingatia kabisa NtI. 2 (22.2%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 0 (0.00%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.	6 (66.7%) walitumia kwa kutozingatia kabisa NtI. 2 (22.2%) walitumia kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. 0 (0.0%) ilitumika kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati. 1 (11.1%) alitumia kwa kuzingatia NtI kwa muda wote.

Jedwali la 8 linaonesha jinsi mbinu ya majadiliano ilivyoshuhudiwa ambapo katika awamu ya kwanza inadhihirisha kuwa walimu 7 sawa na 77.8% walitumia mbinu hii ya majadiliano kwa kutozingatia kabisa NtI, na walimu 2 sawa na 22.2% walitumia mbinu ya majadiliano kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Katika awamu ya kwanza data zinadhihirisha kuwa hapakuwa na mwalimu yeyote aliyetumia mbinu hii ya majadiliano kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati, kwa muda mwingi wala kwa muda wote wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Katika awamu ya pili ya ushuhudiaji data zinadhihirisha kuwa walimu 6 sawa na 66.7% walitumia mbinu hii ya majadiliano kwa kutozingatia kabisa NtI. Walimu 2 sawa na 22.2% walitumia mbinu ya majadiliano kwa kuzingatia NtI kwa nadra sana. Kwa upande mwingine, data za ushuhudiaji katika awamu ya pili zinadhihirisha kuwa hapakuwepo na mwalimu hata mmoja ambaye alitumia mbinu ya majadiliano kwa kuzingatia NtI kwa baadhi ya wakati wala kwa muda mwingi lakini mwalimu 1 sawa na 11.1% alitumia mbinu ya majadiliano kwa kuzingatia NtI kwa wakati wote wa ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Data hii inamaanisha kuwa kuna kiasi kidogo sana cha walimu wanaotumia mbinu ya majadiliano ipasavyo kwa muda wote wakati kiasi kikubwa wanatumia mbinu hii ya majadiliano kwa kutozingatia kabisa mwongozo wa NtI, na wengine wachache wanaitumia

mbinu hii lakini ni kwa nadra sana hali ambayo haikidhi haja ya matumizi sahihi ya mbinu hii.

3.8 MBINU YA NYIMBO

Mbinu ya nyimbo ni miongoni mwa mbinu zilizoshuhudiwa kujitokeza katika madarasa ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Mbinu hii haijabainishwa waziwazi katika mbinu zilizopendekezwa na NtI lakini imeonekana kutumika vilivyo.

Mbinu hii ilijitokeza kwa kila awamu ya ushuhudiaji kwa walimu wote walioshuhudiwa wakitumia nyimbo katika kufundisha Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Matumizi ya mbinu hii yalionekana kufuata utayari wa mwanafunzi na kiwango chake. Wanafunzi walionekana kufurahia mbinu hii kwa kadiri ilivyotumika. Mbinu hii ya nyimbo haikuwekwa bayana na NtI hata hivyo ilionekana kujitokeza sana katika madarasa ya ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Matumizi ya mbinu ya nyimbo yalionekana kumpa mjifunzaji ingizo linalostahili kwani nyimbo zilizingatia kiwango cha lugha walichonacho wanafunzi. Wanafunzi katika hatua ya kwanza walishiriki katika kuimba nyimbo ambazo zililenga kuwapa vitenzi na miundo rahisi ya Kiswahili katika kiwango chao. Nyimbo zilizolenga kumpa maarifa kama vitenzi (katika amri, na mtendwa) na salamu vilitumika katika darasa la ujifunzaji wa ngazi ya kwanza.

Katika madarasa ya Kiswahili nyimbo zilizolenga kuibua kauli mbalimbali za lugha ya Kiswahili zilitumika katika ngazi ya pili na ya tatu ya ujifunzaji wa lugha ili kuwapa wanafunzi maarifa ya utumizi wa kauli hizo. Baadhi ya nyimbo zilitumika kama kichokoo cha mada na kuwapa wanafunzi mwanzo wa kujadili baadhi ya mistari katika nyimbo hizo ili kuweza kufanya mazoezi zaidi katika stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Ingawa mbinu hii haikuwekwa wazi na NtI lakini ilionekana kutumika kwa kuzingatia kiwango cha ingizo ambacho mwanafunzi anatakiwa kukipata kulingana na uwezo wake katika lugha.

Kwa ujumla matokeo yamebainisha mbinu saba za Natharitete ya Ingizo zilizojitokeza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni ambazo ni daiolojia, maswali na majibu, utoaji wa taarifa, uigizaji dhima, matumizi ya vitendo, michezo ya lugha na majadiliano. Mbinu karibu zote zilitumika kwa wajifunzaji wa ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu isipokuwa mbinu ya utoaji taarifa na majadiliano ambazo zilitumika katika ngazi ya pili na ya tatu.

Pamoja na hayo, mbinu ya kutumia nyimbo imejitokeza pia kutumika katika ngazi zote tatu hata kama haitajwi wazi katika Nadhariatete ya Ingizo. Kwa upande wa tathimini ya matumizi ya mbinu hizo, matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya walimu wanaotumia mbinu zilizopendekezwa na Nadhariatete ya Ingizo hawazingatii kwa kiwango kikubwa mwongozo wa Nadhariatete hii kama data zilivyodhihirisha.

4.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Makala hii imebaini kuwa walimu wanaofundisha Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni walitumia mbinu mbalimbali katika kufundisha maarifa kwa wajifunzaji wa Kiswahili kama zilivyodhihirishwa katika matokeo. Sehemu hii imeonesha mjadala kuhusu matokeo ya tathmini ya matumizi ya mbinu hizo kwa kutumia Nathariatete ya Ingizo.

4.1 MATUMIZI YA MBINU YA DAIOLOJIA

Matumizi ya mbinu ya daiolojia yanapaswa kuzingatia uwepo wa mada mtambuka katika mazungumzo ya wajifunzaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa walimu 5 ambao ni sawa na 55.6% katika awamu ya kwanza ya ushuhudiaji na walimu 6 sawa na 66.7% katika awamu ya pili hawakutumia kabisa mbinu hii kwa kuzingatia mada mtambuka wakati wa

uingizaji wa maarifa kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Mada nyingi zilizotumiwa katika daiolojia zilikuwa ni zile za kutunga kutoka kwa mwalimu na zinazopatikana katika matini zilizohifadhiwa vitabuni bila kuzingatia masuala mtambuka. Mada za namna hii hazimpi mjifunzaji uwezo wa moja kwa moja wa kuwasiliana katika jamii anayoishi kwani mambo anayojifunza darasani si yale yanayotokea katika matumizi ya jamii husika. Kutokana na hili mjifunzaji anakosa msamiati unaolengwa wenye shabaha ya kumwezasha kumudu, na kudumu katika mawasiliano na wazawa.

4.2 MATUMIZI YA MBINU YA MASWALI NA MAJIBU

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa maswali yaliyoulizwa na walimu kwa wajifunzaji kwa kiwango kikubwa hayakuzingatia viwango vya wajifunzaji. Maswali yaliyoulizwa na walimu hayakuwa na shabaha yoyote ya kukuza uwezo wa mjifunzaji alionao kutokana na kiwango alichopo. NtI inasisitiza kuuliza maswali ambayo yataibua udadisi kutoka kwa mjifunzaji na kumfikirisha zaidi kutoa tungo zenye miundo inayoendana na kiwango chake. Walimu waliuliza maswali hasa katika madarasa ya ngazi ya pili na ya tatu yaliyowahitaji wajifunzaji kuorodhesha ikiwa ni maarifa ya mjifunzaji katika ngazi ya kwanza kwa mujibu wa vigezo vya ACTFL[3].

Sheninger (2018) anasisitiza kuwa mwalimu ni lazima aweze kuuliza swali kikamilifu ili kuweza kumfikirisha mjifunzaji kutoka katika kundi mahususi katika darasa. Maelezo haya yanaelekeza kuwepo kwa ujuzi wa uulizaji maswali yanayoamsha ari ya kufikiria na kutaka kujifunza zaidi kupitia changamoto inayoibuliwa na swali. Kuuliza maswali yanayoibua udadisi kwa mjifunzaji humsaidia kumudu maarifa kwa mjengo wenye mantiki katika upataji wa taaluma. Katika madarasa ya ujifunzaji tulishuhudia walimu kutokuwa na uwezo wa kuuliza maswali yenye kuibua udadisi kulingana na kiwango cha wajifunzaji wanaowafundisha.

Pia uulizaji wa maswali hayo haukulenga kumpa mjifunzaji ingizo linalofaa na analoweza kustahili. Kumpa mjifunzaji ingizo kubwa sana au dogo sana hakumfanyi yeye kupata ingizo la lugha husika. Hoja hii inafanana na hoja ya Ellis (1985) ambapo anaona kuwa ingizo halitakiwi kuwa kubwa sana wala dogo sana kulingana na kiwango cha mjifunzaji, kwani kwa kufanya hivyo ujifunzaji hauwezi kutokea.

4.3 MATUMIZI YA MBINU YA UTOAJI TAARIFA

Katika mbinu ya utoaji taarifa, utafiti unaonesha kuwa mbinu hii haikuzingatia kiwango cha uelewa wa mjifunzaji. Katika ufundishaji, mbinu hii iliwataka wajifunzaji kuzungumza kwa kutumia vifungu vya maneno tofauti na kiwango cha lugha walichonacho. Mwalimu aliwapa wanafunzi kazi na kisha kuwasilisha darasani. Wajifunzaji hawakuweza kuzungumza kutokana na kiwango cha uelewa walichokuwa nacho. NtI inaweka bayana kuwa mjifunzaji hupata lugha kwa kumpa maarifa yaliyopangika katika mfuatano asilia. Hii ni kinyume na kumpa mwanafunzi mazoezi yanayomlazimisha kuzungumza zaidi tofauti na kiwango chake.

Mawazo haya yanaonekana pia katika makala ya Wu (2010) kuwa maendeleo ya mjifunzaji katika ujifunzaji wa lugha ulio katika mpangilio asili yanatokea ikiwa ingizo wanalopewa wajifunzaji lipo juu kidogo ya ngazi waliyopo kwa wakati huo. Kumpa mazoezi magumu ya kujieleza kwa kutumia lugha lengwa mwanafunzi ambaye uelewa wake ni wa ngazi ya chini ni kumpa ingizo kubwa kuliko anavyoweza kumudu lugha hiyo, na hivyo ujifunzaji hauwezi kutokea kutokana na ingizo kuwa kubwa kuliko vile anavyoweza kumudu.

[3] American Council of Teachers of Foreign Languages

4.4 MATUMIZI YA MBINU YA UIGIZAJI DHIMA

Matokeo ya matumizi ya mbinu ya uigizaji dhima yanaweka bayana kuwa, mbinu hii ilitumika bila kuzingatia kuwa mjifunzaji yupo tayari kufanya maigizo dhima kama mwalimu anavyomuhitaji kufanya. Matumizi ya mbinu hii yalionesha wazi kuwa mwalimu waliwalazimisha wanafunzi kufanya maigizo bila ridhaa yao. Richards na Rodgers (1986) wanasisitiza kuwa, licha ya kuwa lengo kubwa la ujifunzaji Lugha ya Kigeni ni kupata ingizo, lakini ni vyema masuala ya hisia na utayari katika kujifunza yatiliwe maanani. Wanaona kuwa, kuwepo na kipindi cha muda wa kutosha cha mjifunzaji kujifunza lugha kabla ya kuanza kuzungumza lugha hiyo; pia pawepo na utayari wa mjifunzaji kusoma maandiko mbalimbali ili kuweza kulipatia ingizo maana na uzito unaofaa. Kwa hiyo muda na utayari wa mjifunzaji ni muhimu katika kumudu stadi nne za lugha: kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

Richards na Rodgers (1986) wanayapa umuhimu zaidi masuala ya hisia kuliko sababu nyingine za utambuzi alionao mjifunzaji katika kujifunza na kumudu msamiati kuliko kanuni za kisarufi (Crystal, 1987). Mwalimu kuamua kutumia mbinu ya uigizaji dhima kwa wanafunzi bila kuzingatia kuwa wanafunzi wapo tayari kufanya uigizaji humfanya mjifunzaji aone kama darasa linamuhitaji kujifunza sana tofauti na vile anavyoweza kumudu. Katika kufanya uigizaji dhima, mwigizaji ambaye ni mjifunzaji hana budi kuwa au kujifunza msamiati wa kutosha ili kuweza kuzungumza katika igizo husika. Mbinu hii ilipotumika kwa wajifunzaji wa hatua ya kwanza ilionesha kuwa na changamoto kwani wajifunzaji walikuwa na kiasi kidogo sana cha msamiati na miundo ya kuweza kutengeneza sentensi. Kwa wajifunzaji wa hatua ya kwanza uigizaji unapaswa kuhusisha msamiati mchache kuliko utendaji, mfano wa igizo la kununua mboga na matunda sokoni kwa ngazi ya kwanza; kwa kuweka mazingira halisi ya mboga na matunda na wajifunzaji kuuza na kununua kwa kutumia maneno hayo machache waliyo nayo, kunawajengea moyo wa kujiamini na kumbukumbu nzuri.

NtI inaelekeza kuwepo kwa kiwango kilicho bayana kinacholingana na uwezo wa mjifunzaji, na kumpa changamoto anayoweza kuimudu ili mjifunzaji kuweza kupata maendeleo katika kujifunza lugha lengwa. Utumiaji wa mbinu hii kwa wanafunzi wa hatua ya kwanza kunasababisha mjifunzaji kujifunza msamiati mwingi na miundo mingi ikiwa ni tofauti na uwezo wa mjifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Hata hivyo matokeo yanaonesha kuwa baadhi ya madarasa katika hatua ya pili na ya tatu mbinu hii ya uigizaji haikutumika kabisa katika kipindi cha ushuhudiaji. Mbinu hii hwenda ingefaa zaidi katika ngazi hizi za juu kutokana na kuwa wajifunzaji wana msamiati na miundo ya kutosha kuwasiliana kwa kiwango chao.

4.5 MATUMIZI YA MBINU YA VITENDO

Katika ushuhudiaji matokeo yanaonesha kuwa baadhi ya walimu walitumia Lugha ya Kigeni kueleza baadhi ya dhana ambazo hawakuweza kutumia vitendo kueleza dhana hizo. Ili kumpa mwanafunzi idadi ya msamiati, matumizi ya lugha lengwa kufundishia lugha lengwa ni muhimu sana. Wataalamu mbalimbali wanakubaliana kuwa matumizi ya vitendo kama chombo cha mawasiliano darasani ni muhimu sana (Lasern-Freeman na Anderson, 2011). Ying (2019) anasisitiza kuwa mkabala wa kimawasiliano unapaswa kuongozwa kwa matumizi ya vitendo na lugha lengwa katika darasa.

Krashen katika NtI anasisitiza kumpa mwanafunzi ingizo linalofaa na analoweza kulimudu. Katika kumpa mwanafunzi ingizo ni vyema kutumia vitendo, na lugha lengwa ambayo itampa msamiati atakaotumia katika mawasilanao yake. Krashen anaendelea

kusisitiza kuwepo na kiwango kidogo cha ziada ambacho mwanafunzi anaweza kukimudu katika kuendeleza lugha yake. Matumizi ya vitendo halisi yanakataza kuwepo kwa Lugha ya Kigeni katika darasa la ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Matumizi ya vitendo kama chombo cha mawasiliano darasani yanaweka tahadhari ya udhibiti wa idadi ya msamiati katika mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi.

4.6 MICHEZO YA LUGHA

Katika matokeo ya utafiti mbinu ya michezo ya lugha inaonekana kutumika katika hatua zote tatu za ufundishaji yaani hatua ya kwanza, hatua ya pili na hatua ya tatu. Walimu walitumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa hasa katika hatua ya kwanza. Ufundishaji wa hapo zamani kabla ya maendeleo ya teknolojia, walimu waliegemea zaidi katika maongezi na chaki, hivi sasa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia imeibuka michezo mbalimbali inayofaa katika ufundishaji wa lugha (Yaccob & Yunus, 2019).

Licha ya kuibuka kwa umuhimu wa kutumia michezo ya lugha, walimu katika ngazi ya pili na ya tatu walionekana kutumia mbinu hii kwa kiwango kikubwa bila kuzingatia utayari wa mwanafunzi katika kushiriki. Matokeo haya yanaendana na hoja walizotoa Richards na Rodgers (1986) kuwa ni vyema masuala ya hisia na utayari katika kujifunza yatiliwe maanani. Matokeao yanaonesha pia kulikuwa na urudiajirudiaji mwingi wa mchezo wa lugha uliolenga kumpa mjifunzaji maarifa yale yale.

NtI inashughulika na kiwango cha ingizo ambalo mjifunzaji anapaswa kupata katika darasa. Michezo hii ya lugha katika ngazi ya pili ilionekana kutompa mjifunzaji changamoto kwa kuwa malengo ya mchezo yalikuwa hayabadiliki kila wanaporudia kucheza mchezo husika. Pia baadhi ya wajifunzaji hawakuwa tayari kushiriki katika mchezo huo darasani hata hivyo walilazimika kushiriki. Katika mazingira ya ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni, NtI inasisitiza kutoa nafasi kwa mjifunzaji kuwa tayari kushiriki katika matukio mbalimbali darasani, hiari hii inampa mwalimu uhuru kidogo wa kumshawishi mjifunzaji kushiriki katika matukio darasani ingawa mjifunzaji ana uhuru wa kukubali au kukataa.

4.7 MATUMIZI YA MBINU YA MAJADILIANO

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbinu ya majadiliano ilitumika bila kuzingatia masuala mtambuka. Katika kutumia mbinu hii, walimu walishuhudiwa wakitoa mada ambazo hazikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na hali iliyopo au inayoendelea katika jamii au mazingira yanayowazunguka wajifunzaji kwa wakati huo, mfano mjadala kuhusu *maisha ya kijana mfugaji na msichana karani*. Patrick (2019) anaeleza kuwa wafundishaji wa Lugha ya Kigeni wanapata changamoto kwa wakati wa miaka hii zaidi kuliko miaka ya nyuma katika ufundishaji wa Lugha za Kigeni kwa wajifunzaji, kwani wana kiu kubwa ya kuwaona wajifunzaji wao wanajifunza na kuweza kuongea lugha kwa haraka sana.

Kutokana na hilo, wafundishaji hawa wamekuwa wakiwalazimisha wanafunzi kuzungumza kwa njia ya mijadala iliyosanifiwa kwa sababu ya kulazimisha matokeo ya haraka. Pia katika mijadala hiyo mfundishaji hughairi kutumia lugha inayowaunganisha wajifunzaji hata kama ipo na badala yake hutumia lugha ile anayoifundisha tu. Kitendo cha kuwalazimisha wanafunzi kuzungumza bila kuzingatia utayari wao kinawafanya wajifunzaji waogope na kuchukia mchakato mzima wa ujifunzaji kwa kufikiri kuwa hawana uwezo wa kujifunza Lugha ya Kigeni.

Kwa mujibu wa Patrick (2019), Nadhariatete ya Ingizo inatambua na kuthamini mchakato mzima wa ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni kuwa ni imara na madhubuti unaopaswa kusukwa kwa utaratibu unaofaa katika ubongo wa mjifunzaji. Anaongeza kuwa kila binadamu anatambuliwa na nadharia hii kuwa ana uwezo wa kujifunza Lugha ya Kigeni lakini kitendawili kinabaki kuwa ni kwa namna gani mchakato huu wa ujifunzaji unaweza kufanikishwa. Nadhariatete ya Ingizo (Krashen, 1982) inasisitiza kuwa uamiliaji wa Lugha

ya Kigeni unapaswa kutokea pale ambapo wajifunzaji wanapata ujumbe unaoeleweka, na wana uwezo wa kuutumia baada ya mchakato wa ujifunzaji, katika mazingira halisi ya wazungumzaji wa lugha husika; kulingana na Krashen hili ndilo anaona kuwa ni ingizo lenye maana.

Katika madarasa yaliyoshuhudiwa, walimu walitumia mada katika mijadala zilizobuniwa na mwalimu lakini mada hizi hazikuzingatia maswala mtambuka yaliyopo katika jamii; mada ambazo wajifunzaji wangeweza kukutana nazo moja kwa moja katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matokeo yanadhihirisha kwamba, walimu walikuwa na ubunifu hafifu sana wa kuibua dhana ambazo zingewasukuma wajifunzaji kuzungumza, na kukuza lugha kwa kupata ingizo linalofaa kulingana na viwango vyao vya lugha walivyonavyo kwa wakati husika.

4.8 MATUMIZI SAHIHI YA MBINU YA NYIMBO

Matokeo yanadhihirisha kuwa mbinu ya nyimbo ilitumika kwa kuzingatia matumizi sahihi ya NtI na walimu wote kwa awamu zote mbili zilizoshuhudiwa katika ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Walimu walizingatia masuala ya utayari wa mjifunzaji katika kushiriki kuimba. Mbinu hii haitajwi wazi wazi na NtI kama ni mbinu inayoweza kutumika katika kumpa mjifunzaji ingizo lakini walimu walitumia mbinu hii kwa kuzingatia kiwango cha wajifunzaji kama NtI inavyoelekeza. Israel (2013) anaeleza kuwa kuna uhusiano wa kukamilishana kati ya nyimbo na uamiliaji wa lugha. Anaendelea kueleza kuwa, tafiti zinadhihirisha kuwa upo mkamilishano chanya pale ambapo nyimbo zinazotumika kwa utaratibu uliopangwa katika darasa. Israel (keshatajwa) anaona kuwa mbinu za kitamaduni za ufundishaji wa lugha zinapaswa kutathminiwa na badala yake nyimbo ziingizwe kama njia ya kuongeza ufanisi katika ujifunzaji lugha.

Ni wazi kwamba ujifunzaji unatokea kwa mwanafunzi kupata ingizo ambalo analimudu na kwa njia anayoifurahia. Wanafunzi wanapohamasika basi wanajifunza zaidi, na hivyo kupata ingizo kwa urahisi na kwa haraka. Kwa muda wote walimu walipotumia mbinu hii, wajifunzaji walionekana kufurahia na kushiriki kikamilifu. Nyimbo zilizoimbwa zililenga kuwapa wajifunzaji maarifa mbali mbali kama vile vitenzi, sauti, na njeo. Hata hivyo si wajifunzaji wote hupenda kujifunza lugha kupitia mbinu ya nyimbo; inapotokea hali hii, mwalimu hana budi kutumia mbinu mbadala itakayowafaa wajifunzaji wa namna hii kama vile michezo ya lugha, ziara na uigizaji dhima. Moticoe (2008) anasisitiza kuwa nyimbo huzungumza pale lugha inaposhindwa kufafanua dhana husika. Hii ni kweli kwani vionjo na mapigo ya kimuziki humsaidia mwanafunzi kupata ingizo jipya la lugha, na kuacha kumbukumbu la msamiati na miundo kadhaa ya tungo ndani ya fikra zake.

Kwa ujumla, utafiti huu umebainisha wazi kwamba asilimia kubwa ya walimu wanatumia mbinu zilizopendekezwa na Nadhariatete ya Ingizo japokuwa wengi wa walimu hao hawazingatii sana kanuni na miongozo ya namna ya kutumia mbinu hizo kama NtI inavyosisitiza.

5.0 HITIMISHO

Makala hii ililenga kutathmini mbinu zinazotumika kufundishia na kujifunzia Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo. Lengo la kwanza lilikuwa kubaini mbinu za Nadhariatete ya Ingizo zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Katika lengo hili matokeo yamebainisha mbinu saba za Natharitete ya Ingizo zilizojitokeza kutumiwa na walimu katika ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni ambazo ni daiolojia, maswali na majibu, utoaji wa taarifa, uigizaji dhima, matumizi ya vitendo, michezo ya lugha, na majadiliano. Pia, mbinu ya nyimbo imejitokeza hata kama haitajwi wazi katika Nadhariatete hii.

Lengo la pili lilikuwa kutathmini matumizi ya mbinu hizo kwa kutumia Nadhariatete ya Ingizo. Katika tathmini ya mbinu, matokeo yanaonesha kuwa asilimia kubwa ya walimu wanaotumia mbinu za Nadhariatete ya Ingizo hawazingatii kwa kiwango kikubwa kanuni na mwongozo kama inavyosisitizwa katika nadhariatete hii. Mathalani, kwa asilimia kubwa mbinu ya daiolojia imeonekana kutumia mada ambazo si halisi isipokuwa za kutungwa bila kuzingatia masuala mtambuka, mbinu ya maswali na majibu imetumika bila kuzingatia kiwango cha mjifunzaji na hivyo kutompa changamoto mjifunzaji au kumpa changamoto asizoweza kumudu kwa kiwango chake; mbinu ya utoaji taarifa imebainika kumpa mjifunzaji ingizo kubwa zaidi ya vile alivyoweza kutenda kwa lugha aliyonayo. Pia, mbinu ya uigizaji dhima imeonekana kutumika bila kuzingatia utayari wa mwanafunzi kufanya igizo kwa lugha lengwa; mbinu ya majadiliano ilitumika kwa kutumia mada za mijadala ya kubuni ambayo haikuwa na uhusiano na maisha halisi ambayo wajifunzaji watakabiliana nayo baada ya kozi ya lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, mbinu ya nyimbo imedhihirika kutumiwa sana, na ilizingatia utayari wa wajifunzaji, na kiwango cha ingizo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Pamoja na hayo, mbinu karibu zote zimetumika katika ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu isipokuwa mbinu ya utoaji taarifa na mbinu ya majadiliano zilizotumika katika ngazi ya pili na ya tatu.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu tunaweza kuhitimisha kama ifuatavyo: kwanza baadhi ya walimu wa Kiswahili hawana taaluma muhimu ya mbinu na namna ya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Walimu wanaonekana kuwa na taaluma tofauti na uwalimu lakini wanafundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni. Walimu walionekana kujikita zaidi katika ufasaha wa tungo zinazotolewa na wanafunzi na kusahau kuwa ujifunzaji wa lugha ni mchakato na sehemu yake ni kufanya makosa ikiwa ni pamoja na makosa ya kimatamshi na ya kisarufi.

Pili, kiwango cha ingizo hakitiliwi mkazo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Walimu wameshuhudiwa wakifundisha msamiati mwingi kwa wanafunzi bila kujali kiwango, na ujuzi wa wanafunzi. Hili limejitokeza katika ngazi zote tatu. Wanafunzi wamekuwa wakipewa idadi kubwa ya msamiati na wakati mwingine msamiati usioendana na maarifa anayopaswa kupata mwanafunzi kwa somo husika ambapo ni kinyume na misingi ya NtI.

Tatu, mbinu ya nyimbo imeonekana kutumika kwa kiasi kikubwa ingawa haijawekwa bayana na NtI. Mbinu hii imeonekana ikitumiwa na walimu wote katika madarasa ya ngazi ya kwanza, pili na ya tatu. Mbinu ya nyimbo imezingatia masuala mtambuka na utayari wa mwanafunzi katika kushiriki mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Mbinu hii inaonekana kubeba sifa za NtI, na kuwa sehemu ya nadhariatete hii.

Kwa ujumla, walimu wanapaswa kufahamu kuwa kila mwanafunzi anaweza kuathiriwa na tajiriba, uzoefu na ubobevu wao katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni. Pia kila mjifunzaji katika darasa la lugha ni tofauti, na huenda wakahitaji mbinu na ingizo tofauti wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Halikadhalika, mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji unapaswa kuyahusisha masuala mtambuka ili kinachofundishwa kilete maana katika matumizi.

Makala hii imebaini kuwa walimu wanafundisha Kiswahili kwa wageni bila kuzingatia masuala mbalimbali kama vile uchaguzi sahihi wa mbinu, utayari wa mwanafunzi, idadi ya msamiati na mazoezi ambapo vyote hivyo vinaathari moja kwa moja kiwango cha ingizo analopata mjifunzaji. Hivyo, ni vema walimu wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara. Pamoja na hayo, tafiti zaidi zifanyike katika eneo hili ili kujua kiasi gani cha ingizo kinatakiwa kwa mwanafunzi wa ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu, na kwa muda gani. Hii itawawezesha walimu kufundisha kwa kuzingatia kiwango cha maarifa ambayo mjifunzaji anastahili kupata katika kila somo ili kupunguza changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni.

MAREJELEO

Crystal, D., (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Ellis, R. (1985). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.

Gass, S. M., & Mackey, A. (2015). Input, Interaction, and Output in Second Language Acquisition. In B. VanPatten na J. Williams (eds.). *Theories in Second Language Acquisition*, 2, 180-206. New York: Routledge.

Israel, H. F. (2013). Language Learning Enhanced by Music and Song. *Literacy Information and Computer Education Journal (LICEJ)*, 2 (1), 1360-1366.

Krashen, S., & Terrell, T. D., (1983). *The Natural Approach. Language Acquisition in the Classroom*. Oxford: Pergamon Press.

Krashen, S. (1982). *Principles and Practices of Second Language Acquisition*. Los Angeles: Pergamon.

Krashen, S. D. (1985). *The Input Hypothesis: Issues and Implications*. London: Longman.

Larsen-Freeman, D., & Anderson, M. (2011). *Techniques and Principles in Language Teaching (3rd edn).* Oxford, England: Oxford University Press.

Mkomwa, G. (2019). *Dosari za Kimofosintaksia Zinazofanywa na Wanafunzi wa Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kigeni*. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Moticoe, M. (April, 2008). Music that Speaks where Language Fails. *The Times*.

Mtesigwa, P. C. K. (2009). Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano, katika *Kiswahili* 72: 52-67.

Ojiambo, P. (2014). *Kiswahili at the University of Kensas*. Imepakuliwa Septembea 23, 2020. Kutoka Chuo Kikuu cha Kensas: https://www2.ku.edu/~kiswahili/.

Patrick, R. (2019). Comprehensible Input. In *Classics Teaching*, 41.

Richards, J. C. & Rodgers, T. (1986). *Approach and Methods in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Richards, J., & Renandya, W. (2002). *Methodology in Language Teaching: An Anthology of Current Practice*. Cambridge: Cambridge University Press.

Said, S. O. (2018). *Mchango wa Magazeti katika Ufundishaji Stadi ya Kusoma kwa Wajifunzaji wa Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kigeni*. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Sheninger, E. (2018). *Scaffolding Questions to Develop Deeper Understanding*. Imechukuliwa May 3, 2021, from A Principal's Reflections: http://esheninger.blogspot.com/2018/02/scaffolding-questions-to-develop-deeper.html.

Wu, W. (2010). The Application of Input Hypothesis to the Teaching of Listening and Speaking of College English. In *Asian Social Science*, 138.

Yaccob, N. S., & Yunus, M. M. (2019). Language Games in Teaching and Learning English Grammar: A Literature Review. In *Arab World English Journal (AWEJ)*, 209 -217.

Ying, S. (2009). How Can Chinese English Teachers Meet the Challenge of Creating a Learner-Centered, Communicative, Intercultural Classroom to Achieve Optimal Student Learning Outcomes? *Canadian Social Science,* .5 .(6), 81-91.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Ubunifu wa Vijana wa Kitanzania Wanavyotumia Lugha ya Kiswahili katika Kubainisha Utambulisho Wao

Dickson Jonas Mlowezi
dizmlo@yahoo.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira

IKISIRI

Mchango wa makala haya umejikita katika kubainisha ubunifu wa vijana wa Kitanzania wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika kubainisha utambulisho wao, lengo hasa likiwa ni kubainisha matamshi, msamiati na sentensi za Kiswahili zinazotumika na kukubaliwa na vijana wa Kitanzania katika kubainisha utambulisho wao. Ukichunguza lugha inayotumiwa na vijana wa Kitanzania utabaini kuwa ina maarifa ambayo yanaongezeka na kupanuka kila siku kwa miaka ya hivi karibuni. Maarifa hayo yamewachochea wataalamu mbalimbali kufanya tafiti na kuandika makala mbalimbali kwa lengo la kutaka kujua hisia za vijana. Hata hivyo, lugha ya vijana haielezi tu hisia za vijana peke yake bali hutumika pia kuelezea utambulisho wa vijana, kuelezea matatizo yao na fikra zao. Pamoja na tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu lugha ya vijana, hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu lugha ya Kiswahili ya vijana inavyobainisha utambulisho wao. Kutokujua lugha ya vijana ya Kiswahili, wanajamii wengine ambao sio vijana wanakosa kujua hisia za vijana, matatizo na ujumbe wa vijana uliobebwa katika lugha yao. Hivyo, makala haya yamechunguza ubunifu wa vijana wa Kitanzania wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika kubainisha utambulisho wao kwa kubainisha matamshi, msamiati na sentensi zinazotumiwa katika mazungumzo yao. Matokeo haya yameonesha kuwa vijana hutumia lugha kwa namna yao lengo likiwa ni kuficha maana iliyokusudiwa na vijana wenyewe, kuficha siri za vijana zisitoke nje ya vijana wenyewe na kuonesha mshikamano miongoni mwa vijana wenyewe, hivyo matokeo haya ya utafiti yatawasaidia wanajamii ambao sio vijana kujua hisia za vijana, matatizo na ujumbe wa vijana uliobebwa katika lugha yao.

MANENO YA MSINGI:
Ubunifu wa Vijana wa Kitanzania, Lugha ya Kiswahili, Utambulisho

1.0 UTANGULIZI

Akizungumzia kuhusu lugha ya vijana, King'ei na Kobia (2007) wanafafanua kuwa, ni lugha ambayo hutumiwa na vijana wanapokuwa peke yao katika mazungumzo. Vijana wakiwa katika mazungumzo yao, hubuni na kuzua matumizi mapya ya msamiati na sentensi ambazo hupewa maana maalumu ambayo hutumika kuwaunganisha na vijana wenzao, kusisitiza utu wao, kuonesha maarifa yao, kuelezea fikra zao na uwezo wao wa kufanya vitu kama vijana (Samper, 2002; Kiessling na Mous, 2004; King'ei na Kobia, 2007; Hurst, 2009; Ferrari, 2014; Harosh & Erastus, 2018; Hurst-Harosh, 2020). King'ei na Kobia (2007) wanasisitiza kuwa lugha ya vijana hutumiwa na vijana wenyewe kama mbinu ya kuelezea ujumbe fulani ili kuwatenga vijana kutoka katika ulimwengu wa watu wengine wasio katika rika la ujana. Ujumbe huo unaweza kuwa unahusiana na utani, kejeli, kuficha siri kwa mambo kama vile wizi, ujambazi, uuzaji wa bidhaa feki na mauaji. Vilevile lugha ya vijana ni miongoni mwa lugha ambazo si sanifu na zinazotumiwa na makundi ya vijana wa rika la umri unaokaribiana na wenye mahusiano fulani kama vile wanafunzi, vijana wa mitaani,

wapiga debe, wabwiya madawa ya kulevya na kadhalika. Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa vijana huwa na lugha yao ambayo huitumia katika uzungumzaji wao kwa malengo tofautitofauti ikiwa ni pamoja na kufikisha ujumbe mbalimbali miongoni mwa vijana wenzao.

1.1 LUGHA NA UTAMBULISHO

Kuhusu suala la utambulisho, Msanjila na Wenzake (2009) wamefasili kuwa utambulisho ni jumla ya vigezo maalumu vinavyotumika kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii au taifa fulani ili kuonesha kuwa liko tofauti na taifa jingine, jamii fulani iko tofauti na jamii nyingine, kundi fulani liko tofauti na kundi jingine, au mtu fulani yupo tofauti na mtu wa kundi jingine, jamii nyingine au taifa jingine.Kwa kuzingatia fasili hii na kwa kutumia kigezo cha lugha tunaweza kubaini utambulisho wa mtu mmoja mmoja ndani ya jamii, utambulisho wa kundi la watu ndani ya jamii na utambulisho wa jamii. Utambulisho wa mtu mmoja mmoja ni upekee wa mwanajamii katika uzungumzaji wake, upekee huo ndio ambao humtambulisha na kumtofautisha na mzungumzaji mwingine wa lugha hiyohiyo inayozungumzwa katika jamii yake. Akifafanua kuhusu utambulisho wa mtu mmojammoja, Wardhaugh (1986) anasema kwamba, kila mtu ana utambulisho wake ambao umejengeka kutokana na jinsi anavyohusiana na kushirikiana na wengine katika jamii. Mambo yanayoweza kumtambulisha mtu ni lugha yake anayoitumia, rangi ya ngozi yake, dini yake, mahali ambako mtu anaishi, tabaka lake alilomo na ukoo wake. Katika mambo yote hayo, lugha ni kiashiria muhimu kwa sababu ni rahisi mtu kujitofautisha na mtu mwingine kutokana na mtindo wake wa matumizi ya lugha, ikiwemo matamshi yake na lafudhi yake. Kuhusu utambulisho wa kundi la watu ndani ya jamii ni kwamba, kundi fulani hujipambanua na kujitofautisha na kundi jingine ndani ya jamiilugha moja kutokana na mtindo wao wa kuzungumza lugha husika. Makundi katika jamii huweza kuzuka kutokana na tofauti za kielimu, umri, kipato, kazi wanayofanya na mahusiano ya wazungumzaji wa lugha hiyo. Kutokana na sababu za kuibuka kwa makundi ya wazungumzaji wa lugha katika jamiilugha fulani, Msanjila na wenzake (2009) wamebainisha kuwepo kwa makundi ya vijana, wazee, wanawake, wanaume, wanafunzi, wanavyuo, wanamichezo, wasomi, wafanyabiashara, wanajeshi, na kadhalika. Uchunguzi wa kina unaweza kubaini kuwa kila kundi la watu katika jamii hutumia aina fulani ya lugha inayolitambulisha kundi husika. Katika makala haya utambulisho wa aina hii umemakinikiwa ili kubaini namna vijana wa Kitanzania wanavyojibainisha kwa kutumia Kiswahili katika mazungumzo yao.

Aidha, kuhusu utambulisho wa jamii, Coulmas (2005:173) anafafanua kuwa, lugha ni alama ya utambulisho wa jamii, hupendwa kutumiwa kama ishara ya mshikamano na hubainisha aina ya watu wanaotumia lugha hiyo kupitia lugha yao. Anaendelea kusema kuwa, aina yetu ya uzungumzaji hutubainisha kuwa sisi ni nani, tumekulia wapi, msimamo wetu katika maisha na tunataka kutambuliwa kupitia jamii gani. Katika makala haya tutashughulikia utambulisho wa kundi la watu katika jamii kwa sababu tafiti na makala nyingi zilizoandikwa zimeshughulikia suala la utambulisho katika hadhi ya jamii au taifa. Kwa mfano, Msanjila na wenzake (2009:54-56) wamezungumzia suala la majina yanavyoitambulisha jamiilugha ya Wagogo na Amri (2011) amechunguza suala la matumizi ya majina katika utambulisho wa jamii ya Watanzania. Hivyo basi, makala haya yamechunguza suala la utambulisho wa kundi la vijana katika jamii kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili. Tauberet-Keller (1989) kama alivyonukuliwa na Msanjila na wenzake (2009) anaeleza kuwa utambulisho wa mtu, kundi la watu katika jamii au jamii umefungamana na mambo mengi ya kijamii kama vile lugha, utamaduni, mila na desturi, mavazi, chakula, dini, historia ya jamii, siasa na uchumi. Haya yote yakizingatiwa kwa pamoja, husaidia kubainisha utambulisho wa mtu, kundi au jamii ukubalike miongoni mwa jamii. Tabouret-Keller (keshatajwa) amefafanua sifa za msingi za kubainisha utambulisho wa mzungumzaji kuwa ni pamoja na kuzingatia lugha ya mzungumzaji, kuzingatia mahali alikozaliwa

mzungumzaji ambako lugha anayoitumia ndiyo lugha kuu ya mawasiliano na kwamba mzungumzaji hujiona kuwa ni sehemu ya jamiilugha na mwenye dhamana ya kuiendeleza na kuidumisha lugha yake.

Ni dhahiri kwamba uhusiano wa lugha na utambulisho umefungamana ndani ya jamii ambamo mzungumzaji hujitambulisha yeye pamoja na jamiilugha yake. Pamoja na utambulisho wa mtu kufungamana na vipengele vyote vilivyotajwa hapo juu, makala haya yamechunguza aina ya lugha ya Kiswahili inayotumiwa na vijana wa Kitanzania ili kubainisha matamshi, msamiati na sentensi zao.

2.0 KIUNZI CHA NADHARIA

Makala haya ya ubunifu vijana wa Kitanzania wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika kubainisha utambulisho wao yameongozwa na nadharia ya Utambulisho wa Kijamii iliyoasisiwa na Tajfel na Turner (1979). Kwa mujibu wa Tajfel na Turner (1979) nadharia ya utambulisho wa kijamii inaelezea jinsi kundi la watu katika jamii linavyounda umoja wao wa kujipambanua na kujitofautisha na kundi jingine ndani ya jamii moja kutokana na matendo wanayofanya au kutokana na mtindo wa uzungumzaji wanaoutumia. Makundi haya ya kijamii huweza kuzuka kutokana na tofauti za kielimu, kiumri, kipato, kazi wanazofanya na mahusiano ya wazungumzaji wa lugha hiyo. Nadharia hii inaelezea pia misingi ya kisaikolojia ya makundi mbalimbali ya watu kama vile makundi ya kifamilia, kijamii na wachezaji wa michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu na mpira wa pete ambayo huwa ni chanzo muhimu cha ufahari na kujiona kuwa wao ni zaidi ya wengine.

Baadaye nadharia hii ilitumika katika kuelezea masuala ya lugha hasa katika taaluma ya isimujamii (Hogg, 2016). Nadharia ya utambulisho wa kijamii imeteuliwa kutumika katika makala haya kutokana na ukweli kwamba ni nadharia iliyojikita katika kuangalia makundi mbalimbali ya watu katika jamii yanavyojitofautisha na kujitambulisha kwa makundi mengine ya jamii hiyohiyo au jamii nyingine. Turner (1987) anafafanua kwamba, nadharia hii haimuangalii mtu mmoja mmoja bali huangalia watu wanaounda kundi fulani ambalo hujitofautisha na makundi mengine ya kijamii. Katika jamii, utambulisho wa makundi mbalimbali hujibainisha na kujitofautisha na makundi mengine kwa namna yao ya uzungumzaji au mahali watokako. Hii ni sifa muhimu kwa nadharia hii kwani husaidia kujua hisia, tabia na matamanio ya makundi hayo katika jamii. Hivyo basi, kutokana na ufafanuzi huu, mkazo wetu katika utambulisho wa vijana umejikita zaidi katika lugha ya Kiswahili inayotumiwa na makundi ya vijana. Vilevile nadharia hii ya utambulisho wa kijamii inasisitiza umoja wa kundi fulani kujitofautisha kwa namna fulani na watu wa kundi jingine. Kujitofautisha huko hujidhihirisha kutokana na lugha wanayoitumia katika mazungumzo yao, kutokana na sehemu ya kijiografia wanayotoka, kazi wanayofanya na kadhalika. Hivyo nadharia hii ya utambulisho wa kijamii imefaa sana katika makala haya kwa sababu imetumika kuelezea aina ya lugha ya Kiswahili inayotumiwa na vijana katika kujitambulisha na kujitofautisha na makundi mengine ya watu katika jamii pana waishio.

Kwa ujumla ni dhahiri kuwa nadharia ya utambulisho wa kijamii ya Tajfel na Turner (1979) imekidhi lengo katika kuelezea lugha ya vijana kwa sababu vijana hujiona kuwa wao ni wamoja wanaojipambanua, kujitofautisha na makundi mengine ya kijamii na ndio maana vijana hupenda kujitambulisha kwa lugha yao. Kama msingi wa nadharia hii unavyosisitiza kuwa kundi fulani la watu katika jamii hujibainisha na kujitofautisha na makundi mengine kwa namna yao ya kuzungumza, katika makala haya ni wazi kundi la vijana limedhihirisha kwa kujibainisha na kujitofautisha na makundi mengine ya kijamii kwa kuendelea kutumia lugha yao ya vijana ya Kiswahili kwa namna ya pekee na kuwafanya watambulike katika jamii.

3.0 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mbinu za zilivyotumika katika mchakato wote wa utafiti huu. Sehemu hii imegawanywa katika sehemu ndogondogo tano. Sehemu ya kwanza inaelezea eneo la utafiti, sehemu ya pili inaelezea mbinu zilizotumika katika ukusanyaji data, sehemu ya tatu inazungumzia kuhusu sampuli iliyotumika katika utafiti huu na sehemu ya nne inahusu uchanganuzi na mjadala wa data

3.1 ENEO LA UTAFITI

Utafiti huu kuhusu Ubunifu wa Vijana wa Kitanzania wanavyotumia Lugha ya Kiswahili katika Kubainisha utambulisho wao ulifanyika katika mkoa Dar es Salaam, manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke, na mkoa wa Arusha katika wilaya ya Arumeru na Arusha jiji. Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha vilichaguliwa kwa sababu ni sehemu zenye mchanganyiko wa vijana wengi kutoka katika jamii mbalimbali. Mchanganyiko huo ni matokeo ya kukua kwa mikoa hiyo na kuwa sehemu muhimu kwa ajira kwani ofisi nyingi, viwanda vingi na shughuli nyingi za vijana za kujiajiri zipo katika mikoa hiyo. Hii ndio sababu kubwa iliyomfanya mtafiti achague mikoa ya Dar es Salaam na Arusha kufanyia utafiti huu.

3.2 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Katika kuchunguza lugha inayotumiwa na vijana wa Kitanzania katika kubainisha utambulisho wao kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili, mtafiti alitumia mbinu mchanganyiko za ukusanyaji data kama ifuatavyo;

3.2.1 Hojaji

Mbinu hii ya hojaji ilichaguliwa na mtafiti kwa sababu inafaa kufanya ulinganifu wa majibu kutoka kwa watafitiwa walioteuliwa ambao wote huulizwa maswali yanayofanana. Mbinu hii pia ina faida kwa sababu ni rahisi kutumika katika ukusanyaji wa taarifa mbalimbali kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi na ni rahisi kufanya majumuisho ya majibu yanayopatikana. Maswali ya hojaji yalilenga watafitiwa wote wenye kujua kusoma na kuandika. Hojaji zote ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili na ziligawanywa kwa sampuli ya watafitiwa walioteuliwa kutoka katika manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala kwa mkoa wa Dar es Salaam na wilaya ya Arumeru na Arusha jiji kwa mkoa wa Arusha.

3.2.2 Mahojiano

Utafiti huu wa lugha inayotumiwa na vijana wa Kitanzania ulitumia aina mbili za mahojiano yaani mahojiano nusufunge na mahojiano huru. Mtafiti alikuwa na dodoso lenye maswali lililomuongoza katika kuwahoji watafitiwa. Uteuzi wa mbinu hii ulitokana na ukweli kwamba ni mbinu ambayo husaidia kupata taarifa za ziada ambazo si rahisi kuzipata kwa kutumia mbinu ya hojaji. Mbinu hii husaidia kupata mawazo na mtazamo wa watafitiwa kuhusu jambo linalotafitiwa.

3.2.3 Ushuhudiaji

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa yeye kwenda uwandani kushuhudia mwenyewe jinsi vijana wa Kitanzania wanavyotumia lugha wanapokuwa katika muktadha wa matumizi katika maeneo yaliyoteuliwa.

3.3 SAMPULI NA USAMPULISHAJI

Katika utafiti huu mtafiti alichagua kutumia usampulishaji nasibu tabakishi ili umsaidie kupata sampuli katika uwakilishi wa makundi mbalimbali. Katika aina hii ya usampulishaji, jumla ya watafitiwa 96 waligawanywa kwa kuzingatia jinsia zao (wanaume 75 na wanawake 21) kutoka katika wilaya tano za mkoa wa Dar es Salaam na Arusha. Idadi hii ya watafitiwa iliteuliwa kwa sababu ni idadi inayotosheleza kutoa matokeo yanayoaminika kutokana na uteuzi sahihi wa watafitiwa. Uzoefu unaonyesha kuwa katika muktadha wa utafiti huu vijana wa kiume hujihusisha zaidi na makundi tajwa kuliko vijana wa kike ndio maana idadi ya watafitiwa imetofautiana kiidadi.
Aidha, katika kupata sampuli ya watafitiwa hiyo, suala la makundi ya vijana lilizingatiwa ambapo kulikuwa na makundi ya vijana yafuatayo: Wapiga debe[4] 30, Vijana wa mitaani[5] 34 na Vijana wa vijiweni[6] 32. Sababu ya kuchagua makundi mchanganyiko ya vijana ilikuwa ni kuchunguza mtazamo wa kila kundi kuhusu aina ya lugha ya vijana inayotumika katika kuwatambulisha. Vilevile makundi hayo yalisaidia kujua kama kila kundi linatumia aina yake ya lugha au makundi yote yanatumia aina moja ya lugha ya vijana.

Mgawanyo wa Watafitiwa kwa Kuzingatia Makundi ya Vijana

Makundi ya Vijana	**Wanaume**	**Wanawake**	**Jumla**
Wapiga debe	25	5	30
Vijana wa mitaani	25	9	34
Vijana wa vijiweni	25	7	32
Jumla	**75**	**21**	**96**

3.4 UCHANGANUZI DATA NA MJADALA WA MATOKEO

Data zilikazokusanywa katika utafiti huu kwa kutumia mbinu za hojaji, mahojiano na ushuhudiaji zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kusimbisha maudhui. Mbinu ya kusimbisha ilitumika kuelezea aina ya matamshi, msamiati na sentensi za Kiswahili zinazotumika na kukubaliwa na vijana wa Dar es Salaam na Arusha katika kubainisha utambulisho wao.

4.0 UBUNIFU WA VIJANA WA KITANZANIA KATIKA KUJITAMBULISHA

Imebainika kwamba vijana wa Kitazania wanapokuwa katika mazungumzo yao hutumia lugha kwa namna ya tofauti za wazungumzaji wengine wa lugha ya Kiswahili ambao sio vijana. Namna hiyo ya kutumia lugha huwa ina matamshi yake, msamiati wake na sentensi zake. Maelezo yafuatayo yanafafanua zaidi

4.1 MATAMSHI YA LUGHA YA VIJANA

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa vijana wa Kitanzania wanapokuwa katika mazungumzo yao huwa na matamshi yao tofauti na wazungumzaji wengine wa lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo;

---

[4] Wapiga debe ni vijana wanaoshinda katika vituo vya mabasi kwa ajili ya kuwatangazia abiria kuwa basi linaelekea wapi.

[5] Vijana wa mitaani ni vijana wanaopatikana katika mitaa mbalimbali na mara nyingi huwa hawana shughuli maalumu ya kufanya.

[6] Vijana wa vijiweni ni vijana wanaokutana kwenye vijiwe ambapo huwa ni kwa ajili ya kufanya biashara ndogondogo kama vile kushona viatu, kutengeneza baiskeli, kuuza madawa ya kulevya au huwa ni kwa lengo la kusimuliana hadithi mbalimbali zihusuzo mapenzi, wizi, utapeli, ujambazi, masuala ya kisiasa nakadhalika.

4.1.1 Matamshi ya Silabi re badala ya Silabi li

Imebainika kwamba, vijana wa Kitanzania hutamka silabi **re** badala ya silabi **li**. Matamshi haya yanahusu baadhi ya maneno ya Kiswahili yenye silabi **li** mwishoni kama mfano wa 1 unavyoonesha.

Matamshi ya Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
1. (a) Mka**re** mmoja ajitokeze	Mka**li** mmoja ajitokeze
(b) Waka**re** kwanza	Waka**li** kwanza
(c) Yule mtoto ni wa ukwe**re**	Yule msichana ni wa ukwe**li**
(d) Shwa**re** sana	Shwa**li** sana

Matamshi haya ya vijana yanaonesha kuwa vijana wa makundi yote hasa wenye elimu ya sekondari yaani wapiga debe, vijana wa mtaani na vijana wa vijiweni hupendelea sana kutumia matamshi ya silabi **re** badala ya silabi **li**. Matumizi ya silabi hii yametokana na ubunifu wa vijana wa kupamba lugha yao na mara nyingi vijana huitamka silabi hii wakiwa na furaha au wakiwa wanasifia jambo fulani kama vile kumsifia mtu kwa uzuri wake kama mfano wa 1(a)-(c) unavyoonesha. Matamshi haya husikika sana yakitumiwa na vijana wengi wanaosoma shule za sekondari au wenye elimu ya sekondari ambao wakitoka shule hushinda vijiweni. Matumizi haya ya silabi **re** yamevuka mipaka ya matumizi yake na kuingia katika vyombo mbalimbali vya habari kama vile katika stesheni za redio na televisheni hasa katika vipindi vinavyotangaza muziki unaojulikana kama muziki wa kisasa au wa kizazi kipya. Kwa mfano, watangazaji wa redio *Clouds Fm, Clouds Tv, Chanel Five, East Africa Radio, Wasafi Fm, Radio 5* na *Kiss Fm* husikika wakitamka silabi **re** badala ya silabi **li** kwa lengo ya kupamba lugha ya Kiswahili ili iwavutie vijana wengi ambao hutumia lugha hiyo na ambao ni wapenzi wa vipindi vya redio na televisheni hizo.

4.1.2 Matamshi ya Silabi ga

Uchunguzi unaonesha kwamba watafitiwa wote walisikika wakitamka silabi **ga**. Silabi **ga** huongezwa mwishoni mwa Kitenzi cha Kiswahili kinachotumiwa na vijana wa Dar es Salaam kama mfano wa 2 unavyoonesha.

Matamshi ya Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
2. (a) Tunakula**ga** mpaka daza	Tunakula mpaka mwisho
(b) Hakuna**ga** noma	Hakuna tatizo
(c) Tunakimbizia**ga** mishe	Tunashughulikia kazi

Kuhusu matamshi ya silabi **ga,** taarifa zinaonesha kuwa hutumiwa sana na vijana wengi wa Arusha na Dar es Salaam, hasa wapiga debe. Aidha, kutokana na taarifa za watafitiwa, mtafiti alibaini kuwa vijana hawa wapiga debe wanavyotumia silabi **ga** wengi wao wana elimu ya shule ya msingi au hawakusoma shule kabisa. Hata hivyo, matamshi haya ya silabi **ga** yamepata mashiko hivi karibuni ya kutumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili hata ambao sio vijana wapiga debe kutokana na sababu kwamba baadhi ya vyombo vya habari kama vile redio *Clouds Fm* ambayo inafahamika kwa jina la redio ya vijana, *Radio Five* na *Kiss Fm* hupenda kutumia silabi **ga.** Vilevile, wasanii wa muziki wa *bongo fleva* wameanza kutumia silabi **ga** katika nyimbo zao. Kama inavyofahamika muziki wa *bongo fleva* unapendwa sana na vijana, hivyo nyimbo hizo zimesababisha matumizi ya silabi **ga** kuongezeka kwa kasi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya vijana wa Kitanzania. Kwa mfano, msanii aitwaye SUMA LEE katika wimbo wake unaoitwa *Hakuna**ga***, ametumia silabi **ga.** Kadhalika wasanii DIAMOND PLATNUMZ, HARMONISE na ALI KIBA nao hupendelea kutumia silabi $**ga**$ katika nyimbo zao mbalimbali.

4.1.3 Matamshi ya Silabi he badala ya Silabi li

Matokeo yanaonesha kwamba vijana katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha hutamka matamshi ya silabi **he** katika neno la Kiswahili *ukweli* badala ya silabi **li**. Matamshi haya ya silabi **he** katika neno la Kiswahili *ukweli* hujitokeza mwishoni mwa neno na kuchukua nafasi ya silabi **li** kama mfano namba 3 unavyoonesha.

Matamshi ya Lugha ya Vijana	**Kiswahili Sanifu**
3. (a) Mnyamwenga wa ukwe**he**	Mtu kutoka ughaibuni ni mzuri
(b) Yule mtoto wa ukwe**he**	Yule msichana ni mzuri
(c) Mishe sio ya ukwe**he** kimpango	Kazi sio nzuri sana

Kuhusu matamshi ya silabi **he**, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa hutumika sana na vijana wa mitaani ambao hutumia silabi **he** pale wanapotaka kusifia jambo fulani kulingana na mazungumzo yao kama mfano wa 3(a)-(b) unavyoonesha jinsi vijana wanavyomsifia mtu kwa uzuri alionao au pale wanapokuwa wakikandia jambo fulani kama mfano wa 3(c) unavyoonesha jinsi vijana wanavyokandia kazi wanayofanya kuwa sio nzuri. Matamshi ya silabi **he** husikika sana yakitamkwa na vijana wafanyabiashara wa Mkoa wa Dar es Salaam kuliko vijana wa mkoa wa Arusha ambako kuna wafanyabiashara vijana wachache.

4.1.4 Matamshi ya Silabi gi

Matokeo yanaonesha kwamba asilimia nyingi ya watafitiwa wote katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha hutumia silabi **gi** mwishoni mwa Kitenzi, kama vile kubali**gi** badala ya kubali. Hata hivyo hii haina maana kwamba matamshi haya yanahusu Kitenzi kubali**gi** tu bali yanahusu pia na vitenzi vingine kama mfano wa 4 unavyoonesha.

Matamshi ya Lugha ya Vijana	**Kiswahili Sanifu**
4. (a) Ishu zile sizikubali**gi**	Mambo yale siyakubali
(b) Mchizi wako simzimia**gi** hata chembe	Rafiki yako simpendi hata kidogo
(c) Skuli maticha walikuwaga wananikubali**gi**	Shule walimu walikuwa wananikubali sana

Utafiti huu unaonesha kuwa, matamshi haya ya silabi gi ya vijana husikika sana kwa vijana wa vijiweni na vijana wa mtaani ambao wengi wao ni wale ambao hawajasoma shule kabisa au wana elimu ya shule ya msingi. Kutokana na maelezo haya ni wazi kwamba ukimsikia kijana anatamka silabi hiyo basi utamtambua kuwa ama ni kijana wa kijiweni au ni kijana wa mtaani na ana kiwango cha elimu ya msingi au hakusoma shule kabisa.

4.1.5 Matamshi ya Silabi ksi badala ya Silabi ka

Kadhalika matokeo yanaonesha kwamba watafitiwa wote katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha walisikika wakitamka silabi ksi badala ya silabi ka katika neno la Kiswahili ***mzuka***. Matamshi ya silabi ksi katika neno **mzuka** hujitokeza mwishoni na kubadili nafasi ya silabi ka kama mfano wa 5 unavyoonesha.

Matamshi ya Lugha ya Vijana	**Kiswahili Sanifu**
5. (a) Mzuk**si** sana	Safi sana
(b) Jana kulikuwa na mizuk**si** mibaya	Jana kulikuwa safi sana
(c) Kulikuwa mzuk**si** usipime, mtu nyomi	Kulikuwa kuzuri sana, kulikuwa na watu wengi

Matamshi haya ya silabi **ksi** badala ya silabi **ka** mwishoni mwa neno la Kiswahili *mzuka* hutumiwa na vijana wengi wa vijiweni, vijana wa mitaani na vijana wapiga debe. Matamshi haya husikika sana pale vijana wanapokuwa katika mazungumzo yanayowafurahisha au wanapokuwa wakisifia jambo fulani kama vile uzuri wa kitu au tukio

fulani. Kwa mfano, matamshi ya mfano wa 5(b)-(c) yanaonesha jinsi vijana wanvyosifia uzuri wa matukio waliyokumbana nayo. Vilevile matamshi haya ya silabi **ksi** badala ya silabi **ka** katika neno *mzuka* husikika pale vijana wanapokuwa wanaitikia salamu au wanapokubali jambo fulani kama mfano wa 5(a) unavyoonesha.

Kwa mujibu wa watafitiwa inaonekana kwamba matamshi ya lugha ya vijana hutamkwa mwishoni mwa neno la Kiswahili kwa kuongezewa silabi fulani au kubadili nafasi ya neno la Kiswahili lililokuwepo awali.

4.2 MSAMIATI WA LUGHA YA VIJANA

Kadhalika, imebainika kuwa lugha ya vijana huwa na msamiati wake. Maelezo na mifano ifuatayo inafafanua zaidi

4.2.1 Uchanganyaji wa Msimbo wa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza

Makala haya yanaonesha kwamba lugha ya vijana huwa ina msamiati wa Kiswahili ambao umechanganya lugha mbili tofauti au zaidi. Msamiati huo wa lugha ya vijana unaotokana na uchanganyaji wa lugha mbalimbali ni matokeo ya kuwepo wingilugha na utandawazi unaopatikana sana katika mitandao ya *WhatsApp, Instagram*, *Facebook, Twitter, Yahoo, Gmail, Hotmail* na hata katika simu za mikononi. Ifuatayo ni mifano ya msamiati uliochanganywa msimbo unaotumiwa na vijana wa Kitanzania kama ifuatavyo:

Msamiati wa Lugha ya Vijana	**Kiswahili Sanifu**
1. (a) **Kashaini** kisenge	**Kapendeza** sana
(b) Pisi yako **inamaind**i kuuza sura	Msichana wako **anapenda** kujionesha
(c) Mtoto wa **getikal**i leo kaachiwa	Msichana **anayefuatiliwa sana na wazazi wake** leo kaachawa huru
(d) **Majoblesi** tunaungaunga	**Tusio na kazi** tunatafuta

Ukichunguza msamiati huo ni wazi utagundua ni msamiati uliotokana na lugha mbili yaani Kiingereza na Kiswahili. Mfano wa 1(a), msamiati wa **kashaini** umetokana na neno la Kiingereza **shine** (*kung'aa)* lililo ambikwa kiambishi cha Kiswahili **ka-** mwanzoni. Mfano wa 1(b), msamiati wa **inamaindi** umetokana na neno la Kiingereza "*mind"* (*kutilia maanani kitu)* lililoambikwa viambishi awali vya Kiswahili **i-** na **-na-**. Mfano 1(c), msamiati wa **getikali** umetokana na uambatishaji wa neno la Kiingereza *"gate"* (*geti)* na neno la Kiswahili **kali** na mfano wa 1(d), msamiati wa **majoblesi** umetokana na neno la Kiingereza "*jobless" (asiye na kazi)* lililoambikwa kiambishi ngeli **ma-** cha Kiswahili. Maelezo haya yanaonesha kuwa, uchanganyaji msimbo hutumiwa sana na vijana wengi wa kike na wa kiume wanaoshinda mitaani au vijiweni ambao wengi wao wana elimu ya sekondari au elimu ya chuo. Maelezo haya yana maana kwamba, vijana huchanganya maneno wakiwa na lengo la kuonesha ama usomi wao, kuficha siri ya kile wanachokiongelea au wanataka kupamba lugha yao.

4.2.2 Msamiati wa Kubuni

Vilevile vijana wa Kitanzania katika kujitambulisha kwao wanatumia msamiati mpya uliyobuniwa kwa kufuata utaratibu unaofuatwa katika Kiswahili Sanifu. Msamiati huo mpya hubuniwa kutokana na mawazo mapya ya vitu vipya vinavyoibuka kila siku. Wakati mwingine vijana hubuni msamiati mwingine wa maneno yaliyokuwa yakitumika zamani. Hali hii inatokana na ukweli kwamba msamiati ukishazoeleka kwa watumiaji wengi katika jamii, husababisha vijana kubuni msamiati wao ambao hutumika miongoni mwao tu. Vilevile msamiati mpya hubuniwa kutokana na sifa ya lugha ya vijana kuwa na msamiati

unaoibuka na kutoweka baada ya kutumika kwa muda fulani. Mifano ifuatayo inaonesha misamiati iliyobuniwa na vijana.

Msamiati wa Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
2. (a) Mambo yameenda **mkazuzu**	Mambo yamekwenda **sawa**
(b) Mpango wa **tilalila** vipi?	Mpango wa **kunywa pombe** vipi?
(c) Wazinguaji **wamejisanua**	Watu wanoko **wameondoka**
(d) Jana tumekula **dawa** kinoma	Jana tumevuta **bangi** sana
(e) **Kilongalonga** changu kimezingua	**Simu** yangu ya kiganjani imeharibika

Katika mifano hiyo hapo juu, mifano ya 2a-b inaonesha msamiati ambao umebuniwa kutoka katika msamiati uliokuwepo zamani. Katika mfano wa 2a, msamiati wa **mkazuzu** una maana ya **sawa**, zamani ulitumika msamiati kama vile **poa, dole na barida**. Katika mfano wa 2b, msamiati wa **tilalila** una maana ya **pombe,** zamani ulitumika msamiati wa **gambe, mtungi.**

Kwa upande wa mfano wa 2c, msamiati wa **sanua** una maana ya **kuondoka,** zamani ulitumika msamiati wa **timua, jikataa, tembea** au **chanja mbuga**. Mfano wa 2d, msamiati wa **dawa** una maana ya **bangi,** zamani ulitumika msamiati wa **ndumu, kaya, sigara kubwa** na **dawa**. Jambo muhimu la kukumbuka katika mifano ya 2a-d ni kwamba msamiati uliotumika zamani sio kwamba umeachwa kutumiwa kabisa katika mazungumzo ya vijana, la hasha, bali wamebuni msamiati mwingine ambao unatumiwa kama kisawe. Kuhusu mfano wa 2e ni dhahiri kuwa msamiati huu wa **kilongalonga** umetokana na kubuni msamiati mpya uliotokana na mawazo mapya ya vitu vilivyobuniwa miaka ya hivi karibuni.

Msamiati huu wa kubuni mara nyingi hubuniwa na kutumiwa na wapiga debe, vijana wa vijiweni na vijana wa mtaani hasa vijana wa kiume wanapokuwa wakipeana taarifa mabalimbali zinazohusu masuala ya ugomvi, masuala yanayohusu pombe, masuala yanayohusu kuwakandia wanawake na masuala yanayohusu uhalifu kama vile wizi, utapeli, uuzaji na utumiaji wa madawa ya kulevya. Aidha, mtafiti alibaini kuwa vijana wengi wanaokaa vijiweni na kushinda mitaani huwa hawajasoma shule kabisa au wana elimu ya shule ya msingi. Ni vijana wachache sana wenye elimu ya sekondari ambao hukaa vijiweni au mitaani wakiwa hawana shughuli maalumu za kufanya zaidi ya kufanya uhalifu na kuvuta madawa ya kulevya.

4.2.3 Msamiati uliofupishwa

Makala hii pia imebaini kuwa baadhi ya msamiati wa lugha ya vijana wa Dar es Salaam una maneno yaliyofupishwa. Msamiati huo huwa unatokana na ufupishaji wa herufi za mwanzo tu za maneno kama mfano wa tisa (3) unavyoonesha.

Msamiati wa Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
3. (a) Ndinga ya **PT**	Gari la **Polisi**
(b) Watoto wa **TMK** siku hizi wanazingua	Watoto wa **Temek**e siku hizi ni wakorofi
(c) Mtoto **CD** yule	Mtoto yule ni **changudoa**

Hali kadhalika, makala hii inaonesha kuwa baadhi ya msamiati wa lugha ya vijana hasa unaohusu majina ya sehemu, huwa umefupishwa ambapo sehemu ya neno huwekwa pamoja bila kujali kama ni sehemu ya mwanzo, katikati au mwisho wa neno. Mifano ifuatayo inaonesha misamiati ilivyo.

Msamiati wa Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
4. (a) Wamesepa **Gomsi** kitambo sana	Wameenda **Gongo la mboto** muda mrefu sana
(b) Twende zetu **Tengua**	Twende zetu **Tengeru**

(c) **Migo** leo hakufai	**Magomeni** leo hakufai

Msamiati uliofupishwa hutumiwa na makundi yote ya vijana. Vilevile imedhihirika kuwa vijana hawa mara nyingi hutumia msamiati huo ili kuokoa muda, kurahisisha mawasiliano au kutaka kuficha siri ya kile wanachokizungumza. Kuijua lugha hii kunawarahisishia watu ambao sio vijana kuelewa ujumbe wa kile kinachozungumzwa na vijana.

4.3 SENTENSI ZA LUGHA YA VIJANA

Faukwa ya hayo, vijana wa Kitanzania wanapokuwa katika mazungumzo yao huwa na aina zao za sentensi ambazo wanazitumia kujieleza. Maelezo yafutayo yanafafanua hilo

4.3.1 Sentensi Fupifupi

Sentensi zinazotumiwa na vijana wakiwa katika mazungumzo yao huwa ni sentensi fupifupi, zenye neno moja moja na zenye maneno yasiyo kamilika. Sifa hizi zinaonekana katika mifano ifuatayo.

Sentensi za Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
5. (a) Dili chenga	Shughuli hazifanyiki
(b) Mshikaji ishu vipi?	Rafiki shughuli vipi?
(c) Sikilizia	Angalia/subiria
(d) Oya kama kawa kama…….	Kama kawaida kama…..
(e) Kama vipi………	Ukiona vipi……….
(f) Kwarua mishe	Iba kitu
(g) Mazee mokona huyo	Rafiki zangu askari huyo
(h) Potezeeni gemu	Acheni kucheza kamali
(i) Mtaryanda anaibuka	Askari anakuja

Kulingana na mifano hii ni dhahiri kuwa mara nyingi sentensi fupifupi hutumiwa sana na vijana wa mtaani kama vile mateja[7] ambao hawana shughuli maalumu ya kufanya zaidi ya kufanya uporaji. Vijana hawa mara nyingi hutumia sentensi fupifupi na kupeana ishara kuhusu jambao wanalotaka kulifanya ili lisieleweke na watu wengine. Kwa mfano, sentensi ya 5(a)"dili chenga", 5(c)"sikilizia", 5(e) "kama vipi….",5 (f)" kwarua mishe" na 5(i) "mtaryanda anaibuka" ni mifano hai ya sentensi fupifupi zinazotumiwa sana na *mateja*. Kwa mtu ambaye sio kijana asiyeshinda mitaani, hawezi kuelewa ujumbe uliobebwa na wazungumzaji hao na matokeo yake watu wengi sana ambao hukatisha mitaa au vichochoro wanakoshinda vijana hao wa mitaani, huwa ni rahisi sana kwa watu hawa kuibiwa simu, pochi, cheni, mikufu, hereni na fedha. Hivyo basi, kuijua lugha ya vijana kutawasaidia watu wengi ambao sio vijana kujua ujumbe uliobebwa katika lugha ya vijana, hivyo kuepuka mikasa mbalimbali inayoweza kutokea.

4.3.2 Uvunjaji wa Kanuni za Sarufi ya Lugha

Makala haya yamebaini kuwa lugha ya vijana hufuata muundo wa lugha ya Kiswahili. Hii ina maana kwamba msemaji wa lugha huwa anafahamu muundo wa lugha ya Kiswahili ili aweze kuwasiliana na vijana wenzake. Pamoja na lugha ya vijana kufuata muundo wa lugha ya Kiswahili, ni dhahiri kuwa vijana wengi wanapokuwa katika mazungumzo yao huvunja kanuni za lugha ya Kiswahili kwa lengo la kufanikisha mawasiliano yao miongoni mwao. Mifano ifuatayo inonesha jinsi lugha ya vijana inavyokiuka kanuni za lugha ya Kiswahili.

Sentensi za Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
6. (a) Manzi **yule** ni pisi kali	Msichana yule ni mzuri

[7] Mateja ni watu wanaotumia madawa za kulevya kama vile kokeini na heloini.

(b) Kitaa **hiki** wanga wengi	Mtaa huu una wambeya wengi
(c) Mwela hasomeki **yule**	Askari yule haeleweki
(d) Msenge **wewe** hausomeki	Wewe hueleweki

Mifano ya 6(a)-(b) inaonesha dhahiri kwamba sentensi hizi zimeanza na Nomino zikifuatiwa na vionyeshi badala ya kuanza na vionyeshi na kufuatiwa na nomino kama kanuni ya lugha ya Kiswahili ilivyo. Vilevile, mfano wa 6(c) unaonesha kwamba Kivumishi kinafuata baada ya Kitenzi badala ya Kivumishi kukitangulia Kitenzi kama mfano wa 6(c) upande wa kulia unavyoonesha. Kwa upande wa mfano wa 6(d), unaonesha dhahiri kuwa kuna Nomino na Kiwakilishi katika sentensi moja jambo ambalo katika lugha ya Kiswahili haiwezekani kukawa na Nomino na Kiwakilishi kwa wakati mmoja.

Kwa mujibu wa maelezo hayo ni wazi kuwa sentensi ambazo huvunja kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu hutumiwa sana na vijana hasa wapiga debe na vijana wa vijiweni na wengi wao wakiwa ni wavulana ambao hawakusoma shule kabisa au ni wale ambao wana elimu ya shule ya msingi. Vilevile ni dhahiri kuwa uvunjaji wa kanuni za lugha ya Kiswahili umejitokeza sana katika Vivumishi, Vionyeshi na katika Viwakilishi ambapo hukaa sehemu isiyotakiwa kuwepo kwa Kivumishi wao huweka Kivumishi na sehemu isiyotakiwa kuwekwa Kiwakilishi wao huweka Kiwakilishi kama mifano ya 6(a)-(d) inavyoonesha.

4.3.3 Ubadilishaji Msimbo wa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza

Vilevile imebainika kuwa vijana wakiwa katika mazungumzo yao hutumia sana sentensi zinazochanganya maneno ya lugha zaidi ya moja. Vijana hawa wakiwa wanazungumza wenyewe kwa wenyewe huchanganya maneno ya lugha tofauti. Grosjean (2010) anasema kwamba utumiaji wa lugha mbili au zaidi hutokana na kukosekana ama kwa istilahi husika katika lugha inayozungumzwa, mada inayozungumziwa au kutaka kuwabagua watu wasiotakiwa kujua kinachozungumzwa na pia kutaka kuonesha usomi wao. Mifano ifuatayo inaonesha na kufafanua jinsi sentensi za Kiswahili za lugha ya vijana zinavyokuwa na uchanganyaji wa maneno ya lugha mbili tofauti.

Sentensi za Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
7. (a) **Today** tutaibuka club	**Leo** tutakwenda kucheza mziki
(b) **Mnyamwezi** katoka blingbling mbaya	**Kijana Mtanashati** kapendeza sana
(c) **Troo Imetaiti** kinoma	**Suruali imebana** sana

Ukichunguza sentensi za 7 (a)-(c) ni sentensi zilizochanganywa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili na mara nyingi sentensi hizi hutumiwa sana na vijana wanafunzi wa sekondari na waliomaliza elimu ya sekondari wanaoshinda mitaani hasa sehemu za vijiweni. Vijana wanaopendelea kuchanganya maneno ya lugha mbili tofauti ni vijana wote wa kike na wa kiume waliosoma sekondari na elimu ya chuo kikuu au chuo cha kati na huwa na lengo la kutaka watambulike kuwa ni wasomi au hutaka watambuliwe kuwa ni vijana wa kisasa wanaokwenda na wakati.

4.3.4 Maneno ya Mshangao

Lugha ya vijana ina sentensi ambazo zina maneno ya mshangao. Maneno haya ya mshangao huonesha kushtushwa kwa jambo, kufurahishwa kwa jambo au kuchukizwa na kusikitishwa kwa jambo fulani lililotokea. Mifano ifuatayo inafafanua zaidi.

Sentensi za Lugha ya Vijana	Kiswahili Sanifu
8. (a) **Joh!** Yule mtoto namkubali mbafaya	Aah! Yule msichana nampenda sana
(b) **Eeh bhana!** Jana nimemzama yule demu	Aah! Jana nimefanya mapenzi na Yule msichana

(c) **Aisee**! Miyeyusho wewe	Aah! Wewe hueleweki
(d) **Duh!** Demu wako miyayusho kabisa	Loo! Mpenzi wako haeleweki kabisa

Sentensi hizi hutumiwa sana na vijana wa vijiweni wakiwa katika vijiwe vyao huku wakisimuliana na kupashana habari za mambo mbalimbali yanayohusu mapenzi au kukandiana kwa mambo wanayoona hayafai kama mfano wa 8(a)-(d) unavyoonesha.

4.0 HITIMISHO

Katika makala haya tumejadili kuhusu ubunifu wa vijana wa Kitanzania wanavyotumia lugha ya Kiswahili katika kubainisha utambulisho wao. Imebainika kwamba vijana wa Kitanzania wanavyotumia Kiswahili, huwa na namna yao ya kuwasiliana ambayo inawatofautisha na wazungumzaji wengine wa Kiswahili. Kwa ujumla, imedhihirika kuwa lugha ya vijana ina matamshi yake, msamiati wake na sentensi zake ambazo hutumiwa na vijana wakiwa katika mazungumzo yao. Pamoja na vijana kuwa na matamshi yao, msamiati wao na sentensi zao, imedhihirika kuwa matamshi hayo, msamiati huo na sentensi hizo hufuata taratibu na kanuni za lugha ya Kiswahili ingawa kumejitokeza sentensi chache za lugha ya vijana ambazo zinakiuka utaratibu na kanuni za lugha ya Kiswahili. Kwa kuwa katika taaluma ya Isimujamii suala la lugha ya vijana halijashughulikiwa vya kutosha, utafiti huu unapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike kuchunguza athari ya lugha ya vijana wa Kitanzania katika Kiswahili sanifu na namna ambavyo lugha hii inaweza kuchangia katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

MAREJELEO

Amri, J.H. (2011). *Matumizi ya Majina katika Utambulisho wa Jamii ya Watanzania*. M.A (Kiswahili), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Bryman, A. (2004) *Social Research Methods*. New York: Oxford University Press.

Coulmas, F. (2005) *Sociolinguistics: The Study of Speakers' Choice*. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D. and Davy, D. (1969) *Investigating English Style*. London: Longman.

Ferrari, A. (2014). Evolution Of Sheng during the Last Decade. *Les Cahiers d'Afrique de l'Est/The East African Review*, (49), 29-54.

Grosjean, F. (2010). *Bilingual: Life and Reality*. Cabridge: Mass Harvard University Press.

Gumperz, J. J. (1972). "Introduction." Katika J.J. Gumperz and D. Hymes (Wah.) *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. New York: Holt, Rinchart and Winston, Inc.

Hogg, M. A. (2016). Social identity theory. In S. McKeown, R. Haji, & N. Ferguson (Eds.), *Understanding Peace and Conflict through Social Identity Theory: Contemporary global perspectives*. https://doi.org/10.1007/978-3-319-29869-6_1.

Hurst-Harosh, E. (2009). *Tsotsitaal, Global Culture and Local Style: Identity and Recontextualisation in Twenty-First Century South African Townships*. Berlin, De Gruyter Mouton.

Hurst-Harosh, E. (2020). *Youth Language in Africa: Introduction to the Special Issue*. Berlin: De Gruyter Mouton.

Hust-Harosh, E & Erastus, F. K (2018). *African Youth Languages: New Media, Performing Arts and Sociolinguistic Development*. Cham. Switzerland Palgrave Macmillan

Kießling, R., & Mous, M. (2004). Urban youth languages in Africa. In *Africa Spectrum*. 45, 11-41.

King'ei, K. G., & Kobia, J. (2007). Lugha Kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini Kenya, katika *Nordic Journal of African Studies*. 16(3): 320–332.

Kombo, D. K., & D. L. Tromp (2006*). Proposal and Thesis Writing: An Introduction***.** Nairobi: Paulines Publications Africa.

Labov, W. (1972). *Language in the Inner City*. Philadelphia: Pennsylvania University Press.

Mekacha, R.D.K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mlowezi, D. (2012). *Lugha ya Vijana wa Dar es Salaam na Utambulisho Wao: Mifano Kutoka katika Kiswahili*. Tasnifu ya M.A (Kiswahili), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Msanjila, Y.P, Khore, Y.M & Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Price, P.L. (2010) *A Sociolinguistic Study of Language Use and Identity Amongst Galician*. Master Dissertation. The University of Birmingham.

Reuster-Jahn, U., & Kießling, R. (2006) "Lugha ya Mitaani in Tanzania: The Poetics and Sociology of a Young Urban Style of Speaking With a Dictionary Comprising 1100 Words and Phrases". In *Swahili Forum*, 13, 1-196.

Samper, D. A. (2002). Talking *Sheng: The Role of a Hybrid Language in the Construction of Identity and Youth Culture in Nairobi, Kenya*. Doctoral Dissertation, University of Pennsylvania.

Tabouret-Keller, A. (1989). *Seminar dánthropologie du language*. MSH Informations. Bulletin de la Fondation des sciences de l'Homme. 59,15–17.

————(1997). Language and Identity, In F. Coulmas (ed.). *The Handbook of Sociolinguistics*. UK: Blackwell Publishers.

Tajfel, H., & J. Turner (1979). "The An Integrative Theory of Intergroup Conflict". In S. Worchel & W. Austin (Ed*), Psychology of Intergroup Relations*, 33–47.

Turner, J. (1987). "The social Identity Theory of Intergroup Behavior". In S. Worchel and W. Austin (Ed), *Psychology of Intergroup Relations*, 7–24.

Wardhaugh, R. (1986). *An Introduction to Sociolinguistics*. New York, USA: Blackwell.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Mbinu Wanazotumia Rafiki wa Lugha katika Ukuzaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wajifunzaji wa Kiswahili Ikiwa ni Lugha ya Kigeni

Elivira Jovinus
eliviraj12@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Perida Mgecha
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
peridamgecha@gmail.com

IKISIRI
Makala hii inachunguza mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika ukuzaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Malengo yakiwa ni kubainisha mbinu zinazotumiwa na rafiki wa lugha katika ukuzaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, na kueleza umuhimu wa mbinu hizo. Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kwa njia ya usaili na hojaji kutoka kwa marafiki wa lugha. Mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Mwingiliano Jamii. Matokeo ya utafiti yamebainisha mbinu tano zitumiwazo na marafiki wa lugha katika ukuzaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni ambazo ni ziara, majadiliano, maswali na majibu, michezo ya lugha na nyimbo. Pia matokeo yanaonesha kuwa wanafunzi wa Lugha ya Kigeni watamudu stadi ya mazungumzo ikiwa marafiki wa lugha watatumia mbinu zinazostahili kwa kila kiwango cha wajifunzaji. Hivyo, ni muhimu sana taasisi husika kuwa na programu ya mafunzo kwa rafiki wa lugha ambayo itawasaidia kuifanya kazi hiyo kwa weledi. Pia tafiti mbalimbali zifanyike zinazohusu ubunifu wa mbinu bora zinazokwenda na wakati huu wa sayansi na teknolojia ambazo rafiki wa lugha anaweza kuzitumia katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Lugha ya Kigeni.

MANENO YA MSINGI :
Mbinu, Stadi ya mazungumzo, Rafiki wa lugha, Lugha ya Kigeni

1.0 UTANGULIZI

Kwa kiasi kikubwa lugha zote ulimwenguni huwa na stadi maalumu ambazo ni kipimo cha ujuzi wa lugha husika. Stadi za lugha ni ujuzi anaoweza kuwa nao mzungumzaji kwa kuegemea sheria, kanuni na taratibu za lugha husika. Kiswahili kama moja ya lugha kutoka kwenye bohari ya lugha nyingi ina stadi ambazo ikiwa mzungumzaji atazifahamu vyema basi anaweza kuchukuliwa kama mtu anayekifahamu Kiswahili bila kujali ni mzawa ama si mzawa. Stadi hizi zinapaswa kueleweka kwa mzungumzaji (hasa kwa wageni) ili kuepuka makosa ambayo yanaweza kuwa kizuizi cha kufikisha ujumbe uliokusudiwa na mzungumzaji. Ufundishaji wa lugha umejikita katika stadi nne za lugha yaani kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika. Dirga na Wijyat (2018) wanasema stadi za lugha (kusikia, kuzungumza, kusoma na kuandika) ni msingi mkuu katika ufundishaji lugha yoyote ya kigeni. Makala hii imejikita zaidi katika kuchunguza ukuzaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Mawasiliano kwa njia ya lugha mara nyingi ndio humfanya mtu asikilize na au azungumze. Watu wanatumia sana stadi za mazungumzo na kusikiliza katika shughuli zao za kila siku. O'hara (2004) anafafanua kuwa wanafunzi wanapokuzwa katika stadi ya

mazungumzo wanajenga kujiamini wakati wa kuzungumza. Kwa kuzungumza, wanafunzi wanaweza kuuliza maswali, kujieleza na kujenga uzoefu juu ya mambo wanayofundishwa. Vilevile wanafunzi hao hukuza ufahamu wao katika mambo mbalimbali na pia huweza kutoa hisia na mawazo yao kutokana na ujuzi walio nao. Bruce (2005) anaongezea kuwa mazungumzo huwafanya watu kufikiri na kuhisi mambo ya kidhahania na kuwafanya wanafunzi waweze kubuni mazungumzo zaidi, yaani kuwa na umilisi mzuri wa lugha.

Maandiko mbalimbali yanaonesha kwamba uteuzi wa mbinu za kufundishia ni kipengele muhimu katika kufundisha na kujifunza taaluma mbalimbali, baadhi ya wataalamu hao ni Long (1996), Richards na Rodgers (2001), Ndunguru (2004), Brown (2007), na Yulisa (2018). Uteuzi mzuri wa mbinu hurahisisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa katika kujifunza na kufundisha juu ya fani husika. Aidha, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zisipoandaliwa na kutumiwa vizuri hukwamisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ndunguru (2004) amefafanua kwamba umahiri wa mwalimu katika uteuzi wa mbinu za kufundishia ni muhimu. Umahiri huo unahitajika ili umwezeshe mwalimu kuchagua mbinu itakayomrahisishia kufikia malengo ya ufundishaji aliyoyakusudia. Hata hivyo, Long (1996) anafafanua mambo ya ziada ya kuzingatiwa katika uteuzi mzuri wa mbinu za kufundishia ambayo ni kuangalia aina ya mada, aina ya wanafunzi, mazingira ya kujifunzia na kufundishia, viwango vya ujifunzaji kwa wanafunzi husika na kadhalika. Kumekuwa na mwamko mkubwa wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama Lugha ya Kigeni, ambapo baadhi ya mbinu zinazotumika kufundishia na kujifunzia ndizo hizo hizo zimekuwa zikitumiwa na rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya kuzungumza kwa wajifunzaji wa Lugha ya Kigeni.

Makala hii inachunguza mbinu wanazotumia marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Rafiki wa lugha ni mbinu mojawapo inayotumika katika kufundishia Lugha ya Kigeni. Kwa hapa Tanzania, mbinu ya rafiki wa lugha ilianza kutumika Zanzibar kwa kufundishia Kiswahili kwa Wageni mwaka 2010 chini ya usimamizi wa Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni (TAKILUKI) kwa kushirikiana na American Council for International Education. Programu hiyo ilihusisha taasisi ya Swahili Flagship, the African Flagship Languages Initiative (AFLI) na Boren Fellowship Boston kutoka nchi ya Marekani. Hivi sasa mbinu hii inatumika kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwa wanafunzi wa kigeni katika taasisi mbalimbali hapa Tanzania. Rafiki wa lugha ni mbinu ambayo ndani yake ina mbinu zinazomsaidia mjifunzaji kumudu stadi nne za lugha. Hata hivyo, makala hii imejikita katika stadi ya kuzungumza.

1.1 RAFIKI WA LUGHA

Rafiki wa lugha ni rafiki mzawa ambaye ni mwenyeji wa pahala fulani kwa asili. Makala hii imetumia neno *marafiki wazawa* kama marafiki wa lugha ambao ni wenyeji. Neno "Mzawa" lilitumika kwa maana ya mwenyeji wa pahala fulani kwa asili (BAKIZA, 2010). Huu ni mfungamano wa kirafiki baina ya watu wawili (mzawa na mwanafunzi wa kigeni) wanaofungamana katika ujifunzaji wa Kiswahili. Mahusiano hayo hujikita katika kuwasaidia wanafunzi wa kigeni kukamilisha malengo yao.

Katika mazingira ya kawaida mzawa hufahamika kama ni mwenyeji wa kuzaliwa na kukulia katika eneo husika. Hivyo, mzawa wa lugha ya Kiswahili hutarajiwa kuwa ni mweledi wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Katika makala hii rafiki wa lugha imetumika kama mbinu ya ufundishaji kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Rafiki wa lugha anatakiwa kuifahamu lugha husika kwa ufasaha, awe amepata mafunzo yanayohusu programu ya rafiki wa lugha, awe mzawa wa lugha hiyo.

Aidha Nushi na Jenabzadeh (2016) wanasema kwamba marafiki wa lugha wana mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa lugha husika. Mbinu ya rafiki wa lugha huwafanya watu kuwa pamoja kama jamii moja.

Aidha wanaendelea kusema kuwa uchangamfu wa rafiki wa lugha humuondolea mjifunzaji hofu ya kuogopa kukosea katika uzungumzaji na kuendelea kujifunza. Vilevile wanasema lengo kuu la kuwa na rafiki wa lugha ni kumuongezea mjifunzaji ujuzi wa kuzungumza na msamiati. Pia wanaendelea kusema kwamba marafiki wa lugha sio walimu bali wanawasaidia wajifunzaji kuendeleza kile walichonacho kichwani na walichofundishwa na walimu wao.

Timmis (2002) ameweka wazi kuwa mbinu ya matumizi ya rafiki wa lugha ni muhimu kwa wajifunzaji wa Lugha ya Kigeni hasa katika kupata stadi ya mazungumzo kwani mjifunzaji anaona kuwa itakuwa ni vizuri kuzungumza Lugha ya Kigeni pasipo kujulikana kama yeye ni mjifunzaji. Aidha Timmis (2002) anaendelea kusema kuwa, wajifunzaji wa lugha ya Kiingereza wengi wanapenda kuishi kama wazawa hivyo wanapenda kutumia rafiki wa lugha ili kufahamu Kiingereza kwa ufasaha.

Fauzani (2016) alichunguza ujifunzaji wa stadi ya mazungumzo kupitia rafiki wa lugha. Utafiti huo uliwashirikisha wajifunzaji wa shahada ya sayansi ya lugha wa Chuo Kikuu cha Indonesia. Mbinu za aina mbili zilitumiwa na walimu kufundisha stadi hiyo ya lugha kwa wajifunzaji. Mbinu hizo ni mbinu ya kutumia rafiki wa lugha na mbinu ya mijadala darasani. Matokeo yanaonesha kwamba mbinu ya kutumia rafiki wa lugha ilileta ufanisi mkubwa kwa ujifunzaji na ufundishaji wa Lugha ya Kigeni. Wajifunzaji walipata usaidizi mkubwa kutoka kwa rafiki wa lugha katika kujifunza kwao Kiingereza na hatimaye kuimarika uwezo wao wa stadi ya kuzungumza. Utafiti wa Fauzani umekuwa na mchango mkubwa kwa sababu makala hii imeshughulikia mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Kadhalika Jabur (2016) amefanya utafiti kuhusu mbinu ya kutumia rafiki wa lugha katika kujifunza Kiingereza. Washiriki wa utafiti huu walikuwa wanafunzi kutoka Mashariki ya Kati wanaojifunza shahada ya kwanza ya sayansi ya Kiingereza Chuo Kikuu cha Pennsylvania nchini Marekani. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kwamba wanafunzi wa kigeni kutoka Mashariki ya Kati walifaulu sana na kuimarika uwezo wao katika stadi ya kuandika kwa kutumia Kiingereza. Ufanisi huo umetokana na usaidizi mkubwa walioupata kutoka kwa marafiki wazawa wa lugha ya Kiingereza wakati wa kujifunza.

Vilevile Baratayaomi na wenzake (2018) wamefanya utafiti kuhusu mbinu ya kutumia rafiki wa lugha katika kujifunza stadi ya kusoma. Watafitiwa wa utafiti huo walikuwa wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Sultan Ageng Turtayasa nchini Indonesia. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba wanafunzi wamefaulu zaidi ya asilimia 67 katika kujifunza stadi ya kusoma. Ufanisi huo uliimarisha ufasaha wa usomaji matini mbalimbali za Kiingereza ambayo ni Lugha ya Kigeni kwao. Makala hii imejikita katika kuchunguza mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Ikilenga hasa kubaini mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni na kueleza faida za mbinu hizo.

2.0 MBINU ZA UTAFITI

Usanifu kifani ni aina ya usanifu ambao uliwezesha utafiti huu kuteua mahali ambapo taarifa zilikusanywa. Makala hii ilitumia vyuo vitatu katika kukusanya data ambavyo ni Alliance Française Arusha, MS Training Center for Development Cooperation (MS TCDC), na Morden Linguistics African Culture (MOLAC). Pia makala hii ilitumia mkabala wa kitaamuli ambapo data ziliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa mbinu ya kusimbisha maudhui. Katika kupata sampuli, usampulishaji lengwa ulitumika. Sampuli ilikuwa ni marafiki wa lugha wanaowasaidia wajifunzaji kukuza stadi ya mazungumzo katika ujifunzaji wa Kiswahili ikiwa Lugha ya Kigeni. Katika ukusanyaji wa data za makala hii, mbinu ya usaili na hojaji zilitumika; Usaili na hojaji zilitumika ili kubaini mbinu wanazozitumia katika kuwasaidia wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni katika kumudu stadi ya

mazungumzo; pia katika kupata ufafanuzi wa umuhimu wa kila mbinu. Watoa taarifa ambao ni rafiki wa lugha walikuwa 5 kila taasisi, jumla ikiwa 15.

Katika ukusanyaji wa taarifa kinasa sauti, simu ya mkononi, kalamu, kompyuta na kinyonyi vilitumika kutunza kumbukumbu. Uchanganuzi ulifanyika kwa kunukuu taarifa zilizorekodiwa katika kinasa sauti baada ya usaili. Pia, baadhi ya taarifa zilizotoka katika dodoso ziliwekwa katika majedwali maalumu. Mbinu ya kusimba maudhui ilitumika katika uchanganuzi wa data. Aidha katika kutumia mbinu hii ya kusimba maudhui, data zilizopatikana kutoka uwandani zilipangwa katika makundi tofauti tofauti kulingana na malengo ya makala. Ikiwa na maana kwamba data zinazoelekeana kimaudhui ziliwekwa katika kundi moja na kutolewa ufafanuzi.

4.0 MATOKEO YA UTAFITI

Katika sehemu hii matokeo yamewasilishwa yakibainisha mbinu husika pamoja na umuhimu wake. Uwasilishaji wa data kuhusu mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni umeoneshwa kwa muhtasari katika jedwali namba 1 ambalo linaonesha usaili uliofanyika kwa marafiki wa lugha.

Jedwali Na 1: Mbinu Wanazotumia Marafiki wa Lugha katika Kukuza Stadi ya Mazungumzo

Na	Mbinu	Idadi ya Marafiki wa Lugha	Asilimia
1	Ziara	15	100
2	Majadiliano	14	93
3	Maswali na majibu	12	80
4	Michezo ya lugha	10	67
5	Nyimbo	8	53

Data zinaonesha kuwa idadi kubwa ya marafiki wa lugha inatumia mbinu ya ziara, mbinu ya majadiliano na mbinu ya maswali na majibu kwa sababu zinaonekana zinamsaidia mjifunzaji kumudu stadi ya mazungumzo kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko mbinu ya michezo ya lugha na nyimbo. Ufuatao ni uwasilishaji na ufafanuzi wa mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

4.1 MBINU YA ZIARA

Mbinu ya ziara ni mbinu mojawapo inayotumiwa na marafiki wa lugha katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Jumla ya watoa taarifa 15 sawa na asilimia100 walitumia mbinu ya ziara katika kuwasaidia wajifunzaji wa kigeni wa lugha ya Kiswahili. Marafiki wa lugha huandaa ziara mbalimbali za kimasomo na kuambatana na wajifunzaji wa kigeni kwa lengo la kujifunza lugha. Baadhi ya ziara hizo ni: ziara za maeneo ya kihistoria, kiutamaduni, kiuchumi na maeneo ya kijamii. Data zinaonesha kuwa mbinu ya ziara humwezesha mjifunzaji kujifunza mambo kadhaa katika uhalisia wake na kukuza stadi ya mazungumzo. Wanafunzi hupata nafasi ya kuona, kushika, kusikia, kuonja na kutamka maneno mbalimbali ya lugha husika. Hali hiyo humjengea kumbukumbu ya muda mrefu.

Data za utafiti zinaonesha kwamba wajifunzaji wanafurahia sana mbinu hii ya ziara kwa sababu wanapendelea zaidi kutembelea maeneo mbalimbali yanayowazunguka. Baadhi ya maeneo hayo ni sokoni, mahakamani, hospitalini na majengo ya ukumbusho. Kupitia mbinu hii wajifunzaji wanapata nafasi kubwa ya kujifunza msamiati mbalimbali wa Kiswahili kulingana na muktadha husika kama mtoa taarifa mmoja anavyoeleza: "Nilikuwa ninatembea sehemu mbalimbali na wajifunzaji kwa lengo la kujifunza; tulitembelea maeneo ya sokoni, hospitalini, mahakamani, shambani na maeneo ya kihistoria...."

Vilevile data inaeleza kuwa wajifunzaji walijifunza msamiati mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali la 2.

Jedwali Na. 2: Msamiati Mpya Waliojifunza Wanafunzi wa Kigeni Kutokana na Mbinu ya Ziara

Na	Muktadha	Msamiati Mpya Waliojifunza Wanafunzi
1	Sokoni	Machungwa, maembe, ghali, bei, rahisi, fungu, nafuu
2	Hospitalini	Kulazwa, homa, kifo, kuzimia, pole, moja mara tatu, kichefuchefu
3	Maeneo ya Kihistoria	Pango, watumwa, wafalme, mabaki, gofu na uvamizi

Pia, watoa taarifa walieleza kwamba mbinu ya ziara isipoandaliwa na kutumika vizuri inaweza kukwamisha malengo yaliyokusudiwa katika kujifunza lugha hasa katika ujifunzaji wa stadi ya mazungumzo. Hivyo, kukosekana kwa maandalizi mazuri katika mbinu hii kunaweza kusababisha kutokufikiwa kabisa kwa malengo ya ukuzaji wa stadi ya mazungumzo.

4.2 MBINU YA MAJADILIANO

Mbinu ya majadiliano ni mbinu mojawapo inayotumiwa na rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Jumla ya watoa taarifa 14 ambao ni sawa na asilimia 93 walithibitisha hili. Marafiki wa lugha huandaa mada mbalimbali zinazoendana na wajifunzaji wao kwa ajili ya majadiliano. Na majadiliano hayo yanakuwa miongoni mwa wajifunzaji wenyewe na rafiki wa lugha anakuwa mwezeshaji tu. Watoa taarifa walieleza zaidi kuwa majadiliano yanamsaidia mjifunzaji kupata msamiati mpya, sarufi na matamshi. Mbinu hii inafaa katika kuwajengea stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, kama ilivyoelezwa na mtoa taarifa mmoja kama ifuatayo:

> *"........kabla ya kukutana na mwanafunzi mimi au yeye tunaandaa mada ya kujadili, ambapo mimi ninakuwa ninachochea maswali ambayo ni yakumfikirisha ili awe kitovu cha mazungumzo kuliko mimi, kwa hiyo natoa hoja anaielezea na anapokwama anasaidiwa kidogo ili aweze kuendelea na mazungumzo......"*

Pia mtoa taarifa mwingine katika kuonesha matumizi ya mbinu hii katika kujenga stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni, alieleza hivi: "....Ninaandaa mada ya kujadiliana na mwanafunzi ambayo inahusu mambo yanayomzunguka mfano kuhusu familia yake. Hii inasaidia wajifunzaji kumakinika na msamiati unaotumika katika mada husika ...."

Kwa upande mwingine watoa taarifa walifafanua kuwa mbinu ya majadiliano humwezesha rafiki wa lugha na mjifunzaji kuwasiliana kwa urahisi. Rafiki wa lugha hufanya kazi ya kuongoza majadiliano ili hali mwanafunzi ndiye mzungumzaji mkuu. Kwa njia hii, wanafunzi hupata nafasi ya kujadili mada waliyonayo na wanapofikia muafaka, kila mmoja

anatarajiwa kuwa amepata maana ya nyongeza kutoka ile aliyokuwa nayo awali kuhusu mada husika. Hapo mwanafunzi anakuwa amejifunza jambo la ziada na kukuza stadi yake ya mazungumzo. Mmoja wa watoa taarifa alifafanua: "Mbinu hii husaidia kukuza uhusiano kati ya wahusika kwa kuendeleza mazungumzo, kukuza stadi ya mawasiliano kwa njia ya mazungumzo. Majadiliano humwezesha rafiki wa lugha kuelewa kiwango cha msamiati wa wanafunzi wake na uwezo wa kuzungumza."

Pia, mtoa taarifa mwingine alisema: "Kabla ya kukutana na mwanafunzi naandaa zana mbalimbali (kama vile vitu halisi, picha) ambavyo vitawasaidia wanafunzi kuongea na kujadili hoja mbalimbali kutokana na vitu hivyo."

Aidha, baadhi ya data za watoa taarifa zimebainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili katika matumizi ya mbinu hii. Changamoto hizo ni baadhi ya wanafunzi wa kigeni kutokutoa ushirikiano mzuri kwa rafiki wa lugha katika kuimarisha mazungumzo baina yao juu ya mada husika. Hivyo, kupelekea ushiriki mdogo usio na ufanisi. Utafiti umebaini kwamba baadhi ya changamoto hizo husababishwa na marafiki wa lugha kwa kushindwa kwao kuchagua mada rahisi na zenye mvuto zitakazowashawishi wanafunzi wa kigeni kushiriki ipasavyo katika mazungumzo juu ya mada husika. Mbinu ya majadiliano huonesha wazi matokeo ya stadi ya kuzungumza kwa mjifunzaji kulingana na namna wanavyojadiliana.

4.3 MBINU YA MASWALI NA MAJIBU

Mbinu nyingine iliyobainishwa katika kukuza stadi ya mazungumzo ni maswali na majibu. Jumla ya watoa taarifa 12 ambao ni asilimia 80 waliitaja mbinu hii kuwa wanaitumia katika kukuza stadi ya mazungumzo. Mbinu hii humrahisishia mjifunzaji kuweza kufikia stadi hiyo kwani mjifunzaji huweza kupata msamiati na mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha kwa sababu maswali hayo yanakuwa kwenye mfumo wa mahojiano ambayo yatamfanya mjifunzaji kuweza kuzungumza na hii hupelekea stadi ya mazungumzo kufikiwa kirahisi. Watoa taarifa walifafanua zaidi kuwa mbinu hii inamjengea mwanafunzi uwezo zaidi wa kuzungumza na kumwongezea kiwango cha kujiamini na kufikiri; lakini pia kuweza kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu utamaduni wa jamii husika. Watoa taarifa walieleza kuwa mbinu hii wakati mwingine huweza kutumika kuibua mijadala mizuri kutegemeana na kiwango cha mjifunzaji. Wakati wa usaili, mtoa taarifa mmoja alisema: "… ninapokutana na mjifunzaji wangu mara ya kwanza kuna baadhi ya maswali huwa namuuliza mfano, unaitwa nani? Unatoka nchi na jimbo gani? Sasa unakaa wapi na unafanya nini? Hii inamwongezea mwanafunzi uwezo wa kuzungumza …"

Kwa upande mwingine watoa taarifa walieleza kuwa, wakitumia mbinu hii, wajifunzaji wanamudu kujieleza vyema kwa mazungumzo kuliko kwa maandishi. Data hizi pia zilionesha kuwa, wanafunzi wengi humudu kujieleza kwa mazungumzo ikiwa rafiki wa lugha atawauliza wajifunzaji maswali kutokana na picha pamoja na vitu halisi. Mmoja wa watoa taarifa alinukuliwa kwa kusema: "Mjifunzaji wangu alipenda sana kuangalia picha wakati wa mazungumzo, hivyo nilitumia picha hizo kumuuliza maswali mbalimbali…"

Watoa taarifa walieleza kuwa mbinu hii huwapa wanafunzi fursa ya kukuza uwezo wao wakujieleza kwa mazungumzo.

4.4 MBINU YA MICHEZO YA LUGHA

Kati ya mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kujenga stadi ya mazungumzo ni pamoja na michezo ya lugha. Watoa taarifa walieleza kwamba marafiki wa lugha huandaa michezo mbalimbali ambayo itawasaidia wajifunzaji kuweza kujifunza stadi ya mazungumzo pamoja na kupata msamiati mbalimbali na matamshi. Walieleza kwamba ipo michezo tofauti tofauti inayompa mjifunzaji hamu na sababu ya kuzungumza. Mfano, mchezo wa karata, kufananisha picha na msamiati, kubadilishana viti na kurushiana mpira. Mtoa taarifa

mmoja alisema: "Mjifunzaji wangu alikuwa anapenda sana kucheza karata. Kuna baadhi ya maneno ambayo yalikuwa yanachochea mazungumzo kuendelea, mfano neno lamba ni neno ambalo lilikuwa na utata….."

Kwa upande mwingine watoa taarifa walielezea kuwa michezo mbalimbali ya lugha inamsaidia mjifunzaji kupata msamiati tofautitofauti. Pia walielezea kuwa ipo michezo mbalimbali ambayo inamsaidia mjifunzaji kuwa na msamiati wa kutosha mfano mchezo wa kurushiana mpira, mtoa taarifa mmoja alisema: "Wakati nilipokuwa na cheza mchezo wa kurushiana mpira na rafiki yangu nilimuuliza maswali ambayo yalimtaka yeye kutaja jibu na kurudisha mpira kwa kuuliza swali. Hii ilimsaidia kupata msamiati tofauti tofauti na kujifunza matamshi…"

Kutokana na nukuu hizi tunaweza kusema kwamba mbinu ya michezo ya lugha inawasaidia wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kupata maneno mapya, na kujifunza matamshi ya maneno hayo.

4.5 MBINU YA NYIMBO

Nyimbo ni mbinu mojawapo wanayotumia marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Watoa taarifa 8 ambao ni asilimia 53 walieleza kuwa kuna umuhimu wa kuwa na nyimbo zinazowasaidia wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Nyimbo hizo zinaweza kuwa zile anazozifahamu rafiki wa lugha au zilizorekodiwa na kuhifadhiwa kwa njia mbalimbali kama vile kinyonyi, kompyuta na simu. Watoa taarifa hawa walieleza kwamba nyimbo hizo zinakuwa zinaendana na malengo ya wajifunzaji; nyimbo zinamsaidia mjifunzaji kupata matamshi kwa kuimba pamoja na rafiki wa lugha. Hapa rafiki wa lugha anahitaji kupitia nyimbo kabla ya kukutana na mjifunzaji wake ili kuhakikisha nyimbo zinakuwa na matamshi na maneno rahisi yanayosikika kwa mjifunzaji. Mtoa taarifa mmoja alisisitiza kuwa: "….nasikiliza nyimbo kabla ya kukutana na mjifunzaji wangu, naangalia nyimbo hizo kama zitampatia matamshi kupitia maneno mbalimbali katika nyimbo, …"

Vilevile mtoa taarifa mwingine alinukuliwa akisema: "Mjifunzaji anapata wakati mzuri wa kuburudika huku akijifunza matamshi kutokana na nyimbo mbalimbali alizozisikiliza na hii humsaidia kumudu stadi ya mazungumzo kwa sababu wakati mwingine anaweza kuzungumza kile alichokisikiliza…."

Watoa taarifa walieleza kuwa, mbinu hii ikitumika katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, wajifunzaji huweza kujifunza maneno mapya na hatimaye huyatumia katika maisha yao ya kila siku. Pia wanaeleza kuwa baadhi ya wajifunzaji wanapoanza mazungumzo au kama ni wa hatua ya kwanza, wanakuwa hawajaweza kuzungumza vizuri na kutamka baadhi ya maneno. Wakati wa usaili, mtoa taarifa mmoja alisema: "Baadhi ya wajifunzaji tunapokutana nao huwa hawawezi kuzungumza vizuri, tunapokaa nao kwa muda fulani tunawafundisha nyimbo za kuvutia na wanaziimba, basi wajifunzaji hawa wanaweza kuzungumza."

Vile vile mtoa taarifa mwingine alipoulizwa kuhusu mbinu anazotumia katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wake wa Kiswahili alisema hivi: "Kupitia nyimbo tunazoimba wajifunzaji wetu huweza kuzungumza kwa wepesi zaidi na kusitasita kunapungua"

Kutokana na data za watoa taarifa, inaonesha kuwa nyimbo ni mbinu muhimu inayotumiwa na marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

5.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Makala hii imebaini kuwa marafiki wa lugha hutumia mbinu anuai katika kujenga stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni na kila mbinu ina

umuhimu wake kama ilivyojidhihirisha katika matokeo. Haya yote yinajadiliwa kama ifuatavyo;

5.1 MBINU YA ZIARA

Mbinu ya ziara ni mbinu ambayo inatumiwa na marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Matokeo yanaonesha kuwa mbinu ya ziara inawasaidia wajifunzaji kumudu stadi ya mazungumzo kutokana na msamiati wanaoupata kutoka katika miktadha mbalimbali. Katika kushadidia hili, TIE (2003) wanaeleza kuwa, mbinu ya ziara huwawezesha wanafunzi kutembelea mahali na kufanya uchunguzi kwa wakati mmoja. Njia hii huwasaidia wanafunzi kuwa wadadisi, kwani wanapokwenda kwenye ziara huona na kuchunguza vitu vya aina mbalimbali. Wanafunzi huuliza maswali na pia hujadiliana juu ya mambo wanayoyaona. Hivyo basi, wanafunzi hawa hujifunza maneno mapya ambayo baadaye huyatumia katika maisha yao ya kila siku.

Kutokana na matokeo ya utafiti, mbinu ya ziara inawasaidia sana wajifunzaji kupata maneno mapya, maneno hayo mengine ni rasmi na mengine si rasmi kwasababu ya kutembelea mazingira tofautitofauti kama maeneo ya kihistoria, kiutamaduni, kiuchumi na maeneo ya kijamii. Mbinu ya ziara huongeza msamiati kwa wajifunzaji. Vygosky (1978) katika nadharia ya Mwingiliano Jamii amefafanua kiwango cha uelewa cha mjifunzaji katika kujifunza kwake. Mbinu ya ziara ni mbinu ambayo inamsaidia mjifunzaji wa kiwango cha awali, kati na cha juu kuyatalii maeneo mbalimbali ambapo kwa kufanya hivyo mjifunzaji anaweza kuwa na upeo mkubwa wa kumudu stadi ya mazungumzo kwasababu kupitia maeneo hayo anapata msamiati tofautitofauti.

Hivyo, mbinu ya ziara ni mbinu muhimu katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji kwa kuwa inahusisha vitendo na vitu halisi; pia mbinu hii ni nzuri kwasababu inatumika kwa wajifunzaji wenye kiwango cha awali, kati na juu.

5.2 MBINU YA MAJADILIANO

Mbinu ya majadiliano ni mbinu wanayoitumia marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Marafiki wa lugha huwaandalia wanafunzi wa kigeni aina mbalimbali za mada na kuanzisha mazungumzo baina yao kwa lengo la kujifunza. Mada hizo hujikita kuzungumzia mambo mbalimbali, kama vile mambo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. Wanafunzi wa kigeni hupata mazoezi makubwa katika kujifunza lugha ya Kiswahili hususani stadi ya kuzungumza na kusikiliza kwa pamoja chini ya usimamizi wa marafiki wa lugha. Mbinu hii inawasaidia wajifunzaji katika kumudu stadi ya mazungumzo kwasababu inawasaidia kupata msamiati mpya, namna ya kutamka na inakuza uwezo wao wa lugha. Wataalamu wengi kama vile Baker na Westrup (2003), Klancar (2006) na Kayi (2006) katika kushadidia hili wamependekeza njia ya majadiliano itumike katika ufundishaji wa wanafunzi stadi ya mazungumzo ili waweze kukuza uwezo wao wa lugha. Hivyo, marafiki wa lugha pia hutumia mbinu hii katika kukuza stadi ya mazungumzo. Vygosky (1978) katika nadharia yake ya Mwingiliano Jamii amefafanua kiwango cha uelewa cha mjifunzaji kuwa mbinu ya majadiliano ni mbinu ambayo inatumika kwa wajifunzaji ambao viwango vyao ni vya kati na juu kwasababu mjifunzaji anakuwa ameshamudu baadhi ya msamiati.

Mbinu ya majadiliano ni mbinu muhimu ambayo inawasaidia wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kwa kuwapatia msamiati mpya na kujifunza jinsi ya kutamka baadhi ya maneno na kukuza uwezo wao wa lugha. Mbali na hayo mbinu hii ina changamoto kwa wajifunzaji kwasababu baadhi ya wajifunzaji hushindwa kupata msamiati mpya ikiwa kinachojadiliwa kipo nje ya kiwango chao cha ujifunzaji hivyo hushindwa kuendeleza mjadala.

5.3 MBINU YA MASWALI NA MAJIBU

Mbinu ya maswali na majibu ni mbinu waliyoitumia marafiki wa lugha katika kuwasaidia wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni kumudu stadi ya mazungumzo kwasababu inamsaidia mjifunzaji kuongeza kiwango cha kujiamini na kufikiri, huwapa wajifunzaji fursa ya kukuza uwezo wao wa kujieleza kwa mazungumzo. Abbasi (2011) amethibitisha hayo pia, anasisitiza kuwa mbinu hii ni bora kuliko mbinu nyingine kwa sababu wanafunzi hukuza ufahamu wao kupitia mazungumzo. Ili kukuza stadi ya mazungumzo, rafiki wa lugha aulize maswali na wanafunzi wajibu, lakini pia rafiki wa lugha atoe fursa ya kuulizwa maswali na anatakiwa ayajibu kwa ukamilifu. Wanafunzi wapatiwe nafasi ya kutosha ya kuuliza au kujibu maswali bila ya kuwakemea, wala kuyapuuza maswali yao. Uhusiano wa namna hii ukiimarishwa, utawawezesha wanafunzi kujenga maana ya wanachofundishwa na pia wataweza kujifunza msamiati mpya kila siku, na si kujifunza tu bali pia wataweza kutumia msamiati huo. Hivyo ni dhahiri kuwa kupitia mbinu ya maswali na majibu mjifunzaji anaweza kujifunza stadi ya mazungumzo kwa urahisi zaidi.

Wakati mwingine wajifunzaji wanashindwa kumudu stadi ya mazungumzo, kutokana na baadhi ya marafiki wa lugha kutotumia kwa usahihi mbinu ya maswali na majibu. Wengine hushindwa kuyaweka wazi maswali ambayo yanapelekea wajifunzaji kuweza kuzungumza kwa urefu bila kuchoka. Hivyo, ili mbinu hii iweze kufikia malengo ya mjifunzaji marafiki wa lugha hawana budi kuweka wazi maswali hayo na yasiwe ya kuwachosha.

5.4 MBINU YA MICHEZO YA LUGHA

Mbinu ya michezo ya lugha ni mbinu mojawapo wanayoitumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Mbinu hii ni muhimu katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa sababu wajifunzaji wanapata ingizo la msamiati na matamshi. Pia matokeo yanaonyesha kuwa michezo mbalimbali inawasaidia wajifunzaji kufanya mazungumzo na kupata msamiati tofauti tofauti.

Haya pia yameelezwa na Littlewood (1981) kwamba michezo kama vile kuunganisha picha iliyopalanganywa, michezo ya loto, kufananisha picha na msamiati, huwasaidia sana wajifunzaji kufanya mazungumzo. Pia matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba mbinu ya michezo ya lugha inamsaidia mjifunzaji kupata maneno mapya ambayo atayatumia katika maisha yake ya kila siku. Baker and Westrup (2003) na Kayi (2006) wanaeleza kuwa mbinu ya michezo ikitumika katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, wajifunzaji huweza kujifunza maneno mapya na hatimaye huyatumia katika maisha yao ya kila siku. Mbinu hii ina mchango chanya kwa wajifunzaji wa lugha hususani wanapojifunza stadi ya mazungumzo. Hii inamaanisha kwamba wanafunzi wa kigeni hujifunza zaidi kupitia mbinu hii kutokana na usaidizi wa karibu wanaoupata kutoka kwa watu wa karibu wanaowazunguka. Pamoja na hayo mbinu hii ina changamoto kwani mjifunzaji hukosa uwanda mpana wa kuzungumza. Hii ina maana ya kwamba marafiki wa lugha wanapotumia michezo ya lugha matendo yana kuwa mengi kuliko maneno na maneno yake yanajirudiarudia. Hivyo, marafiki wa lugha hawana budi kuwa wabunifu wanapotumia michezo ya lugha, ikiwezekana wachague michezo ambayo ina msamiati wa kutosha.

5.5 MBINU YA MYIMBO

Mbinu nyingine wanayoitumia marafiki wa lugha katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni ni matumizi ya nyimbo. Nyimbo hizi zinaweza kuwa zile wanazozifahamu marafiki wa lugha au zilizorekodiwa na kuhifadhiwa kwa njia mbalimbali kama vile kinyonyi, kompyuta, simu na mazungumzo ya ana kwa ana na wana jamii. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa kutokana na nyimbo mbalimbali, mjifunzaji anapata wakati mzuri wa kuburudika huku akijifunza matamshi

kupitia maneno mbalimbali katika nyimbo. Nyimbo huwafurahisha wajifunzaji hivyo kuwafanya wazungumze. Kupitia mbinu hii mwanafunzi hupata fursa ya kusikiliza aina mbalimbali za mitindo ya sauti za lugha ya Kiswahili kutoka kwa wazawa wa lugha. Israel (2013) anaona kuwa mbinu za kitamaduni za ujifunzaji wa lugha zinapaswa kutathiminiwa na badala yake nyimbo ziingizwe kama njia ya kuongeza ufafanuzi katika ujifunzaji lugha.

Hii ina maana ya kwamba ujifunzaji unatokea kwa wajifunzaji kupata msamiati au maneno ambayo watayamudu kwa njia wanayofurahia. Wajifunzaji wanapohamasika basi wanajifunza zaidi na hivyo kupata msamiati wa kutosha kwa haraka. Nyimbo zilizo nyingi zinalenga kuwapa wajifunzaji maarifa mbalimbali kama vile vitenzi, sauti na njeo mbalimbali.

Schumann (1978) anaeleza kuwa ujifunzaji wa lugha lazima ufungamane na utamaduni wa jamii husika. Hivyo, kutokana na hoja hii ni dhahiri kuwa kupitia mbinu ya nyimbo inayotumiwa na marafiki wa lugha mjifunzaji anaweza pia kujifunza utamaduni wa lugha anayojifunza.

Pamoja na hayo mbinu hii ina udhaifu inapotumiwa kwa wajifunzaji wa kiwango cha awali, hii ina maana ya kwamba wimbo unapokuwa na maneno mengi mapya kwa kiwango cha awali ni vigumu mjifunzaji kuweza kumudu msamiati kwa sababu anakuwa hajapata maneno ya kutosha au hajamudu lugha vizuri. Katika kutumia mbinu hii marafiki wa lugha hawana budi kufahamu viwango vya ujifunzaji. Hii itasaidia katika uteuzi wa nyimbo ambazo atatumia katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni.

Hivyo matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbinu ya ziara, majadiliano, maswali na majibu na michezo ya lugha hutumika kwa kiasi kikubwa katika ukuzaji wa stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Hii ni kwa sababu mbinu hizi zinapendwa sana na wajifunzaji na ni mbinu zinazopelekea wajifunzaji kumudu stadi ya mazungumzo kwa haraka. Kwa upande mwingine mbinu ya nyimbo inaonekana kutumika kidogo sana katika mbinu ya rafiki wa lugha. Hii ni kutokana kuwa nyimbo zinapotumika kwa muda mrefu zinamchosha mjifunzaji. Pia utafiti umeonesha kuwa kila mbinu ina umuhimu wake katika kukuza stadi ya mazungumzo.

6.0 HITIMISHO

Makala hii imechunguza mbinu wanazotumia rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni. Malengo yakiwa kubaini mbinu wanazotumia marafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Kiswahili ikiwa ni Lugha ya Kigeni na kueleza umuhimu wa kila mbinu. Matokeo yamebainisha mbinu tano zitumikazo na rafiki wa lugha katika kukuza stadi ya mazungumzo, mbinu hizi ni ziara, majadiliano, maswali na majibu, michezo ya lugha na nyimbo. Pamoja na mbinu hizi kutumika katika kukuza stadi ya mazungumzo pia hutumika katika ufundishaji wa Lugha ya Kigeni kwa ujumla. Pia matokeo yanaonesha kuwa kila mbinu ina mchango mkubwa pale inapotumika ipasavyo kama vile kuwaongezea wajifunzaji msamiati mpya, kuimarisha matumizi fasaha ya lugha yakiwemo matamshi sahihi, pia kumpa ujasiri wa kuzungumza bila hofu ya kukosea.

Kwa upande mwingine, inaonesha kuwa baadhi ya marafiki wa lugha hawazingatii viwango vya ujifunzaji na uchaguzi sahihi wa mbinu. Hivyo, ni muhimu sana taasisi husika kuwa na programu ya mafunzo kwa marafiki wa lugha ambayo yatawasaidia kuifanya kazi hiyo kwa weledi. Pamoja na hayo yote ni vema tafiti mbalimbali zifanyike zinazohusu ubunifu wa mbinu bora zinazokwenda na wakati huu wa sayansi na teknolojia ambazo zinaweza kutumika katika kufundisha na kukuza stadi ya mazungumzo kwa wajifunzaji wa Lugha ya Kigeni.

MAREJELEO

Abbasi, A. M. (2011). A Survey in Teaching Strategies in ESL Classroom. *Language in India*, 11, 313-329.

Baker, J., & Westrup, H. (2003). *Essential Speaking Skills: A Handbook for English Language Teachers*. London: Continuum.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.

Baratayaomi, W., Syafriza, S., & Pahamzah, J. (2018). Improving Students' Reading Comprehension By Using Peer Assisted Learning Strategies (PALS) in EFL Contexts. *International Journal of Language and Literature,* 2 (2).

Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching (5th edn)*. New York: Longman.

Bruce, T. (2005). *Early Childhood Education*. London: Hodder Education Publishers.

Dirga, R., & Wijayati, P. (2018). How Can Teacher Assess Reading Skills of Generation Z Learners in German Language Class? *The Consortium of Asia-Pacific Education Universities (CAPEU)*, 1-7. doi:10.1088/1757-899X/296/1/012026.

Fauzan, U. (2016). Enhancing Speaking Ability of EFL Students through Debate and Peer Assessment. *EFL Journal*, 1 (1). http://dx.doi.org/10.21462/eflj.v1i1.8.

Klancar, N. I. (2006). Developing Speaking Skills in the Young Learnes Classroom. *TESL Journal*. Vol. XII, No. 11.

Israel, H. F. (2013). Language Learning Enhanced by Music and Song. *Literacy Information and Computer Education Journal (LICEJ) 1362*.

Timmis, I. (2002). Native-Speaker Norms and International English: a Classroom View. *ELT Journal*, 56 (3), 240-249. https://doi.org/10.1093/elt/56.3.240.

Jabur, Z. (2016). The Impact of Out-of-Class Friends' Interaction on Second Language Writing.*Theory and Practice in Language Studies*, 171-189.

Kayi, R. (2006). Teaching Speaking: Activities to Promote Speaking in a Second Language. *The Internet TESL Journal,* 12 (11).

Long, M. (1996). The Role of the Linguistics Environment in Second Language Learning Acquisition. In W. C. Ritchie, & T. K. Bhatia (eds). *Handbook of Second Language Learning Acquisition,* 413 -468). New York: Academic Press.

Mtesigwa, C. K. P. (2009). Utayarishaji wa Vitabu vya Kufundishia Kiswahili kama Lugha ya Kigeni: Haja ya Kuzingatia Mkabala wa Mawasiliano, katika *Swahili* (72), 52-67.

Ndunguru, S. N. (2004). *Kanuni na Mbinu za Kufundishia*. Dar es Salaam : Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Nushi, M. & Jenabzadeh, H. (2016). Busuu: the Mobile App.*The TESL Reporter*, 49(2).O'hara, M. (2004). *Teaching 3 – 8 (2nd edn)*. London: Continuum.

Richards, J. C. & Rodgers, T. S. (2001). *Approaches and Methods in Language Teaching*. New York: Cambridge University Press.

Schumann, J. (1978). The Acculturation Model for Second-Language Acquisition. *Second Language Acquisition and Foreign Language Teaching*, 27- 50.

Vygotsky, L. S. (1978). *Mind in Society*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Yulisa, D. (2018). Learning to Listen: Listening Strategies and Listening Comprehension of Islamic Senior High School Students. *Jurnal Pendidican Dan Pengajaran* 5 (1). DOI:10.19109/ejpp. v5i1.2046.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Tathimini ya Athari za Mabadiliko ya Kifani na Kimaudhui katika Ushairi wa Bongo Fleva katika Jamii

Getruda Modest Ngakoka
ngakokagetrude@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Neema George Mturo
neemamturo@yahoo.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii

IKISIRI
Kazi za kifasihi zimekuwa na athari nyingi katika jamii mbalimbali. Moja kati ya kazi za kifasihi ni ushairi ambao pia ni pamoja na Bongo Fleva. Makala haya yametathimini athari mbalimbali zitokanazo na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva, hii ni kutokana na hali ya ushairi huu kushika kasi zaidi katika jamii na kutumika maeneo tofauti tofauti. Aidha pamoja na kuonekana kuwa una athari kwa wanajamii kwa ujumla. Data za makala haya zilikusanywa kupitia mbinu za uchanganuzi wa matini pamoja na mbinu ya usaili. Uchanganuzi na mjadala wa data uliongozwa na Nadharia ya Umaksi. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa zipo athari chanya na hasi zinazosababishwa na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Makala haya yatawasaidia wasanii na wanajamii kwa ujumla kujua ni athari zipi wanazozipata kutokana na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva na namna ya kukabiliana na athari hizo.

MANENO YA MSINGI:
Athari, Mabadiliko, Fani, Maudhui, Ushairi, Bongo Fleva

1.0 UTANGULIZI

Fasihi simulizi ni kongwe kuliko fasihi andishi. Ulimwenguni fasihi simulizi imejidhihirisha kupitia hadithi, ushairi, ngomezi, maigizo, mazungumzo na semi, fasihi simulizi imekuwa ikibeba dhima mbalimbali kama vile kuelimisha, kuburudisha na kuonya jamii. Fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi ambao una tanzu nyingi. Mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ni ushairi. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema ushairi ni utungo unaotumia lugha ya mkato yenye mnato na mvuto katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii.

Kuna aina mbalimbali za ushairi ambazo ni pamoja na nyimbo, maghani, ngonjera, tenzi na mashairi. Aidha, Omari (2009) anasema kuwa utanzu wa ushairi una tanzu nyingi ambapo mashairi ya Bongo Fleva ni moja ya utanzu wa ushairi. Pia, Omari (keshatajwa) anaongeza kwa kusema kuwa muziki wa Bongo Fleva ulitokana na muziki wa Hip Hop, ambapo muziki huu wa Hip Hop uliasisiwa na Wamarekani wenye asili ya Kiafrika katika mji wa Bronx huko New York katika miaka ya 1970, nchini Tanzania unakadiliwa kuwa uliingia miaka ya 1980 vijana walianza kuimba fukweni mwa bahari na baadaye kwenye sherehe mbalimbali. Msanii wa kwanza kutoa kanda ya rap na kuimba alikuwa anaitwa Saleh Jabir. Hali kadhalika Mwanjoka (2011), Mbilinyi (2011) na Reuster-Jahn na Hacke (2014) wanaeleza kuwa katika kipindi hiki vijana wengi hususani wale waliotoka katika familia zenye uwezo walianza kuimba mashairi (muziki) ya *rap* kwa kuiga nyimbo zilizokuwa zikiimbwa na wanamuziki wa Marekani wakati huo.

Ushairi wa Bongo Fleva unaleta athari nyingi katika jamii, madai haya yanatokana na kuwepo kwa mabadiliko mbalimbali ya kifani pamoja na kimaudhui katika ushairi huo. Wamitila (2003) na Ngure (2003) wanashadidia hoja hii kwa kusema kuwa nyimbo hubeba mawazo mazito yenye dhamira ya kuonesha uhusiano wa jamii na mazingira au hali mbalimbali za kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa. Tafiti zao zimeonesha kuwa utanzu wa

nyimbo huakisi mabadiliko ya mifumo na mitindo ya maisha ya jamii kulingana na mazingira. Kadhalika, Indede (2008), katika makala yake ameona kuwa yapo mabadiliko mbalimbali yaliyotokea na yanayoendelea kutokea katika ushairi wa Kiswahili na pia zipo sababu zilizopelekea kutokea kwa mabadiliko hayo. Mojawapo ya sababu hizo ni pamoja na utangamano katika mifumo mbalimbali ya kielimu.

Ni wazi kuwa ushairi wa Bongo Fleva umekuwa na athari hasi na chanya japo athari hasi zimekuwa zikionekana moja kwa moja. Hali hii imepelekea wanajamii kuuona kuwa ni ushairi usiofaa kwa mfano Samwel (2011), akichambua maelezo ya Chachage (2002), Suriano (2006) na Omari (2009) anabainisha kwamba muziki wa Bongo Fleva umepingwa na watu wa kada mbalimbali kwa madai kwamba unapotosha jamii. Wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati mbalimbali wa kidini na kimaadili wamekuwa wakiupinga sana muziki wa Bongo Fleva na kuuhusisha na uhuni, mmomonyoko wa maadili na athari za utamaduni wa Kimarekani. Baadhi ya mambo yanayotumika kuushambulia muziki huu ni mavazi ya wasanii wa Bongo Fleva na lugha wanayoitumia.

Aidha, Kanyange (2015), anadhihirisha kuwa ushairi unao nafasi ya kuleta athari chanya katika jamii kama vile kuelimisha na kufichua maovu. Kanyage (keshatajwa) anaeleza kuwa nyimbo kupitia maudhui yake ambayo ni ya uadilifu yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta athari chanya katika jamii na mtu binafsi. Hali kadhalika, Mtey (2015) katika utafiti wake ameweza kuonesha kuwa muziki wa Bongo Fleva una mchango mkubwa katika jamii kwani unaelimisha, unaburudisha, unakosoa na kutoa muongozo katika jamii. Hii inaonesha kuwa mashairi ya Bongo Fleva pia huwa na athari chanya katika jamii kupitia vipengele vyake vya kifani na kimaudhui na hivyo kukubalika katika jamii na watu wa kada tofauti tofauti.

Naye Samwel (2011) anaeleza kwamba, mashairi ya Bongo Fleva yanabeba ujumbe pia kuhusiana na masuala ya mapenzi. Anasema hivi kwa sababu baadhi ya wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati mbalimbali wanadai kwamba, mashairi ya Bongo Fleva yanazungumzia mapenzi kuliko mambo mengine ya msingi. Mawazo haya ni muafaka katika kuchochea makala haya kwa sababu yameonesha kwamba, wimbo ama shairi linaweza kuandikwa kulenga jambo fulani mfano, mapenzi, siasa na uchumi na hatimaye kuleta athari katika jamii husika ya watu.

Pia, Khalifa (2012) amefanya utafiti kuhusiana na masuala ya kijinsia katika ushairi wa Bongo Fleva. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, ushairi wa Bongo Fleva unamsawiri mwanamke katika mtazamo hasi ukimlinganisha na mwanaume kwa kiasi kikubwa ingawa yapo mashairi machache yanayomsawiri mwanamke katika mtazamo chanya. Makala haya yameshughulikia mabadiliko mbalimbali ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva, vichocheo vya mabadiliko hayo pamoja na kufanya tathimini ili kuona athari hasi na chanya zinazojitokeza katika jamii ya Kitanzania kutokana na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva.

2.0 MKABALA WA UTAFITI, USANIFU WA UTAFITI NA ENEO LA UTAFITI

Mkabala uliotumika katika makala haya ni mkabala wa kitaamuli. Mkabala huu ulitumika kwa sababu data zilizopatikana kutokana na malengo ya utafiti zilihitaji kufafanuliwa na kuelezewa kwa kina kupitia maelezo kwa kadri majibu ya watoa taarifa yalivyoendana na makala haya. Pia Katika makala haya uchanganuzi kifani kama aina mojawapo ya usanifu wa utafiti ulitumika kuelezea makala haya yalivyofanyika, ambapo uchanganuzi kifani ni aina ya usanifu ambao unauwezesha utafiti kuteua mahali na vitu ambavyo vitashughulikiwa. Jumla ya mashairi tisa ya Bongo Fleva yalitumika kama mfano, mashairi hayo ni pamoja na Profesa J '*Ndiyo Mzee*', Afande Sele '*Kioo cha Jamii', Wananiita Sugu* wa Mr2, *Mikasi* wa Ngwair, *Mr Politician* wa Nakaya, *Wapo* wa Harmonize, , I Miss U, African Beaty na *Baba lao* wa Diamond. Vilevile tulikusanya maoni kutoka kwa wananchi

baadhi. Mashairi ya wasanii hawa yaliteuliwa kutokana na umaarufu wa wasanii hao na mashairi yao katika historia ya Bongo Fleva. Sababu nyingine pia ni kutokana na wingi wa wasanii pamoja na nyimbo zao, mtafiti aliwateua wachache kuwakilisha kundi kubwa. Aidha, makala haya yalitumia mkabala wa kitaamuli ambapo data ziliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa maelezo kupitia mbinu ya kusimbisha maudhui, hii ni kutokana na aina ya utafiti uliofanyika.

Utafiti uliozaa makala haya ulifanyika maktabani katika jiji la Arusha ili kuweza kupata data zilizohitajika katika kukamilisha makala haya. Watafiti waliweza kupata aina ya data walizokusudia yaani mashairi ya Bongo Fleva kwa urahisi kwa kuwa ndipo walipokuwepo wakati wote wa utafiti. Kadhalika, utafiti huu ulifanyika uwandani katika jiji la Arusha. Hii ni kwa sababu watafiti waliweza kuwa karibu na watoa taarifa wao kwani ndilo eneo ambalo watafiti walikuwepo wakati wote wa utafiti uliozaa makala haya.

2.1 WANGO, SAMPULI NA USAMPULISHAJI

Katika kipengele hiki tumeelezea wango, sampuli pamoja na njia ya usampulishaji zilizotumika katika utafiti huu. Utafiti uliozaa makala haya ulitumia mashairi ya Bongo Fleva, ambapo mashairi ya wasanii na vikundi vya washairi yalitumika katika kupata taarifa zilizohusu utafiti huu. Hali kadhalika, wananchi wa mkoani Arusha, wilaya ya Arumeru walishiriki katika kutoa taarifa zilizohitajika, kwa sababu wananchi hao ni walengwa wakuu katika suala la athari zinazotokana na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Aidha Sampuli iliyotumika ni mashairi ya Profesa J '*Ndiyo Mzee'*, Afande Sele '*Kioo cha Jamii', Wananiita Sugu* wa Mr2, *Mikasi* wa Ngwair, *Mr Politician* wa Nakaya, *Wapo* wa Harmonize, I Miss U, *African Beauty* na *baba lao na* za Diamond. Katika kutoa taarifa sahihi kuhusiana na utafiti. Pia wananchi kumi na mbili kutoka mkoa wa Arusha wilayani Arumeru walitumika katika kutoa taarifa, hii ni kutokana na urahisi wa namna ya kuwafikia kwani walikuwepo katika eneo ambalo mtafiti alikuwepo wakati wote wa utafiti.

Katika makala haya, Watafiti walitumia aina ya usampulishaji lengwa, ambapo aina hii ya usampulishaji lengwa ilitumika katika kupata mashairi ya Bongo Fleva toka kwa wasanii tajwa kwani ndilo kundi lenye sifa zilizoweza kutoa taarifa sahihi katika utafiti uliozaa makala haya, ambapo watafiti waliyapakua mashairi hayo kutoka katika mtandao pamoja na vibanda vya kurusha miziki. Aidha, aina hii ya usampulishaji lengwa ilitumika pia katika kuwapata watoa taarifa ambao ni wananchi wa mkoa wa Arusha wilaya ya Arumeru. Watafiti walitumia mbinu ya urahisi au ukaribu wa kupatikana kwa watafitiwa pamoja na mbinu ya kujitolea, ambapo mtafiti aliwaomba wananchi hao wa mkoani Arusha kwa ajili ya kuwasaili na kuweza kupata taarifa alizokuwa anazitafuta kwa ajili ya kukamilisha makala haya.

2.2 MBINU ZA UKUSANYAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

Mbinu ya uchanganuzi wa matini pamoja na mbinu ya usaili zilitumika. Mbinu hizi mbili yaani mbinu ya uchanganuzi wa matini na mbinu ya usaili zilitumika ili kuweza kupata taarifa sahihi kutokana na malengo mahususi ya utafiti. Pia, katika mbinu ya usaili watafitiwa waliweza kuwa huru zaidi katika kueleza mawazo yao kwa kina pamoja na kurekebisha pale walipoona kuwa wamekosea. Katika makala haya, mbinu hii ya uchanganuzi wa matini ilitumika kwa kutumia mashairi ya Bongo Fleva. Watafiti walizitafuta na kuzisikiliza kwa umakini wa hali ya juu na kisha kuchambua fani na maudhui mbalimbali katika mashairi hayo ili kuweza kupata na kuchambua vichocheo vinavyosababisha mabadiliko katika fani na maudhui katika ushairi huu wa Bongo Fleva ikiwa ni katika hatua za kukamilisha makala haya.

Vilevile katika makala haya, tulitumia mbinu ya usaili ilitumika kwa wananchi ili kuweza kutoa maoni yao kuhusiana na mada tajwa huku watoa taarifa hao wakipata wasaa

mzuri wa kujieleza kwa mapana zaidi na kupata fursa ya kurekebisha majibu yao kwa kadri ya uhitaji wa mtafiti. Mbinu hii ilisaidia katika kuchambua vichocheo pamoja na athari za mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Pia katika mchakato mzima wa kuchanganua data watafiti walizingatia malengo mahususi ya utafiti, kupitia mbinu ya uchanganuzi wa matini pamoja na majibu ya watoa taarifa mmoja mmoja kwa njia ya usaili na kuanza mchakato wa kuzichanganua data hizo ili kufikia hitimisho. Vile vile, watafiti walitumia mbinu ya kusimbisha maudhui kwani watafiti walizigawa data zao katika makundi na kisha kuzipa misimbo kabla ya kuzichanganua kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Aidha, majibu yaliyopatikana katika utafiti yalichambuliwa kwa njia ya maelezo.

3.0 MATOKEO YA UTAFITI

3.1 MABADILIKO KATIKA USHAIRI WA BONGO FLEVA

Watafitiwa katika utafiti uliozaa makala haya waliweza kubainisha na kuelezea aina za mabadiliko ambayo kwa mtazamo wao wanaona kuwa yametokea katika ushairi wa Bongo Fleva tangu pale walipoanza kuusikiliza mpaka hivi sasa. Yafuatayo ni baadhi ya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva ambayo yameainishwa na kuelezewa na watafitiwa kupitia mbinu ya usaili.

3.1.1 Mabadiliko katika Maudhui

Watafitiwa wote 12 waliweza kuzungumzia suala la mabadiliko katika maudhui ya ushairi wa Bongo Fleva kwa ujumla ambapo walieleza ya kuwa kadri siku zinavyozidi kwenda mbele ndivyo ambavyo dhamira na ujumbe kutoka kwa wasanii wa ushairi huu vinavyozidi kujikita zaidi katika mapenzi kuliko dhamira na ujumbe mwingine. Mmoja kati ya watoa taarifa akitolea mifano ya mashairi ya Nakaya "Mr Politician" (2009) na Afande Sele 'Kioo cha Jamii' (2003) huku akilinganisha na shairi la Diamond kama 'Baba Lao' (2019), aliweza kusema kuwa wasanii Nakaya na Afande Sele katika mashairi yao ya miaka ya nyuma yalikuwa na dhamira na ujumbe ambao unaelimisha jamii tofauti na mashairi ya Diamond ambaye ni msanii mkubwa kwa sasa na mashairi yake mengi hayana ujumbe unaolenga kuelimisha jamii bali ni masuala ya mapenzi na kujisifia na starehe za pombe. Mfano shairi lifuatalo linaloitwa *Baba Lao* la Diamond:-

Ngoma kwa ngoma ni kopo kopo

Leo ndani twakesha popo

Waiter sambazia moko moko

Moja baridi moja moto

Mmechoka eti? Aah wapi

Mnataka lala aah? wapi

Tungi limezidi? aah wapi

Tuzime muziki? aah wapi

Aidha ukiangalia shairi la Nakaya utaona kabisa ni shairi ambalo anatumia anawakosoa viongozi juu ya unafiki wao kwa wananchi wanaowapigia kula. Kwa kuwa na ahadi nyingi wakati wa kuomba kula lakini mwisho wa siku wanawaacha wananchi wakiwa na maisha magumu sana . Mfano ubeti wa pili katika shairi lifuatalo la *Mr Politician*

Hivi leo sioni mabadiliko

Hali imekuwa ngumu

Nawe watajirika

Elimu mbaya

Afya inazorota

Barabara hazipitiki

Vijana hawana ajira

(Iyeeee x3)

Mifano wa mashairi hayo hapo juu inatonyesha wazi kuwa kuna utofauti mkubwa katika mashairi haya. Mashairi ya miaka 2010 kurudi nyumba mengi yao yalikuwa yanabeba maudhui mazito yanayogusa jamii kwa kiasi kikubwa japo hata yasiyo na ujumbe mzito yalikuwepo lakini si kama kuanzia miaka 2012 mpaka 2022 hali imekuwa tofauti, shairi ambalo litaelezea mambo mengine ya kijamii ukiachana na mapenzi lazima msanii huyo awe amepewa pesa na upande fulani ndiyo ataandaa wimbo, labda unaohusiana na siasa au maswala mengine ya kijamii.

Aidha, mtoa taarifa aliongezea kwa kusema kwamba baadhi ya mashairi ya miaka ya sasa huchochea uhasama katika jamii, hii ni kutokana na tabia ya baadhi ya wasanii kujigawa katika makundi na kisha kushindana kiasi cha kusababisha chuki kati yao na kwa hadhira yao, mfano Diamond na Harmonise'.

3.1.2 Mabadiliko katika Uhalisia

Kati ya watafitiwa 12 walioshiriki katika usaili, watafitiwa wawili waliweza kugusia suala la uhalisia katika ushairi wa Bongo Fleva kama moja kati ya mabadiliko katika ushairi huu. Watafitiwa hawa walisema kuwa kadri siku zinavyozidi kwenda uhalisia katika ushairi wa Bongo Fleva umekuwa ukipungua, hii ni kwa upande wa maudhui yanayoimbwa pamoja na kinachooneshwa kuwa ni cha kuiga tamaduni za jamii za watu wa Ulaya na Marekani na kuachana kabisa na tamaduni za Afrika hususani Tanzania. Mfano mmoja kati ya watafitiwa hao alitoa mfano wa shairi la msanii Diamond linaloitwa '*African Beauty*' ambalo linamsifia msichana wa Kiafrika na wakati huo huo mavazi na muonekano na sifa za msichana huyo siyo za Kiafrika katika uhalisia.

3.1.3 Ushairi Umekuwa ni Ajira ya Kudumu

Baadhi ya watafitiwa katika utafiti huu walieleza ya kuwa moja kati ya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva ni kufanyika kuwa ajira ya kudumu kwa wasanii wenyewe, waongozaji wao, wasimamizi wao pamoja na walinzi wao kwani wasanii wakubwa siku hizi wamekuwa wakitembea na walinzi wao. Mmoja kati ya watafitiwa hawa ametoa mfano wa msanii Harmonize na Diamond ambao wamejiajiri na pia wameajiri vijana wengine kwa namna mbalimbali ikiwemo kuwa na walinzi wao popote pale walipo. Naye mtoa taarifa mwingine aliongezea kwa kusema kuwa "vijana wengi siku hizi wamekuwa wakikimbilia katika sanaa ya ushairi wa Bongo Fleva kutokana na hali halisi ya ukosefu wa ajira kwa vijana".

3.1.5 Kuzuka kwa Aina nyingi za Bongo Fleva

Mmoja kati ya watafitiwa wa utafiti huu alisema kuwa badiliko lingine katika ushairi wa Bongo Fleva ni kuzuka kwa aina nyingi za ushairi wa Bongo Fleva. Hii ni kutokana na ushindani mkubwa uliopo katika soko la sanaa hii ambapo kila msanii hutaka kujitofautisha na mwingine na pia kutaka mashabiki wengi. Mtafitiwa huyo alitoa mfano wa aina

mbalimbali zilizoweza kuibuka ndani ya Bongo Fleva ikiwa ni moja kati ya mabadiliko, aina hizo ni pamoja na Singeli na Hip Hop Singeli, pia aliweza kuwataja wasanii wa aina hizo ambao ni pamoja na Dullah Makabila, Sholo Mwamba na Meja Kunta.

3.1.6 Midundo katika Uwasilishaji wa Mashairi ya Bongo Fleva

Watafitiwa sita waliweza kueleza juu ya mabadiliko katika midundo ya mashairi ya Bongo Fleva ambapo walieleza kuwa hapo awali wasanii walikuwa wakiegemea zaidi katika ujumbe ambao walikusudia kuufikisha kwa hadhira. Hali hiyo imekuwa ikibadilika kwa kasi kubwa na kwamba hivi sasa wasanii huegemea zaidi katika upande wa midundo ambayo hutoa burudani hadhira huku wakisahau suala la ujumbe unaolengwa. Watafitiwa hawa wanaitaja midundo ya nchi nyingine kama vile ya Afrika Kusini, Nigeria na India kuwa inatumika sana katika mashairi ya Bongo Fleva. Mmoja kati ya watafitiwa alitoa mfano wa shairi la msanii Diamond liitwalo 'Baba Lao' na kusema kuwa shairi hilo halina ujumbe wa kuijenga jamii bali msanii aliegemea katika mdundo pekee. Mfano wa shairi hili la Diamond linalopatikana katika ubeti wa nane;-

Mzuka ukipanda na hili shati navua (acha uongo)

Mzuka ukipanda na hili bukta navua (acha uongo)

Jamani navua (acha uongo)

Mama navua (acha uongo)

Mwenzenu navua (acha uongo)

Eeh kuna basata

Mtu akisikiliza shairi yaan hapati yale maudhui ya msingi ambayo yanaweza yakajenga jamii na mtu akaweza kujifunza kilichozingatiwa zaidi hapa ni huo mdundo tu.

3.2 VICHOCHEO VYA MABADILIKO KATIKA USHAIRI WA BONGO FLEVA

Vipo vichocheo kadha wa kadha vilivyopelekea mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Watoa taarifa wa utafiti huu waliweza kuviiainisha na kuvitolea ufafanuzi baadhi ya vichocheo hivyo katika ushairi wa Bongo Fleva. Yafuatayo ni maoni ya watoa taarifa hao juu ya vichocheo hivyo pamoja na ufafanuzi wake;

3.2.1 Kukua kwa Sayansi na Teknolojia na Utandawazi

Hiki ni moja kati ya vichocheo ambavyo vimetajwa kwa wingi kufuatia majibu ya watoa taarifa ambapo zaidi ya nusu ya watoa taarifa yaani watoa taarifa 8 kati ya 12 wameweza kuainisha kuwa ukuaji ama maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi imekuwa ni kichocheo kikubwa katika kuleta mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Mmoja kati ya watoa taarifa alieleza kuwa sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi umeweza kufanya wasanii wa Bongo Fleva kuweza kuchanganyika na wasanii wa nchi nyingine na hivyo kujikuta wakiiga tamaduni za watu wengine. Pia, kupitia utandawazi hadhira imekuwa ikipakua mashairi hayo katika vyanzo mbalimbali mara tu wasanii wanapozitoa kazi zao jambo ambalo limewasaidia wasanii katika kuuza kazi zao.

3.2.2 Soko la Ajira na Mahitaji ya Wanajamii

Hapa baadhi ya watoa taarifa waliona kwamba moja kati ya sababu ama vichocheo vya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva ni pamoja na kutaka kuendana na soko la ajira pamoja na kukidhi mahitaji ya wanajamii. Hii ni kwa sababu wasanii wengi wamekuwa wakifanya sanaa ya Bongo Fleva kuwa ndiyo ajira yao kuu ambayo huitegemea katika

kuwapatia kipato na kuendesha maisha yao na pengine familia na ndugu zao, hivyo basi wamekuwa wakijaribu kuibadilisha kifani na hata kimaudhui ili kuweza kushinda katika ushindani uliopo kati ya wasanii hao. Vilevile mahitaji ya wanajamii yameweza kuchangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Mtafitiwa mmoja alisema:-

> *…. jamii ya sasa nchini Tanzania imekuwa ikihitaji burudani zaidi kuliko ujumbe unaopatikana katika mashairi ya Bongo Fleva. Jambo hili limewasukuma wasanii wengi kubadilisha baadhi ya vitu katika mashiri kwa kutaka kukidhi mahitaji ya wanajamii ambao ndiyo hadhira kuu.*

Watoa taarifa hawa waliongezea kwa kusema kuwa jamii ya sasa kwa kiasi kikubwa imekuwa ikihitaji kusikia ujumbe wa aina moja yaani mapenzi kwa namna tofauti tofauti pamoja na kusikia midundo mizuri. Hivyo basi ushairi wa Bongo Fleva unakuwa ukibadilika badilika na kujikita zaidi katika mapenzi.

3.3 ATHARI ZA MABADILIKO YA USHAIRI WA BONGO FLEVA KATIKA JAMII

Mbali na kubaini na kuchambua vichocheo vya mabadiliko ya ushairi wa Bongo Fleva, watafiti walifanikiwa pia kubaini athari mbalimbali zinazoikumba jamii ya Watanzania kufuatia mabadiliko ya ushairi huo kutoka kwa watoa taarifa za utafiti huu. Watafiti waliweza kuzigawa athari hizi katika mafungu mawili yaani athari chanya na athari hasi. Yafuatayo ni maelezo kutoka kwa watoa taarifa juu ya athari hizo.

3.3.1 Athari Chanya

3.3.1.1 Kukuza Kipato

Hapa watoa taarifa waliweza kuzungumzia kukuza kipato kwa namna mbalimbali ambapo kwa upande wa kwanza ni kwa wasanii wenyewe. Kutokana na urahisi wa kuuza kazi zao kupitia mitandao ya kijamii wasanii hao wameweza kuufanya ushairi wa Bongo Fleva kuwa ni biashara ambayo inawaingizia kipato halali kama ajira nyingine. Pia baadhi ya wasanii hawa wamekuwa wakiwaajiri wasanii wengine na walinzi na kuwalipa mishahara, mfano msanii Harmonize ambaye amewaajiri wasanii wengine kama Ibrah na Country Boy. Msanii Diamond ameweza kuwaajiri wasanii kama Rayvan na Mbosso Khan. Aidha wakurugenzi, waongozaji na wapiga picha wameweza kujipatia kipato kutokana na mabadiliko ya ukuaji katika ushairi huu wa Bongo Fleva. Vile vile, serikali imekuwa ikijipatia mapato kutokana na tozo za kodi kutoka kwa wasanii na vikundi vya washairi wa Bongo Fleva kama ilivyo kwa biashara nyingine nchini.

3.3.1.2 Kupata Burudani

Jamii imekuwa ikiburudika kutokana na mabadiliko yanayoendelea kutokea katika ushairi wa Bongo Fleva. Ambapo kutokana na kuwa na midundo mizuri, picha zenye kuonesha vizuri pamoja na kuwepo kwa matukio mbalimbali yanayofanywa na wasanii wa Bongo Fleva kama vile kuweka wazi maisha yao ya kila siku kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, wanajamii hujiburudisha kupitia vitu hivyo. Mmoja kati ya watoa taarifa alisema:- kuwa "baada ya kuchoshwa na shughuli zake za kila siku yeye hujiburudisha na mashairi ya Bongo Fleva na kujisikia furaha huku uchovu wake ukitoweka".

3.3.1.3 Kukuza Lugha ya Kiswahili

Watoa taarifa wametaja kuwa kwa kiasi fulani ukuaji wa Lugha ya Kiswahili umetokana na mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Licha ya kuwa wasanii huchanganya lugha ya Kiingereza na lugha nyingine lakini kwa kiasi kikubwa hutumia lugha ya Kiswahili. Kutokana na utandawazi mashairi haya husikika sehemu mbalimbali za dunia na hivyo

kuwahamasisha watu wa mataifa mengi kuifahamu lugha ya Kiswahili. Pia, kutokana na ushirikiano wa wasanii wa Bongo Fleva na wasanii wa mataifa mengine kama Nigeria, lugha ya Kiswahili imeweza kupata wazungumzaji wengi kutokana na ukweli kwamba wasanii wa nje pamoja na hadhira yao hujifunza lugha hii, kitu ambacho hakikuwepo katika miaka ya 1980 mpaka miaka ya 2000. Mtafitiwa mmoja alisema:-

> *....kwa mfano Diamond mwaka 2017 akiwa nchini Gabon alitumbuiza wimbo wa Baba Lao na kuwa kivutio kikubwa kwa nchi mbalimbali. Pia aliimba wimbo wa nchi ya Tanzania na kushirikiana na nchi mbalimbali wakati anaimba, kwa hiyo nyimbo hizo zimechangia katika kukuza lugha ya Kiswahili ikizingatiwa kwamba Diamond amekuwa akisafiri mataifa mbalimbali na katika mataifa hayo amekuwa akitumbuiza mashairi yake ya bongo fleva kwa lugha ya Kiswahili.*

Watafiti hawa wanaona mchango mkubwa wa Diamond katika kulisukuma gurudumu la Kiswahili yaani kukuza lugha ya Kiswahili katika mataifa mbalimbali. Kwani kutokana na utandawazi kukua zaidi imepelekea Diamond kufahamika zaidi katika mataifa mbalimbali ulimwenguni na hata mataifa hayo kujifunza kiswahili na wengine kujifunza nyimbo zake. Katika miaka ya 1980 mpaka miaka ya 2000 wasanii wengi hawakuweza kutambulika na hata kukuza lugha ya kiswahili kutokana na kwamba hakukuwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yangewafanya watambulike sana mfano akina Profesa J ambao waliimba nyimbonzuri sana miaka hiyo.

3.3.2 Athari Hasi

3.3.2.1 Kuharibu Utamaduni

Watoa taarifa wengi waliweza kueleza kuwa kutokana na mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva utamaduni wa Kitanzania umekuwa ukiharibika. Hii ni kutokana na wasanii wa ushairi huu kuiga tamaduni za mataifa mengine hasa mataifa ya Ulaya na Marekani. Mmoja kati ya watoa taarifa alieleza kuwa kutokana na tabia ya wasanii wa Bongo Fleva kuiga tamaduni za mataifa ya nje kama vile kutoboa masikio na pua na kusuka nywele kwa wanaume, vijana wa Kitanzania wamekuwa wakiiga kwa kufanya vivyo hivyo jambo ambalo linaharibu utamaduni wa Mtanzania. Kwa upande wa mavazi pia kutokana na wasanii wa Bongo Fleva kuvaa aina ya mavazi ya watu wa mataifa ya nje kama vile mavazi yanayoonesha nusu utupu katika video na matamasha yao vijana na watoto wamekuwa wakiiga na kuyavaa sehemu mbalimbali hata katika nyumba za ibada bila hata kuogopa. Mfano mzuri ni katika ushairi wa Diamond unaoitwa *The African beaty* video yake katika ushairi huu mwanamke amevaa nguo ambazo haziendani na utamaduni wa kiafrika hata yeye mwenyewe Diamond amevaa hivyo.

Hali kadhalika, lugha ikiwa ni moja kati ya utamaduni imekuwa ikiharibika kwa namna moja ama nyingine. Hii ni kutokana na wasanii wa ushairi wa Bongo Fleva kutumia lugha isiyo rasmi ambapo maneno kama vile 'mlupo' na 'mitungi' kama yalivyotumika katika shairi la msanii 'Ngwair' liitwalo '*Mikasii*', ubeti wa nne 'Tungi' na 'Bifu' kutoka katika shairi la msanii Diamond liitwalo '*Baba Lao*', 'mitikasi' katika shairi la msanii Mr 2 liitwalo '*Wananiita Sugu*' na maneno baadhi yamekuwa si mazuri kutamkwa hadharani katika jamii zetu. Matumizi ya maneno hayo yamekuwa yakitumika ndani ya jamii katika miktadha mbalimbali. Mfano wa mashairi hayo ni

Mitungi, *blanti, mikasi*

Kaa ukitaka kuvinjari nasi

Basi mfukoni mwako nawe uwe safi

Kulewa tushalewa kilichobaki mikasi

Washikaji milupo tutapata wapi?

***Milupo l**abda itaa ya kati*

So tunaenda vipi kwa miguu au kwa basi?

Usiku huu bora tuchukue taxi

Poa basi tusipoteze wakati

Ks ks naita taxi ('Ngwair'2007.)

3.3.2.2 Kuchochea Uovu na Uchonganishi

Kama walivyoeleza watoa taarifa katika utafiti kuwa mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva yamechochea ongezeko la maovu kama vile ulevi wa kupitiliza na zinaa. Hii ni kutokana na aina ya ujumbe ambao wasanii wamekuwa wakiusisitiza katika mashairi yao ambapo ujumbe mwingi ni kuhusu mapenzi, ulevi na starehe nyingine nyingi. Katika hali hiyo hiyo, ushairi wa Bongo Fleva umekuwa ukichochea uchonganishi ambapo wasanii kwa wasanii wamekuwa wakigombana na kuimba mashairi yenye kuchochea uchonganishi huo. Mfano ni Diamond kuwa na ugomvi na Harmonize, Diamond katika wimbo wake wa *Baba Lao* anaonyesha kujidai na kuonesha kwamba yeye ni baba lao hata kama Harmonize, kaondoka kwenye kundi lake hawezi kumfikia.

Mbali na uchonganishi na ugomvi kati ya wasanii wenyewe, hadhira imekuwa ikiathirika na uchonganishi huo kwa namna moja ama nyingine. Hii ni kutokana na hadhira kuwa na mapenzi kwa msanii ama kundi fulani na hivyo kutokana na ugomvi na mashairi ya wasanii yenye kuendeleza chuki baina yao, wanajamii nao wanajikuta wakijenga chuki kwa wale walio na mapenzi kwa wasanii ama kundi la wasanii wa tofauti na wao. Mfano ni kutoka katika makundi mawili pinzani yanayofanya vizuri katika Bongo Fleva yaani WCB linaloongozwa na Diamond na '*Konde Gang'* linaongozwa na Harmonize ambao chanzo cha ugomvi wao ni baada ya msanii Harmonize kuhama toka kundi la WCB na kuanzisha kundi lake liitwalo '*Konde Gang*'. Mfano shairi hili la *Baba Lao* ubeti wa tatu Diamond akimsema Harmonize baada ya kutengengana naye na kuenda kuanzisha kundi lingine:-

Asa twende kisamugile, sambamba hapo vipi inabamba?

Inogile inatamba, basi chanika musamba

Eeh wataweza kweli? aah wapi

Kushindana nasi? Aah wapi

Hata wakiungana? Aah wapi

Matusi kututukana? Aaah wapi

Shairi hilo linaonyesha jinsi Diamond akimfumbia fumbo Hamornize kwa kusema hata ama amehama kundi lake na kwenda kuanziasha kundi linguine hawatamuwza hata kidogo kwani yeye ni baba lao yaani hakuna mu kumshinda katika mziki

4.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Katika kipengele hiki, matokeo yamewasilishwa na kuchambuliwa kama yalivyopatikana uwandani

4.1 VICHOCHEO VYA MABADILIKO YA KIFANI NA KIMAUDHUI KATIKA USHAIRI WA BONGO FLEVA

Kwa kupitia mbinu ya usaili, watafiti waliweza kubaini kuwa yapo mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika ushairi wa Bongo Fleva pamoja na vichocheo vinavyopelekea kutokea kwa mabadiliko hayo katika ushairi huu wa Bongo Fleva.

Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yanaonesha kuwa baadhi ya mabadiliko hayo ni pamoja na mabadiliko katika maudhui, ambapo matokeo hayo yanaonesha kuwa maudhui katika ushairi wa Bongo Fleva hubadilika siku hadi siku. Maudhui ya zamani yalijikita zaidi katika masuala ya kisiasa, kitamaduni, kiuchumi na kijamii japo machache yalizungumzia mapenzi lakini kwa sasa maudhui ya mapenzi yameshamiri zaidi kuliko maudhui mengine. Matokeo haya hayapishani sana na matokeo ya utafiti uliofanywa na Msuya na Lupokela (2012) ambao kwa upande wao walieleza kuwa ushairi hasa wa Bongo Fleva ni muhimu katika kuelezea masuala mbalimbali kama vile siasa na malezi katika jamii ambavyo pia ni miongoni mwa maudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Pamoja na kufanana huku kwa matokeo ya utafiti wa Msuya na Lupokela (wameshatajwa) yanatofautiana na utafiti huu kwani utafiti huu umeonesha kuwa Bongo Fleva kwa kiasi kikubwa inazungumzia maudhui ya kimapenzi. Matokeo ya utafiti huu yanakwenda sambamba na mawazo ya Karl Maksi ambaye alieleza kuwa namna ya kufikiri kwa mwanadamu hutegemea mabadiliko ya mfumo wa uzalishaji mali unavyoendeshwa katika jamii.

Pia, mabadiliko katika uhalisia ni moja kati ya matokeo ya utafiti yaliyojadiliwa katika makala haya juu ya mabadiliko yanayotokea katika ushairi wa Bongo Fleva.Utafiti unaonesha kuwa mashairi ya Bongo Fleva kadri siku zinavyokwenda yamekuwa yakipoteza uhalisia wake katika nyanja mbalimbali kama vile lugha inayotumika, maleba na mandhari inayotumika katika uwasilishaji wa mashairi hayo kwa hadhira ambayo ni jamii ya Watanzania. Hoja hii inazidi kuthibitisha ukweli wa mawazo ya Karl Maksi juu ya mabadiliko ya kihistoria katika msingi wa uzalishaji mali yanavyoathiri jamii.

Hali kadhalika, ongezeko la wasanii ilitajwa kuwa ni mojawapo ya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Utafiti unaonesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la wasanii katika ushairi wa Bongo Fleva ambalo husababisha kuwepo kwa ushindani mkubwa katika utungaji na uimbaji wa ushairi huu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa idadi ya wasanii wa ushairi wa Bongo Fleva imekuwa ikiongezeka kutokana na sababu mbalimbali ambazo baadhi ya sababu zilizotajwa ni pamoja na ukosefu wa ajira.

Ushairi wa Bongo Fleva umekuwa ni ajira ya kudumu, hii ni moja kati ya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti ni kwamba vijana wengi wamepata ajira kutokana na ushairi wa Bongo Fleva ambapo miongoni mwa ajira hizo ni pamoja na waimbaji wenyewe kama vile Marioo, Mimi Mars, Vanessa Mdee na Ruby, pia ajira kwa wakurugenzi na waongozaji wao kama vile Salamu SK, Mkubwa Fella na Babu Tale kwa kuwataja kwa uchache. Mawazo haya yanafanana na mawazo ya Senkoro (2003) na Engel (2008) katika tafiti zao. Senkoro (keshatajwa) akizungumzia suala la uchumi alieleza kuwa muziki wa Bongo Fleva ni moja ya chanzo cha ajira kwa wasanii hao, kwani wao hutumia muziki huo kama bidhaa wanayoiuza kwa watu baada ya kuizalisha. Naye Engel (keshatajwa) katika utafiti wake anaeleza kuwa, jamii ya vijana imejiingiza katika muziki kwa madhumuni ya kujipatia ajira ndiyo sababu nyimbo zao huzungumzia zaidi masuala yanayoisibu jamii. Hivyo, tafiti hizi zinadhihirisha kuwa ushairi wa Bongo Fleva ni moja kati ya vyanzo vya ajira kwa wanajamii wa Kitanzania.

Kuzuka kwa aina nyingi za ushairi wa Bongo Fleva pia ilitajwa kuwa ni moja kati ya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva, hii ni kutokana na ushindani uliopo katika soko la sanaa hii. Aina hizo ni pamoja na Singeli na Hip Hop Singeli ambazo pia hupendwa na jamii ya Watanzania. Wasanii waliowahi kutunga mashairi ya aina hizi mpya za Bongo Fleva ni pamoja na Sholo Mwamba, Dullah Makabila, Profesa J, Major Kunta, Malkia Caren na Mr Lava lava kwa kuwataja baadhi. Kutokana na kuzuka kwa aina nyingine za Bongo Fleva kama zilivyoainishwa na watoa taarifa kumeleta uwanja mpana wa burudani na pia kumesaidia katika kukuza soko la ajira kwa jamii kwani aina hizo nyingi zimesababisha

kuwepo kwa wasanii wengine wapya katika ushairi wa Bongo Fleva. Kama ambavyo Karl Maksi alizungumzia suala la mabadiliko ya kihistoria katika jamii namna yanavyoleta malumbano ya kiuchumi, katika hali hii binadamu huamua njia mbalimbali za kujikwamua kiuchumi ikiwemo shughuli zinazohusiana na ushairi wa Bongo Fleva.

Vile vile, mabadiliko ya midundo katika uwasilishaji wa mashairi ya Bongo Fleva yalitajwa na watoa taarifa katika utafiti, ambapo watoa taarifa walieleza kuwa wasanii wa ushairi huu wa Bongo Fleva wamekuwa wakiegemea katika suala la kutengeneza midundo mizuri yenye kuvutia hadhira wake na wakati mwingine wakijisahau kuhusu ujumbe unaotakiwa kuufikia jamii. Ni ukweli kuwa kadri siku zinavyokwenda mbele ndivyo ambavyo midundo mipya katika uwasilishaji wa ushairi wa Bongo Fleva inavyoongezeka na kufanya ushairi huu kuvutia sana japokuwa kwa upande mwingine wasanii hujisahau katika suala la kuzingatia ujumbe.

Pia, kupitia usaili wa watoa taarifa inaonyesha wazi kwamba, vipo vichocheo vya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva kama ifuatavyo;

Kukua kwa sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi, watoa taarifa walieleza kuwa ni kichocheo kimojawapo katika mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Watoa taarifa hao walieleza kuwa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi vimewafanya wasanii wa Bongo Fleva kupata uzoefu wa aina tofauti tofauti kutoka kwa wasanii wengine wa nje ya Tanzania. Jambo hilo limewasababishia wasanii wa ushairi wa Bongo Fleva kuiga baadhi ya vionjo, aina ya ujumbe na dhamira pamoja na maleba kutoka katika mataifa mengine na hivyo kuleta mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Mawazo haya yanaendana na mawazo ya Low (2011) katika utafiti wake juu ya muziki wa Bongo Fleva ambapo alifafanua kuwa moja kati ya sababu za kuzuka na kukua kwa muziki wa Bongo Fleva Tanzania ni pamoja na utandawazi. Kukua huko kwa sayansi na teknolojia ni moja kati ya mabadiliko ya mifumo ya uzalishaji mali ambayo Maksi aliwahi kuzungumzia katika nadharia yake kwamba husababisha kutokea kwa jambo fulani ndani ya jamii.

Kadhalika, harakati za kuendana na soko la ajira na mahitaji ya wanajamii ilitajwa kuwa ni moja kati ya vichocheo vya mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Ushairi wa Bongo Fleva umekuwa ukibadilika badilika kadri siku zinavyokwenda mbele kutokana na ukweli kwamba wasanii wa ushairi huu hutunga mashairi yao kulingana na soko la ajira ambapo huangalia zaidi mahitaji ya jamii kwa wakati husika. Kwa mfano, kwa mujibu wa watoa taarifa walisema kwamba miaka ya 2010 mpaka 2020 jamii inahitaji zaidi kuburudika pamoja na kuzungumzia masuala ya kimapenzi kwa namna hasi na chanya. Hali hii huwasukuma wasanii kutunga mashairi yao kuendana na mahitaji ya jamii ili kuweza kupata soko la mashairi hayo na hivyo kupelekea mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Majibu kama haya yalipatikana pia katika utafiti uliofanywa na Senkoro (2003) ambaye katika utafiti wake alieleza kuwa nyimbo za Bongo Fleva hulenga zaidi soko kuliko hata maudhui. Hii ni kutokana na jamii kuwa na matabaka ambayo yapo kwenye harakati za kugombea uchumi, siasa na faida za kijamii kama yalivyo mawazo ya Maksi, hivyo washairi wa Bongo Fleva hutaka kuendana na matakwa ya hadhira ambayo ni jamii inayowazunguka.

Kuendana na wakati na matukio pia ilitajwa na watoa taarifa kuwa ni miongoni mwa vichocheo katika mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Hapa watoa taarifa walichanganua kuwa wasanii wa ushairi wa Bongo Fleva wamekuwa wakitunga mashairi yao kutokana na wakati na matukio fulani katika jamii ya Kitanzania. Ni wazi kuwa matukio kama vile kampeni za kisiasa, vifo vya viongozi wa nchi na wasanii wenyewe, majanga ya kitaifa na kimataifa kama vile ugonjwa utokanao na virusi vya Korona na mengineyo mengi huwafanya wasanii kutunga mshairi, ambapo katika matukio hayo wasanii wa Bongo Fleva huweza kutunga mashairi yahusuyo matukio hayo muhimu katika jamii. Wazo hili halipo mbali sana na wazo la Omari (2009) ambaye anadhihirisha hili kwa kusema kuwa nyimbo nyingi za Bongo Fleva huenda sambamba na matukio au masuala ya

kijamii kwa maana kwamba wasanii hutunga nyimbo zao kwa kuangalia masuala ya kijamii. Katika kushadidia matokeo haya Nadharia ya Umaksi inaeleza wazi kuwa kutokana na harakati za kutaka faida za kijamii wanadamu hujaribu kuendana na mabadiliko ya kihistoria.

4.2 TATHIMINI YA ATHARI ZA MABADILIKO YA KIFANI NA KIMAUDHUI KATIKA USHAIRI WA BONGO FLEVA

Sanjari na kubaini na kuchambua mabadiliko pamoja na vichocheo vya mabadiliko hayo katika ushairi wa Bongo Fleva, makala haya yaliweza kufanya tathimini ya athari zitokanazo na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva. Ufuatao ni mjadala kuhusu majibu ya watoa taarifa juu ya athari hizo;

4.2.1 Athari Chanya

Kukuza kipato ni moja kati ya athari chanya zilizotajwa na kufafanuliwa na watoa taarifa katika utafiti uliozaa makala haya, ambapo watoa taarifa walifafanua kuwa kutokana na hali ya ushairi wa Bongo Fleva kufanyika ajira kwa wasanii, wasimamizi, waongozaji, walinzi na hata wauzaji na wasambazaji wa mashairi haya, kipato kimeongezeka kwa mtu mmoja mmoja, makampuni na taifa kwa ujumla kutokana na kodi wanazozitoa katika mfuko wa taifa. Utafiti uliofanywa na Engel (2008) ulikuja na matokeo kama haya kwani Engel (keshatajwa) alionesha kuwa vijana wengi wamejiingiza katika ushairi wa Bongo Fleva kwa madhumuni ya kujipatia kipato hali ambayo pia hukuza pato la taifa na la mtu mmoja mmoja katika jamii. Matokeo haya yanatokana na urazini wa wanajamii ambao umeupa thamani ushairi wa Bongo Fleva kwa kuona kuwa una faida kwa baadhi ya watu ndani ya jamii kama yalivyo mawazo ya Karl Maksi katika Nadharia ya Umaksi.

Aidha, jamii imekuwa ikipata burudani kutokana na mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva. Watoa taarifa za utafiti walieleza kuwa wanajamii wengi wakubwa kwa wadogo hupenda kujiburudisha kupitia mashairi haya ya Bongo Fleva ambapo wengine baada ya kazi za kutwa nzima huburudishwa na mashairi haya wakiwa maeneo tofauti tofauti kama kumbi za starehe na nyumbani. Pia mashairi ya Bongo Fleva hutumika katika kutoa burudani kwa watu katika sherehe na matukio mbalimbali kama vile harusi. Mfano ni shairi la msanii Diamond liitwalo '*Iyena*' na shairi la msanii Aslay liitwalo '*Ndoa*' ambapo mashairi hayo yanaelezea furaha ya harusi ama ndoa na hivyo kutumika katika kutoa burudani katika harusi. Mtey (2015) alifanya utafiti juu ya dhamira za Bongo Fleva pamoja na hadithi fupi za magazeti ya udaku na kupata matokeo yanayofanana na haya kwani aliweza kutaja burudani kama moja kati ya athari wanazozipata wanajamii baada ya kusoma na kusikiliza kazi hizo. Karl Maksi katika Nadharia ya Umaksi alieleza dhahiri kuwa namna ya kufikiri kwa mwanadamu ndiko kunamuwezesha mwanadamu huyo kueleza yale yaliyomzunguka na kuyaona kuwa ni ya kweli, kama ambavyo matokeo ya utafiti yanavyoonesha kuwa Ushairi wa Bongo Fleva huwaburudisha hadhira.

Pia, mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva yamesaidia katika kukuza lugha ya Kiswahili ikiwa ni moja kati ya athari chanya za mabadiliko hayo. Utafiti ulionesha kuwa kutokana na kuwepo kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi, kumekuwa na muingiliano kati ya wasanii wa Bongo Fleva na wasanii wa nchi nyingine kama Ghana na Marekani. Mfano wa wasanii wa Bongo Fleva waliowashirikisha wasanii wa mataifa mengine ni kama vile, Diamond aliyewashirikisha wasanii Tiwa Savage na Mr Flavour kutoka nchini Nigeria, Nandy akimshirikisha msanii Koffi Olomide kutoka nchini Kongo na Jux akimshirikisha msanii Nyashinski kutoka nchini Kenya. Hii imepelekea baadhi ya wasanii wa nje na hadhira yao kuifahamu lugha ya Kiswahili na hata kujifunza pamoja na kuitumia. Sanjari na hayo, mashairi haya ya Bongo Fleva yamechangia

kupatikana kwa msamiati na lugha mbalimbali za misimu mfano 'kama kawa', 'mwana', 'dingi' na 'mshua' katika lugha ya Kiswahili.

4.2.2 Athari Hasi

Kuharibu utamaduni wa Kitanzania ni miongoni mwa athari hasi zilizoweza kubainishwa na kutolewa ufafanuzi na watoa taarifa katika utafiti uliozaa makala haya, watoa taarifa walifafanua kuwa mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuharibu tamaduni za Kitanzania kwani wasanii huiga tamaduni za kigeni hasa kutoka bara la Ulaya na Marekani. Tamaduni hizo ni kama vile namna ya uvaaji, uzungumzaji na lugha kwa ujumla. Kwa upande wa lugha, watoa taarifa walieleza kuwa maneno yatumiwayo na wasanii wa Bongo Fleva huifanya lugha ya Kiswahili kuonekana kuwa ni ya kihuni. Makala haya yanajadili kuwa, mbali na maneno hayo kuichafua lugha ya Kiswahili na kuonekana kuwa ni ya kihuni, maneno hayo hayo kwa upande mwingine husaidia katika kukuza lugha kwani baadhi ya maneno hayo husanifishwa na kuwa msamiati rasmi katika lugha.

Samwel (2011) katika utafiti wake alieleza kuwa muziki wa Bongo Fleva unapingwa na watu wa kada mbalimbali kwa madai kuwa unapotosha jamii na kuuhusisha na uhuni, mmomonyoko wa maadili na athari za utamaduni wa Kimarekani. Kadhalika, wazo hili linashadidia Nadharia ya Umaksi juu ya urazini wa mwanadamu unavyoweza kukipa thamani kitu au jambo fulani kwani urazini wa wanajamii ndio unaopelekea wanajamii kufikiri kuwa mabadiliko katika ushairi huu wa Bongo Fleva yamechangia katika kuharibu tamaduni za Kitanzania.

Pia, athari hasi nyingine ni kuchochea uovu na uchonganishi katika jamii, ambapo watoa taarifa walieleza kuwa mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva yamechangia katika kuongezeka kwa maovu kwa maana ya kuwa kutokana na ujumbe ambao wasanii walio wengi huusisitiza kama vile ulevi. mfano katika shairi la msanii Diamond liitwalo '*Nataka kulewa'*, ngono zembe, mfano katika shairi la msanii Mbosso Khan liitwalo '*Baikoko'* na starehe nyingine nyingi.

Kwa upande mwingine, mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva yamekuwa yakileta athari hasi ya kuchochea ugomvi katika jamii ambapo baadhi ya wasanii wao kwa wao wamekuwa na ugomvi wa kimuziki na hata kupelekea ugomvi huo katika maisha yao ya uhalisia. Mbali na ugomvi baina ya wasanii, hali hii imekuwa ikiwaathiri hata hadhira ambayo ni wanajamii kwa kuwa wamejikuta wakiegemea upande fulani wa msanii hali ambayo huleta uchonganishi kati ya mashabiki wa msanii mmoja na mwingine. Karl Maksi katika Nadharia ya Umaksi aliweza kuonesha kuwa namna ya kuhisi na kufikiri kwa mwanadamu humpelekea kuamini kile anachokiona kuwa ni sahihi kama ambavyo matokeo haya yanavyoonesha kuwa uovu na uchonganishi huweza kusababishwa na mabadiliko katika ushairi wa Bongo Fleva kutokana na utunzi na matendo ya wasanii wa ushairi huu.

5.0 HITIMISHO

Makala haya yamejadili tathimini ya athari za mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva katika Jamii. Katika mjadala huo mabadiliko katika nyanja mbalimbali katika ushairi wa Bongo Fleva yalijadiliwa, pia, vichocheo vya mabadiliko hayo pamoja na athari chanya na hasi za mabadiliko hayo katika jamii. Japokuwa zipo athari hasi zitokanazo na mabadiliko ya kifani na kimaudhui katika ushairi wa Bongo Fleva kama zilivyojadiliwa, athari chanya za mabadiliko hayo zimeonekana kuwa na umuhimu katika jamii ikiwemo wasanii wa mashairi ya Bongo Fleva, wanajamii ambao ndio hadhira na serikali kwa ujumla.

MAREJELEO

Chachage, S. L. (2002). *'Ndani ya Bongo', Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni*, Idara ya Sosholojia, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Indede, F. N. (2008). Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake Katika Ushairi wa Kiswahili, katika *Swahili Forum, 15, 73-94.*

Kanyange, E. K. (2015). *Maudhui ya Uadilifu katika Nyimbo za Joseph Ngala*.Tasinifu Shahada ya Umahiri. Chuo kikuu cha Nairobi. Nairobi.

Khalifa, A. I. S. (2012). *Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania*. Tasinifu Shahada ya Umahiri.Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Dar es Salaam.

Low, N. (2011). *Dhima ya Nyimbo za Bongo Fleva Zihusuzo Ukimwi*. Tasnifu ya Umahiri. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Msuya, M. B., & Lupokela, A. P. (2012). Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi kwa Jamii, katika *MULIKA,* Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

Mtey, F, J. (2015). *Ulinganishi wa Kidhamira wa nyimbo za Bongo Fleva na Hadithi fupi za Magazeti ya Udaku*. Tasinifu Shahada ya Umahiri.Chuo kikuu cha Dodoma.

Mulokozi, M. M & Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. TPH. Dar es Salaam.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari, Nairobi:* Phonex Publishers. Ngure, Dar-es-salaam.

Omari, S. (2009). *Hip Hop As Popular Literature*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa),: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dares Salaam

Reuster-Jahn, U., & Hacke, G. (2014). The Bongo Fleva Industry in Tanzania and Artists: Strategies for Success. Katika *Bongo Media Words: Producing and Consuming Popular Culture in Da es Salaam.*

Samwel, M. (2011). Siasa katika Nyimbo za Mapenzi za Bongo Fleva, katika Omari, S. & Mrikaria, G. (wah), katika *MULIKA*, 30 & 31, 6-28.

Senkoro, F. E. M . K. (2003). Rethinking Popular Arts and Culture in the 21st Century Africa. Makala yaliyowasilishwa katika maadhimisho ya 30 ya *CODERSRI.*

Suriano, M. (2006). *Hip Hop and Bongo Flavour music in Contemporary Tanzania: Youths Experiences, Agency, Aspirations and Contradictions.* Paper submitted For the conference "Youth and the Global South: Religion, Politics and the Making of Youth in Africa, Asia and the Middle East", Dakar, 13–15 October, 2006.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*, Focus publications Ltd, Nairobi.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha Ya Kimasai-Irkisongo

Editha Siphael Mollely
Edithamollel2@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Perida Mgecha
peridamgecha@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii

IKISIRI

Unyambulishaji ni kipengele muhimu sana katika lugha kwani ndio msingi mmojawapo wa uundaji wa maneno. Makala hii imejikita katika kuchunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Malengo mahususi yakiwa ni kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo, na kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi hivyo. Utafiti umeongozwa na nadharia ya Mofolojia Leksia na nadharia ya Kioo. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa mbinu ya usaili na tafsiri, na uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia mbinu ya muktadha na kusimba maudhui. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kimasai-Irkisongo ina viambishi nyambulishi bainifu kama ilivyodhihirika katika kauli saba za vitenzi vilivyo chunguzwa japokuwa kauli ya kutendea na kutendwa zinatumia baadhi ya viambishi vinavyofanana. Kuna ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi katika lugha hii: vipo vinavyofuata mzizi moja kwa moja, vinavyofuata viambishi vingine, na viambishi vinavyotokea kabla au baada ya mzizi wa kitenzi tu au kabla na baada ya mzizi wa kitenzi kwa wakati mmoja. Utafiti umebaini kuwa kauli ya kutendesha ndiyo kauli pekee yenye viambishi nyambulishi vinavyotokea kabla na baada ya mzizi wa kitenzi. Kutokana na matokeo haya tunaona ni muhimu dhana ya unyambulishaji inayoukiliwa na uongezaji wa viambishi baada ya mzizi wa vitenzi itazamwe kwa upya ili iweze kukidhi lugha kimajumui.

MANENO YA MSINGI:
Unyambulishaji, Viambishi, Ruwaza

1.0 UTANGULIZI

Unyambulishaji ni sifa mojawapo kuu kati ya sifa muhimu za kimajumui za lugha nyingi duniani. Gawasike (2012) anaeleza kuwa katika mchakato wa unyambulishaji wa vitenzi kuna uwezekano wa uundaji wa maneno mapya au upanuzi wa maana za maneno. Hein na Nurse (2008), pia Katamba (1993) wanabainisha makundi makuu matano ya lugha ambayo ni lugha chambuzi, lugha ambatani, lugha unganishi, lugha ambishi na lugha mchanganyiko.

Barani Afrika zaidi ya miaka 40 iliyopita Greenberg (1963) alionesha kuwa lugha hizi zimegawanyika katika jamii lugha kuu (4) nne ambazo ni lugha za Nija-kongo, lugha za Nilo-Saharan, lugha za Afroasiatiki na lugha za Khoisani. Aidha jamii lugha za Nija-kongo nazo zimegawanyika katika makundi madogomadogo ambayo mengi yanakubali unyambulishaji. Makundi hayo ni pamoja na jamii lugha ya Benue ambapo lugha za Kibantu zimo ndani yake. Lugha za Afroasiatiki ni pamoja na Kimbulu (Ki-iraki) ambacho ni miongoni mwa jamii lugha inayopatikana katika kundi dogo la Kushitiki ya Kusini. Khoisani ni jamii lugha zinazotokea Afrika ya Kusini, Botswana na Nubia. Hapa Tanzania jamii lugha hii inawakilishwa na kabila la Kisandawe, Hatsa, Kindega, Tindiga na Hadzapi (Nurse na Heine, 2008). Aidha kundi la Nilotiki ni jamii lugha inayozungumzwa zaidi Sudani kusini, Tanzania, Uganda na Kenya. Jamii lugha hii imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni Nilotiki Mashariki ambapo kuna Kimasai na Kiturkana, Nilotiki Magharibi ambapo kuna Kijaluo na Kidinka; na Nilotiki Kusini ambapo kuna Kikalenjin na Kidatooga (Chet, 1989).

Nchini Tanzania, mgawanyo wa lugha umefanyika kwa kugawanya lugha katika makundi manne (4). Makundi hayo ni jamii lugha ya Kibantu ambapo lugha nyingi zinaingia hapa kama vile Kipare, Kichaga, Kisukuma kwa kutaja baadhi, jamii lugha ya Kushitiki ambapo Kimbulu kinahusika, jamii lugha ya Khoisani ambapo Kisandawe, Hatsa, Kindega, Tindiga na Hadzapi zinahusika. Kundi la mwisho ni Nilotiki ambapo lugha ya Kimasai imo katika kundi hili (Rugemalira, 2005).

Tafiti nyingi zimeonesha kuwa lugha nyingi duniani zinakubali unyambulishaji. Baker (1985) alifanya utafiti katika lugha ya Kijapani na Kibemba ambapo amebainisha kuwa lugha hizi zinaruhusu mfuatano wa viambishi nyambulishi. Barani Afrika pia lugha nyingi zimethibitika kuwa zinakubali unyambulishaji. Pia Baker (1985) huyohuyo alifanya utafiti katika lugha ya Pular ikiwa ni mojawapo ya jamii lugha za Fula inayozungumzwa nchini Gunea, Gunea-Bisau, Sierra Leon, Senegal, na wazungumzaji wachache kutoka nchini Mali. Katika utafiti huu imethibitika kuwa lugha hii nayo inakubali unyambulishaji.

Kadhalika unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kibantu umeendelea kuthibitisha sifa ya umajumui wa lugha. Asiime (2011) alichunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Runyankore; Charwi (2013) alichunguza unyambulishaji katika lugha ya Kikurya; Emanueli (2013) naye alichunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kijita; Gituru (2019) kadhalika alichunguza unyambulishaji katika lugha ya Kigichugu kwa kutaja baadhi.

Mbali na wanazuoni hao, wapo wataalamu waliofanya tafiti mbalimbali katika lugha zingine ambazo si za Kibantu na Kimasai kikiwemo. Dimmendaal (2016) alichunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kiturkana ambayo ni mojawapo ya lugha za Nilotiki-Mashariki. Anabainisha kuwa kitenzi cha Kiturkana kinaweza kutanuliwa kwa kuongezwa viambishi kabla na baada ya mzizi. Anaendelea kusema kuwa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kinailotiki unahusisha mfumo wa viambishi; akisisitiza kuwa kauli ya kutendesha ndiyo kauli ya pekee yenye kiambishi kinachotokea mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. Aidha utafiti huu umedhihirisha kuwa unyambulishaji katika lugha ya Turkana unathibitika katika namna mbalimbali kulingana na mwelekeo (hali timilifu dhidi ya hali isiyo timilifu, hali arifu dhidi ya hali ya kuamuru na nyinginezo) pamoja na hadhi ya irabu katika mzizi.

Pia kuna tafiti mbalimbali za kiisimu ambazo zimefanyika kuhusu lugha ya Kimasai. Lota (2015) amefanya utafiti katika eneo la leksia katika lugha ya Kimasai; na Payne (2010) amefanya utafiti katika nyanja ya fonolojia katika lugha ya Kimasai. Payne (keshatajwa) anasema kuwa lugha ya Kimasai hutokea katika minasaba tofauti mbali na konsonati zingine zenye minasaba. Aidha anabainisha kuwa lugha ya Kimasai ina sauti ya Koromeo /h/ iliyotokana na sauti /ʃ/ ya kihistoria ambayo huweza kutokea katika maumbo matatu ya *[ʃ], [c] na [h]*. Levergood (1987) ameandika juu ya utangamano wa irabu *'Maasai vowel harmony'*. Katika makala yake anaonesha uhusiano uliopo baina ya irabu za ulimi zinazounda mzizi wa neno. Anabainisha kuwa lugha ya Kimasai ina irabu 9 kama anavyosema Lindsey (2013). Aidha, Kimasai ni lugha yenye toni juu na toni chini ambapo wakati mwingine toni hizi huunganika na kutengeneza umbo la kontua (kontua ya kitoni). Pia Tucker na Mpayei (1955) wanaongezea kuwa toni ndio njia madhubuti ya kuwasilisha maana sahihi za maneno. Wanasema kuwa lugha ya Kimasai ina seti mbili za tangamano la irabu ambazo ni irabu zenye mwinuko wa ulimi, na zile zisizo na mwinuko wa ulimi. Wanadhihirisha kuwa tangamano la irabu limejikita katika matamshi ya maneno.

Aidha Karani (2013) ameandika juu ya vitenzi vya Kiarusha na anabainisha kuwa Kiarusha kina vitenzi vitatu: kitenzi kikuu, kitenzi kisaidizi na kitenzi kishirikishi. Karani (2018) anadhihirisha kuwa lugha ya Kimasai ina madaraja mawili ya vitenzi (vitenzi vya daraja la kwanza na vitenzi vya daraja la pili) ambavyo vinatenganishwa kulingana na mofo-fonolojia ya kitenzi husika. Vitenzi vya daraja la kwanza vina mzizi unaoanza na konsonati au irabu yoyote isipokuwa irabu *i* au *e* mfano katika vitenzi *Yeu*, 'Taka', *Kiɲ* 'Menya', *Dol* 'Ona', *Sir* 'Andika '*Ok* 'Kunywa' *Nyorri*,'Penda' na *Yieer* 'pika'.

Aidha vitenzi vya daraja la pili ni vitenzi ambavyo vinaanza na irabu *i*- au *e*- kama katika mfano *Irraga* 'Lala', *Isiije* 'Chachuka', *Idim* 'Weza', *Idurr* 'Hama', *Isika* 'Toroka'. Karani (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa vitenzi vya daraja la pili vina irabu nyambulishi ishilizi za aina tatu katika mzizi ambazo ni -*a*, -*e* au -*o*. Kwa mfano;

(a) *E-irrag-**a** enkerai.*
'Mtoto amelala'.
*(b) E-suj-**e** Olaiyoni.*
'Kijana ameoga'
(c) *E-iken-**o** yeyo Omulango.*
'Mama amefunga mlango'.

Dimmendaal (1983) anafafanua kuwa katika lugha ya Kimasai viambishi nyambulishi vya kutendesha vinavyotokea mwanzoni mwa mzizi vinaweza kubadili vitenzi vya daraja la kwanza kuwa vitenzi vya daraja la pili lakini kwa vitenzi nyambulishi vya daraja la pili -*yie/ -i.e* havibadili daraja husika. Aidha Tucker na Mpayei (1955) wamechunguza vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi pamoja na tabia zingine za kimofolojia katika muundo wa vitenzi vya Kimasai.

Pamoja na jitihada hizi zote za watafiti kuchunguza lugha ya Kimasai kwa uelewa wa watafiti hakuna utafiti unaohusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Unyambulishaji ni kipengele muhimu sana kwani ndio msingi mmojawapo wa uundaji wa maneno katika lugha. Hivyo makala hii imechunguza kipengele cha unyambulishaji katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo kwa kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo na kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi hivyo katika lugha ya Kimasai-Irkisongo.

2.0 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mbinu mbalimbali zilizotumika katika kufanikisha kazi hii. Mbinu hizo ni pamoja na mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango, usamplishaji, sampuli, mbinu za ukusanyaji data, na uchanganuzi wa data.

2.1 MKABALA, USANIFU WA UTAFITI NA USAMPULISHAJI

Makala hii imetumia mkabala wa kimaelezo kwa kuwa ni mkabala uliojikita katika maoni ya watoa taarifa kama anavyosema Cresswell (2014). Mkabala wa kimaelezo ndio uliowawezesha watafiti kupata ufafanuzi na maelezo ya kina kuhusu viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo kwa kuwataka watoa taarifa kutafsiri vitenzi na sentensi kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda kwenye lugha ya Kimasai-Irkisongo. Kadhalika mkabala huu umewawezesha watafiti kuchanganua data na kuandika makala inayofafanua vyema viambishi nyambulishi vya vitenzi, na ruwaza za utokeaji wa vinyambua hivyo.

Usanifu wa utafiti ni mpangilio wa utafiti ambao unaeleza utafiti utakavyoanza au ulivyoanza, utakavyofanyika au ulivyofanyika tangu kukusanya data mpaka kuchambua (Ponera, 2019). Makala hii imeongozwa na usanifu wa kifenomenolojia kwa kuwa unyambulishaji wa vitenzi ndiyo fenomena ambayo imechunguzwa. Utafiti huu unaohusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo ulifanyika mkoa wa Arusha, Wilaya ya Monduli, kata za Monduli juu, Engutoto na Lashaine. Watafiti walichagua eneo hili kwa kuwa ndipo wanapopatikana wamasai wanaozungumza Kimasai asilia.

Yin (2011) anasema kuwa usamplishaji ni kitendo cha kuchagua sampuli ya watu na kutumia data zilizokusanywa kama misingi ya taarifa ya utafiti. Katika Makala hii mbinu za usamplishaji zilizotumika ni usamplishaji lengwa na usamplishaji tajwa.

Usampulishaji lengwa ulitumika kuchagua sampuli ya wamasai ambao hawajawahi kuhamahama, wanaojua Kimasai na Kiswahili, na wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea, lengo likiwa ni kuwapata watoa taarifa wenye data sahihi kwa ajili ya makala hii. Watoa taarifa wa utafiti huu walikuwa wa jinsia ya kike na ya kiume. Watafiti walizingatia jinsia kwa sababu kulingana na mila na desturi za Kimasai kazi na wajibu zimegawanywa kulingana na umri na jinsia. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa vitenzi kama pika, fua, onja, lisha, fagia, kamua kwa kutaja baadhi vimepatikana vyema pamoja na vinyumbuo vyake kwa wanawake. Kadhalika vitenzi kama vile oa, lima, fuga, piga, kwa kutaja baadhi vimepatikana kwa usahihi zaidi kwa wanaume.

Usamplishaji tajwa ulifanyika kwa kuanza na mtoa taarifa mwenye sifa zilizotajwa, kisha kufanya naye mahojiano, na baada ya hapo kumuomba amtaje mtoa taarifa mwingine mwenye sifa kama zake. Sampuli iliyochaguliwa ni ya watu 18 ambapo watoa taarifa 6 (wanawake 3 na wanaume 3) walitoka katika kata ya Monduli juu, 6 (wanawake 3 na wanaume 3) kutoka Engutoto, na 6 (wanawake 3 na wanaume 3) kutoka katika kata ya Lashainei. Watafiti walitumia idadi hii kwa kuwa utafiti wa kimaelezo hutumia watafitiwa wachache kupata taarifa nyingi. Jedwali la 1 linaonesha idadi ya watoa taarifa.

Jedwali 1: Sampuli ya Watoa Taarifa

No	Sampuli	Kata	Umri
1	Wanawake 3 Wanaume 3	Monduli juu	50
2	Wanawake 3 Wanaume 3	Engutoto	50
3	Wanawake 3 Wanaume 3	Lashainei	50
Jumla 18		Jumla ya kata 3	

Batibo (1982) anasema kuwa watoa taarifa ni watu wenye umri usiopungua miaka 25 na kuendelea kwa kuwa ujuzi wao umekwisha kukamilika na wanakubalika katika jamii ya watumiaji wa lugha hiyo. Anaendelea kusema kuwa watoa taarifa wenye umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea wana uhakika wa kutoa taarifa sahihi kuliko wa chini ya miaka hiyo ambao wanaweza kuwa wameathiriwa na lugha ya Kiswahili au lugha nyingine. Watafiti walichagua watoa taarifa wenye umri kati ya miaka 50 na kuendelea kwa kuwa ni wango lenye umri mkubwa kiasi kwa hiyo wanaumilisi wa lugha ya Kimasai-Irkisongo. Watoa taarifa wanawake walitumiwa ili kuweza kukamilisha taarifa ambazo hazikupatikana vyema kutoka kwa wanaume kadhalika watoa taarifa wanaume walitumiwa kukamilisha taarifa ambazo hazikupatikana vyema kutoka kwa wanawake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika mila na desturi za Kimasai kuna shughuli zinazofanywa na wanawake na shughuli zinazofanywa na wanaume hivyo kuna baadhi ya vitenzi ambavyo hutumiwa zaidi na wanawake na vingine hutumiwa zaidi na wanaume. Kwa hiyo kuchanganya jinsia kumewezesha utafiti huu kupata data zinazohitajika kwa ukamilifu wake.

2.2 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Watafiti walitumia mbinu za tafsiri na usaili katika kukusanya data.

2.2.1 Tafsiri

Chelliah na De Reuse (2011) wanasema kuwa mbinu ya tafsiri ni mchakato wa kutafsiri kishazi au sentensi kutoka katika lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa ili kubaini vipengele vya kisarufi vilivyopo katika lugha lengwa. Katika mbinu ya tafsiri, ziliandaliwa

sentensi za Kiswahili 80 zilizoundwa kwa kutumia vitenzi 10 vya Kiswahili kisha kuwapa watoa taarifa wazitafsiri kwenda kwenye lugha ya Kimasai-Irkisongo. Kila kitenzi na kinyumbuo chake kilitungiwa sentensi kulingana na muktadha wa kinyumbuo husika katika sentensi. Watoa taarifa 6 wanaume wanaojua kusoma na kuandika, na 6 wanawake wanaojua kusoma na kuandika kutoka katika kata 3 teule (Monduli juu, Engutoto na Lashainei) walipewa kila mmoja sentensi 80 zilizotungwa kutokana na kauli 8 za vitenzi wazitafsiri kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kimasai. Aidha watafitiwa wote walipewa sentensi zinazofanana, lengo likiwa ni kuhakiki tafsiri iliyofanyika. Watafiti waliamua kutumia mbinu ya tafsiri kwa kuwa ndio njia iliyoweza kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo katika miktadha mbalimbali kupitia sentensi hizo zilizotafsiriwa, na kupata ruwaza za utokeaji wa viambishi hivyo.

2.2.2 Usaili

Ponera (2019) anafafanua usaili kuwa ni njia mojawapo ya kukusanya taarifa ambayo inahusu mazungumzo baina ya mtafiti na mtafitiwa wake kuhusu mambo ambayo mtafiti anataka kuyafahamu. Watafiti walitumia mbinu ya usaili wa ana kwa ana ambapo vitenzi vya Kiswahili 19 pamoja na vinyumbuo vyake viliandaliwa. Watoa taarifa 6 (3 wanaume na 3 wanawake) wawili kutoka katika kila kata kati ya kata tatu teule (Monduli juu, Engutoto na Lashainei) walifanyiwa usaili, na kila mtoa taarifa alikalimani jumla ya vinyumbuo 152. Vinyumbuo hivi hivi ndivyo vilivyotumiwa kuwasaili watoa taarifa wote na pia vingi ndivyo vilivyohusika katika kutungia sentensi zilizotumika katika mbinu ya tafsiri. Wakati wote huo watafiti walikuwa wakirekodi usaili kwa njia ya kinasa sauti. Watafiti waliamua kutumia mbinu hii pia ili kuweza kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo, na kupata ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Aidha mbinu hii ilisaidia kuhakiki data zilizopatikana kwa mbinu ya tafsiri.

2.3 UCHANGANUZI WA DATA

Ponera (2019) anafafanua kuwa uchanganuzi wa data ni mchakato wa kuzishughulikia taarifa za utafiti ili kupata maana pamoja na kupata data chache zinazohitajika. Aidha, kuainisha data ni mchakato unaoweka data nzima katika makundi tofauti ya hali moja kulingana na ufanano wa sifa, hivyo data zilizopatikana zilipangwa kulingana na malengo mahususi ya utafiti.

Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya muktadha na mbinu ya kusimba maudhui. Katika mbinu ya nadharia ya muktadha data zilizochanganuliwa ni zile zilizodondolewa kulingana na muktadha wa watoa taarifa. Hii ina maana kwamba vitenzi vilivyoshugulikiwa vilihusiana na shughuli wanazozifanya wamasai pamoja na eneo wanamoishi (Monduli). Vitenzi hivyo ni kama lima, pika, vuna, fuga, kunywa kwa kutaja baadhi. Vitenzi hivi ni vile vinavyonyumbuka kutoka katika kauli moja kwenda katika kauli nyingine. Katika mbinu ya kusimba maudhui, watafiti walitengeneza misimbo kutokana na ruwaza za viambishi nyambulishi zilizopatikana katika data za vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo, na kisha wakazipa tafsiri mpya kulingana na maudhui yake.

3.0 MATOKEO YA UTAFITI

Makala inahusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Data zimewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na malengo mahususi ambayo ni kubainisha viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo, na kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Matokeo

ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kimasai-Irkisongo ina viambishi nyambulishi na ruwaza zinazoukiliwa na viambishi hivyo kama ifuatavyo;

3.1 VIAMBISHI NYAMBULISHI VYA VITENZI KATIKA LUGHA YA KIMASAI

Hili ni lengo la kwanza la utafiti ambalo lilikusudia kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Utafiti unaonesha kuwa, lugha ya Kimasai ina viambishi nyambulishi kama ilivyochunguzwa katika kauli 7 ambazo ni kauli ya kutendea (TDEA), kutendwa (TDW), kutendewa (TDEW), kutendesha (TDSH), Kutendeka (TDK), kutendana (TDAN), na kutendeana (TDEN).

3.1.1 Kauli ya Kutendea

Kauli ya kutendea ni kauli inayoeleza hali ya mtendaji kutenda jambo kwa kuhusisha ala inayotumika, mahali panapotendeka tendo hilo, sababu ya kutenda tendo husika na tendo kufanywa kwa niaba. Data zinaonesha kuwa viambishi nyambulishi vya kauli ya TDEA ni -*aki*, -*oki* na -*ie* kama inavyofafanuliwa katika jedwali la 2 hapa chini.

Jedwali 2: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDEA katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda	Kauli ya kutendea
Taranya 'Imba'	*Ta-rany-**aki*** 'Imbia'
Nchira 'Lia'	*Nch-ir-**aki*** 'Lilia'
Tapejo 'choma'	*Ta-pej-**oki*** 'Chomea'
Tooro 'Fagia'	*To-or- **oki*** 'Fagilia'
Tooke 'Chota'	*To-ok-**oki*** 'Chotea'
Tuturo 'Lima'	*Tu-tur-**oki*** 'Limia'
Tonyarra 'Penda'	*To-nyorr-**ie*** 'Pendea'
Tooko 'Kunywa'	*To-ok-**ie*** 'Nywea'
Imbirribira 'Fikiri'	*Imbirribir-**ie*** 'Fikiria'
Nchopo 'Vaa'	*Nchop-**ie*** 'Valia'
Takwenia 'Cheka'	*Ta-kwen-**ie*** 'Chekea'

Katika jedwali hapo juu, viambishi vilivyokolezwa wino -***aki***, -***oki*** na -***ie*** ndivyo viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendea.

3.1.2 Kauli ya kutendwa

Kauli ya kutendwa ni kauli inayoashiria jambo kufanywa na mtu mwingine au tendo kumpata mpokeaji yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani. Viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa ni -*aki, -oki*, na -*ie* kama inavyofafanuliwa na jedwali la 3 hapa chini.

Jedwali 3: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDW katika Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda	Kauli ya kutendwa
Taranya 'Imba'	*Eta-rany-**aki*** 'Imbwa'
Tamera 'Lewa'	*Eite-mer-**akine*** 'Leweshwa'
Tooro 'Fagia'	*Eto-or-**oki*** 'Fagiwa'
Tapejo 'Choma'	*Eta-pej-**oki*** 'Chomwa'
Tuturo 'Lima'	*Etu-tur-**oki*** 'Limwa'
Tonyora 'Penda'	*Eto-nyorr-**ie*** 'Pendwa'

Aidha baadhi ya sentensi zilitafsiriwa kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kimasai-Irkisongo kama ifuatavyo.

a. *Etarany**aki** Osinkolio esidai.*
'Wimbo umeimbwa vizuri'
b. *Etapej**oki** inkiri esidai.*
'Nyama imechomwa vizuri
c. *Etoor**oki** intokitin pookin.*
'Vitu vyote vimefagiwa'.
d. *Etutur**oki** enguruma epapa.*
'Shamba la baba limelimwa'.
e. *Enyorr**ie** kakuyani koko enye.*
'Bibi anapendwa na wajukuu zake'.

f. *Etemer**akine** ilpayani te nkajino.*
'Wazee wameleweshwa nyumbani kwako'.

Hivyo mofu zilizokolezwa katika kauli ya kutendwa ***-aki*** na ***-oki*** ndiyo viambishi nyambulishi vya kutendwa ingawa kuna vighairi katika baadhi ya vitenzi kama vile ***-ie*** katika *Tonyorie* 'Pendwa' na ***-akine*** katika kitenzi *Etemerakine* 'Leweshwa'

3.1.3 Kauli ya Kutendewa

Kauli ya kutendewa ni kauli inayoashiria jambo kufanywa na mtu mwingine kwa lengo la kumsaidia mtu mwingine au kitu kingine. Katika kauli hii data zinaonesha viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendewa ni *-ak-*, *-ok-*, *-ik-* na *-ie*. Jedwali la 4 linafafanua zaidi.

Jedwali 4: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDEW katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya Kutenda		Kauli ya Kutendewa na Kutendwa	
Taramata	'Fuga'	*Eta-ramat-**ak**-aki*	'Fugiwa'
Taranya	'Imba'	*Eta-rany-**ak**-aki*	'Imbiwa'
Mbirribira	'Fikiri'	*E-imbirribir-**ak**-aki*	'Fikiriwa'
Nchira	'Lia'	*E-ish-ir **ak**-aki*	'Liliwa'
Toomonu	'Omba'	*Eto-mono-**ok**-oki*	'Ombewa'
Tapejo	'Choma'	*Eta-pej-**ok**-oki*	'Chomewa;
Tooro	'Fagia'	*Eto-or-**ok**-oki*	'Fagiliwa'
Tutoro	'Lima'	*Etu-tur-**ok**-oki*	'Limiwa'
Intau	' Vua'	*Eita-**ik**-aki*	'Vuliwa'
Tapalaki	'Samehe'	*Eita-pal-**ik**-aki*	'Samehewa'
Tonyorra	'Penda'	*E-nyorr-**ie***	'Pendewa'

Vilevile kuna tafsiri za sentensi zilizofanywa na watafitiwa kutoka katika lugha ya Kiswahili kwenda katika lugha ya Kimasai-Irkisongo kama zifuatazo:

a. *Etarany**ak**aki enkerai Osinkolio.*
'Mtoto ameimbiwa wimbo'.
b. *Eita**ik**aki enkerai ilikarashin.*
'Mtoto amevuliwa nguo'.
c. *Etutur**ok**oki iyook enkurma.*

'Sisi tumelimiwa shamba'.

d. *Kanyoo enyorr**ie** inkakuyani koko enye?*
Bibi anapendewa nini na wajukuu zake?

Data inaonesha kuwa kiambishi -***ak***-, -***ok***-, -***ik***-, na -***ie***- ndivyo viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendewa. Hata hivyo kiambishi -***ik***- na -***ie*** ni vighairi katika kauli ya kutendewa.

3.1.4 Kauli ya Kutendesha

Kauli ya TDSH ni kauli inayoonesha namna tendo linavyotendeka kwa kulazimishwa, kushawishi katika kuleta ithibati. Katika kauli hii kiambishi nyambulishi cha kutendesha ni *Int+I*- na -*ie*. Haya yamethibitishwa katika jedwali la 5 hapa chini.

Jedwali 5: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDSH katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda		Kauli ya kutendesha	
Taranya	'Imba'	***Inta***-*rany-a*	'Imbisha'
Temera	'Lewa	***Inte***-*mer-a*	'Lewesha'
Tooko	'Kunywa'	***Into***-*ok-o*	'Nywesha
Taapashe	'Epuka'	***Inta***-*paashe*	'Epusha'
Talaa	'Lipa'	***Inta***-*laa*	'Lipisha'
Talang'a	'Vuka'	***Inta***-*lang'-ie*	'Vusha'
Takwenia	'Cheka'	***Inta***-*kwen-ie*	'Chekesha'
Ingurana	'Cheza'	*Inguran*-**ie**	'Chezesha'
*Irrag*a	'Lala'	*Irrag*-**ie**	'Laza'
Imbirribira	'Fikiria'	*Imbirribir*-**ie**	'Fikirisha'
Iuda	'Ruka'	*Iud*-**ie**	'Rusha'
Taama	'Kula'	*Taam*-*i***e**	'Lisha'
*Kwet*a	'Kimbia'	*Kwet*-**ie**	'Kimbiza'

Hivyo data inadhihirisha kuwa kiambishi cha kutendesha ***Int+I***- ni kiambishi pekee kinachotokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kiambishi hicho kinatokea katika vitenzi vya daraja la kwanza vinavyoanza na konsonati. Aidha imebainika kuwa kiambishi -***ie*** katika data hapo juu ni kiambishi kingine cha kutendesha kinachotokea baada ya mzizi wa kitenzi katika vitenzi vya daraja la pili vinavyoanza na irabu ***e*** au ***i***. Mfano vitenzi: *Ingurana* 'Cheza, *Irrag*a 'Lala' na *Imbirribira* 'Fikiria'. Makala hii imeonesha pia kuwa katika kauli ya kutendesha kuna vitenzi vichache vya daraja la kwanza ambavyo vinakubali kupokea kiambishi cha kutendesha -*ie* baada ya mzizi kama kitenzi *Kwet**ie*** 'Kimbiza' na *Taam**ie*** 'Lisha'.

Hata hivyo imebainika kuwa katika vitenzi vya daraja la kwanza vipo vitenzi ambavyo viambishi vyote viwili yaani ***Int+I*** -na -***ie*** vinatokea kwa pamoja kama ilivyo katika neno

Inta*-kwen-* ***ie*** 'Chekesha' na ***Inta****-lang'-***ie*** 'Vusha'. Hali hii inapotokea kiambishi cha upande wa kushoto (kabla ya mzizi) ndicho kinachobeba dhana ya kutendesha, na kile kinachotokea baada ya mzizi (-*ie*) hubeba dhana ya utumizi/ukifaa/udhahania.

3.1.5 Kauli ya Kutendeka

Kauli ya kutendeka ni hali inayodokeza sifa ya kubadili tendo na kuwa katika hali ya uwezekano wa kufanyika au kutofanyika. Viambishi vya kauli ya kutendeka ni -*ai* na -*oi* kama inavyoonekana kwenye jedwali la 6 hapa chini.

Jedwali 6: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDK katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda		Kauli ya kutendeka	
Tonyora	'Penda'	*E-nyorr-* ***ai***	'Pendeka'
Taranya	'Imba'	*E- rany-****ai***	'Imbika'
Taramata	'Fuga'	*E- ramat-****ai***	'Fugika'
Toomonu	'Omba'	*E- omon-****oi***	'Ombeka'
Tooko	'Kunywa'	*E- ok-****oi***	'Nyweka'
Tooku	'Chota'	*E-okun-****oi***	'Choteka'
Tooro	'Fagia'	*E- or-* ***oi***	'Fagilika'
Tapejo	'Choma'	*E- pej-****oi***	'Chomeka'
Tuturo	'Lima'	*E- tur-****oi***	'Limika'

Baadhi ya sentensi zenye vinyumbuo vya kauli ya kutendeka zilitafsiriwa kutoka katika Kiswahili kwenda katika Kimasai-Irkisongo kama ifuatavyo:

*Enyor****ai*** *Asha.*
'Asha anapendeka'.
*Erany****ai*** *Osinkolio lenye esidai.*
'Wimbo wake unaimbika vizuri'.
*Etur****oi*** *enkoruma esidai.*
'Shamba limelimika vizuri'.
*Eor****oi*** *enkaji esidai.*
'Nyumba imefagilika vizuri'.
*Eomon****oi*** *esayata.*
'Sala inaombeka'.
*Eok****oi*** *kule.*
'Maziwa yananyweka'.

Data inadhihirisha kuwa viambishi nyambulishi vya TDK ni -***ai*** na -***oi*** katika vitenzi vingi vilivyotafitiwa na makala hii.

3.1.6 Kauli ya Kutendana

Kutendana ni hali inayorejelea tendo lifanywalo na kiima kuwa ndilo hufanywa pia na yambwa. Mofu hii ndiyo inayotuambia kuwa kila muhusika katika kiima hutenda tendo lilelile kwa mwenzie kama inavyoonekana katika jedwali la 7.

Jedwali 7: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TNDAN katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda	Kauli ya kutendana
Taranya 'Imba'	*E- ta- rany-ate* 'Imbiana'
Iemisho 'oa'	*E- a-m-ate* 'Oana'
Tonyorra 'Penda'	*E-nyorr-ate* 'Pendana'
Toomonu 'Omba'	*E-too-mon-ote* 'Ombana'
Talaa 'Lipa'	*E-laa-kin-ote* 'Lipana'

Data inadhihirisha kuwa viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendana ni *-ate* na *-ote* na katika kauli hii, ni vitenzi vichache vinavyokubali kunyambuliwa.

3.1.7 Kauli ya Kutendeana

Kimofolojia kauli ya kutendeana ni kauli inayohusisha pande mbili katika utendaji wa kiwango sawa, ni kauli inayojumuisha kauli mbili ambazo ni kauli ya kutendeana na kauli ya kutendana kama inavyoonekana katika jedwali la 8 hapa chini.

Jedwali 8: Viambishi Nyambulishi vya Kauli ya TDEA katika Vitenzi vya Lugha ya Kimasai-Irkisongo

Kauli ya kutenda	Kauli ya kutendeana
Tonyorra 'Penda'	*Eto-nyorr-okin-ote* 'Pendeana'
Talaa 'Lipa'	*Eta-la-akin-ote* 'Lipiana'
Taranya 'Imba'	*Eta-rany-akin-ote* 'Imbiana'
Lemisho 'Oa'	*Ea-m-akin-ote* 'Oleana'
Toomonu 'Omba'	*Eto-omon-okin-ote* 'Ombeana'
Tuturo 'Lima'	*Etu-tur-okin-ote* 'Limiana'

Viambishi vilivyokolezwa ***-akin-*** na ***-okin-*** ndivyo vinavyoonesha hali ya kufanyiana jambo, na vimejitokeza kwa wingi katika vitenzi vingi vya kauli hii katika lugha ya Kimasai-Irkisongo.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, kauli nyingi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo zina viambishi nyambulishi bainifu isipokuwa katika kauli ya kutendea na kutendwa ambapo kauli hizo hutumia baadhi ya viambishi vinavyofanana.

3.2 RUWAZA ZA UTOKEAJI WA VIAMBISHI NYAMBULISHI KATIKA VITENZI VYA LUGHA YA KIMASAI-IRKISONGO

Lengo la pili la makala hii ni kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo. Ruwaza ni ule mfuatano wa viambishi nyambulishi vya kauli mbalimbali za vitenzi. Aidha ruwaza za viambishi nyambulishi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo vipo katika makundi matatu; kundi la kwanza ni ruwaza za viambishi nyambulishi vinavyofuata mzizi wa kitenzi moja kwa moja, kundi la pili ni la viambishi nyambulishi vinavyofuata viambishi vingine na kundi la tatu ni la viambishi vinavyotokea kabla na au baada ya mzizi wa kitenzi.

3.2.1 Ruwaza za Viambishi Nyambulishi Vinavyofuata Mzizi wa Kitenzi Moja kwa Moja

Katika makala hii, imebainika kuwa ruwaza mojawapo ya utokeaji wa viambishi hivi ni mfuatano wa kiambishi kimoja kinachofuata mzizi moja kwa moja. Data zinazothibitisha haya ni za kauli ya kutendea, kutendwa, kutendeka na kutendana.

3.2.1.1 Ruwaza za Utokeaji waViambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendea

Viambishi vya TDEA katika vitenzi vya Kimasai-Irkisongo hutokea mara baada ya mzizi wa kitenzi na ndicho kiambishi cha mwisho katika kauli hiyo. Rejea mfano wa 1 hapo chini.

Mfano wa 1

Kauli ya kutendea

Ta-rany-**aki** 'Imba'
Ta-pej-**oki** 'Chomea'
To-or-**oki** 'Fagilia'
To-ok-**oki** 'Chotea'
Tu-tur-**oki** 'Limia'
To-nyorr-**ie** 'Pendea'
Ta-kwen-**iki** 'Chekea'

Hivyo data inaonesha kuwa utokeaji wa viambishi nyambulishi vya kutendea katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo hufuata mzizi moja kwa moja.

3.2.1.2 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendwa

Viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa hutokea mara baada ya mzizi kama inavyothibitika katika mfano wa 2 hapa chini.

Mfano wa 2:

Kauli ya kutendwa

E-itemer-akine 'Leweshwa'
E- tarany-aki 'Imbwa'
E-toor-oki 'Fagiwa'
E-titor-oki 'Limwa'
E-took-oki 'Chotwa'
E-tapej-oki 'Chomwa'
E- tonyorr-ie' Pendwa'

Hivyo katika Kimasai-Irkisongo viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa hufuata mzizi moja kwa moja.

3.2.1.3 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendeka

Utafiti unaonesha kuwa viambishi nyambulishi katika TDK hutokea mara baada ya mzizi wa kitenzi na ndicho kiambishi cha mwisho katika kitenzi. Mfano wa 3 hapa chini unathibitisha kauli hii.

Mfano wa:3

Kauli ya Kutendeka
a. *E-nyorr-ai-* 'Pendeka'
b. *E- rany-ai* 'Imbika'
c. *E-tur-oi* 'Limika'
d. *E-pej-oi* 'Chomeke'
e. *E-or-oi* 'Fagilika'
f. *E-ok-oi* 'Nyweka'
g. *E- Omon-oi* 'Ombeka'

Data katika mfano wa 3 inathibitisha kuwa viambishi vya kauli ya kutendeka katika vitenzi vingi vya lugha ya Kimasai-Irkisongio huwa ni -*ai* na -*oi* ambazo hufuata mzizi moja kwa moja.

3.2.1.4 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendana

Data zilionesha kuwa viambishi nyambulishi vya kauli ya TDAN hutokea mara baada ya mzizi wa kitenzi. Mfano wa 4 unafafanua zaidi.

Mfano wa 4:
Kauli ya Kutendana
Eta-rany-ate 'Imbana'
Ea-m-ate 'Oana'
E- nyorr-ate 'Pendana'
E- omon-ote 'Ombana'
E-la-akin-ote 'Lipana'

Kiambishi -*ate* na -*ote* ndivyo viambishi nyambulishi vinavyofuata mzizi moja kwa moja na ni viambishi vya mwisho katika vitenzi vya kauli husika.

3.2.2 Viambishi Nyambulishi Vinavyofuata Viambishi Vingine

Viambishi hivi hutokea pale ambapo viambishi vya kauli mbili tofauti vinatokea katika kitenzi kimoja; kiambishi kimoja kinatokea kwanza kisha kiambishi kingine kinafuata. Hali hii imeonekana katika kauli ya kutendewa na kutendwa, pia katika kauli ya kutendeana na kutendana.

3.2.2.1 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendewa na Kutendwa

Katika makala hii, imebainika kuwa viambishi nyambulishi katika kauli ya TDEW katika lugha ya Kimasai-Irkisongo ni -*ak*- na -*ok*- ambavyo hutokea mara baada ya mzizi kisha kufuatiwa na viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa ambavyo ni -*aki* na -*oki* kama inavyoonekana katika mfano wa 5 hapa chini.

Mfano wa 5:

Kauli ya kutendwa		**Kauli ya kutendewa na kutendwa**	
Eta-la-aki	'Lipwa'	*Eta-la-ak-aki*	'Lipiwa'
Eta-rany-aki	'Imbwa'	*Eta-rany-ak-aki*	'Imbiwa'
Etu-tur-oki	'Limwa'	*Etu-tur-ok-oki*	' Limiwa'
Eta-pej-oki	'Chomwa'	*Eta-pej-ok-oki*	'Chomewa'
Eite-mer-akine	'Leweshwa'	*Eite-mer-akine*	'Leweshewa'

E-nyorr-ie	'Pendwa'	*E-nyorr-ie*	'Pendewa'

Pamoja na ruwaza hiyo iliyoukiliwa na utokeaji wa viambishi -*ak*- na -*ok*- kuna viambishi vingine vinavyokiuka kaida hiyo ambapo katika kitenzi *Enyorr-ie* 'Pendewa' na *Eitemer-akine* 'Leweshwa', kiambishi -*ie* na -*akine* vinabeba dhana ya kauli zote mbili: kauli ya kutendewa na kauli ya kutendwa. Aidha kauli ya kutendewa -*ak*- inaambatana na -*aki* kauli ya kutendwa wakati kauli ya kutendewa -*ok*- hutokea pamoja na -*oki* ambayo ni kauli ya kutendwa.

3.2.2.2 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi katika Kauli ya Kutendeana na Kutendana

Data imedhihirisha kuwa viambishi nyambulishi vya TDEN -*akin*-na -*okin*- vinatokea mara baada ya mzizi kisha kufuatwa na viambishi vya kutendana -*ate* na -*ote*. Kiambishi -*akin*- kinaambatana na -*ate* wakati kiambishi -*okin*- kinafuatana na kauli ya kutendana -*ote*. Mfano wa 6 unafafanua kaida hiyo.

Mfano wa 6:

Kauli ya kutendana		Kauli ya kutendeana na kutendana	
E-nyorr-ate	'Pendana'	*E-to-nyorr-akin-ote*	'Pendeana'
E-la-akin-ote	'Lipana'	*E-ta-la-akin-ote*	'Lipiana'
E-tarany -ate	'Imbana'	*E-ta-rany-akin-ote*	'Imbiana'
-		*E-tu-tur-okin-ote*	'Limiana'
-		*E-ta-pej-okin-ote*	'Chomeana'
E-omon-ote	' Ombana'	*E-to-omon-okin-ote*	'Ombeana'

Viambishi vilivyokolezwa wino ndivyo vinavyoonesha ruwaza ya viambishi vya kauli mbili tofauti kutokea katika kitenzi kimoja: kauli ya kutendeana na kauli ya kutendana.

3.2.3 Ruwaza za Utokeaji wa Viambishi Nyambulishi Kabla na au Baada ya Mzizi wa Kitenzi

Ruwaza hii inaukiliwa na viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendesha ambavyo hutokea kabla na au baada ya mzizi wa kitenzi. Kiambishi *Int+I*- hutokea kabla ya mzizi wakati kiambishi -*ie* hutokea baada ya mzizi wa kitenzi mfano wa 7 unathibitisha ukweli huu.

Mfano wa 7:

Inta-rany-a	'Imbisha'
Inte- mer-a	'Lewesha'
Into-ok-o	'Nywesha'
Inta-la-a	'Lipisha'
Intu-tur-o	'Limisha'
Inta-paashe	'Epusha'
Inta-lang'-ie	'Vusha'
Inta-kwen-ie	'Chekesha'
In-guran-ie	'Chezesha'
Iud-ie	'Rusha
Kwet-ie	'Kimbiza'

Im-birribir-ie 'Fikirisha'
Taam-ie 'Lisha'

Hivyo viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendesha vinaweza kutokea kabla ya mzizi wa kitenzi tu (7a-f) au kutokea baada ya mzizi wa kitenzi tu (7i-m) au kutokea kabla na baada ya mzizi wa kitenzi kwa pamoja kama ilivyo katika (7g-h).

Kwa ujumla matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa lugha ya Kimasai-Irkisongo ina viambishi nyambulishi katika kauli saba zilizochunguzwa na utafiti huu. Katika viambishi nyambulishi hivyo, vipo vinavyojitokeza katika kauli mbili tofauti. Mfano viambishi nyambulishi *-aki* na *-oki* ni viambishi vinavyojitokeza katika kauli ya kutendea na kutendwa. Aidha ruwaza za utokeaji wa viambishi hivyo zimebainika kuwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la viambishi vinavyofuata mzizi moja kwa moja, kundi la pili ni la viambishi vinavyofuata viambishi vingine, na kundi la tatu ni la viambishi vinavyotokea kabla au baada ya mzizi wa kitenzi tu au kabla na baada ya mzizi wa kitenzi kwa wakati mmoja. Matokeo yaliyowasilishwa hapa yatajadiliwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

4.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti unaohusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Mjadala huu umejikita katika malengo makuu mawili ambayo ni kubainisha viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai na kueleza ruwaza ya utokeaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo.

Utafiti ulionesha kuwa lugha ya Kimasai-Irkisongo ina viambishi nyambulishi katika kauli mbalimbali zilizochunguzwa. Bearth (2003) anasema kuwa kila lugha inasadikika kuwa na minyumbuliko kulingana na sarufi ya lugha husika. Hoja hii imethibitishwa na kauli saba za vitenzi vya Kimasai-Irkisongo vilivyochunguzwa katika makala hii ambapo kauli hizo ni: kauli ya kutendea, kauli ya kutendwa, kauli ya kutendewa, kauli ya kutendesha, kauli ya kutendeka, kauli ya kutendana na kutendeana.

Kauli ya kutendea ni kauli inayoeleza hali ya mtendaji kutenda jambo pakiwa na ala inayotumika, mahali panapotendeka tendo hilo, sababu ya kutenda tendo husika, mwelekeo wa tendo na tendo kufanywa kwa niaba (Mgullu, 1999). Utafiti umebainisha kuwa viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendea ni -***aki***, -***oki***, na -*ie*. Viambishi -***aki***, -***oki*** na -***ie*** ndiyo viambishi ambavyo vimejitokeza zaidi katika vitenzi vingi huku kiambishi -***ie*** kikiwa ni kiambishi kinachobeba dhana ya utumizi/ukifaa na udhahania. Kitenzi *Took*-***ie***, 'Nywea', hapa kikombe ndicho kifaa kinachotumika kunywea; *Tonyorr*-***ie*** 'Pendea' na *Imbirribir*-***ie*** 'Fikiria' ni vitenzi vinavyobeba dhana ya udhahania. Kapasky (1982) na Katamba (1993) katika nadharia ya Mofolojia Leksia (ML), mhimili wake wa kwanza unafafanua kuwa umbo la neno linaweza kuelezwa kwa kupitia maumbo mbalimbali yaani mofu zenye maana zinazohusiana. Hivyo mofu -***aki***, -***oki***, na -***ie*** ni maumbo mbalimbali yenye maana ya kutendea.

Kihore na wenzake (2008) wanafafanua kuwa mofu ya kutendwa huashiria kiwakilishi cha tendo kumpata mpokeaji yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani. Utafiti umebainisha viambishi nyambulishi katika kauli ya kutendwa kuwa ni -***aki***, -***oki***, -***i*** na -***akine***. Viambishi -***aki*** na -***oki*** ni viambishi vinavyojitokeza zaidi katika vitenzi vingi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo. Hata hivyo viambishi -***aki*** na -***oki*** vinatumika katika kauli mbili ambazo ni kauli ya kutendea na kauli ya kutendwa. Pamoja na hayo bado kauli hizi zinasimama kama kauli mbili tofauti kwa kuwa zinatofautiana katika toni, mkazo na muktadha wa matumizi husika. Massamba (1982) anafafanua kuwa toni ni sifa inayowakilisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi na ambayo huweza kubadili maana ya neno au sentensi hiyo kisemantiki au kisarufi. Hivyo tofauti za

maana katika kauli ya kutendwa na kutendea zinajibainisha tu kwa kuzingatia toni na sio viambishi husika.

Katika kauli ya kutendewa mofu zinazoukilia kauli hiyo ni -***aki***-, -***ok***, -***ik***- ***iki***- na -***ie***-. Massamba na wenzake (2004) wanasema kuwa "kiambishi huandamana na mzizi hatua kwa hatua". Hii ina maana kuwa kiambishi huandamana na kiambishi nyambulishi kingine na vingine hufanya hivyo. Katika lugha ya Kimasai-Irkisongo, viambishi nyambulishi vya kutendewa vimeambatana na viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa kadhalika viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendeana vimeambatana na vile vya kauli ya kutendana. Hali hii imejitokeza pia katika utafiti uliofanywa na Gituru (2019) katika lugha ya Kigichugi ambayo lugha hiyo inaruhusu mifuatano ya viambishi nyambulishi viwili au zaidi. Kwa hiyo kuna baadhi ya sifa za lugha za Kibantu kama hii ya mfuatano wa viambishi nyambulishi zinajitokeza pia katika lugha za Kinailotiki (Kimasai).

Pamoja na hayo makala imebainisha viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendesha kuwa ni ***Int+I-*** na -***ie***. Ashton (1997) anafafanua kuwa kutendesha hufanyika hasa kukiwa na uhusika wa aina mbili: moja kuna mtu au watu wanaofanya watu wengine wafanye jambo fulani na pili kuna mtu au watu wanaowafanya wafanye tendo fulani na mtu mwingine. Kutendesha hutumika kuonesha namna tendo linavyotendeka aidha kwa ulazima, ushawishi au katika kutolea ithibati. Imebainika kuwa katika lugha ya Kimasai-Irkisongo viambishi nyambulishi vinaweza kutokea kabla ya mzizi, baada ya mzizi, au kabla na baada ya mzizi wa kitenzi kwa wakati mmoja. Aidha kauli ya kutendesha ndiyo kauli pekee yenye viambishi nyambulsihi vinavyotokeza kabla ya mzizi wa kitenzi. Hoja hii inasawiri kauli ya Dimmendaal (2016) katika utafiti wake aliofanya kuhusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Turkana ambayo ni moja kati ya lugha za Nilotiki-Mashariki. Dimmendal (keshatajwa) amebainisha kuwa unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za kinailotiki unahusisha viambishi nyambulishi vingi lakini kiambishi cha kutendesha ndicho kiambishi cha pekee kinachoambikwa kabla ya mzizi wa kitenzi.

Hivyo lugha ya Kimasai-Irkisongo na Kiturkana zinafanana katika sifa hii ya kuwa na viambishi nyambulishi kabla na baada ya mzizi wa kitenzi kwa sababu lugha hizi zote zinapatikana katika seti moja ya lugha yaani Nilotiki-Mashariki. Hata hivyo kauli hii inatofautiana na dhana ya unyambulishaji kama inavyoukiliwa katika lugha nyingi za Kibantu Kiswahili kikiwemo ambapo dhana ya unyambulishaji inafasiliwa kuwa ni kuongeza viambishi baada ya mzizi wa kitenzi.

Pia viambishi vinavyotokea kabla ya mzizi ***Int+I-*** ndivyo vinavyotawala zaidi katika kauli hii kwa sababu kiambishi cha kutendesha kinachotokea mwanzoni mwa kitenzi kinabadili vitenzi vya daraja la kwanza kuwa vya daraja la pili kama alivyosema Dimmendal (1983) pamoja na Tucker na Mpaayei (1955). Aidha imebainika kuwa viambishi vya kutendesha ***Int+I***- katika Kimasai-Irkisongo vinatofautiana na vimbishi vya kutendesha katika Kimasai-Parakuyo ambapo kiambishi hicho ni ***It+I***-, hii ni kulingana na utafiti wa Karani (2018). Tofauti hizi ni za kifonolojia kwa kuwa hizi ni lahaja mbili tofauti kati ya lahaja nyingi za lugha ya Kimasai.

Katika viambishi vyambulishi (-***ie*** ikiwemo) vinavyotokea baada ya mzizi vimebainika kuwa ni vya namna mbili; namna ya kwanza ni ile inayofanya kazi ya kutendesha na ya pili ni ile inayofanya kazi ya kuonesha hali ya utumizi/ukifaa/udhahania kulingana na namna kitenzi hicho kilivyotumika kwenye sentensi. Hali hii imedhihirika pia katika utafiti uliofanywa na Karani (2018) katika Kimasai-Parakuyo. Wailiga (2011) anaeleze kuwa viambishi nyambulishi vya kutendesha katika lugha za Kibantu-Kiswahili ni (-iz, -ish, -z, -esh, -lish, -lez, -lesh, -ny, -liz, -fy na -s) ambavyo vyote vinatokea mara baada ya mzizi wa kitenzi.

Aidha imebainika kuwa kuna vitenzi vinavyobeba viambishi vyote viwili yaani ***Int+I***-na -***ie*** kwa wakati mmoja kama kwenye ***Inta***-*lang'*-***ie*** 'Vusha' na ***Inta***-*kwen*-***ie*** 'Chekesha',

hali hii inapotokea kiambishi ***Int+I***- cha kabla ya mzizi wa kitenzi ndicho kinachofanya kazi ya kutendesha lakini kile cha baada ya mzizi wa kitenzi -***ie*** ni kiambishi kinachofanya kazi ya kuonesha utumizi/ukifaa/udhahania.

Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa utokeaji wa viambishi nyambulishi vya kutendesha vinachagua pa kutokea aidha kabla ya mzizi na au baada ya mzizi wa kitenzi kulingana na daraja la kitenzi husika. Aidha utokeaji wa viambishi viwili katika kitenzi kimoja hutegemea kazi ya viambishi hivyo katika kitenzi ndani ya sentensi.

Pamoja na hayo imebainika kuwa viambishi vya kauli ya kutendeka ni-***ai*** na -***oi***. Viambishi hivi vimesadifu hoja ya Ashton 1997 kuwa kauli ya kutendeka ni kauli inayodokeza sifa ya kubadili tendo kuwa katika hali ya uwezekano wa kufanyika au kutokea kwa jambo. Viambishi -***ai*** na -***oi*** pia vimesadifu kanuni ya Kioo ya Baker (1985) inayofafanua kuwa maana za viambishi zinapaswa kujitokeza katika vitenzi husika. Hii ina maana kuwa, dhana ya kutendeka itaonekana tu iwapo kuna kiambishi cha kutendeka. Hivyo viambishi -***ai*** ni -***oi*** ndivyo vinavyobeba dhana ya kutendeka katika vitenzi husika.

Ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo vimebainishwa wazi katika makala hii. Imeonekana kuwa ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi katika lugha ya Kimasai zinasadifu kauli ya Katamba (1993) inayosema kwamba viambishi vina mpangilio maalumu, na mpangilio huo hutofautishwa kulingana na uhusiano wa kisemantiki. Ruwaza za viambishi nyambulishi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo vipo katika makundi matatu ambapo kundi la kwanza ni lile linalofuata mzizi moja kwa moja, kundi la pili ni lile linalofuata viambishi vingine na kundi la tatu linahusu viambishi nyambulishi vinavyotokea kabla na au baada ya mzizi wa kitenzi.

Viambishi vinavyotokea mara baada ya mzizi ni vile ambavyo Massamba (2004) ameviita ni vya hatua ya kwanza. Viambishi nyambulishi hivi ni pamoja na vya kauli ya kutendea (-***aki***, -***oki*** na -***ie***), kauli ya kutendwa (-***aki***, -***oki***, -***ie*** na -***akine***), kutendeka (-***ai*** na -***oi***) na kutendana (-***ate*** na -***ote***). Ruwaza hii inafanana na ya lugha za Kibantu kama ilivyothibitishwa na Gituru (2019) katika lugha ya Kigichugu. Pia Waihiga anathibitisha haya kwa kusema kuwa, katika lugha ya Kiswahili ruwaza inayofuata mzizi moja kwa moja ni katika kauli ya kutendea, kutendwa, kutendewa, kutendeka, kutendana na kutendeana. Hali hii inaonesha wazi kuwa licha ya kwamba Kiswahili na Kimasai ni lugha mbili fotauti, lakini zinafanana katika sifa hii ya viambishi nyambulishi kufuata mzizi moja kwa moja.

Pia imebainika kuwa viambishi nyambulishi vinavyofuata viambishi vingine ni pamoja na viambishi vya kauli ya kutendewa na kutendwa pia vile vya kauli ya kutendeana na kutendana. Mfuatano huu unakinzana na Hyman (2003) kama anavyopendekeza kuwa kauli ya kutendea hutangulia kauli ya kutendwa. Katika Kimasai-Irkisongo kuna tofauti kwa kuwa kauli ya kutendewa hutangulia kauli ya kutendwa, kadhalika kauli ya kutendeana kutangulia ile ya kutendana. Viambishi nyambulishi katika kauli ya kutendewa vinaukiliwa na viambishi nyambulishi -***ak***-, -***ok***-, -***ik***-, na -***ie*** kisha kufuatiwa na viambishi vya kutendwa -***aki***, -***oki***, -***ie,*** na -***akine***. Katika kauli ya kutendeana kadhalika vinaanza viambishi vya kutendeana -***akin***- na -***okin***- kisha vya kutendana -***ate*** na -***ote***.

Hali hii inajitokeza kwa namna ya tofauti katika baadhi ya lugha za Kibantu mfano katika Kigichugu ambayo ilitafitiwa na Gituru (2019). Makala hii imebainisha mfuatano wa viambishi zaidi ya kimoja isipokuwa kauli zinazoonesha mfuatano usio sawa na unaobainishwa na makala hii. Makala hii imebaini mfuatano kati ya TDEW+TDW, TDEN+TDAN lakini katika Kigichugu ni tofauti. Kwa hiyo viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo vinaakisi Kanuni ya Kioo ya Baker (1985) katika mhimili wa pili unaosema mifuatano ya viambishi nyambulishi vya uundaji wa vitenzi huthibitisha unyambulishaji katika vitenzi husika vikiakisi miundo kisemantiki. Hii ina maana kwamba kila kinyumbuo katika kitenzi kina maana kisarufi kutokana na utokeaji wake.

Aidha viambishi nyambulishi vinavyotokea kabla na au baada ya mzizi wa kitenzi vimebainika katika kauli ya kutendesha. Viambishi vinavyotokea kabla ya mzizi ni ***Int+I-***na ndivyo vinavyotofautisha unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kinailotiki na lugha za Kibantu ambapo unyambulishaji wake unahusisha uongezaji wa viambishi baada ya mzizi wa kitenzi. Waihiga (2011) amefafanua kuwa katika lugha ya Kiswahili viambishi nyambulishi vya vitenzi vinatokea baada ya mzizi wa kitenzi. Amethibitisha hayo kwa kutumia kauli ya kutendea, kutendwa, kutendewa, kutendeka, kutendesha, kutendana na kutendeana.

5.0 HITIMISHO

Makala hii imechunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Malengo mahususi yakiwa kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo na kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo. Matokeo ya uafiti yanaonyesha kuwa; lugha ya Kimasai-Irkisongo ina viambishi nyambulishi katika kauli saba zilizochunguzwa. Viambishi nyambulishi katika kauli ya kutendea ni *-aki*, *-oki*, na *-ie*. Viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendwa ni *-aki*, *-oki, -akine*, na *-ie*, viambishi vya kutendewa ni *-ak-*, *-ok-*, *-ik-*, na *-ie*.

Viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendesha ni ***Int+I-*** na ***-ie***. Viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendeka ni ***-ai***, na ***-oi***, kauli ya kutendana ni-***ate*** na-***ote*** wakati kauli ya kutendeana ni -***akin***-na-***okin***-. Aidha katika viambishi nyambulishi vya kauli ya kutendesha, imebainika wazi kuwa baadhi ya viambishi hivyo vinatokea mwanzoni mwa kitenzi tofauti kabisa na viambishi nyambulishi vingine. Hali hii imeibua umuhimu wa pekee katika makala hii kwani ni dhahiri kuwa tafiti nyingi zilizofanyika katika lugha Kibantu, zinathibitisha kuwa unyambulishaji unahusu uongezaji wa viambishi baada ya mzizi tu. Hivyo utokeaji wa viambishi nyambulishi kabla ya mzizi unaibua upya haja ya kuitazama dhana ya unyambulishaji katika namna nyingine tofauti na awali.

Pia makala imeweka wazi ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi vya vitenzi vya lugha ya Kimasai-Irkisongo kwa kuweka katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lile linalofuata mzizi moja kwa moja kama katika kauli ya kutendea, kutendwa, kutendeka na kutendana. Kundi la pili ni lile linalofuata viambishi vingine ambapo kundi hili linahusisha viambishi vyambulishi vya kauli ya kutendewa na kutendwa, pamoja na kutendeana na kutendana. Kundi la tatu ni lile lenye viambishi vinavyotokea kabla na au baada ya mzizi wa kitenzi ambapo huhusisha kauli ya kutendesha.

Hivyo Makala imeweza kukidhi malengo yake kwa kubainisha viambishi nyambulishi vya vitenzi katika lugha ya Kimasai-Irkisongo, na kueleza ruwaza za utokeaji wa viambishi nyambulishi katika vitenzi vya lugha hii.

Kutokana na matokeo ya makala hii inapendekezwa kuwa ipo haja ya kuitazama kwa upya dhana ya unyambulishaji ambayo imekuwa ikichukuliwa kuwa ni "kitendo cha kuongeza viambishi baada ya mzizi wa kitenzi". Dhana hii imeonekana kuwa jumuishi mno kwani haikutazamwa kwa kina katika jamii lugha nyingine. Hii ni kutokana na makala hii ambayo imebainisha kuwa katika lugha ya Kimasai-Irkisongo kuna vitenzi ambavyo unyambulishaji wake unatokea pia mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi.

Aidha kuna haja ya kufanya tafiti nyingine nyingi iwezekanavyo katika lugha hii kutokana na mawanda yake mapana ambayo yamesababisha lugha hii kugawanyika katika lahaja zaidi ya 27. Lugha hii imesambaa na inazungumzwa katika maeneo mengi nchini Tanzania na Kenya. Msambao huu ndio unaozidi kuibuza lahaja kila iitwapo leo. Pia kuna uhitaji wa kuchunguza tofauti za kimatamshi zinazopatikana katika lahaja za Kimasai ili kuweza kuziainisha vyema. Kwa mantiki hii kuna haja ya kujitoma ndani zaidi ili kuchunguza maeneo mengine ya kitaalamu kama vile fonolojia, semantiki, pragmatiki na mofosintaksia.

VIFUPISHO

Ke	Mwanamke
Me	Mwanaume
ML	Mofolojia Leksia
TDEA	Kauli ya kutendea
TDAN	Kauli ya kutendana
TDEN	Kauli ya kutendeana
TDEW	Kauli ya kutendewa
TDK	Kauli ya kutendeka
TDSH	Kauli ya kutendesha
TDW	Kauli ya kutendwa

MAREJELEO

Ashton, E. O. (1994). *Swahili Grammar: Including Intonation*. London: Longman Group Ltd.

Asiime, C. (2011). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Lugha ya Runyankole*. Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Baker, M. (1985). The Mirror Principle and Mophosyntactic Explanation. *Linguistic Inquiry,* 17 (4), 745-749.

Batibo, H. M. (1982). *Mawazo ya Mwanzo kuhusu Uhusiano wa Lahaja za Kiisimu* (Makala ya Semina), Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Berth, T. (2003). Syntax. In D. Nurse, & R. Philipson, *The Bantu Languages*. London: Routledge, 125-144.

Charwi, Z. M. (2013). Unyambulishaji na Dhana ya Uelekezi katika Lugha ya Kikurya katika S. Omar, & R. Peterson. *Kioo cha Lugha,* 11, 58-77.

Chelliah, S. L., & De Reuse, W. J. (2011). *Hand Book of Descriptive Linguistics Fildwork*. London, Ne w York: Springer Science + Bussines Meudia.

Chet, A. (1989). *The Syntax of the Nilotic Languages:* Themes and Variations. Berlin: D. Reimer.

Cresswell, W. J. (2014). *Educatinal Research, Planning, Conducting and Evaluating Qualitative and Quantitative Research*. Boston: Parsonal Educational Limited.

Emmanuel, F. (2013). *Mnyumbuliko wa Vitenzi katika Lugha ya Kijita*. Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Dimmendaal, G J. (2016). *On Verbal Derivation in Nilotic: The Case of Turkana*. University of Cologne: North Rhine.

Dimmendaal, G. J. (1983). The two Morphological Verb Classes in Nilotic. In R. Vosen, & M. Bechhaus-Gerst (eds.), *Nilotic Studies* 2, 269-309. Berlin: Dietrich Reimer.

Gawasike, M. (2012). Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili. Katika *Kioo cha Lugha*, 10 (1).

Gituru, W. M. (2019). *Unyambulishaji wa Vitenzi katika Kigĩchũgũ*. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Chuka.

Greenbergs, J. H. (1963). *The Language of Africa*. India University Research Centrer in Athropology, folklore and Linguistics. Publication 25The hague: Mouton.

Heine, B., & Nurse, D. (2008). *A Linguistic Geography of Africa*. New York: Cambrige University Press.

Karan, M. (2013). *The Arusha Verbs*. M.A Kiswahili, University of Dar es Salaam.

Karan, M. (2018). *Syntactic Categories and the Verb- Argument Complex in Parakuyo Maasai*. PhD Thesis, Stellenbosch University.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: Macmillan Press Ltd.

Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Hokororo, J. I. (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu; Sekondari na Vyuo*. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiparsky, P. (1982). *Lexical Phonology and Morphology*. Stanford: Stanford University Press.

Livergood, B. (1987). *Topics in Arusha Phonology and Morphology PhD dissertation*. University of Texas Austin.

Lota, L. (2015*). Mabadiliko ya Kifonolojia toka Etimolojia ya majina ya Sehemu katika Lahaja ya Kisongo na Kiarusha katika Kimasai.* Tasnifu ya Umahiri wa Stadi za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D. P. B. (1982). *Aspect of Accent and Tone in Ci-Ruuri*. TUKI: Dar es Salaam University Press.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Payne, D. L. (2010). *Maasai Language Project, Cross Dialect Lexicography, Text and Verbs Database,* htpp://ww.oregon.ed-maasai Retrieved on January 2021.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rugemalira, J. M. (2005*). A Grammar of Runyambo*. Dar es Salaam: LOT Publications Grammar series no 1.

Tucker, A. N., & Mpaayei, J. T. O. (1955). *A Maasai Grammar with Vocubulary*. London: Longmans Green & Co.

Tumaini University Makumira (2017). *TUMA Research Manual*. Usa-River, Arusha: Tumaini University Makumira.

Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Sababu za Utoaji wa Majina ya Koo katika Jamii ya Wameru

Joyce Henock Nyiti
joycehenock@yahoo.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Perida Mgecha
peridamgecha@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii

IKISIRI

Makala hii inachunguza sababu zilizotumiwa na jamii ya Wameru kutoa majina ya koo zao. Malengo yakiwa kwanza, kubainisha majina ya koo; pili, kueleza sababu za kutoa majina hayo. Makala hii imeongozwa na nadharia ya Maana kama Matumizi. Ni ukweli kwamba watu wamekuwa wakipewa majina ya koo pasipo kujua sababu za kupewa majina hayo. Lengo la makala hii ni kuipa jamii maarifa yanayohusiana na majina ya koo zao ili kuendelea kuutunza utamaduni na historia ya majina katika jamii ya Wameru. Mbinu ya usampulishaji lengwa na tajwa zimetumika katika kuwapata watoa taarifa,na taarifa zimekusanywa kwa njia ya usaili na usimulizi. Data zimechanganuliwa kwa mbinu ya usimulizi na kusimba maudhui. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa majina ya koo za jamii ya Wameru jumla yapo 26. Pia sababu zilizotumika katika kutoa majina ya koo za Wameru ni jitihada katika kazi, matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya kivita, tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama. Makala hiiinapendekeza kuwa ili jamii iweze kutunza utamaduni na historia ya majina ya koo zake ni muhimu viongozi wa koo waweke mikakati, na kuisimamia ambayo itawezesha jamii kupata maarifa yanayohusu majina ya koo zao; hii itasaidia hata vizazi vijavyo kujua historia ya majina ya koo zao na utamaduni wao kwa ujumla.

MANENO YA MSINGI

Utoaji wa majina, Majina ya koo, Wameru

1.0 UTANGULIZI

Suala la utoaji majina katika jamii lilianza karne nyingi zilizopita na kila jamii duniani ilihusika na utoaji wa majina kwa watu wake, majina hayo yalikuwa nasababu zake. King'ei (2010) anasemajamii ilielewa maana na sababu za utoaji wa majina hayo kwa kuwa yalitumia lugha yao.Kwa ujumla mchakato wa utoaji majina ya asili ni tukio muhimu la kijamii na kiutamaduni hivyo hufanya kazi ya kuonesha uhusiano uliopo kati ya jamii na lugha yake katika kuitunza historia ya majina yake. Aidha, wataalamu mbalimbali wamebainisha aina za majina ambayo jamii huyatoa kwa ama mtu mmoja mmoja, makundi, hali mbalimbali, matukio au kwa sehemu mbalimbali.Msanjila (2009) anabainisha aina za majina yanayotolewa kwa watu kama vile majina mahususi, majina ya familia na majina ya koo; anafafanua kuwa majina hayo hutolewa ili kuweza kuwatambua watu na kumtofautisha mtu mmoja na mwingine au familia moja na nyingine. Makala hii inabainisha majina ya kooza Wameru, na kufafanua sababu za kutoa majina hayokatika jamii ya Wameru. Makala imegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni utangulizi, mbinu za utafiti, ubainishaji wa majina ya koo, sababu za kutoa majina hayo, mjadala wa matokeo ya utafiti na hitimisho.

1.1 HISTORIA YA WAMERU

Wameru ambao hapo awali walijulikana kama*N'rwa/Varwa* ni jamii ya watu wanaopatikana wilayani Arumeru katika mkoa wa Arusha nchini Tanzania. Lugha yao hujulikana kama Kimeru. Kwa mujibu wa LOT (2009:2) lugha ya Kimeru inakadiriwa kuwa

na wazungumzaji 217003 ikiwa ni lugha ya 39 kwa ukubwa Tanzania. Wameru walitokea upande wakusini, na mashariki mwa mlima Meru. Spear (1997) anaeleza kuwa japo ushahidi wa Kihistoria unaonesha kuwa Wameru walitokea Usambaa, ushahidi wa kiisimu unaonesha kuwa Wameru walikuwa Wachaga kutoka Magharibi mwa Kilimanjaro,hii ni kutokana kuwa lugha ya Wameru na Wachaga wa magharibi mwa Kilimanjaro inafanana kiisimu kwa sehemu kubwa. Katika karne ya 17 baada ya Wachaga kuongezeka nakuwa na uhaba wa ardhi walianza kuelekea upande wa mlima Meru kupitia pori la Sanya wakaweka makazi yao katika eneo la mlima Meru.

Spear (1997) anasisitiza kuwa ushahidi wa kihistoria unaodai kuwa Wameru walitokea Usambaani na wa kiisimu unaodai kuwa Wameru wametokana na Wachaga (Wamachame na Wasiha) unaleta mgongano wa kutokubaliana kuhusu asili ya Wameru. Lakini ukweli ni kwamba lugha ya Kimeru inafanana sana kiisimu na lahaja za Kichaga ambazo ni Kimachame na Kisiha; wakati Kimeru hakina ufanano wa karibu kabisa na Kisambaa; kwa maneno mengine hakuna ushahidi wa kiisimu wa kina kutoka Kisambaa unaojidhihirisha katika lugha ya Kimeru. Kitu kikubwa ni kwamba Wameru walijitenga na ndugu zao Wachaga wakiwa kama kundi dogo ili wapate ardhi ya kutosha na wajitawale wenyewe baada ya vita kutokea miongoni mwao.Watu hao walielekea sehemu ya mlima Meru au vilima vilivyo karibu na mlima Meru ili kuishi huko wakiamini kuwa hakutakuwa na wanyama wakali lakini pia waliamini kuwa ingekuwa rahisi kwao kuwasiliana kwa njia ya kuwasha moto ambao ungetoa moshi ili kujua kuwa ndugu anayeishi kwenye kilima kingine yuko hai. Kwahiyo, jina la *N'rwa* limetokana na neno ro/rwa ambalo katika lugha ya Kimeru ni kitendo cha kuelekea kaskazini au mlimani. Hivyo *N'rwa* ni mpandaji yaani mtu anayeelekea kaskazini au kupanda mlimani; mtu anayeelekea kaskazini au kilimani mara kwa mara katika lugha ya Kimeru huitwa *Meero/Meerwa*.Wamisionari wa kwanza ambao walikuwa Wajerumani walipofika katika eneo la Meru walishindwa kutamka*Meero/Meerwa*, badala yake wakatamka *Meru* na huo ndio ukawa mwanzo wa jina la Meru. Aidha jamii ya Wameru inaonekana imeundwa nakoo zilizotokana na sababu tofauti tofauti.

1.2 MAJINA YA KOO

Kivenule (2013) anaeleza kuwa ukoo ni muungano wa familia kadhaa zenye utambulisho fulani ambao unaweza kuwa utambulisho wa alama, jina au mwelekeo mmoja. Lakini mara nyingi utambulisho ambao huufanya muungano wa familia utambulike kama ukoo baina ya jamii za Kiafrika ni jina, na jina hilo huwa na maana na sababu ambazo huhusishwa moja kwa moja na kile kilichofanywa na mwanzilishi wa ukoo husika.Kwa hiyojamii hufanya mchakato wa utoaji majina kwa kutumia lugha yao ambayo huwafanya waweze kubainisha maana za majina hayo.Joho (2011) anaeleza kuwa utoaji wa majina ni tukio la kijamii na kiutamaduni lenye kuonesha sababu na historia ya majinaambazo hufahamika na jamii husika kutokana na kutumia lugha yao.

Maelezo ya Joho (2011) na Kivenule (2013) yanathibitishwa na jamii zilizochunguzwa kuhusu majina mbalimbali waliyoyatoa.Mathalan, Hassan (2017) alichunguza fasili ya majina ya mitaa ya mjini Unguja, lengo mojawapo katika utafiti wake lilibaini kuwa majina ya miji mingi ya Unguja yametokana na majina ya miti iliyopo kwenye maeneo hayo ambapo mti wa mwembe ndio uliozaa majina mengi kutokana na shughuli zilizofanywa katika eneo hilo la miembe. Mtaa wa Mwembeshauri ulipewa jina hilo kutokana na Waafrika kutoka sehemu mbalimbali kukusanyika hapo ili kushauriana na kujadiliana mambo ya kisiasa katika harakati za kudai uhuru. Vilevile, mtaa waMwembemimba ulipewa jina hilo kwa sababu wajawazito waliwekwa hapo chini ya mwembe kusubiri gari la wagonjwa la kuwapeleka hospitali ya Mnazi mmoja kwa ajili ya kujifungua. Pia Rashid (2017) alichunguza michakato na mbinu zilizotumika katika uundaji wa majina ya mitaa katika wilaya ya mjini Unguja na kubaini kuwa mtaa wa Kisiwandui ulipewa jina hili kwa

sababu ya shughuli za kijamii za kuhifadhi wagonjwa wa ndui katika sehemu hiyo ili wachukuliwe kupelekwa hospitalini.Mji wa Mwembetanga ulipewa jina hili kwa sababu ya kujihusisha na ushonaji wa matanga kwa ajili ya shughuli za uvuvi.Tafiti hizizilionesha kuwa jamii zilikuwa na maarifa yanayohusu sababu za kutoa majina hayo.

Tafiti zingine zilichunguza majina mahususi ya watukwa mfano,Anusa (2016)alichunguza vigezo kadhaa ambavyo Wayao huvitumia kuwapa watu majina, na hata baadhi ya watu huvitumia kujipa majina. Vigezo alivyobainishani tabia au sifa aliyonayo mtu, hisia za wazazi na imani katika jamii, hali au mazingira, kazi aliyonayo mtu, matukio, maumbile au rangi ya mwili, wakati na mahali. Pia Resani (2016) alichunguza majina ya Wabena nchini Tanzania,utafiti ulibainisha majina kama*Twihuvila* ambalo maana yake ni tunamtegemea. Sababu za mtu huyu kupewa jina hili ni kutokana na bidii ya kufanya kazi, hatimaye kuwa tegemeo katika familia. Kwa upande mwingine, watu wenye tabia zenye kurudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi katika jamii ya Wabena hupewa majina kama vile *Muhemedzi* ambalo lina maana ya mtu mwenye tabia ya kuombaomba, sababu ya kupewa jina hili ni kutokana na tabia yake ya kuombaomba, hivyo hutambulishwakwa jamii kuwa ni mvivu.

Aidha Nchimbi(2017) alichunguza tafsiri za majina ya Kibantu na kubaini kuwa baadhi ya majina ya Kibantu yalitolewa kwa sababu ya changamoto za uzazi, kwa mfano katika jamii ya Wanyamwezi mtoto wa kike au wa kiume akizaliwa kwa kutanguliza miguu huitwa *Kashindye* na kwa Wasukuma huitwa *Kashinje*. Kwa upande wa Wabena jina la *Msigwa* hupewa mtoto wa Kiume likimaanisha aliyeachwa kutokana na kifo cha baba yake. Pia nchini Kenya jina la *Mbiti* hutolewa kwa mtoto likiashiria matumaini kidogo ya kuishi. Vilevile, nchini Nigeria mtoto wa kiume aliyezaliwa baada ya kifo cha baba yake huitwa *Babatunde* yaani baba karudi. Kwa ujumla tafiti zinazohusu majina mahususi ya watu pia zimedhihirisha kuwa jamii zilizochunguzwa zina maarifa kuhusu maana na sababu za kutoa majina kwa jamii zao.

Uchunguzi wa Kivenule (2013) ulibaini kuwa zipo sababu za kihistoria za kupewa jina la ukoo huo kama anavyoeleza kuwa*Kivenule* ambalo lina maana ya ujasiri vitani lilitolewa kwa wahusika kwa sababu ya uwezo wa kutumia silaha za asili,na umaarufu wao katika upiganaji wa vita ndani ya himaya ya Wahehe. Vilevile, Kalekwa (2018) alichunguza majina ya koo za Wasukuma na kubaini kuwa majina ya koo yalisababishwa na matendo yanayokubalika na yasiyokubalika katika jamii ya Wasukuma.Kwa mfano *Nimi*alipewa jina hilo kwa sababu ya kuwa mkulima hodari na *Kitwanga* alikuwa na mazoea ya kutwanga. Kwa upande mwingine *Mayunga* alipewa jina hilo kwa sababu ya kupenda kuzurura.

Kwa upande mwingine Spear (1997) alipochunguza kuhusu historia ya jamii ya Wameru alibaini kuwepo kwa tatizo la Wameru wengi la kutokuwa na maarifa yanayohusu sababu za kupewa majina ya koo zao. Pia swali linalohusu sababu za kutoa majina linaulizwa na Mutembei (2009) kuwa kwa nini watu hutoa majina ya mahali, matukio, watu au vitu? Matokeo ya utafiti wa Spear (1997) na swali la Mutembei (2009) yamewafanya watafiti waonekuwa ni muhimu kubainisha majina ya koo, na kuchunguza sababu za kutoa majina hayo katika jamii ya Wameru Makala hii inasaidia jamii ya Wamerukupata maarifa yanayohusu sababu hizo kwani wasipozifahamu watapoteza asili, utamaduni na historia ya majina yao ya koo.

2.0 MBINU ZA UTAFITI

Makala hii inatokana na utafiti wa uwandani ambao umechunguza sababu za kutoa baadhi ya majina ya koo katika jamii ya Wameru. Uchaguzi wa mbinu za utafiti umeongozwa na mada na malengo ya utafiti. Mbinu hizo ni pamoja na mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, eneo, mchakato wa usampulishaji na sampuli, mbinu za ukusanyaji data, uzingatiaji wa itikeli na namna data zilivyochanganuliwa.

2.1 MKABALA WA UTAFITI

Makala hii imetumia mkabala wa kimaelezo kukusanya, kuwasilisha na kuchanganua taarifa. Sababu ya kutumia mkabala huu nikwamba taarifa zilizohitajika zinahusu historia ya jamii ambayo ilipatikana kwa njia ya maelezo. Mligo (2016) anaeleza kuwa kama utafiti unalenga kutafsiri maana ya jambo fulani katika jamii utafiti huo huwa wa kimaelezo. Sambamba na hayo, Bryman (2012) anasema utafiti unaohusiana na historia ya maisha ya watu huhitaji kukusanya taarifa kwa kupata maelezo kutoka kwa watoataarifa.

2.2 USANIFU WA UTAFITI

Utafiti huu ni wa kifani kwa sababu umechunguza jamii moja katika eneo moja maalumu, pia ni jambo moja tu lililochunguzwa ambalo ni majina ya koo. Pia ni utafiti wa kifani kwa kuwa ulilenga kupata maarifa ya kina kuhusu utoaji wa majina ya koo za Wameru.Mligo (2016) anasisitiza kuwa usanifu wa kifani huhusika na kupata maarifa ya kina kuhusu fenomena moja. Taarifa za utafiti zilipatikana kwa kuzikusanya kutoka uwandani, zikawasilishwa kisha zikachanganuliwa. Baadaye taarifa hizo zilijadiliwa na mwisho ziliwekwa katika muhtasari na kutolewa mapendekezo.

2.3 ENEO LA UTAFITI

Taarifa zilikusanywa kutoka wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha katika jamii ya Wameru. Sababu za kuchagua eneo hili ni kwamba ndilo eneo kuu zinapopatikana koo zote za jamii ya Wameru. Utafiti ulifanyika katika eneo zima la wilaya ya Arumeru kutokana na koo za jamii ya Wameru kutawanyika katika wilaya nzima. Sababu ya mtawanyiko huu ni kwamba jamii ya Wameru imeundwa na makabila mbalimbali ambapo waanzilishi wa koo hizi walipofika katika eneo la Arumeru walifikia sehemu tofautitofauti ndani ya eneo la Arumeru ili kupata maeneo ya kufugia na kulima. Spear (1997) anaeleza kuwa wakati Wameru walipohamia katika eneo la mlima Meru kila mwanzilishi wa ukoo wa Wameru alifikia eneo tofauti na mwanzilishi wa ukoo mwingine ili kuwa na eneo la kumtosha kwa shughuli mbalimbali.

Kwa upande mwingine eneo hili limechaguliwa kutokana na wanajamii wake kuwa ni watu wasiopenda kuhamahama wala kuchangamana na makabila mengine na kama wakichangamana ni kwa kiasi kidogo sana hivyo kusababisha kuwepo Wameru ambao wameweza kuitunza asili na historia ya kabila lao. Kutochangamana kwa Wameru na jamii zingine kunatokana na kujishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo yao ya urithi ambayo kwa uzoefu hayauzwi wala kutolewa kwa wageni, hata yakiuzwa ni kwa kiasi kidogo hasa sehemu ambazo zinapakana na miji. Kwa hiyo sababu hizo zilizobainishwa zimefanya eneo hili liwe na sifa zote za kuwa na taarifa zilizohitajika kulingana na malengo ya makala hii.

2.4 SAMPULI NA USAMPULISHAJI

Sampuli ya utafiti huu ilikuwa wazee 17 wa jamii ya Wameru walio na umri wa miaka kuanzia 65 na kuendelea ambao ni wanawake na wanaume. Watafiti waliwachagua kama wawakilishi kutoka katika kundi kubwa ambalo ni jamii ya Wameru. Katika jamii ya Wameru neno wazee hueleweka kuwa ni wanaume tu. Lakini katika makala hii kigezo kilichoangaliwa kwa sampuli husika ni umri na si jinsia kwani kuwa na maarifa kuhusu majina ya koo hakuhusiani na kuwa ama mwanamke au mwanaume ila kitu cha muhimu ni maarifa aliyonayo mtoataarifa. Sababu za kupendelea umri huu ni kwamba hawa ni watu ambao wana tajiriba na uzoefu mkubwa wa maisha ikiwemo kuwa na uelewa kuhusiana na historia ya koo za jamii ya Wameru.

Usampulishaji lengwa na tajwa ndio uliotumiwa kuwapata watoataarifa kutoka kwenye jamii ya Wameru. Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza kuwa usampulishaji ni

mchakato wa kuchagua vitafitiwa kutoka kwenye kundi kubwa kwa namna ambayo vitafitiwa hivyo vitaweza kuliwakilisha kundi kubwa.

Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa kuwachagua*Washili*7 ili kutoa taarifa za koo zao. Sababu ya kutumia usampulishaji lengwa ilikuwa kuwapata viongozi wa koo kwani kigezo kimojawapo cha kupewa cheo cha *Ushili* ni uwezo wa kuwa na taarifa nyingi kuhusu koo zao.Mugenda na Mugenda (2003) wanafafanua kuwa usampulishaji lengwa ni mbinu inayomruhusu mtafiti kutumia watoataarifa anaofahamu kuwa wana taarifa zinazotakiwa kulingana na malengo ya utafiti wake. Usampulishaji lengwa pia ulitumika kuchagua eneo, nawango la utafiti.

Ponera (2019) anaeleza kuwa mbinu ya usampulishaji tajwa humtaka mtafiti kuwa na utambuzi juu ya mtu mmoja au wawili wanaofaa kutoa taarifa kulingana na mada husika. Kisha mtu au watu hao humwelekeza mtafiti kwa mtu mwingine anayefaa kwa ajili ya kuendelea kupata taarifa zaidi. Kwa ujumla mbinu ya usampulishaji tajwa inafaa pale ambapo wango la utafiti lenye taarifa zinazohusiana na utafiti halifahamiki.

Usampulishaji tajwa ulitumiwa kuwachagua watoataarifa 10 waliokuwa na taarifa za kukamilisha taarifa pale ambapo viongozi wa koo hawakutosheleza taarifa zilizohitajika. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba upo uwezekano mkubwa wa kuwa na watu katika jamii ambao si viongozi wa koo lakini kutokana na tajiriba ya maisha yao wana taarifa nyingi kuhusu koo zao, na jamii inawafahamu. Kwa hiyo, mtoataarifa wa kwanza alipatikana kwa njia ya usampulishaji lengwa ambao ulitumika mara moja tu kumpata, baada ya mtoataarifa huyo kuhojiwa alimtaja mtu mwingine mwenye taarifa zilizohitajika, mbinu ya kutajana ndiyo iliyoendelea kutumiwa mpaka watafiti walipokamilisha kukusanya taarifa walizozihitaji.

2.5 MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

Data za makala hii zimekusanywa kwambinu ya usaili na usimulizi.

2.5.1 Njia ya Usaili

Katika kukusanya taarifa,watafiti walifanya usaili wa ana kwa ana na watoataarifa. Watafiti walitumia mwongozo wa usaili wenye maswali funge yaliyowawezesha kupata majina ya koo za jamii ya Wameru. Pia watafiti walitumia maswali huru ili kupata taarifa kuhusu sababu za utoaji wa majina ya koo za jamii ya Wameru. Mahojiano yalifanywa baada ya kusikiliza simulizi kuhusu sababu za kutoa majina ya koo za Wameru ili kukamilisha taarifa ambazo zilikuwa hazijatosheleza mahitaji ya lengo la makala hii. Watafiti walitumia mwongozo wa maswali kuwahoji watoataarifa huku wakisisikiliza na kuandika kile kilichokuwa kikielezwa na watoataarifa wao. Sababu za kutumia njia ya usaili ni kutokana na ufaafu wake kwa mtoataarifa anayejua na asiyejua kusoma wala kuandika, na inarahisisha kupata taarifa nyingi kwa muda mfupi. Pia, ni rahisi kwa mtoataarifa kufafanuliwa na kueleweshwa swali pale ambapo hakuelewa. Vilevile, kwa ufahamu wa watafiti watu wenye umri wa miaka 65 na zaidi hupenda kuzungumza zaidi kuliko kuandika, hivyo watoataarifa walipohojiwa walikuwa huru zaidi kutoa taarifa zilizotakiwa.

2.5.2 Njia ya Usimulizi

Njia ya usimulizi ilitumika kukusanya taarifa kuhusu sababu za utoaji wa majina ya koo katika jamii ya Wameru ambapo watafiti waliandaa mwongozo uliowataka watoataarifa kutoa historia inayohusu sababu za kutoa majina ya koo za Wameru. Kabla ya kuanza kukusanya taarifa watafiti waliwaeleza watoataarifa kuwa taarifa zinazokusanywa ni kwa matumizi ya utafiti wa kitaaluma. Pia waliwaeleza kuwa watarekodiwa kwa kinasa sauti lakini kutakuwa na usiri wa rekodi hizo. Kwa hiyo watafiti walisikiliza simulizi na kurekodi

taarifa hizo.Sababu ya kutumia njia hii ni kwamba inamruhusu mtoataarifa kutoa taarifa kwa kina kulingana na tajiriba yake ya maisha. Kwahiyo, njia ya usimulizi ilikuwa muafaka kwani watafiti waliweza kupata taarifa nyingi na sahihi kulingana na mahitaji ya malengo ya makala hii.

2.6 UCHANGANUZI WA DATA

Mligo (2012) na Bryman (2012) wanaeleza kuwa, baada ya kumaliza mahojiano au simulizi na wahojiwa mtafiti huwa na habari zilizorekodiwa katika mazungumzo ambayo si rahisi kueleweka na mtu mwingine isipokuwa mtafiti na wahojiwa/wasimulizi tu.Kwa hiyo, ili kuwa na taarifa zenye maana kulingana na malengo ya makalawatafiti walifanya yafuatayo: Walisikiliza rekodi ya simulizi na usaili kwa kurudiarudia kwa makini, baadaye wakapunguza taarifa zisizohusiana na malengo ya makala na kubakia na taarifa chache zinazohusiana namajina ya koo na sababu za utoaji wa majina hayo katika jamii ya Wameru, halafu wakapanga taarifa katika makundi na kuyapa misimbo, mwisho waliunganisha datazinazofanana au kukaribiana ili kupata dhamira.

Data za utafiti zilifafanuliwa kwa mbinu ya kimuktadhana usimulizi. Kimuktadha, ufafanuziulizingatia mazingira ya watoataarifa ambao ni Wameru ili kuhakikisha kuwa maelezo yaliyotolewa yanaendana na kile kilichosimuliwa na jamii hiyo. Watafiti walifanya hivyo ili Wameru waweze kuelewa taarifa hizo kirahisi na waweze kuzitumia baadaye kwa vizazi vijavyo. Hivyo, idadi ya majina ya koo za Kimeru yalibainishwa, nasababu za utoaji wa majina hayo zikafafanuliwa kwa uwazi.

2.5 ITIKELI

Katika makala hii Watafiti walizingatia itikeli kama ifuatavyo: kwanza, watafiti walipata barua kutoka chuoni iliyowatambulisha kwa mamlaka husika katika eneo walilofanyia utafiti. Pili, watafiti waliwaeleza watoataarifa sababu za kufanya utafiti na kuyaweka wazi malengo ya utafiti. Tatu, watafiti walitunza siri za utafiti kutoka kwa watoataarifa na walizitumia katika masuala ya kitaaluma tu. Vilevile watafiti walishirikiana kwa karibu sana na wale wote waliowezesha kukamilika kwa makala hii ikiwa ni pamoja na kutumia lugha inayostahili kulingana na utamaduni wa kundi husika.

3.0 MATOKEO YA UTAFITI

3.1 MAJINA YA KOO KATIKA JAMII YA WAMERU

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa majina ya koo za Wameru jumla yapo 26. Majina hayo ni Akyoo, Ayo, Isangya, Kaaya, Kimuto, Kitali, Kitomari, Kyungai, Mafie, Mandola, Manang, Maturo, Mungure, Mbise, Nanyaro, Nassari, Ndosi, Ngira, Nyari, Nyiti,Pallangyo, Sarakikya, Sikawa, Sumari, Urio na Vanika. Utafiti umebaini sababu kadhaa zilizotumika kutoa majina hayo kama zilivyowasilishwa na kuchambuliwa katika sehemu ya 3.2.

3.2 Sababu Zilizotumiwa Kutoa Majina ya Koo za Jamii ya Wameru

Majina ya koo katika jamii ya Wameru yana historia inayotokana na waanzilishi wake. Kila jina la ukoo linahusishwa na historia ya kile kilichofanywa na mwanzilishi wa ukoo husika, hivyo historia hiyo ndiyo inayochukuliwa kama sababuza kutolewa kwa jina la ukoo husika.Baadhi ya sababu zilizobainishwa kuwa zilitumiwa kutoa majina ya kooza jamii ya Wameru ni pamoja na jitihada katika kazi, matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya kivita, tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama.

3.2.1 Majina ya Koo Yaliyotokana na Jitihada katika Kazi

Jitihada ni nguvu ya ziada ambayo mtu huongeza kwenye kazi ambayo anaifanya ili aweze kufikia malengo yake kama alivyopanga. Kuhusiana na utoaji wa majina ya koo mwanzilishi wa ukoo ndiye aliyeonesha jitihada hiyo hadi kupewa jina la ukoo wake. Utafiti unaonesha kuwa ukoo wa*Kitomari* ulipewa jina hilo baada ya mwanzilishi wa ukoo huo kuamua kujitenga na ndugu zake akaenda kuanzisha maisha yake sehemu nyingine. Mtoataarifa mmoja alisimulia kuwa;

> *"Sababu za mwanzilishi wa ukoo wa Kitomari kupewa jina hilo ni jitihada aliyokuwa nayo katika kazi baada ya kufanya maamuzi ya kwenda kuanzisha makazi yake sehemu nyingine na kujitegemea.Mwanzilishi wa ukoo huo alijibidisha na kuyamudu maisha, na baadaye akaanzisha familia yake ambayo aliweza kuiendeleza, ndipo baadaye akaitwa Kitomari jina hili likimaanisha mtu mwenye jitihada."*

Hata hivyo katika mahojiano katibu wa ukoo alieleza kuwa neno jitihada katika lugha ya Kimeru ni *utomari*lakini mwanzilishi wa ukoo huo hakuitwa *utomari* kwanibaadhi ya wanajamii walimdharau hivyo wakamwita ***Ki****-tomari*.Kwa hiyo ***Ki-***ilitumiwa kuonesha dharau yaani mwanzilishi huyo alishushwa thamani na kuonekana ni *kimtu*yaani asiyekuwa na maana. Pamoja na kumwona ni mtu duni bado wengi wa wanajamii walimwona kuwa ana jitihada, kwa hiyo akaitwa *Kitomari*.

3.2.2 Majina ya Koo Yaliyotokana na Matendo ya Kihistoria

Haya ni matendo ambayo yalifanywa na waanzilishi wa koo husika hivyo yamebeba historia ya koo hizo. Matendo hayo ni kama vile kutembea sana, kukataa kutii maelekezo na kukataa kurejea nyumbani kwa wazazi kusaidia majukumu mbalimbali. Kwa hiyo majina waliyopewa waanzilishi wa koo yalitokana na matendo waliyoyatenda. Koo hizo ni*Kaaya; Kulleiye, Kyuta, Nsaiya na Nyiti*.

Makala hii inaonesha kuwa sababu ya Kaaya kupewa jina hilo ni kutokana na mwanzilishi wa ukoo huo aliyeitwa Kisarika kuwa na tabia ya kuondoka na kurudi katika jamii ya Wameru bila kujulikana alikokuwa anakwenda. Mtoataarifa mmoja alisimulia kuwa;

> *"Kisarika alikuwa na kawaida ya kuondoka katika jamii ya Wameru na kurudi katika mazingira ya kutatanisha ambayo yaliwafanya watu waone kama anatumia nguvu za kichawi. Pamoja na kuondoka na kurudi kwa mazingira ya kutatanisha kila aliporudi aliwaletea Wameru mbegu za kahawa, kunde, migomba na ulezi. Lakini kutokana na kuogopa tabia yake ya kuondokaondoka aliambiwa kaa iyya yaani kaa hapa naye alitulia sehemu moja bila kuondoka tena."*

Mshili[8] wa ukoo wa *Kaaya* alieleza kuwa kila mara *Kisarika* alipotaka kuondoka wenyeji walimzuia wakimwambia *kaa iyya*'kaa hapa'. Kwakuwa alitii, wenyeji walimpa makazi yake katika eneo liitwalo Akeriili asiondoke tena. Kuanzia hapo akaitwa *Kaa iyya*jina hililikimaanisha kaa hapalakini baadaye jina hilo lilibadilika kimatamshi na kuwa *Kaaya*. Kwa hiyo sababu ya kupewa jina la *Kaaya* ni matendo ya mwanzilishi wa ukoohuo ya kuondoka mara kwa mara na kurudi baadaye, hivyo, akazuiwa kwa kuambiwa *kaa iyya* ili asiondoke tena.

Aidha, *Mshili* wa ukoo wa *Kaaya* aliongezakuwa ukoo wa *Kaaya* ulizaakoo ndogo tatu ambazo zilitokana na watoto watatu wa kiume wa mwanzilishi wa ukoo huo kutokana na matendo yao. Data inaonesha kuwa katika maisha ya kawaida vijana hao walipangiwa majukumu na baba yao ili waweze kuendesha maisha lakini kila mtoto alikuwa na mwitikio tofauti ambao ulikuwa chanzo cha jina la ukoo mdogo katika ukoo wa *Kaaya*. Mtoto wa kwanza alipopangiwa jukumu alijibu kuwa anaondoka na atakwenda kujitegemea wala hatarudi tena hapo nyumbani, katika Kimeru alisema *nkeenda kake niuyaa n'ndi*

[8]*Mshili*nineno la Kimerulenyemaanayakiongoziwaukoo.

n'ndekyutaa shimuni akaitwa *Kyuta*. Mtoto wa pili naye alipotumwa akasema nimekataa, katika lugha ya Kimeru alisema *nalleya* akaitwa *Kuleiye* na mtoto watatu alimwambia baba yake kuwa nitabaki na wewe hapa yaani *nsaa iyya*akaitwa *Nsaiya*. Hivyo mwitikio wa kila mtoto ukaanzisha ukoo mdogo wa *Kaaya*, koo hizo ni*, Kaaya-Kuleiye, Kaaya-Kyuta* na *Kaaya-Nsaiya*.

Mshili aliongeza kuwa familia zilizo katika aina hizo tatu za koo zimekuwa na tabia zile zile zilizosababisha waanzilishi wa koo zao kupewa majina ya*Kuleiye,Kyuta* na *Nsaiya*. *Mshili* alitoa mfano kuwa wanapokuwa katika vikao vya ukoo kiongozi wa familia ya *Kuleiye* ana kawaida ya kuamua kupinga na kuikataa hoja fulani lakini anapoulizwa sababu anasisitiza tu kuwa amekataa wala hatoi sababu.

Ukoo wa*Nnyiti*pia ulipewa jina hilo kwa sababu ya matendo ya mwanzilishi wa ukoo wao. Mtoataarifa mmoja alisimulia kuwa;

> *"Jina la Nnyiti lilitolewa baada ya Nnyiti kumgomea kaka yake aliyeitwa Nnko kushiriki kutafuta nguvu za ziada za kupata mifugo.Nnko alitaka aende msituni na Nnyiti kutafuta 'mtoto wa shetani' ili awalinde pamoja na kuiongeza mifugo yao lakini Nnyiti alikataa na kuweka msimamo wa kutokwenda, ndipo Nnyitiakamwambia kaka yake kuliko kushiriki kitendo hicho ni bora ahame eneo hilo. Kwa hiyo, Nnyiti aliamua kuondoka kuelekea eneo liitwalo Sura upande wa Ushili na kuanzisha makao yake hapo."*

Katika mahojiano mtoataarifa mwingine alieleza kuwa;

> *"Katika lugha ya Kimeru kitendo cha mtu kukataa au kugoma kufanya jambo fulani aliloagizwa kinaitwa 'nyita' na mtu mwenye tabia hiyo ya kugoma huitwa Nnyiti. Kwa hiyo kutokana na kugoma kumchukua shetani wa kuwasaidia kulinda na kuiongeza mifugo yao, mwanzilishi huyo wa ukoo alipewa jina la Nnyiti yaani mtu aliyekataa."*

Matokeo haya yana maana kuwa katika jamii watu hutenda matendo mbalimbali, matendo hayo yanaweza kuwa mazuri au mabaya, matendo mazuri yana faida zake na matendo mabaya yana hasara zake. Kwa mfano *Kisarika*alipoambiwa *kaa iyya*(kaa hapa)alikuwa mtii hatimaye akapewa eneo la kuishi nacheo cha kuwa kiongozi wa ukoo lakini*Kulleiye, Kyuta* na *Nnyiti*walipokataa kutii yale waliyoambiwa waliishia kufarakana na ndugu zao, na kwenda kutafuta eneo jingine la kuishi.

3.2.3 Majina ya Koo Yaliyotokana na Matukio ya Kipekee

Matukio mbalimbali katika jamii huweza kutumika kutoa majina kwa watoto wanaozaliwa kipindi hicho, lakini pia watu wazima huweza kupewa majina yanayotokana na matukio hayo. Katika jamii ya Wameru majina waliyopewa waanzilishi wa koo za *Ayo* na *Mungure* yalitokana na matukio yasiyo ya kawaida katika utamaduni wao kama vile mazoea ya kufanya jambo fulani kwa kurudia rudia, na mwanaume kuonyesha woga.

Ukoo wa*Ayo* ulipata jina hilo kutokana na tukio ambalo halikuwa la kawaida katika jamii ya Wameru lililofanywa na msichana. Jina la ukoo wa*Ayo* lilipewa Wameru ambao kwa asili walikuwa Wanandi kutoka Kenya. *Mshili*wa ukoo alisimulia kuwa;

> *"Sababu za kupewa jina la ukoo waAyo ni kutokana na msichana aliyempenda mwanaume mmoja katika familia ya mwanzilishi wa ukoo huo na kujenga mazoea ya kumtembelea mara kwa mara baada ya kushindwa kuficha upendo aliokuwa nao kwake. Tukio lile halikuwa la kawaida katika mila na utamaduni wa Wameru. Kwa hiyo watu walipomwona yule msichana akipita kwenda kumtembelea mpenzi wake walisema ayo sambura illya yaani msichana ndiye huyo, wakimaanisha kuwa msichana ambaye habari zake zimeshangaza watu ndiye huyo anayepita. Hivyo, kila mara walipomwona yule msichana anapita mwanzilishi wa ukoo huo mzee Lumbuwa na familia yake walisema ayo sambura ilya, neno ayo likimaanisha huyo, kwa hiyo wakapewa jina la Ayo."*

Pia katika mahojiano watoataarifa walieleza kuwa kwa kipindi hicho kulikuwa na uvamizi wa mara kwa mara wa Wamasai na Wakibosho ambao walikuwa wakiiba mifugo ya Wameru. Data ilionesha kuwa kutokana na mwanzilishi wa ukoo wa *Ayo*kuwa mwogakila aliposikia kelele kutoka mashariki au magharibi alipiga kelele ya kuashiria kuwa vita imeanza huku akisema *ayo firra* akimaanisha kuwa vita imeanza hivyo watu wawe tayari. Katika jamii ya Wameru ni fedheha kubwa kama mwanaume ataonesha woga hata kama kuna kitisho kikubwa. Kwa hiyo kutokana na tukio hilo la aibu la kupiga kelele za woga akaitwa *Ayo*, jina hilo lilikua hadi kufikia kuwa jina la ukoo wao.

Ukoo mwingine uliotokana na matukio ya kipekee niukoo wa *Mungure* ambao *Mshili* wake alieleza kuwa ukoo wa *Mungure* ulipewa jina hilo kutokana na vijana wa kiume kula ukoko baada ya kutoka kuchunga mifugo na kukosa chakula. Tukio hilo lilishangaza kwani kwa utamaduni wa Wameru wanaume hawaruhusiwi kula ukoko isipokuwa wanawake na watoto. *Mshili* alieleza zaidi kuwa zamani katika jamii ya Wameru vijana walikuwa wakichunga mifugo kwa pamoja kutokana na hofu ya wanyama wakali pamoja na wezi wa mifugo. Kutokana na kuchunga pamoja chakula chao pia kilipikiwa sehemu moja, hivyo, walipaswa kurudisha mifugo kwa wakati mmoja katika eneo lililokuwa limetengwa ili waweze kula pamoja. Endapo mtu alichelewa kurudisha mifugo kwa wakati, chakula chote kililiwa.

Katika mahojiano watoataarifa walifafanua kuwa siku ambayo jina la *Mungure* lilianza ni kwamba vijana wa familia hiyo walipotoka kuchunga mifugo walikuta wenzao wameshakula chakula chote na ukoko pekee ndio ulikuwa umebaki. Ukoko katika lugha ya Kimeru huitwa *makure* lakini kama ukoko huo umezidi weusi huitwa *mun'kure*. Vijana wa ukoo huo walianza kuitwa *Mun'kure*mara tu baada ya kula ukoko. Jina hilo liliendelea kukua na hatimaye likawa jina la ukoo wao ambalo baadaye lilibadilika na kuwa *Mungure*. Mtoataarifa mmoja aliongeza kuwa inasadikika kwamba watu wa ukoo wa *Mungure* ni weusi sana kutokana na waanzilishi wa ukoo huo kula ukoko uliokuwa umeungua sana.

Kwa hiyo matukio ambayo waanzilishi walifanya yalitumiwa kutolea majina ya ukoo ili kuwafundisha watu na kuwaonya wasiendelee kufanya matendo ya aibu katika jamii zao ambayo hayaendani na utamaduni wa jamii. Kwa mfano kitendo cha msichana kumpenda na kumfuata mwanaume nyumbani kwake na kitendo cha wanaume kula ukoko ni vitendo visivyokubalika katika utamaduni wa Wameru.

3.2.4 Majina ya Koo Yaliyotokana na Mazingira ya Kivita

Vita hutokea katika jamii mbalimbali duniani na vita hivyo huweza kusababisha mambo mbalimbali kama vile maafa. Mazingira hayo huweza kutumiwa na jamii kuwapa watu majina yanayohusiana na vita. Katika jamii ya Wameru ukoo wa*Mbise* ulipewa jina hilo kutokana na mazingira ya vita.

Utafiti unaonesha kuwa *Mbise* ndio ukoo wa kwanza kuanzishwa katika jamii ya Wameru. Ukoo huu ulitokana na mwanzilishi wake aliyeitwa *Lamireny* ambaye alikwenda kuishi katika msitu wa mlima Meru kutokana na uvamizi wa Wakibosho na Wamasai waliokuwa wakiiba mifugo ya Wameru. Jina la ukoo wa *Mbise* lilitokana na neno la Kimeru *n'bvise* au *kubvise* yenye maana ya mfiche au jifiche.

Watoataarifa walieleza kwamba sababu za kuitwa *Mbise* ni kwamba baada ya Wakibosho na Wamasai kuanza kuwavamia na kuwaua Wameru ili wachukue mifugo yao *Lamireny*ambaye ni mwanzilishi wa ukoo huo na familia yake walikwenda kujificha kwenye msitu wa mlima Meru ili aweze kupambana na adui zake huku familia yake ikiwa salama. Aidha mwanzilishi huyo wa ukoo alikuwa akishuka kutoka msituni kwenda kupambana na adui zake na kurudi kujificha. Hivyo, alipokuwa akitafutwa na adui zake watu walimwambia '*kubvise*' wakimaanisha jifiche na wengine waliwaambia ndugu zake '*n'bvisen*' wakimaanisha mficheni. Baada ya kuyatumia sana hayo maneno watu wakampa jina la *N'bvisen*. Kadri siku zilivyokwenda jina la *N'bvise*n lilikua mpaka kufikia kuwa jina laola

ukoo. Kwa hiyo mbali nauwepo wa vita, mbinu aliyoitumia mwanzilishi wa ukoo huo katika kuwalinda watu wake ilimpa heshima kubwa ndiyo maana mbinu hiyo ikazaa jina la ukoo wa *Mbise*.

3.2.5 Majina ya Koo Yaliyotokana na Tabia ya Mtu Binafsi

Katika jamii wapo watu wenye tabia zinazokubalika na zisizokubalika na jamii,kwa hiyo watu hao huweza kupewa majina yanayorejelea tabia zao ili kufundisha au kuonya watu wengine katika jamii. Utafiti unaonesha kuwa tabia zilizosababisha majina ya koo katika jamii ya Wameru ni ubinafsi/uchoyo aliokuwa nao mwanzilishi wa ukoo wa *Akyoo,* na ukarimu waliokuwa nao waanzilishi wa koo za*Nnko* na *Pallangyo*.

*Mshili*wa ukoo wa *Akyoo* alieleza kuwa ukoo huu una asili ya Wasonjo ambao walitokea Arusha Chini wakiwa kundi dogo na kufika eneo la Meru. Kutokana na uchache waokiongozi wao aliomba na kukubaliwa kushirikiana na ukoo wa *Ayo* ili wasaidiane katika shughuli za kimila kama kulipa gharama za mtu aliyeuawa na mtu wa ukoo wake. Kiongozi huyo alikubaliwa kwa masharti kuwa *Ayo* atakuwa ndiye kaka na yeye atakuwa mdogo wake.

Watoataarifa walieleza kuwa sababu ya kupewa jina la *Akyoo* ni tabia ya uchoyo na ubinafsi aliyokuwa nayo mwanzilishi wa ukoo huo. Kwa kuwa *Akyoo* alipofika Meru alikuwa na baadhi ya mifugo, aliendelea kupata utajiri wa ng'ombe na kumfanya aheshimiwe zaidi kuliko *Ayo*ambaye alikuwa kaka yake. Utajiri huo wamifugo ulimfanya awe ndiye anapokea mahari zinazolipwa kwenye familia zao, lakini alianza kuwa na tamaa ya kumiliki mali yote ya mahari aliyopaswa kukabidhiwa*Ayo* ambaye ni baba wa msichana. Kwa kuwa jamii iliongozwa na mila, viongozi wa mila walimtaka *Akyoo* ampatie*Ayo*haki yake, ndipo kwa hasira *Akyoo* alitoa akisema *akyo* akimaanisha hicho/hiyo, kuanzia hapo mwanzilishi huyo akapewa jina la *akyo*kutokana na mazoea ya kutumia neno hilo kila alipolazimishwa kumpatia mtu haki yake. Kadri familia yake ilivyokua ndivyo jina lilikua na hatimaye likawa jina la ukoo ambalo baadaye lilibadilika matamshi na kuwa *Akyoo*.

Ukoo wa*Nnko* ulipata jina hilo kwa sababu ya tabia ya ukarimu wa mwanzilishi wa ukoo wao. Watoataarifa walisimulia kuwa *Nnko* ni jina la ukoo ambalo lilitokana na tabia ya ukarimu aliyokuwa nayo mwanzilishi wake, waliongeza kuwa baba wa mwanzilishi wa ukoo wa *Nnko* alikuwa ni Mmasai na mara kwa mara mwanzilishi huyo akiwa mtoto alimsikia baba yake akimwambia *ngo* wakati akimpatia kitu chochote akimaanisha chukua. Kutokana na ukarimu aliokuwa nao mtoto huyo kila walipofika wageni nyumbani kwao aliwapa vitu akisema *ngo* hivyo watu wakampa jina la *Ngo*. Kadri muda ulivyozidi kwenda jina hili lilifahamika na watu wengi.

Katika mahojiano *Mshili*wa ukoo wa *Nnko* alieleza kuwa baada ya kukua mwanzilishi wa ukoo huo alikwenda kuanzisha familia yake eneo linalosadikika kuwa ni kijiji cha Mulala huku akiendelea kuitwa *Ngo*, hivyo, yeye na familia yake wakatambulika kwa jina la *Ngo* na baadaye likawa jina la ukoo wao. Kwa hiyo mwanzilishi wa ukoo wa *Nnko* alipewa jina hilo kwa sababu ya ukarimu wa kuwapa watu vitu huku akiwaambia *ngo* lakini *Mshili* alieleza kuwa baadaye jina la *Ngo* lilibadilika na kuwa *Nnko*.

Katika mahojiano zaidi watoataarifa wa ukoo huu walieleza kuwa ukoo wa *Nnko* ulipewa jina hilo kwani kutokana na ukarimu wao kila ilipofika kipindi cha kwenda kuomba mvua mlima Meru, familia ya *Nnko* ambayo ilikuwa ikiishi eneo la kijiji cha Mulala kilichopo karibu kabisa na mlima Meru walijitolea kufyeka njia hiyo. Katika lugha ya Kimeru njia iliyofyekwa kwenye pori kwa lengo la kupitisha mifugo na watembea kwa miguu huitwa *nnko*. Lengo laolilikuwa kuweka mazingira rafiki ya kupita watu wa ukoo wa *Mbise* ambao kwa taratibu za Kimeru ndio huenda mlima Meru kuomba mvua wakati wa kiangazi sehemu alikozikwa mwanzilishi wa ukoo wao (mzee *Lamireny*) huku wakipeleka sadaka mbalimbali ambazo huwekwa katika jiwe kubwa lililopo karibu na kaburi lake. Waombaji hao hutakiwa kuwa na njia inayopitika ili wasisumbuke kupita. Kwa hiyo kutokana na kufyeka pori mara kwa mara ili njia ipatikane wakaitwa *Nnko*.

Ukoo wa*Pallangyo*pia walipewa jina hilo kwa sababu ya tabia ya ukarimu aliyokuwa nayo mzee*Lataiyo*ambaye ndiye mwanzilishi wake. Mzee *Lataiyo* aliishi katika eneo la Kilinga lililopo karibu na msitu wa hifadhi ya wanyama ya Arusha ambapo ipo njia inayokwenda mpaka mlima Meru, njia hiyo ndiyo iliyotumiwa na Wameru waliokwenda eneo la mlima Meru kuomba mvua pamoja na kuomba kuponywa magonjwa mbalimbali.*Mshili* wa ukoo wa *Pallangyo* alieleza kuwa sababu ya kupewa jina la *Pallangyo* ni tabia ya ukarimu iliyomfanya mwanzilishi wa ukoo huokuongeza maji kwenye vyakula vya kimiminika ili viweze kutosha watu waliokuwa wakifika nyumbani kwake kila mara walipokuwa wanakwenda mlima Meru kuomba mvua na kuponywa magonjwa.

Mshili alifafanua zaidi kuwa wakati watu wa ukoo wa *Mbise* walipokwenda kuomba mvua katika mlima Meru walipita na kupumzika kidogo nyumbani kwa mzee *Lataiyo* kwa vile palikuwa karibu na njia inayoelekea mlima Meru lakini kutokana na ukarimu wake, mzee *Lataiyo* alipenda sana kila mgeni anayefika kwake apate japo chakula kidogo. Utafiti unaonesha kuwa kwaWameru wakati huo vyakula ambavyo vilikuwa rahisi kuwa navyo nyumbani vikiwa tayari kwa kuliwa ni vya kimiminika kama maziwa ya mtindi, uji na *loshoro* ambacho ni chakula cha asili cha Wameru. Ili chakula hicho kiwatoshe wageni wote *Lataiyo* aliamua kukiongeza maji na matokeo yake kikawa chepesi sana ambacho katika lugha ya Kimeru hupewa sifa ya kuwa *ipala njwaa*ikimaanisha chakula chepesi cha kiminininika.

Mtoataarifa mmoja alisimulia kuwa;

> *"Watu waliokuwa wanakwenda kuomba mvua mlima Meru walikula chakula kwa mzee Lataiyo na waliporudi nyumbani walisimulia kuwa wamepewa chakula lakini kilikuwa ipala njwaa yaani chakula hicho kilizidishwa maji au kilikuwa chepesi sana. Matumizi ya neno hilo yaliendelea kwa muda mrefu ndipo mzee Lataiyo akapewa jina la Ipala njwaa na baadaye likakua hadi hatua ya kuwa jina la ukoo lakini lilibadilika na kuwa Pallangyo."*

Kwa ujumla tabia ya uchoyo na ya ukarimu zimetumiwa kutoa majina ya koo ili kuitunza historia ya kila ukoo lakini pia kufundisha jamii kuwa miongoni mwao wapo watu wenye tabia zisizokubalika kwa mfano uchoyo na ubinafsi aliokuwa nao *Akyoo*kwa upande mwingine tabia zinazokubalika kama ukarimu aliokuwa nao *Nnko* na *Pallangyo*.

3.2.6 Majina ya Koo Yaliyotokana na Sifa zaWanyama

Wanyama waishio porini ni wengi lakini katika makala hii mnyama aliyesababisha jina la ukoo ni nyani ambaye katika lugha ya Kimeru huitwa *ifie* akiwa mmoja na *mafie* wakiwa wengi. Utafiti unaonesha kuwa ukoo huu uliitwa *Mafie* baada ya mwanzilishi wake kuokolewa na nyani kutoka juu ya mti katika msitu mkubwa ambamo aliachwa na kaka yake aitwaye *Mungure*.

Mtoataarifa mmoja alisimulia kuwa;

> *"Sababu ya Mafie kuachwa msituni na kaka yake ni wivu wa mali. Ndugu hawa walikuwa wafugaji wa ng'ombe lakini Mafie alifanikiwa kuwa na mifugo mingi kuliko kaka yake aitwaye Mungure. Katika jamii ya Wameru kwa kipindi hicho mtu aliyekuwa na mifugo mingi aliheshimiwa zaidi kwa hiyoMungure akaanza kumwonea wivu mdogo wake na mwisho Mungure akapanga kumwua Mafie.*

Mtoataarifa mwingine aliendelea kusimulia kuwa;

> *"Siku moja Mungure alipanga safari ya kwenda kurina asali naMafie msituni. Kwa kawaida kwa Wameru kijana mdogo ndiye hupanda juu ya mti, hivyo walipofika msituni walifunga kamba (ngamia) vizuri na Mafie akaitumia kupanda mtini kushusha mizinga ya asali. Akiwa anaendelea na kazi hiyo ndipo kaka yake akaidondosha kamba ile kwa makusudi na kuondoka nayo pamoja na asaliakamwacha mdogo wake juu ya mti. Mafie alishindwa*

kushuka kwenye mti kwani ulikuwa mnene mithili ya mbuyu lakini kwa bahati nzuri mti ulikuwa na matunda hivyo aliyala pamoja na asali.

Siku chache baadaye nyani mkubwa alifika pale akala matunda na kuondoka lakini tayari alimwona Mafie. Siku iliyofuata nyani alirudi kula matunda akamwona tenaMafiendipo alipomsogelea na kumgeuzia mgongo kumruhusu apande. Baada ya kusita kidogoMafie alipanda mgongoni kwa nyani kisha nyani akashuka naye. Nyani alimsindikiza Mafie kwa kufuata sehemu ambayo Mungure alipita hadi wakafika nyumbani. Walipofika walimkuta Mungure amechinja ng'ombe waMafie wanafanya sherehe kwani alikwishatoa taarifa kuwa Mafie ameuawa na Wanyama porini".

Katika mahojiano watoataarifa walieleza kuwa *Mafie* alipofika nyumbani alichukua ile kamba (ngamia) waliyoitumia msituni akaikunja katikati mbele ya umati na kuikata huku akisema kuanzia leo nimekata uhusiano na kaka yangu *Mungure*. *Mafie* alieleza kuwa ndugu yake ni nyani kwa sababu nyani ndiye aliyemwokoa na kifo na baada ya kumaliza tukio hilo aliondoka na nyani kwenda kuanzisha mji wake karibu na msitu. Hii ndiyo sababu ya kupewa jina la ukoo wa *Mafie* yaani watu waliookolewa na nyani. Hii inamanisha kwamba wanyama wanaweza kuwakilisha tabia mbalimbali za watu ikiwemo tabia za watu wakarimu kama nyani alivyofanya. Sifa nzuri ya nyani ndiyo iliyomfanya apewe heshima ya kulitumia jina lake kama ishara ya kumshukuru,na pia kuifundisha jamii kuwa wapo watu wakatili katika jamii na hata katika familia lakini pia wapo watu wachache ambao wanaweza kuwa na ukarimu wa kuokoa maisha ya wenzao.

Hivyo makala hii imechambua sababu zilizotumika kutoa majina ya koo za Wameru ambazo ni jitihada katika kazi, matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya vita,tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama.Sehemu inayofuata nimjadala wa matokeo ya utafiti.

4.1 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Mjadala huu umeongozwa nanadharia ya Maana kama Matumizi ya Wittgenstein (1930) pamoja, na maandiko mengine yanayohusiana na makala hii.

4.1.1 Majina ya Koo katika Jamii ya Wameru

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika jamii ya Wameru yapo majina ya koo za Wameru yapatayo 26 ambayo yapo katika makundi mawili; koo kubwa na koo ndogo. Nadharia ya Maana kama Matumizi iliyoasisiwa na Wittgenstein (1930) inasisitiza kuwa ni muhimu kufahamu maneno, ishara na alama mbalimbali katika lugha na baada ya kufahamu maneno yaliyo katika lugha ambayo kwa muktadha huu ni majina ya koo ndipo maana na sababu zake zinaweza kufafanuliwa. Katika jamii zingine pia yamebainishwa majina mbalimbali ya koo na ya watu. Mathalani, Kalekwa (2018) alibainisha majina ya koo za Wasukuma, pia Anusa (2016) alibainisha majina mbalimbali ya asili ya Wayao, na Resani (2016) akabainisha majina ya watu katika jamii ya Wabena. Aidha Spear (1997) alifanya utafiti kuhusu historia ya Wameru ambapo alibainisha jumla ya majina 26 ya koo za Wameru. Hivyo matokeo ya Spear yanafanana na matokeo ya lengo la kwanza la makala hii.

4.1.2 Sababu Zilizotumika Kutoa Majina ya Koo Katika Jamii ya Wameru

Anusa (2016) anaeleza kuwa kila jamii duniani hutoa majina kwa watu wake kutokana na sababu mbalimbali. Majina ya koo ni sehemu ya majina ya watu, majina hayo hutolewa ili kuitambulisha jamii na kuitofautisha na jamii nyingine. Kwa hiyo jamii ya Wameru

ilianzisha koo mbalimbali kwa kutumia sababu ambazo ni jitihada katika kazi, matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya kivita, tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama.

Nadharia ya Maana kama Matumizi ya Wittgenstein (1930) inafafanua kuwa sababu za kutumia maneno, ishara na alama fulani katika lugha hutoka ndani ya muktadha maalum wa lugha husika na siyo nje ya muktadha huo. Mtaalamu huyu amefananisha sababu hizo nakanuni za hisabati ambazo zikitumiwa nje ya mazingira ya hisabati zinaweza kusababisha sintofahamu ya majibu. Anaeleza kuwa kanuni husaidia kuondoa sintofahamu nyingi katika hisabati. Wittgenstein alitumia namba sifuri kueleza kuwa kumekuwa na mjadala mrefu kuhusu nini kinachomaanishwa na alama (sifuri) na ni kwa vipi alama hiyo inaweza kumaanisha namba. Katika mtazamo wa Wittgenstein kanuni ndizo zinazosababisha majibu fulani hata kama namba ni zilezile. Alitumia mfano wa kanuni za ukokotozi ili kuondoa sintofahamu za majibu yanayotokana na namba sifuri ambapo alikokotoa $5 + 0 = 5$ lakini $0 \times 6 = 0$ na majibu yote ni sawa katika muktadha wa hisabati. Hivyo katika jamii ya Wameru majina ya koo zao hutolewa kutokana na sababu mbalimbali zilizotokana na waanzilishi wa koo husika, majina hayo hutofautiana kutokana na historia tofauti za waanzilishi wake. Sababu hizo zimefananishwa na kanuni zilizotumika kukokotoa hisabati, na kutoa majibu tofauti ambayo ni sahihi katika muktadha wake. Hivyo kila sababu ni sahihi kulingana na kile kilichofanywa na mwanzilishi wa ukoo husika.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa sababu za kupewa jina la ukoo wa*Kitomari* ni jitihada katika kazi.Hii inamaanisha kuwa kufanikiwa kwa mwanzilishi wa ukoo huo ndiko kulimfanya aheshimiwe na jamii ya Wameru, na kupewa jina la ukoo lenye tafsiri ya jitihada kwa sababu katika utamaduni wa Kiafrika bidii katika kazi humpa mtu heshima katika jamii. Hivyojina la*Kitomari*limetumiwa ilikuwahamasisha watu katika jamii ya Wameru na jamii zingine kuwa na bidii katika kazi ili kufanikiwa katika maisha. Zipo jamii zingine pia ambazo hutumia kigezo cha jitihada kutoa majina ya koo, mathalani Kalekwa (2018) anabainisha majina ya koo za Wasukuma yaliyotolewa kwa sababu ya jitihada mbalimbali katika maisha. Kwa mfano *Nkwabi* alipewa jina hili kutokana na jitihada za kutafuta kipato cha kuendeshea maisha. Vilevile *Ng'wihambi* alipewa jina hilo kutokana na juhudi za kufanya vitu vikubwa hata mahali ambapo hakuwa na uwezo. Kwa ujumla matokeo ya tafiti zote mbili yamefanana kwani sababu kubwa ya kutumia kigezo cha jitihada kutoa majina ya koo katika jamii ya Wameru, na Wasukuma ni kuhamasisha watu kuwa na jitihada katika kazi na kutokata tamaa.

Matokeo ya utafiti pia yanaonesha kuwa matendo ya kihistoria yalitumiwa kutoa majina ya koo za *Kaaya (Kuleiyye,Kyuta*na*Nsaiyya)*na *Nyiti*. Joho (2011) anaeleza kuwa tukio la utoaji wa majina hufanywa na jamii ili kuonesha historia ya jamii husika kwa lengo la kuifundisha jamii hiyo. Kwa hiyomatendo yalitumiwa kuwapa waanzilishi wa koo majina yanayoonesha historia ya kile walichokifanya, ili kuifundisha jamii kuwa wapo watu wanaofanya matendo yanayokubalika na yasiyokubalika na yote yana athari katika maisha.Kwa mfano *Kaaya*na*Nsaiyya* walionesha utii na usikivu wakapewa mahali pa kuishi lakini *Nyiti*, *Kyuta*na *Kuleiyye*walifanya matendo yaliyoashiria kukosa utii yaani kukataa kutii walichoelekezwa kufanya hatimaye waliishia kujitenga na jamii.

Katika jamii zingine pia matendo mbalimbali ya watu yalitumiwa kutoa majina maalum ya watu na hata majina ya mahali. Anusa (2016), Resani (2016) na Kalekwa (2018) wanabainisha majina maalum ya watu yaliyosababishwa na matendo yanayokubalika na yasiyokubalika katika jamii zao.PiaHassan (2017) anaonesha kuwa majina ya miji ya Unguja ambayo asili yake ni mti wa muembe yalisababishwa na matendo ya watu yaliyofanywa katika eneo la miti hiyo. Kwa hiyo majina yaliyotokana na matendo yamekuwa yakitumiwa na jamii mbalimbali ili kuhifadhi historia ya jamii hiyo.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwamatukio ya kipekee yalitumiwa katika jamii ya Wameru kutoa majina ya koo. Matukio hayo ni yale ambayo yanakwenda kinyume na utamaduni wa Wameru. Kwa Wameru watu walipofanya mambo yanayokwenda kinyume

na utamaduni wao, moja ya njia zilizotumiwa kuirekebisha jamii ni kuwapa watu majina kutokana na matukio hayo. Mfano ni majina ya*Ayo* na *Mungure*, lengo la kutoa majina hayo lilikuwa kukomesha tabia zisizoendana na utamaduni wa Wameru lakini pia kuitunza historia ya koo hizo.Mlokozi (1996) anaeleza kuwa makabila mbalimbali ya Kibantu hutoa majina kwa watu kwa kutumia matukio kama vile mvua kubwa, njaa na watoto kuzaliwa kabla ya wakati ili kutunza historia ya majina hayo. Anusa (2016) naNchimbi (2017) wanaonesha kuwa jamii zingine pia zinatoa majina kwa watu wakekwa kutumia matukio mbalimbali. Mfano niWayao na jamii zingine za Kibantu.

Matokeo mengine ya utafiti yanaonesha kuwa Wameru walitumia mazingira ya vita kutoa majina ya koo, mfano ni jina la *Mbise*.*Mbise* alitumia mbinu ya kujificha na kumfanya awashinde adui zake, mbinu hiyo ilipewa heshima na hatimaye kutumia neno hilo la kujificha kama jina la ukoo wake. Pia Kivenule (2013) anaonesha kuwa jina la ukoo wa*Kivenule* lilitokana na mazingira ya vita kutokana na uwezo wa familia ya *Kivenule* katika kulenga shabaha kwa kutumia mkuki na mshale hivyo kufanikiwa kuwaangamiza adui zao, kwa hiyo mbinu hiyo ikapewa heshima ya kuwa jina la ukoo. VilevileNchimbi (2017) anaonesha kuwa jamii ya Wajita ilitumia mazingira ya vita kutoa majina kwa watu lakini walitumia kigezo cha kuzaliwa wakati wa vita. Lengo la jamii hizi kutumia mazingira ya vita kutoa majina ni kuwa na kumbukumbu za kihistoria hasa kuhusu vita vilivyowahi kutokea katika jamii zao.

Matokeo mengine yanaonesha kuwa tabia ya mtu binafsi ni sababu ya kuibuka kwa jina la ukoo. Tabia zilizobainishwa ni ubinafsi/uchoyo uliooneshwa na mwanzilishi wa ukoowa *Akyoo*na ukarimu uliooneshwa na waanzilishi wa koo za*Nnko* na *Pallangyo*. Katika jamii ya Wameru sababu ya kutoa majina ya koozinazoonesha tabia ni kuonesha kuwa katika jamii wapo watu wenye tabia mbalimbali kama alivyopewa *Akyoo*kutokana na ubinafsi ili kufundisha wengine wasiwe na tabia kama hizo. Kwa upande mwingine watu walipewa jina linaloonesha tabia inayofaa kuigwa na jamii kama*Nnko* na *Pallangyo*ambao majina yao yanarejelea ukarimu, lengo lilikuwa kuwahamasisha watu wengine kuwa na tabia nzuri kama hiyo. Anusa (2016) anaonesha pia kuwa kwa Wayao tabia mbalimbali za watu zilitumiwa kuwapa majina. Lakini katika andiko hili majina maalum ya watu ndiyo yaliyotumiwa;kwa mfano*Akwilola* ni jina alilopewa mtu kwa sababu ya tabia ya kuangaliaangalia vitu vya watu na *Chipelenganya* ni jina alilopewa mwanaume kwa sababu ya tabia yake ya kuachaacha wanawake aliowaoa. Kutokana na ujumbe uliobebwa na majina haya jamii inajifunza kuacha tabia zisizofaa miongoni mwao.

Kadhalika matokeo mengine yanabainisha kuwa sifa nzuri ya mnyama ilifanya jina lake litumiwe kama jina la ukoo katika jamii ya Wameru. Wema wa nyani wa kumwokoa *Mafie* kutoka juu ya mti, na hatimaye kumpeleka nyumbani ndio ulikuwa sababu ya kutoa jina la ukoo wa *Mafie*. Matokeo haya yanaonesha jinsi mnyama anavyoweza kubeba sifa ya binadamu na kuonesha tabia yake kama nyani alivyobeba sifa ya binadamu wenye ukarimu na huruma. Kwa hiyo katika jamii wapo watu ambao wanaweza kutenda wema hata pasipo kutarajiwa kama nyani alivyotokea msituni na kumwokoa *Mafie*. Kalekwa (2018) pia anaonesha kuwa sifa za wanyama na ndege zilitumiwa kutoa majina maalum ya watu kama *Mbiti* aliyepewa jina hilo kwa sababu ya ulafi kama fisi, *Shimba* alipewa jina hilo kwa sababu ya ujasiri kama simba na *Shayayi* alipewa jina hilo kwa sababu ni mjanja kama sungura. Kwa ujumla majina ya wanyama yanatumiwa kuwakilisha sifa na tabia za watu ambao wamo miongoni mwa jamii ili kuirekebisha jamii kulingana na utamaduni wao.

Hivyo, utafiti huu umebainisha jumla ya majina ya koo za jamii ya Wameru 26. Imekuwa ni rahisi kubaini majina ya koo kwa idadi kwa sababu jamii ya Wameru inajibainisha kwa uwazi kwa kuwa watu wake hawana utamaduni wa kutoka na kwenda kuishi katika mikoa mingine au sehemu iliyo mbali na nyumbani kama ilivyo kwa makabila mengi hapa Tanzania. Pia matokeo yameonesha sababu zilizotumika katika kutoa majina ya

koo ambazo ni jitihada katika kazi, matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya kivita, tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama.

5.1 HITIMISHO

Makala hiiimechunguza majina ya koo na sababu za kutoa majina hayo katika jamii ya Wameru. Matokeo yanaonesha kuwa yapo majina 26 ya koo za jamii ya Wameru ambayo yapo katika makundi mawili; koo kubwa na koo ndogo. Pia makala imefafanua sababu mbalimbali zinazotumika kutoa majina hayo, na sababu hizo zinahusishwa na historia za waanzilishi wake. Sababu hizo ni jitihada katika kazi,matendo ya kihistoria, matukio ya kipekee, mazingira ya vita, tabia ya mtu binafsi na sifa za wanyama.

Makala hiini muhimu kwani inachangia kupata maarifa yanayohusiana na isimujamii.Piani muhimu kwa jamii ya Wameru kwakuitunza historia itakayoelezea visaviini vya jamii ya Wameru kwa vizazi vijavyo kwani wakikosa maarifa haya watakuwa wamepoteza asili, historia na utamaduni wao.

Makala hii inapendekeza kuwa viongozi wakoo waanzishe na kusimamia utekelezaji wa mikakati itakayohakikisha kuwa jamii inapewa maarifa kuhusu historia za majina na utamaduni wao ili waweze kurithisha maarifa hayo kwa vizazi vijavyo. Pamoja na kuwepo kwa makala hii, utafiti wa namna hii unaweza kufanywa katika jamii nyingine kwani jamii zinatofautiana katika asili, historia na utamaduni.

MAREJELEO

Anusa, A. C. (2016). *Maana za Majina ya Watu katika Jamii ya Wayao*.Tasnifu ya Shahada ya Umahiri ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bryman, A. (2012). *Social Research Methods*. United States: Oxford University Press.

Hassan, H. (2017). *Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja*. Tasnifu ya Kuhitimu Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Joho, H. A. (2011). *Matumizi ya Majina katika Utambulisho wa Jamii ya Watanzania*. Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kalekwa, L. B. (2018). *Uchambuzi wa Kiisimujamii wa Majina ya Koo za Kisukuma, Wilaya ya Misungwi*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Kivenule, A. (2013). Chimbuko na Historia ya Uhehe. *Html Blog Spot .Com*.

Languages of Tanzania Project. (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Mligo, E. S (2016).*Introduction to Research Methods and Report Writing*.U.S.A: An Imprint of Wipf and Stock Publishers

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimujamii, Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003).*Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Laba Graphics Services Ltd.

Mulokozi, M. M. (1996).*Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A. K. (2009). *UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Nchimbi, F. (2017).Tafsiri ya Majina Maalumu ya Kibantu: Umuhimu na Changamoto. *Mkwawa Journal of Education and Development*,1, (1), DOI: https://doi.org/10.37759/mjed.2017.1.1.4

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*.Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rashid, M. O. (2017). *Michakato na Mbinu Zilizotumika katika Uundaji wa Majina ya Mitaa katika Wilaya ya Mjini Unguja*.Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Isimu ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Resani, M. (2016). Maana katika Majina ya Wabena Nchini Tanzania. *Mulika, 35*.

Spear, T. (1997). *Mountain Farmers: Moral Economies of Land and Agricultural Development in Arusha and Meru*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Wittgenstein, L. (1922). *Tractatus Logico-Philosophicus*. Ogden, C. K. (trans.). London: Routledge & Kegan Paul.

TUMA Journal of Social Sciences
TJSS VOL. 1, NO 1, 2022
Print ISSN: 2820-2775
Website: https://www.makumira.ac.tz
A Journal of Tumaini University Makumira; Faculty of Education, Humanities, and Science

Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* Wakati wa Utandawazi

Benjamin Gambaloya
gambaloyab@gmail.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii
na
Neema George Mturo
neemamturo@yahoo.com
Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira-Idara ya Humanitia na Stadi za Jamii

IKISIRI

Makala haya yanahusu nafasi ya mwanamke na mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* wakati wa utandawazi. Watafiti wengi wamesawiri suala la jinsia katika tamthiliya ya Kiswahili kwa kumchora mwanamke pekee kuwa ndiye anayekandamizwa na kunyanyaswa katika jamii. Miongoni mwao ni Ngozi (1977), Muhando (1982), Mirikau (2011), Caleb (2013) na George (2014). Swali la msingi la kujiuliza; Je ni mwanamke pekee ndiye anayekandamizwa na kudhalilishwa wakati huu wa utandawazi katika jamii? Makala haya yalichunguza nafasi ya mwanamke na mwanaume katika Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* ili kuweka bayana. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya matumizi ya matini halisi na usaili na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kusimba maudhui na masimulizi. Aidha makala haya yaliongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji. Matokeo ya makala haya yanaonyesha kuwa si mwanamke pekee anayekandamizwa katika jamii, bali pia wanaume nao wanakandamizwa na kudhalilishwa. Matokeo yalibainisha kuwa mwanamke ni kiongozi wa kiimla, mkandamizaji na mnyanyasaji. Mwanaume amesawiri kama mkandamizwaji na mnyanyaswaji.

MANENO YA MSINGI:
Nafasi ya Mwanamke, Nafasi ya Mwanaume, Tamthiliya ya Kiswahili, Utandawazi

1.0 UTANGULIZI

Mwaka 1975 ulitangazwa na umoja wa mataifa kuwa ni mwaka wa wanawake (Muhando, 1982). Mwaka huo ulilenga kumkomboa mwanamke kutoka katika ukandamizaji na unyanyasaji. Baada ya kutangazwa kwa mwaka wa kumkomboa mwanamke (1975), waandishi wengi wa Tamthiliya walianza kuandika kuhusu ukombozi wa mwanamke, miongoni mwao ni Muhando (1976) *Hatia* na (1982) *Nguzo Mama,* Ngozi (1977) *Machozi ya Mwanamke*. Aidha katika kipindi hiki cha utandawazi nchi zilizoendelea zimekuwa zikitoa mikopo katika nchi zinazoendelea kwa masharti ya kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa nafasi sawa na wanaume katika sekta zote. Hiki ni kigezo cha kupata mkopo ama msaada kupitia benki kuu ya dunia na mashirika ya kifedha ya kimataifa (Shao, 2004). Hali hii imesababisha nchi nyingi ikiwemo Tanzania kuwa na mpango-mkakati wa kuwapatia elimu, huduma za afya, kumiliki mali kama vile ardhi na nyumba, kupata ajira na nafasi za uongozi wanawake sawa na wanaume.

Nchini Tanzania katika uchaguzi wa mwaka 2015 wanawake wengi walipata nafasi ya kuchaguliwa kupitia viti maalumu na kuwa wabunge. Hivyo ndani ya bunge kukawa na idadi kubwa ya wanawake wabunge tofauti na hapo awali. Idadi hii ilitokana na kanuni ya kupata wabunge wanawake wa viti maalumu isemayo: Idadi ya wabunge wote mara asilimia 40 (Tume ya Uchaguzi: 2015). Katika tamthiliya ya Kiswahili wataalamu wengi wameandika ama wametafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika jamii, miongoni mwao ni Wamitila (2002), Mtiro (2005), Mirikau (2011), George (2014) na Saro (2017). Wote wanahitimisha kwa kuonyesha kuwa mwanamke anasawiriwa kama mshauri, mlezi wa familia, mvumilivu,

jasiri, mchapakazi na mwenye mapenzi ya kweli. Mambo haya yamekuwa ni wajibu wa mwanamke yeyote katika jamii za kiafrika kabla na baada ya utandawazi.

Kwa upande hasi mwanamke amesawiriwa kama chombo cha starehe, asiye na maamuzi, kiumbe dhaifu, hapaswi kumiliki mali kama vile ardhi, pesa na nyumba. Kabla ya utandawazi mwanamke aliona kuwa mambo haya ni mambo ya kawaida na hayakumkandamiza hivyo alichukulia kuwa ni sehemu ya maisha yake ya kawaida ndani ya utamaduni wake. Kwa nini wajibu wa mwanamke ulionekana ni ukandamizaji? Baada ya utandawazi mambo haya yameonekana kuwa ni ukandamizaji, uonevu na udhalilishaji kwa mwanamke. Wataalamu hawa wamechambua taswira ya mwanamke katika jamii kwa mawanda yake. Mawanda haya yalitusaidia kuchunguza usawiri wa jinsia katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* wakati wa utandawazi. Swali la msingi tunalopaswa kujiuliza je, ni mwanamke pekee ndiye anayekandamizwa na kudhalilishwa wakati huu wa utandawazi? Makala haya yalisawiri nafasi ya mwanamke na mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili: *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* ili kuweka bayana swali hili.

2.0 MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii inahusu mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data alizotumia mtafiti katika makala haya ili kuweka bayana Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili wakati wa Utandawazi: Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Kitanzi* (2017). Mbinu za utafiti zilijumuisha wango, sampuli, usampulishaji, mkabala wa utafiti, usanifu wa utafiti, njia za ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data na itikeli.

2.1 MKABALA, USANIFU WA UTAFITI NA USAMPULISHAJI

Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa kitaamuli. Mkabala wa kitaamuli hutumia mbinu za kimaelezo na kifafanuzi katika kutafuta maarifa ya kutatua tatizo fulani au kuongeza maarifa kama ilivyosemwa na (Ponera, 2019:11). Mkabala wa kitaamuli ulisaidia katika kufafanua hoja, mawazo na data kutoka maktabani na uwandani ili kudhibiti lengo la makala haya. Mkabala huu uliwezesha watafiti na watoa taarifa kutoa maelezo kwa kina na taarifa zao kuchanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kina; kuhusu nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* wakati wa utandawazi.

Mpangilio wa ukusanyaji na uchanganuzi wa data za utafiti huu ulilenga kuhusisha uhalisia wa malengo mahususi ya utafiti na uwezo wa kumudu mchakato wa utafiti kama walivyosema (Cresswell, 2014) na Mligo (2012). Utafiti huu ulitumia usanifu wa kifenomonolojia ambapo fenomena ni kitu, tabia, tukio, hali, mwelekeo, dhana, uzoefu au jambo halisi na mahususi ambalo uwepo wake unadhihirika. Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili: Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* ndiyo fenomena yenyewe iliyochunguzwa. Katika utafiti huu usanifu wa kifenomenolojia ulitumika kuchunguza Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili: Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi*. Watafiti walichambua kwa kina tamthiliya zilizoteuliwa ili kuyaweka wazi yasiyo bayana katika jamii kupitia tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* kuhusu Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya hizi. Vile vile watafiti waliwahoji watoa taarifa katika jamii ya Meru wilaya ya Arumeru ili kuhusianisha na hali halisi katika jamii. Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Arusha, ulihusisha data za maktabani na uwandani.

Ponera (2019) anasema wango ni idadi au kundi la watoa taarifa kadri ya mwelekeo wa mada ya utafiti na malengo mahususi ya utafiti husika. Wango la utafiti huu lilikuwa matini halisi yaani Tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi*, pili ni wahadhiri, wanafunzi wa chuo kikuu cha Tumaini Makumira, maafisa ustawi wa jamii. Utafiti huu ulitumia usampulishaji kusudio. Babbie (1999) anafasili usampulishaji kusudio au lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa

sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kudhibiti lengo la utafiti wake kwa urahisi. Mbinu hii ya usampulishaji kusudio au lengwa ilitumika ambapo tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* zilitumika kudhibiti lengo mahususi la makala haya. Mbali na mbinu hii kutumika katika kuteua matini hizi mbili, pia mbinu hii ilitumika kuwateua wahadhiri, wanafunzi, na maafisa ustawi wa jamii. Tajiriba (kuwa na taarifa faafu) ilikuwa chanzo cha kuteuliwa kwao ili kudhibiti lengo la makala haya.

Sampuli ambayo ni sehemu ya wango ilitumika katika kudhibiti lengo mahususi la utafiti huu. Sampuli lazima iwe timilifu ili kutoa majibu kamili ya tatizo la utafiti husika kama anavyosema (Cresswell 2014). Sampuli ilikuwa na jumla matini halisi 2, wahadhiri 2 na wanafunzi 2 wa shahada ya umahiri kutoka chuo kikuu cha Tumaini Makumira ambao wamesoma kozi ya tamthiliya ya Kiswahili. Wanafunzi 2 wa lugha na utamaduni kutoka chuo cha TCDC pamoja na maafisa ustawi wa jamii 2 wilaya ya Arumeru katika halmashauri ya Meru. Aidha matini halisi; tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* zilitumika kuweka bayana nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya Kiswahili wakati wa utandawazi.

2.2 MBINU ZA UKUSANYAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka maktabani na uwandani. Taarifa hizo zilisaidia kujibu, kufafanua au kudokeza jambo lolote kuhusiana na malengo mahususi ya utafiti. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya matumizi ya matini andishi na kusimba maudhui. Mbinu ya matumizi ya matini andishi ni mbinu inayotumika kuchambua majarida, magazeti pamoja na matini za mazungumzo ambazo hazijaandikwa (Tromp na Kombo, 2006). Katika kuyafikia malengo mahususi ya utafiti huu

Upatikanaji wa data kupitia njia hii ulifanyika kwa kufuata hatua zifuatazo: kwanza kuwa na usomaji makini kuanzia sura ya kwanza hadi ya mwisho kama simulizi. Pili kusoma kwa kuchambua kwa makini sanjari na unukuzi wa data za msingi katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi*. Tatu ni usomaji na uchambuzi wa nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya zilizoteuliwa ulifanyika. Hata hivyo aya, sentensi ama neno linalohusiana na lengo mahususi la makala haya lilinukuliwa. Mbinu ya matumizi ya matini andishi ziliwasaidia watafiti kupata data za msingi kutoka maktabani katika vitabu vilivyoteuliwa.

Mbinu ya usaili au mahojiano pia ilitumika. Tromp na Kombo (2006) wanasema kuwa mahojiano ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizwaji wa maswali kwa njia ya mdomo au mahojiano. Usaili ulifanyika kati ya mtafiti na watoa taarifa uwandani. Katika usaili huu nyenzo kuu iliyotumika ni dodosa kwa wahadhiri, wanafunzi na wafanyakazi wa dawati la jinsia. Usaili huu ulifanyika ana kwa ana na kuandika kwa wale waliokosa nafasi ya kukutana ana kwa ana na mtafiti. Mbinu hii iliwezesha kuibuka pia maswali ya ziada wakati wa mahojiano yaliyowezesh kupata taarifa za kutosha kujibu swali ya utafiti na kudhibiti lengo mahususi la utafiti. Aidha usaili huria ulimpa mtoa taarifa kutoa maelezo yenye utondoti (urefu na ya kina) ulitumika. Mbinu hii ilitumika kwa mtafiti kuandaa maswali ya mwongozo wa mahojiani, kuwataarifu watoa taarifa kuhusu utambuzi na umuhimu wa kutoa taarifa zao katika utafiti huu. Kisha kuwaomba ridhaa ya ushiriki wao katika utafiti huu ili kujenga muamana nao.

Uchanganuzi wa data. Ponera (2019) anasema uchanganuzi wa data ni mchakato wa kuzishughulikia taarifa za utafiti zilizokusanywa ili kupata maana pamoja na kupata data chache zinazohitajika. Mchakato huu ulihusisha mambo makuu matatu ambayo ni upunguzaji data, udhihirishaji wa taarifa mpya pamoja na uwekaji ithibati. Data hizi zinaweza kutoka uwandani ama maktabani. Ufaafu wa data hizi ni data kuwa na uwezo wa kudhibiti malengo mahususi ya utafiti huu. Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia

mbinu mbili za uchambuzi wa data ambazo ni mbinu ya kusimba maudhui na mbinu ya usimulizi.

Mbinu ya kusimba maudhui huchambua vema data zenye uchangamani mkubwa wa dhana na mitazamo kuhusu jambo fulani. Robson (2011) anaunga mkono hoja hii kwa kusema kuwa, hii ni mbinu inayofafanua ujuzi, tajiriba, maana na uhalisia wa jambo kwa watafitiwa. Katika ukamilifu wa mbinu hii, Watafiti walifuata hatua zifuatazo: kwanza kuzizoea data kwa kuzisoma data zilizokusanywa na kupatikana kutoka katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* kwa umakini. Pia katika data za uwandani watafiti walisoma data na kusikiliza zaidi ya mara moja ili kubainisha na kutathimini nafasi ya mwanamke na mwanaume. Pili Watafiti walitengeneza misimbo mbalimbali kwa kuzingatia lengo mahususi maana, uhusiano na hali. Tatu watafiti waliunganisha misimbo inayolandana ili kuunda sura ama tafsiri ya kimaudhui kulingana na lengo mahususi la utafiti. Watafiti walihusisha sura hizo za kimaudhui za lugha na malengo ya utafiti na kuunda tafsiri mpya kimaudhui. Kwa jumla uchambuzi wa data ulifanyika kwa kufuata hatua pambanuliwa hapo juu kwa kuongozwa na lengo la makala haya ambalo ni kutathimini nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya Kiswahili wakati wa utandawazi.

Mbinu ya usimulizi huitambulisha matini kuwa ni umbo lililokamilika kimaarifa na kitaarifa kuhusu jamii iliyokusudiwa. Ponera (2019) anasema matini ni chombo ambacho watu hukitumia kujiwakilisha na kuuwakilisha ulimwengu wao na kujipambanua kupitia simulizi. Usimulizi ni nyenzo muhimu ambayo humtambulisha mtu na jamii yake. Mbinu hii ni faafu katika uchanganuzi wa data zinazotokana na usaili na simulizi. Kama mbinu ya uchanganuzi wa data, usimulizi huwa na sifa ya kuzingatia dhana ya wakati, dhima ya mhusika na uhusika wake katika simulizi. Mtafiti hujikita katika simulizi na vipashio vya kikronolojia vinavyosaidia kuleta maana (Ponera, 2019:94).

Watafiti Walitumia mbinu hii ya usimulizi kuchanganulia data kama ifuatavyo: kwanza watafiti walipitia data zake zote za usimulizi kutoka maktabani na uwandani kwa kumakinikia jinsi lugha ilivyosawiri uhusiano wa kijinsia (mwanaume na mwanamke) katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi*. Pili Watafiti walihusianisha data walizopata (simulizi) na hali halisi ya kimaisha ndani ya jamii ili kutathimini nafasi ya mwanamke na mwanaume katika jamii kikronolojia. Mpangilio huu wa kikronolojia ulisaidia watafiti kuunda misimbo mbalimbali ya lugha, kuunganisha misimbo hiyo kisha kutengeneza ruwaza mpya kimaana kutokana na misimbo hiyo. Misimbo hiyo iliwasaidia watafiti kutathmini nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya Kiswahili wakati wa utandawazi na hali halisi katika jamii.

3.0 MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa ili kudhibiti lengo la utafiti huu kutoka maktabani na uwandani. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutathimini nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* wakati wa utandawazi.

3.1 NAFASI YA MWANAMKE NA MWANAUME KATIKA TAMTHILIYA *KIVULI KINAISHI*

Mwandishi wa tamthiliya *Kivuli Kinaishi* ametathmini nafasi ya mwanamke na mwanaume kwa kutumia wahusika wake Bi. Kirembwe, Wari, Wasichana, Mtangazaji, Bi. Kizee na Mtolewa kwa kina. Kila jinsia amepambanua nafasi yake vyema. Mwanamke amepambanuliwa kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo:

3.1.1 Mwanamke kama Kiongozi mwenye Itikadi za Kiimla

Mwandishi amempambanua mwanamke kama kiongozi ndani ya jamii mwenye itikadi za kiimla. Anamtumia Bi. Kirembwe kama kiongozi anayeongoza Giningi kwa sheria anayoitaka yeye mwenyewe. Aidha katika utawala wa Bi. Kirembwe anatoa adhabu kali na lugha ya vitisho kwa yeyote anayejaribu kupinga utawala wake. Mwandishi anasema:

BI. KIREMBWE: Nani anayetaka ugomvi nami?

WAZEE WOTE: Hakunaaaa! (Hata wazee wanaonyesha woga sasa)

BI. KIREMBWE: Nani anayetaka kukalia kiti changu?

WARI NA WAZEE WOTE: Hakunaaaaaa!

Chanzo (Mohamed, 1990:42-43)

Hapa mwandishi amemchora mwanamke kama kiongozi dikteta asiyetaka kupingwa wala kushauriwa. Mwanamke anayetajwa hapa ni Bi. Kirembwe mtawala wa Gingingi. Kauli hizi zilisemwa na Bi. Kirembwe akiwauliza Wazee wakati wa sherehe za kumwingiza Mtolewa Giningi. Hali hii ni tofauti kabisa kwa mwanamke wa kiafrika kabla ya utandawazi kuwa na uwezo wa kuuliza maswali ya kidikteta kama haya. Baada ya utandawazi na wanawake kupewa nafasi katika jamii na hata kuwa viongozi ubabe na jeuri zilianza kuonekana. Bi. Kirembwe ni kielelezo tu.

Mwandishi anaendelea kumpambanua mwanamke kama kiongozi ndani ya familia kwa kumpa hadhi kama mama na baba. Mwandishi anasema:

MTANGAZAJI: (kwa heshima kubwa)

Mama……baba…….

Mama upande mmoja na baba upande mwingine.

Mama na baba wakati mmoja.

Chanzo (Mohamed,1990:56).

Vifungu hivi vinamchora mwanamke Bi. Kirembwe kama kiongozi katika ngazi ya familia na jamii. Mwandishi anaonyesha katika jamii ya Giningi mwanamke ni baba na mama (Bi. Kirembwe) hakuna mwingine isipokuwa Bi Kirembwe kwa sababu yeye ni mama na baba wakati mmoja. Haya yalisemwa na Mtangazaji katika sherehe ya kuingizwa kwa Mtolewa Giningi.

3.1.2 Mwanamke kama Mkandamizaji na Mkatili

Mwandishi Mohamed (keshatajwa) amemchora mwanamke kama mkandamizaji na mkatili asiye na huruma anapotekeleza adhima yake ya ukandamizaji. Mwandishi anathibitisha hii akimtumia Bi. Kirembwe. Mwandishi anasema:

MLINZI: (Anamburuta mkulima) Huyu Bi Kirembwe…………

BI KIREMBWE: (Anasita kidogo……anasema) kwa nguvu za kisheria na kanuni za kichawi zinazotawala Giningi unalaaniwa…..unalaaniwa kwa hamasa na ghadhabu kali ya kuondolewa mikono unayoringia.

MKULIMA: (Aliyekuwa akitetemeka muda wote huo anajitupa miguuni mwa Bi Kirembwe)

Nisamehe Bi Kirembwe……

Chanzo (Mohamed, 1990:66-67)

Mwandishi anaendelea kuthibitisha ukandamizaji kwa kumtumia Bi. Kirembwe (mkandamizaji) na Mkulima (mkandamizwa) anapomuhukumu. Mwandishi anasema:

BI KIREMBWE: *Sasa aje mwalimu………*

Analetwa mwalimu kama walivyoletwa wale wa mwanzo.

BI KIREMBWE: *(Huku kamshika kichwa mwalimu) Unalaaniwa kwa hamasa…… na adhabu kali ya kukatwa ulimi unaoringia unapokuwa darasani.*

MWALIMU: (Aliyekuwa akitetemeka kuliko mkulima…..) Nisamehe mama; nisamehe

baba….. Nina watoto,wenzi na wahisani mimi…..

BI KIREMBWE: *Ha, ha, ha ,……(Akicheka kicheko cha kikatili zaidi) Ndivyo mlivyo ….wakati ukiwadia mnalia kama wanawake waliofiwa……..*

Chanzo (Mohamed, 1990:67-68)

Bi Kirembwe anatekeleza ukatili huu kwa wanaume bila huruma yoyote. Ukatili huu unawakumba mkulima na mwalimu kwa kutaja baadhi ili kukidhi hasira yake. Mkulima na Mwalimu walishindwa kutimiza majukumu yao kutokana na uongozi mbaya wa mabavu wa Bi. Kirembwe. Bi. Kirembwe anawakandamiza kwa kuwapa hukumu isiyo halali kwao katika sherehe ya kuingizwa Giningi Mtolewa. Mfano Mkulima kukatwa mikono ni uonevu na Mwalimu kukatwa ulimi ni adhabu ambazo si halali kwao. Changamoto za chakula na elimu Giningi zilitokana na serikali (serikali ya Bi. Kirembwe) kutotimiza wajibu wake.

3.1.3 Mwanamke kama Mtu Asiyepokea Fikra Mpya

Mwandishi Mohamed (keshatajwa) amemchora mwanamke kama kiumbe asiyetaka mabadiliko, kupokea mawazo chanya kutoka kwa mtu yeyote akiwa kwenye nafasi yake kama kiongozi. Mwandishi anasema:

MTOLEWA: *Fikra zangu ndizo fikra zako na zako ndizo zangu zimeshaumana.*

BI KIREMBWE: *La! Hasha! Fikra zako zinaingilia zangu, lakini sina hakika kama zitafanikiwa. Nionavyo hazitafanikiwa, kwani fikra zako zimekaliwa na zangu na si kinyume chake. Hatutaki fikra mpya hapa Giningi.*

Chanzo (Mohamed, 1990:52)

Bi Kirembwe anakataa fikra mpya kutoka kwa Mtolewa aliyekuwa na elimu ya kutosha ili kuleta maendeleo katika jamii ya Giningi. Bi Kirembwe alikataa ili kumwonyesha Mtolewa kuwa yeye ni kiongozi na hahitaji msaada wa mawazo yoyote mapya kutoka kwa mtu mwingine. Kauli hii aliitoa katika sherehe ya kuingizwa kwa Mtolewa Giningi.

3.1.4 Mwanamke kama Msaliti

Mwandishi amemchora mwanamke kama msaliti kupitia kwa mhusika wake Bi Kirembwe. Bi Kirembwe anawasaliti wenzake wote. Mwandishi anasema;

MTOLEWA: *Wahenga walitwambia kwamba chungu cha kupikia ni chetu sote, chetu*

pamoja na kupakua pia ni chungu chetu pamoja, ilikuwaje Bi Kirembwe

akakihodhi?

Bi. Kilembwe kile kilichokuwa cha wote (chungu) alikimiliki yeye pekee na kuwaweka kando wenzake. Kitendo cha kuwaweka kando wenzake wakati walipewa wote ni usaliti . Kauli hii inatolewa na Mtolewa alipokuwa akijibu maswali ya mwangi wa sauti yake.

3.1.5 Mwanaume kama Mkombozi

Mwandishi Mohamed (1990) amemchora mwanaume kama mkombozi wa jamii katika harakati za ujenzi wa jamii mpya. Anathibitisha hilo kwa kumtumia mhusika wake Mtolewa: Mwandishi anasema:

BI. KIREMBWE: Eeh! (Anashtuka ….. Anashangaa) Umebiwa nini?

MTOLEWA: Unga wa rutuba ……

BI KIREMBWE: Unga wa rutuba ……. mbaya …….sikujua kwa nini sikukutambua tokea zamani? ……Ah, majuto mjukuu kweli! …huo unga wa rutuba ndio uliowapa Wari hawa,

MTOLEWA: Ndiyo

Chanzo (Mohamed, 1990:112-113)

Dayalojia hii inamwonesha Bi Kirembwe akijuta kumkaribisha Mtolewa ambaye kawalisha Wari unga wa rutuba (elimu) ili kujikomboa. Sasa utawala wa Bi Kirembwe wa ukandamizaji unaelekea mwisho na Mtolewa anaikomboa jamii yake. Harakati za Mtolewa kuikomboa jamii yake kutoka katika ukandamizaji na ukatili wa Bi. Kirembwe, hapa mwanaume anapambanuliwa kama mkombozi ndani ya jamii yake.

3.1.6 Mwanaume kama Mhisani

Mwandishi Mohamed (1990) amemchora mwanaume kama mhisani kupitia kwa mhusika wake mwalimu. Mwalimu anategemewa na familia yake (wenzi na watoto). Mwandishi anasema:

MWALIMU: Ukinikata ulimi nitasemaje mimi? Nina watoto, wenzi na wahisani mimi ……….

Chanzo (Mohamed, 1990:68)

Mwalimu alitegemewa na wanafunzi, watoto na wenzi wake ambao maisha yao yalimtegemea yeye. Kauli hii inathibitisha mwalimu kama mwanaume kuwa yeye ni mhisani. Japokuwa Giningi kuna changamoto nyingi zinazosababishwa na serikali kutotimiza majukumu yake lakini Bi. Kirembwe anamhukumu kukatwa ulimi bila kujali uhisani wake. Kauli hii ya uhisani ilitolewa na mwalimu alipokuwa akijitetea asipate hukumu kutoka kwa Bi. Kirembwe.

3.2.0 Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya *Kitanzi*

Mturo (2017) ametathmini nafasi ya mwanamke na mwanaume kwa mapana yake akimchora mwanamke kama mkandamizaji, asiye na maadili ndani ya ndoa yake hata kwa wazazi wake. Anamchora mwanaume kama mvumilivu na anayekandamizwa na mkewe katika ndoa yake. Haya yanathihirika kupitia kwa wahusika Mama Linda (pezo), Baba Linda (Wandema), Joshua na Sara kama ifuatavyo:

3.2.1 Mwanamke kama Mtu Asiye na Maadili katika Ndoa

Mturo (2017) amemchora mwanamke kwa kumpambanua kama mtu asiye na maadili katika ndoa kupitia kwa wahusika wake wawili mama linda (Pezo) na Sara. Nyumbani kwa Wandema, Wandema anafanya kazi zote za nyumbani kinyume na kaida ndani ya jamii kwa wanandoa. Mwandishi anasema:

NYUMBANI KWA WANDEMA

Ndani ya geti hilo pembeni mwa jiko nyuma ya nyumba. Wandema anaendelea kuosha vyombo ndani ya chumba kilichoko ndani ya jumba hilo juu ya kitanda cha nane kwa nane blaketi jeupe mithili ya theluji lilimfunika Mama Linda (Pezo). Amezama usingizini huku mumewe akipambana na vyombo nje.

Chanzo (Mturo, 2017:6)

Mama Linda anadhihirisha ukosefu wa maadili kwa kulala usingizi na kumwachia mumewe kazi zote za nyumbani. Kaida ndani ya jamii mwanamke ndani ya nyumba ama mwanamke jikoni. Kitendo cha Mama Linda (Pezo) kumwachia kazi zote mumewe na yeye kulala kwa raha mstarehe ni ukosefu wa maadili katika ndoa.

Mwandishi anaendelea kumchora mwanamke kama mtu asiye na maadili katika ndoa pale anaposema:

MAMA LINDA: Nimeshakwambia vyombo au nguo za kufua, kazi hizo hufanywa hapa mbele ya nyumba. Pili kama kuna mtu akigonga geti,kama ulikuwa unaosha vyombo unapaswa kwenda kufungua geti huku ukiendelea kusugua sufuria na utafanya hivyo hivyo wakati wa kufua nguo (Wandema akadakia).

WANDEMA: Lakini mke wangu …………

MAMA LINDA: (Akakatizwa ghafla na sauti kali) lakini nini? Nenda huko kaendelee na kazi.

Chanzo (Mturo, 2017:8-9).

Kitendo cha Mama Linda kutaka mume wake afanye kazi za kuosha vyombo na kufua nguo mbele ya nyumba, kufungua geti huku akisugua sufuria, kisha kumkatiza kauli mume wake ni ukosefu wa maadili ndani ya ndoa. Lengo la Mama Linda ni kutaka mume wake adhalilike kwa kila mtu afikae malangoni kwao.

Aidha mwandishi amemchora Sara kama mwanamke asiye na maadili katika ndoa. Sara hapiki chakula akimsubiri mumewe Joshua kutoka kazini aje ampikie. Huu ni ukosefu wa maadili kwa mwanamke. Mwanamke anayejitambua katika jamii yetu hawezi kubaki nyumbani akimsubiri mumewe aje kutoka kazini ampikie akiwa buheri wa afya. Mwandishi anasema:

SARA: Yaani saa hizi ndio unakuja kupika ili nile? Mbona unataka kuniua njaa mtoto wa watu! Wewe si unajua ratiba ya kupika? (akiwa mwenye uchovu mumewe anafungua mlango wa gari na kushuka).

JOSHUA: Yaani badala ya kuniuliza juu ya nini kilichonisibu hadi kuchelewa wewe unahitaji kula tu!

SARA: …. Anza na vyombo kwanza halafu ndiyo uingie jikoni. Yaliyokuchelewesha yananihusu nini? Mimi ninachojua ni kwamba ninaishi ili nile na ninakula ili niishi. Mambo yako sitaki kuyajua ………. kapike bwana.

Chanzo (Mturo, 2017:10-11)

Dayalojia hii inajitokeza nyumbani kwa Joshua alipokuwa amewasiri na muda ulikuwa umemtupa mkono ili kutekeleza ratiba yake ya jikoni ili mkewe ale chakula. Mwanamke mwenye maadili jiko ni mali yake (mwanamke jiko mume mahitaji). Kauli hii ilikuwa tofauti katika nyumba ya Joshua na mkewe. Joshua mtafuta mahitaji na mpishi nyumbani na mkewe ni mlaji tu. Haya yanajitokeza baada ya kuingia kwa utandawazi. Utandawazi umewaathiri wanawake mpaka hawaogopi kuwaamrisha waume, wanaona ni sawa na ni haki yao. Kabla ya utandawazi wanawake hawakuwa na mienendo hii ya ujeuri.

3.2.2 Mwanamke kama Mkandamizaji katika Ndoa

Mwandishi amemchora mwanamke kama mkandamizaji katika ndoa kwa kumtumia Sara na Mama Linda kama wanandoa wakandamizaji wanaowakandamiza wanaume wao na wanaume kuiona ndoa ni karaha na si fanaka. Mwandishi anasema:

SARA: Unajifanya mjanja siyo? …….. usiku wa leo mimi na wewe.

JOSHUA: Tobaaaaaa! Aaaaaa! Jamani mateso gani haya? Haya mateso gani unanipa?

Chanzo (Mturo,2017:12)

Kauli hizi zilimtoka Joshua baada ya kujitupa katika kitanda ambacho godoro lake lililotota maji ndoo sita zilizomwangwa na Sara kwa sababu ya hasira kwa nini Joshua akanunue chakula hotelini badala ya kumpikia mkewe Sara.

Mwandishi anaendelea kuthibitisha ukandamizaji wa Sara kwa mumewe pale anaposema:

JOSHUA: Nitateseka hivi mpaka lini? "kweli mfungwa hachagui' lakini hili gereza langu ni kali. Ee Mungu kwa msaada wako naomba kikombe hiki kinitoke.

Chanzo (Mturo,2017:12)

Tafakari za malalamiko na masikitiko ya Joshua yalitokana na ukandamizaji anaotendewa na mke wake sara. Mazungumzo haya yanaonyesha kuwa Joshua anakandamizwa za mke wake Sara.

Mwanaume mwingine anayekandamizwa ni Baba Linda (Wandema) na mke wake Mama Linda (Pezo). Mwandishi anasema:

WANDEMA: Kwa miezi michache nilifurahia ndoa yangu jambo ambalo zao lake ni mtoto wetu Linda, baada ya hapo ndoa ikageuka jela. Shughuli za ndani mfanyakazi ni mimi, kufua nguo dobi mimi na pia hakuna chakula nisichojua kupika.

BABA PEZO: (Baada ya muda simu ya Wandema inaita) uko wapi wewe umesahau kuwa vyombo vya jana havijaoshwa, nguo hazijapigwa pasi na wala chakula hakijapikwa? Sasa kaa huko lakini utakaporejea utanieleza vizuri. Huna adabu kabisa (simu ilikatwa).

MAMA PEZO: Kama sauti ya Pezo vile?

BABA PEZO: Siyo kama, ni yeye………. Kijana wangu endelea.

WANDEMA: Sasa nitaendelee kusema nini? Mimi niliyokuwa nataka kuwaeleza mmeyasikia kwa masikio yenu wenyewe.

Chanzo (Mturo, 2017:31)

Simu ya Mama Linda (Pezo) kwa Wandema na maelezo yake yanaonyesha ukandamizaji. Pia kitendo cha ndoa ya Wandema kugeuka jela na Wandema kugeuka dobi akishinikizwa na mkewe ni ukandamizaji. Ukandamizaji wa Pezo kwa mumewe unabainika kupitia simu aliyopiga Pezo kwa Wandema wakati akiwaeleza wakweze madhira anayotendewa na mkewe. Utandawazi umemwathiri Mama Linda na anaona ukandamizaji anaofanya kwa mume wake ni sawa. Anaona kuwa mume wake kumtumikia yeye kama dobi, mpishi na kumnyima furaha ya ndoa yao jambo la kawaida. Jambo hili si sawa, hata huko ughaibuni ambako utandawazi ulianzia suala la mume kubaki nyumbani na kufanya kazi ni makubaliano ya mume na mke kwa kuzingatia maslahi ya familia kiuchumi.

3.2.3 Mwanamke kama Msaliti

Mwandishi Mturo (2017) amemsawiri ama kumchora mwanamke kama msaliti kupitia kwa mhusika Sara. Sara ni mke wa Joshua lakini alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na bosi wake Wandema. Mwandishi anasema:

WANDEMA: Wandema naye akaamka kuutumia upenyo huo kumwandikia Sara ujumbe kwa

simu yake ya mkononi, ujumbe ulisomeka hivi; "Sara mimi ni mzazi mwenzio. Naomba usiniaibishe kwa wafanyakazi wangu…… nakutumia sh 500,000………

SARA: (Huku akitaka kujibu ujumbe wa Wandema anatabasamu tabasamu hilo ni kutokana na sh 500,000 kuingia katika akaunti yake ya mpesa) Chanzo (Mturo, 2017:55)

Kitendo cha Sara kuwa karibu na Wandema na kumwita mzazi mwenziye akitii maagizo ya Wandema huku akimkandamiza Joshua mumewe ni usaliti kwa mumewe.

3.2.4 Mwanamke kama Mdhalilishaji

Mwandishi amemchora mwanamke kama mdhalilishaji na udhalilishaji huo anaufanya kwa mwanaume. Mwandishi anamtumia Pezo (Mama Linda) kuthibitisha hili. Mwandishi anasema:

PEZO: Vyombo vinavyotoa harufu ya kila aina amevikusanya toka jikoni na kuleta sebuleni na kutapakaza kila mahali.

MAMA PEZO: Kwa nini unamjeruhi mumeo?

PEZO: Haya yote mmeyapata wapi?

BABA PEZO: Toka getini honi zimepigwa mara ngapi? Haya ukaona hivyo haitoshi na mumeo

ukamfungia nje. Bado hilo lisingetosha ukamtupia nguo zake nje.

Chanzo (Mturo, 2017:44-45).

Mazungumzo haya kati ya Pezo na wazazi wake yanaonesha namna Pezo (Mama Linda) anavyomdhalilisha mumewe (Baba Linda) mbele ya wakwe zake. Haya yanatokea baada ya Baba Linda kwenda kuwaeleza wakwe zake udhalilishaji anaotendewa na mkewe na wao kuongozana na mkwe wao na kushuhudia yale yote waliyoelezwa na Wandema.

3.2.5 Mwanaume kama Mwathirika wa Ukandamizaji

Mwathirika ni mtu anayepatwa na jambo linalomsababishia madhara pasi kujua. Mturo (2017) amemchora mwanaume katika tamthiliya ya *Kitanzi* kama mwathirika wa ukandamizaji kutoka kwa mwanamke. Mwandishi anasema:

JOSHUA: Funguo zote ziko chumba alicholala mkewe. …… Alijilaza juu ya kochi bila kupata usingizi hadi saa nane na nusu usiku… Asubuhi nyumbani kwa Sara, Sara amekwisha ondoka kuelekea kazini na kumwacha mumewe akiwa amelala sebuleni. …… Baada ya mahojiano ya muda mrefu na waziri mkuu ofisini kwake, alijulishwa kuwa

ameshushwa cheo chake cha kuwa mkurugenzi wa jiji na kwamba atapangiwa kazi nyingine.

Chanzo (Mturo, 2017:14-17).

Kitendo cha Joshua kukandamizwa na mkewe kwa kulazwa kwenye kochi kutokana na milango yote kufungwa na mkewe pia mkewe kujifungia katika chumba chao cha kulala. Hii ilikuwa adhabu kwake kutokana na kuchelewa kurudi nyumbani hivyo kushindwa kumpikia mke wake. Hali hii inasababisha Joshua kulala kwa tabu sebuleni na kuchelewa kuamka

hivyo anachelewa kazini na Waziri mkuu anaamua kumshusha cheo. Mwandishi anaendelea kusema:

JOSHUA: Sasa sina kazi mtaani mimi nimekuwa gumzo yaani natembea uchi. Vyanzo vya haya yote ni yeye sara! Sara! Sara mke wangu! Unajina zuri, sura nzuri lakini roho yako balaa…….. huyu mke wangu badala ya kuwa msaidizi sasa amekuwa kero na mzigo kwangu.

Chanzo (Mturo, 2017:22)

Haya ni majuto ya Joshua, kufukuzwa kazi, nyumbani pachungu na mke kawa mwiba. Matokeo ya ukandamizaji ambao alitendewa na mkewe. Haya yanamtokea Joshua akiwa katika ndoa na mkewe Sara.

Pia mwandishi amemchora mwathirika wa ukandamizaji mwingine. Wandema kama mwathirika wa ukandamizaji kutoka kwa mkewe. Mwandishi anasema:

WANDEMA: Wazazi wangu, tambueni kuwa Pezo ni mke wangu niliyemchagua mwenyewe,

atakuwa mzazi bora wa familia yangu. Kwa maana hii sina haya ya kumsemea mabaya ambayo hayatendi. Tangu nilipomwoa moyo wangu ulifurahi sana kuwa nilijua nimepata mke. Kwa miezi michache nilifurahia ndoa yangu jambo ambalo zao lake ni mtoto wetu linda. Baada ya hapo ndoa ikageuka jela. Shughuli za ndani mfanyakazi ni mimi, kufua nguo dobi mimi, na pia hakuna chakula nisichojua kupika.

Chanzo (Mturo, 2017:30-31).

Maelezo haya anayotoa Wandema kwa wakwe zake yanaonyesha namna ambavyo amekuwa mwathirika wa ukandamizaji kutoka kwa mkewe Pezo (Mama Linda).

3.3.6 Mwanaume kama Mdhalilishwaji

Mwanaume amechorwa kama mtu anayedhalilishwa na mwanamke. Mwandishi anathibitisha hili kupitia Wimbo ambao Chizi aliimba kutokana na maisha ya Wandema na namna alivyokuwa akidhalilishwa nyumbani kwake.
Mwandishi anasema;

*WIMBO: Ooooo bosi huyo! Anaosha vyombo, anafua nguo *2*

*Nani huyo! Wandema! Nani huyo! Wandema *2*

Kesho asubuhi anavaa suti, tayari ni bosi,

Na nyumbani kwake hata hafurukuti.

Nani huyo! Wandema! Nani huyo! Wandema!

Chanzo (Mturo, 2017:26)

Chizi aliimba kupambanua maisha ya Wandema, akieleza udhalilishaji unajitokeza nyumbani kwa Wandema. Mwandishi anaendelea kuthibitisha hili anaposema:

WANDEMA: (akiendelea kusikiliza sauti hiyo kwa umakini) ni sauti ya Chizi. (huku akiwahi getini kama atamwona Chizi ili kumpa kitu kidogo ili kumsihi asiyaseme aliyoyaona, alipotoka nje ya geti ….. Chizi kuhamaki ….. akatimua mbio ….. kuingia getini Mama Linda ameshika bakora)

WANDEMA: Huu msala mwingine

MAMA LINDA: Hivi wewe unamatatizo gani? Ukiniona nimenyamaza unaniona mjinga eee! Umetoka wapi?

Chanzo (Mturo, 2017:26-27)

Wandema anamkimbiza Chizi ili kumweleza asitoe siri ya udhalilishaji unaomwandama japokuwa hakufanikiwa. Anaporudi ndani anakutana na mkewe ameshika fimbo na kuulizwa swali ambalo mazingira yake ni udhalilishaji. Mwandishi anasema:

WANDEMA: Huu msala mwingine. (Huku akipunguza mwendo).

MAMA LINDA: Hivi wewe una matatizo gani? Ukiniona nimenyamaza unaniona mjinga ee! Umetoka wapi?

Chanzo (Mturo, 2017:26-27).

Mazungumzo haya yanaonyesha namna Wandema anavyodhalilika na mdhalilishaji wake ni mke wake.

3.3.7 Mwanamke kama Mtu mwenye Tamaa ya Pesa

Tamaa ni hamu kubwa ya kufanya jambo au kujawa na matarajio ya kupata kitu. Mwandishi amemchora mwanamke kama mtu mwenye tamaa, mpenda pesa na mwenye kutumia jinsia yake kupata pesa. Mwandishi anathibitisha haya kwa kumtumia Sara. Mwandishi anasema:

WANDEMA: Naomba usiniaibishe kwa wafanyakazi wangu…… nakutumia sh 500,000 kama

fidia samahani sana.

SARA: (huku akitaka kujibu ujumbe wa wandema anatabasamu tabasamu hilo ni kutokana na sh 500,000 kuingia katika akaunti yake ya mpesa).

Chanzo (Mturo, 2017:55)

Tabasamu la Sara baada ya kuona ujumbe wa mpesa ni dhahiri linadhibitisha kuwa ni mwenye tamaa ya pesa. Haya yanatokea baada ya Wandema kuuthamanisha msamaha wake na laki tano na msamaha unakubalika kwa tabasamu kutoka kwa Sara.
Mwandishi anaendelea kuthibitisha kuwa Sara ni mtu anayependa pesa pale anaposema:

SARA: Jana nilikwambia kuwa sina muda wa kupoteza sasa nilipe gharama zote nilizotumia niondoke ……..

AFISA: Daaah! Mrs Joshua laki moja yote labda nikupe 40,000/= …… dah! akajitahidi kumpa Sara 80,000/= bila mafanikio. Mchuano ni laki moja tu. Hatimaye akakubali kutoa laki moja.

SARA: Ukome kupigapiga simu bila uchunguzi …….

Chanzo (Mturo, 2017:62-63).

Dayalojia hii ni Sara akimkabili Afisa ustawi wa jamii baada ya kumsubiri Joshua (mumewe) aliyepeleka mashitaka kwa Afisa ustawi wa jamii, pamoja na kupeleka mashitaka hakutokea. Sara akadai nauli ya laki moja ya kufika hapo ofisini. Dai la laki moja halikuwa na ulazima. Haikuhitaji kulazimisha malipo ya kuitikia wito isipokuwa tamaa ilimsukuma Sara kudai pesa (malipo).

3.4.0 Data za Uwandani

Sehemu hii inawasilisha data kutoka uwandani. Kazi ya fasihi haitoki katika ombwe hutoka katika jamii. Mwanafasihi hutumia lugha kueleza kile kilichoko katika jamii ama kuweka wazi, bayana kile ambacho kimejificha katika jamii. Watafiti walienda uwandani pia ili kuthibitisha kile kilichopo katika tamthiliya teule za utafiti huu na kuwahoji watoa taarifa kadhaa ili kuthibiti lengo mahususi ya utafiti huu akifanya usaili na watoa taarifa kama inavyoonekana hapa chini.

3.4.1 Usawiri wa Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya Kiswahili

Watoa taarifa walitoa taarifa zao kwa kumsawiri mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya Kiswahili kama inavyoelezwa katika nukuu hii:

> *Mwanamke anakandamizwa zaidi kuliko mwanaume katika tamthiliya nyingi. Mfano katika tamthiliya ya Nguzo Mama na Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe mwanamke amekandamizwa sana. Lakini katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi na Kitanzi mwanaume anakandamizwa pia mfano Wandema, Joshua na Mwalimu.*
>
> *Chanzo (Uwandani, 2021)*

Pia watoa taarifa wengine walieleza kuwa usawiri wa kijinsia wengi wanafikiri kuwa ni kuzungumzia namna mwanamke pekee anavyokandamizwa, lakini jinsia ni mwanamke na Mwanaume. Hivyo mwanamke na mwanaume wamesawiriwa kwa namna chanya na hasi kama wanavyosema:

> *Waandishi wengi wameandika wakimchora mwanamke akikandamizwa na mwanaume lakini katika jamii wapo wanaume wanaokandamizwa na wake zao. Waandishi wengi hawajaliweka wazi jambo hilo vitabuni. Kwa ujumla mwanamke amechorwa kama kiongozi (Bi. Kirembwe) katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi, mvumilivu (Bi. Pili) katika tamthiliya ya Nguzo Mama. Mwanamke pia amechorwa kama mtu shupavu katika ujenzi wa jamii mpya mfano Jalia katika tamthiliya ya Morani. Mwanaume amechorwa kama mkombozi katika ujenzi wa jamii mpya mfano Mtolewa katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi pia mhujumu uchumi mfano Nungunungu katika tamthiliya ya Morani. Lakini kuna wanawake ni wachawi na wanajulikana katika jamii. Nadhani umewahi sikia kesi za mauaji ya wabibi/wazee wengi wao hawa ni wachawi wanawanyanyasa watu kwa kutumia nguvu za kishirikina kama Bi'Kirembwe.*

Pia mtoa taarifa mwingine alizungumzia usawiri wa jinsia baina ya mwanamke na mwanaume anasema:

> *Mwanaume ni shujaa, mbabe, mlevi na mkatili kwa mke wake mfano Sudi katika tamthiliya ya Nguzo Mama pamoja na Madahiro katika tamthiliya ya Machozi ya Mwanamke. Lakini mwanamke amechorwa kama mshauri na mwenye mikakati mizuri ya kuinua Nguzo Mama Bi. Nne katika tamthiliya ya Nguzo Mama. Pia mwenye hekima na busara vile vile mvumilivu mfano Mke wa kwanza wa madahiro. Hata hivyo mwanamke pia amechorwa kwa namna hasi kama kahaba na mwenye tamaa ya pesa na vitu mbalimbali mfano Bi. Tano katika tamthiliya ya Nguzo Mama. Aidha mwanamke hana maamuzi yake mwenyewe kila jambo analofanya anatengemea uamuzi wa mume wake. Kwa jumla mwanamke ametwezwa/kudhalilishwa katika tamthiliya nyingi lakini mwanaume amekwezwa mfano Madahiro katika tamthiliya ya Machozi ya Mwanamke. Mwanaume hakosei kila analofanya ni sahihi.*
>
> Chanzo (Uwandani, 2021)

4.0 MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii ni mjadala wa kina kuhusu matokeo ya utafiti huu.

4.1 NAFASI YA MWANAMKE NA MWANAUME KATIKA TAMTHILIYA *KIVULI KINAISHI*

Lengo la makala haya ni kutathimini nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* na *Kitanzi* limefikiwa kutokana na data za upili (maktabani) zinazoonyesha nafasi ya mwanamke na mwanaume katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (1990). Pamoja na data hizo, data za uwandani zinathibitisha yale yaliyoandikwa na mwandishi katika kazi yake kuwa hayatoki katika ombwe bali yanatoka katika jamii. Mwanamke na mwanaume wamechorwa katika nafasi mbalimbali kuthibitisha kile kilichopo ndani ya jamii kwa kutumia wahusika mbalimbali katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* kama ifuatavyo:

4.1.1 Mwanamke kama Kiongozi mwenye Itikadi za Kiimla

Mwandishi amempambanua mwanamke kama kiongozi ndani ya jamii mwenye itikadi za kiimla. Bi. Kirembwe anaiongoza jamii ya Giningi kimabavu ama kiimla kwa kufanya atakavyo yeye. Hataki mtu yeyote kumpinga wala kumhoji katika utawala wake. Na mtu yeyote anayejaribu kujenga hoja tofauti na mawazo yake anamwadhibu kwa adhabu kali. Lugha ya vitisho inatawala kinywa na ulimi wake. Kila mtu anamwogopa Bi. Kirembwe. Bi'Kirembwe kuwa mama wa mama, mama na baba kwa wakati mmoja ni uthibitisho wa kuwa ni mtawala wa kiimla. Hali hii imekuwa tofauti sana na namna ambavyo mwanamke amechorwa katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* ambayo imetafitiwa na George (2014) anasema mwanamke amechorwa kama kiumbe duni kisichoweza kujitegemea chenyewe bila nguvu ya mwanaume.

Aidha kutokana na tajiriba na mwitiko wa wasomaji wa tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* wamethibitisha kuwa ndani ya jamii wanamoishi wapo wanawake ambao wanatumia uongozi kama dhamana ya kuwakandamiza watu wanaowaongoza hasa pale wanapotoa maoni tofauti na mawazo ya viongozi hao.

4.1.2 Mwanamke kama Mkandamizaji na Mkatili

Mwandishi Mohamed (1990) amemchora mwanamke kama mkandamizaji na mkatili asiye na huruma anapotekeleza adhima yake ya ukandamizaji. Mwandishi anathibitisha hili akimtumia Bi. Kirembwe. Ukandamizaji na ukatili unaofanywa na Bi'Kirembwe unabainika kupitia kwa mkulima na mwalimu kwa kutaja baadhi. Mkulima anahukumiwa kwa kosa la kuzalisha kidogo. Mkulima anakwama kuzalisha kutokana na serikali ya Giningi chini ya utawala wa Bi'Kirembwe kushindwa kutoa pembejeo kwa wakulima.

Hali hii imekuwa kinyume na majibu ya utafiti yaliyobainishwa na George (2014) yakimsawiri mwanamke kama kiumbe kinachonyanyasika katika jamii kutokana na mfumo dume unaomkandamiza. Anaendelea kusema wanawake wa Patata walidharauliwa na kunyanyaswa walikuwepo kwa ajili ya kuzaa tu. Patata hawakuona umuhimu mwingine wa mwanamke.

Aidha utafiti ulibainisha kuwa Bi'Kirembwe ni mkandamizaji na mkatili kwa sababu serikali yake imeshindwa kutoa mahitaji ya msingi kwa jamii anayoiongoza. Katika jamii yetu leo wapo wanawake wanaoendelea kufanya ukandamizaji kwa jamii nzima na wanaume, japokuwa wanaume wengi hawaripoti ukandamizaji unaowatokea. Wazo hili linasawiri nadharia ya mwitiko wa msomaji iliyoasisiwa na Holland na Bleich (1984) wanaposema mwitiko wa msomaji huathiriwa na tajiriba yake, masuala ya kijamii na kiutamaduni yanayomzunguka msomaji. Kutokana na mila na desturi mwanaume kukandamizwa na mwanamke ni aibu. Hivyo kaida hii ndani ya jamii inasababisha ukandamizaji na ukatili kwa wanaume usiwekwe wazi ama kujulikana kwa watu wengi. Kabla ya utandawazi hakukuwa na habari yeyote ya wanaume kukandamizwa na wanamke.

Baada ya utandawazi kuenea wanawake wakapata elimu kupitia semina mbalimbali wakabadilika kutoka kuwa wasaidizi kwa waume wao na kuwa wakandamizaji.

Vile vile Waziri wa afya hapa nchini Tanzania Dkt Dorothy Gwajima alithibitisha pia uwepo wa ukandamizaji na ukatili pia kwa wanaume lakini wanaume wengi wanaokatiliwa wanakaa kimya tu kwa hekima. Waziri alisema haya alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Februari 2, 2021. Huu ulikuwa ni uthibitisho wa video ya Waziri wa afya akipambanua mwitiko wake kuhusu ukandamizaji na ukatili kwa wanaume.

4.1.3 Mwanaume kama Mkombozi

Mwandishi Mohamed (1990) amemchora mwanaume kama mkombozi wa jamii katika harakati za ujenzi wa jamii mpya. Harakati za Mtolewa kuikomboa jamii yake kutoka katika ukandamizaji na ukatili wa Bi. Kirembwe dhahiri shahiri mwanaume anapambanuliwa kama mkombozi ndani ya jamii yake. Pamoja na changamoto nyingi ambazo Mtolewa anapitia kutokana na utawala wa kiimla wa Bi'Kirembwe anapambana na kuhakikisha jamii ya Giningi inapata unga wa rutuba (elimu) ili kujikomboa. Wapo wanaume wengi katika jamii wanaopambana si kukomboa jamii yao tu bali pia familia zao.

Hali hii imekuwa tofauti kwa mujibu wa utafiti wa Mtiro (2005) utafiti wake ulibainisha kuwa wanaume wamekuwa wakiishi kwa kuwategemea wake zo kama nguvukazi katika tamthiliya ya *Machozi ya Mwanamke*. Pesa zinazopatikana kutokana na mauzo ya mavuno mwanaume (Madahiro) huitumbua peke yake na hutumia pesa hizo kuwanyanyasa ama kuoa mke mwingine. Pia George (2014) amemchora mwanaume kama tegemezi kwa mkewe katika tamthiliya ya *Nguzo Mama*. George (keshatajwa) anasema Sudi anaishi kwa kutegemea pesa ya ujasiriamali unaofanywa na Bi. Pili. Sudi huchukua pesa kwa Bi. Pili kwa nguvu kama si kulazimisha kupewa ama kuiba kwa mkewe. Aidha katika maisha halisi ya jamii yetu wapo wanaume wanaopambana kuhakikisha familia zao zinakuwa katika misingi mizuri kiuchumi na kijamii.

Pamoja na jitihada zao hizi hasa katika familia wanawake wengi wanawalaghai watoto wao kwa misemo "nani kama mama", kuwa wao ndiyo wamekuwa wakiwahudumia kuliko baba zao. Wakisahau kuwa watafutaji wa familia zao ni waume zao. Wanaume hawa huishia kupata msongo wa mawazo na kufa kutokana na manyanyaso kutoka kwa watu waliowatafutia kila kitu (wenzi na watoto) wangali wananguvu.

Haya yalibainishwa na watoa taarifa kupitia video fupi inayozungumza kuhusu siku ya mwanaume duniani yaani tarehe 19.11 kwa kila mwaka. Video hiyo inampambanua mwanaume kuwa ni shujaa ambaye mwisho wake ni majuto kwa sababu aliowahangaikia angali ana nguvu hawamthamini tena. Japo pia kuna wanaume katika baadhi ya jamii wamekuwa wakiwatumia wanawake kama chombo cha uzalishaji mali huku wao wakistarehe wakati mwingine hata kuoa wanawake wengine ili waweze kuwatumikisha.

4.1.4 Mwanaume kama Mhisani

Utafiti ulionyesha kuwa mwandishi Mohamed (1990) amemchora mwanaume kama mhisani kupitia kwa mhusika wake Mwalimu. Mwalimu anategemewa na familia yake, wenzi na watoto pamoja na wanafunzi wake anaowafundisha. Japokuwa Giningi kuna changamoto nyingi zinazosababishwa na serikali kutotimiza majukumu yake lakini Bi. Kirembwe anamhukumu kukatwa ulimi bila kujali uhisani wake. Serikali ya Giningi haikuweka mazingira mazuri kwa walimu kuweza kufundisha. Hata katika jamii yetu leo wapo walimu ambao wamekuwa wakijitolea wakiamini kuwa ualimu ni wito.

Hali hii ni tofauti na Ngozi (1977) amemchora mwanaume kama mtu mvivu ambaye maisha yake kiuchumi yanawategemea wenzi wao kama nguvu kazi katika tamthiliya ya *Machozi ya Mwanamke*. Mtiro (2005) katika utafiti wake ulionyesha kuwa Madahiro

anapopata pesa kutokana na mauzo ya mavuno anazitumia kuoa mke mwingine na kunywa pombe. Vile vile George (2014) katika utafiti wake anasema mwanaume ni mtu wa kulelewa na anamtumia mke wake kama chanzo cha kipato chake (Sudi).

Kutokana na tafiti mbalimbali na waandishi wengi kumchora mwanaume kama mkandamizaji, mnyanyasaji na mdhalilishaji kwa mwanamke. Utafiti huu ulionyesha kuwa mwanaume ni mkombozi wa jamii na mhisani ndani ya jamii japokuwa amekandamizwa na mwanamke.

4.2.1 Nafasi ya Mwanamke na Mwanaume katika Tamthiliya ya *Kitanzi*

Utafiti ulionyesha kuwa Mturo (2017) ametathmini nafasi ya mwanamke na mwanaume kwa mapana yake akimchora mwanamke kama mkandamizaji, asiye na maadili ndani ya ndoa yake hata kwa wazazi wake. Kwa tajiriba na mwitiko wa mtafiti wa tamthiliya hii, mwanaume anaonekana kuwa ni mtu anayekandamizwa, anayedhalilishwa na kunyanyaswa na mkewe katika ndoa yake. Hoja hii inasadifu nadharia ya ufeministi kwa wafeministi wenye msimamo mkali ambao kwao mwanaume si kitu na hana umuhimu wowote kwa mwanamke na wanaona mwanamke anaweza kuishi bila mwanaume na hata akazaa watoto kwa kutumia uzazi wa chupa na akaishi na mwanamke mwenzie. Hii ndiyo sababu Mama Linda (Pezo) na Sara hawaoni thamani ya waume zao, hawana mapenzi nao, hawawajali wala kuwaheshimu zaidi wamewafanya kuwa watumishi wao. Kwa Mama Linda mwanaume alionekana ana kazi moja tu ya kumpatia ujauzito na baada ya hapo hana umuhimu naye. Malalamiko ya Wandema kukosa furaha katika ndoa yake yanathibitisha hilo (uk 30-31).

4.2.2 Mwanamke kama Mtu Asiye na Maadili katika Ndoa

Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa Mturo (2017) amemchora mwanamke kwa kumpambanua kama mtu asiye na maadili katika ndoa kupitia kwa wahusika wake wawili Mama Linda (Pezo) na Sara. Nyumbani kwa Wandema, Wandema anafanya kazi zote za nyumbani kinyume na kaida ndani ya jamii kwa wanandoa. Hali hii inadhihirisha ukosefu wa maadili kwa Mama Linda kwa kuamua kulala usingizi na kumwachia mumewe kazi zote za nyumbani.

Wandema anaosha vyombo na kufanya kazi za jikoni huku mke wake amelala raha mstarehe. Vile vile anamwamrisha kufua nguo mbele ya nyumba, kufungua geti huku akisugua sufuria, na kumkata kauli mume wake asemapo ni ukosefu wa maadili ndani ya ndoa. Lengo la Mama Linda ni kutaka mume wake adhalilike kwa kila mtu afikae malangoni kwao.

Tajiriba na utamaduni wa jamii unaonyesha kuwa mwanamke ndiye mwenye nyumba na mmiliki wa jiko. Yaani ndiye anashughulika na masuala ya ndani kama vile kufanya usafi wa vyombo na kupika chakula. Kitendo cha Mama Linda (Pezo) kumwachia kazi zote mumewe na yeye kulala kwa raha mstarehe na kutoa kauli zisizo na staha kwa mumewe ni ukosefu wa maadili kwa mwanamke katika ndoa yake. Katika maisha halisi ya jamii yetu wapo wanawake wenye tabia kama Mama Linda. Kuna wanawake ambao wamekuwa wakosefu wa maadili katika ndoa zao na kusababisha waume wao kuchukia familia na ndoa zao.

4.2.3 Mwanamke kama Mkandamizaji katika Ndoa

Utafiti ulionyesha kuwa mwandishi Mturo (2017) amemchora mwanamke kama mkandamizaji katika ndoa kwa kumtumia Sara na Mama Linda kama wanandoa wakandamizaji wanaowakandamiza wanaume wao na kuiona ndoa ni karaha na si fanaka. Kitendo cha Joshua kuchelewa kutoka kazini na mke wake Sara kukaa nyumbani bila kufanya kazi yoyote akisubiri mumewe aje ampikie ni ukandamizaji. Joshua anapoacha kupika na kuamua kwenda kununua chakula hotelini mkewe anaghadhabika na kuamua

kulowanisha kitanda kwa maji ni ukandamizaji. Kitendo cha kulowanisha kitanda kwa maji na Joshua kukosa pa kulala ni ukandamizaji.

Kwa mujibu wa nadharia ya mwitiko wa msomaji, tajiriba na uzoefu ndani ya jamii wanawake wa aina ya Sara wapo. Mwitiko wa watoa taarifa wengi ulionyesha kuwa wapo wanawake wa aina ya Sara na Mama Linda wanaowakandamiza waume zao na waume zao kuishi wakigugumia kwa maumivu ya ukandamizaji wa wake zao kila uchao. Hata hivyo watoa taarifa walisema kuwa ukandamizaji huu hauwekwi wazi na wanaume hawa ili kulinda heshima yao mtaani ama katika jamii yetu. Mambo haya ya wanaume kukandamizwa na wake ao yamesababishwa na utandawazi. Wanawake wengi wanaiga mambo kutokana na utandawazi na kuacha desturi zetu.

4.2.4 Mwanamke kama Mdhalilishaji

Mwanamke amechorwa kama mdhalilishaji wa mwanaume. Mwandishi anamtumia Pezo (Mama Linda) kuthibitisha hili pale ambapo Mama Linda anampangia Baba Linda aoshe vyombo mbele ya nyumba, afungue geti huku anasugua sufuria pia kumnyima unyumba mpaka anaenda kulalamika kwa wakwe zake.

Hali hii imekuwa tofauti katika matokeo ya utafiti wa Massuod (2018) yanayomsawiri mwanamke ni mtu wa kupigwa. Massuod (keshatajwa) anasema imezoeleka katika jamii mwanamke anapomkosea mume wake hutarajia kupigwa ili kumfanya mwanaume aishiwe na hasira na maisha yao yaendelee kama kawaida. Jambo hili limeingia katika saikolojia ya wanawake na hata baadhi ya wanaume kudhani kuwa kumpiga mwanamke ndiyo kumfanya asiendelee na tabia fulani ambayo amekuwa nayo (Richard, 2000).

Kwa mujibu mwitiko wa watoa taarifa uwandani walidai kuwa wapo wanaume baadhi wanaotupiwa vilago vyao nje na kudhalilishwa katika familia na jamii yetu. Ushahidi unaonyesha kuwa kuna kesi kadhaa kwa wanaume kutelekeza familia zao na sababu za utelekezaji huo ni udhalilishaji unaofanywa na wanawake kwa waume wao. Wanaume hao wanapofika katika ofisi za ustawi wa jamii husema walikimbia udhalilishaji. Kutokana na hayo kile alichokiandika mwandishi Mturo (keshatajwa) ni dhahiri shahiri kuwa kipo na ni bayana katika jamii. Hivyo si mwanamke pekee anayedhalilishwa pia wapo wanaume wanaodhalilishwa na wanawake wakati huu wa utandawazi.

4.2.5 Mwanaume kama Mwathirika wa Ukandamizaji

Mwathirika ni mtu anaepatwa na jambo linalomsababishia madhara pasi kujua. Mturo (2017) amemchora mwanaume katika tamthiliya ya *Kitanzi* kama mwathirika wa ukandamizaji kutoka kwa mwanamke (mkewe). Kitendo cha Joshua kukandamizwa na mkewe na kulazwa kwenye kochi sebuleni kutokana na milango yote kufungwa ni ukandamizaji. Pia kitendo cha mke wake kumfanya kuwa mpishi bila kujali majukumu yake ya kiofisi ni ukandamizaji pia. Haya yote yanaleta wimbi kubwa la mawazo kwa Joshua linalosababishwa na ukandamizwaji anaotendewa na mkewe, anachelewa kupata usingizi. Hali hii inamsababisha achelewe kuamka na hatimaye kuchelewa kwenda kazini na Waziri mkuu anaamua kumshusha cheo. Majuto ya Joshua, kufukuzwa kazi, nyumbani pachungu na mke kawa mwiba ni matokeo ya ukandamizaji ambao anatendewa na mkewe. Haya yanamtokea Joshua akiwa katika ndoa na mkewe Sara. Wazo hili linasawiri mwitiko wa msomaji, tajiriba ya jamii kuwa mke ni msaidizi kwa mumewe. Majuto ya Joshua yanaonyesha kuwa mke wake si msaidizi kwake bali ni mwiba umchomao kila uchao. Aidha utafiti ulionyesha kuwa mwandishi anamchora Baba Linda (Wandema) kama mwathirika wa ukandamizaji kutoka kwa mkewe Mama Linda (Pezo).

Wandema amekuwa dobi, mpishi wa kila aina ya chakula nyumbani kwake lakini pia anakosa nafasi ya kufurahia ndoa yake na mkewe. Ndoa imegeuka jela na yeye ndiye

mfungwa. Dhana hii imedhibitisha nadharia ya mwitiko wa msomaji isemayo kwamba masuala ya kijamii na kiutamaduni yanayomzunguka msomaji ndiyo yanayoathiri mwitiko wake. Kwa maana hiyo manyanyaso anayofanyiwa Wandema katika ndoa yake yanabeba dhana hiyo (unyanyasaji) kutokana na kwamba katika jamii ya kiafrika mwanaume hastahiri kufanya kazi hizo (kuosha vyombo, kusugua masufuria huku akifungua geti, kupika huku mkewe kalala kwa raha mstarehe). Aidha katika jamii ya mataifa ya magharibi mwanaume kupika, kulea mtoto, kuosha vyombo na wakati mwingine mwanamke hana kazi yoyote ile ni kitendo cha kawaida.

Hivyo wasomaji wa tamthiliya ya Kitanzi walithibitisha ndani ya jamii wapo wanaume wanaokandamizwa na wake wao. Wengine wananyamaza kwa hekima na wengine wanachukua hatua za kuacha familia zao na kuondoka. Pia wapo wanaoamua kupambana na ukandamizaji huo kwa kupigana na hatima ya wanaume wanaochukua hatua ya kupambana na wenza wao kwa nguvu mara nyingi huwa ni majanga kama vile mauaji au kuachiana ulemavu. Hivyo si mwanamke pekee anayekandamizwa bali pia wanaume wapo wanaokandamizwa.

4.2.6 Mwanaume kama Mdhalilishwaji

Utafiti ulionyesha kuwa mwanaume amechorwa kama mtu anayedhalilishwa na mwanamke. Mwandishi anathibitisha hili kupitia wimbo ambao Chizi aliimba kutokana na maisha ya Baba Linda (Wandema) na namna alivyokuwa akidhalilishwa nyumbani kwake. Wimbo wa Chizi unaonesha Wandema ni bosi, anaosha vyombo, anafua nguo nyumbani lakini asubuhi anavaa suti, tayari ni bosi na hana kauli. Chizi aliimba kupambanua desturi ya Wandema, akieleza mambo ambayo yanamdhalilisha Wandema.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa Wandema anamkimbiza Chizi ili kumweleza asitoe siri ya udhalilishaji unaomwandama ama kutendewa nyumbani kwake japokuwa hakufanikiwa kumpata Chizi kwani chizi alikimbia alipomwona Wandema akimfuatilia. Wandema anarudi ndani akijua kuwa siri yake imefichuka

Kutokana na tajiriba ya jamii na masuala ya kijamii na kiutamaduni yanayomzunguka msomaji kama nadharia ya mwitiko wa msomaji inavyoeleza Mama Linda (mke wa Wandema) ni kielelezo cha baadhi ya wanawake katika jamii. Ndani ya jamii wapo wanawake wanaowadhalilisha waume zao kwa kuwashinikiza kufanya kazi za ndani ambazo wao wanapaswa kuzifanya. Kitendo cha mwanaume kuosha vyombo kwa kushinikizwa na mke wake katika jamii nyingi za kitanzania ni udhalilishaji. Mwanaume huosha vyombo na kufanya kazi za ndani kumsaidia mke wake kwa hiari. Wakati mwingine mke anapokuwa mgonjwa mume hufanya kazi zote za ndani. Huu ni mwitiko wa msomaji. Hivyo wapo waume wanaodhalilishwa na wanawake katika familia ama ndani ya jamii yetu kwa kushinikizwa kuosha vyombo, kufua nguo na kupika. Mambo haya huwadhoofisha kiakili na kimwili kwa sababu huona kuwa ni ukandamizaji na udhalilishaji kwao.

5.0 HITIMISHO

Katika sehemu hii matokeo ya msingi ya makala haya yalijadiliwa. Mjadala huu ulilenga kuthibiti lengo mahususi ya utafiti huu. Vile vile mjadala ulifanyika ukiongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji ili kupata tajiriba ya wanajamii na kuhususha baadhi ya tafiti zilizomchora mwanamke katika tamthiliya. Mjadala huu unaonyesha kuwa pamoja na kuwepo kwa tafiti nyingi zilizohitimisha kwa kusema kuwa mwanamke anakandamizwa. Katika tamthiliya ya Kivuli Kinaishi na Kitanzi matokeo ya utafiti yameonyesha kwa kumpambanua mwanamke kama kiongozi katika ngazi ya familia na jamii, mkatili na mkandamizaji na asiyepokea fikra mpya (Bi. Kirembwe). Pia amesawiriwa kama mtu asiye na maadili katika ndoa, mkandamizaji katika ndoa, mdhalilishaji, msaliti na mwenye tamaa ya pesa (Mama Linda na Sara). Kinyume na haya mwanaume amepambanuliwa kama

mkombozi (Mtolewa), mhisani (Mwalimu), pia mkandamizwaji na mdhalilishwaji (Wandema na Joshua). Pia utafiti huu umeonyesha kwamba unyanyasaji na udhalilishaji kwa wanaume umetokana na wanawake wengi kuathiriwa na masuala ya utandawazi na kuona kwamba mwanaume anaweza akawa kama mwanamke na akanyanyasika kama wanawake wanavyonyanyasika.

MAREJELEO

Babbie, E. (1999). *Basics of Social The Research*. Belmont: Wads worth Publishing Company.

BAKITA (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) ltd.

Caleb, C. W. (2013). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Nguzo Mama na Mama Ee*. Haijachapishwa Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Cresswell, W. J. (2014). *Educational Research, Planning, Conducting and Evaluating Quantitative and Qualitative Research*. Boston: Personal Education Limited.

George, G. M. (2014). *Usawiri wa Mwanamke katika Tamthiliya Teule za Penina Muhando*. Haijachapishwa Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Gwajima, D. (2021, 2 Februari). (Akirekodiwa na Jamii TV) Waziri Dkt Gwajima awataka wanaume wanaofanyiwa vitendo vya ukatili kufunguka. Ilichukuliwa kutoka Mtandaoni (Video) *https://www.youtube.com/watch?v=LJjF11-sVms.*

Tromp, D. L & Kombo, D. K. (2006). *Proposal and Thesis Writing. An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Massuod, I. A. E. (2018). *Kuchunguza Nafasi ya Mwanamke katika Tamthiliya ya Alikiona*. Haijachapishwa Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mirikau, S. A. (2011). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya za Wamitila*. Haijachapishwa Tasnifu ya Uzalimili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Mligo, S. E. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam. Beumenial Gathering (EGYS)

Mohamed. S. A. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi. Oxford University Press.

Mtiro, C. (2005). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya mbili za Kitanzania Alikiona na Kivuli Kinaishi*. Haijachapishwa Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mturo, G. N. (2017). *Kitanzi*. Dar es Salaam: B&L International Ltd.

Muhando, P. (1976). *Hatia*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ngozi, I. S. (1977). *Machozi ya Mwanamke*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Richard, A. (2000). *Ebrahim Hussein: Swahili Literature & Individualism*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota.

Robson, C. (2011). Katika Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Saro, S. J. (2017). *Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya: Mfano wa Riwaya ya Utengano*. Haijachapishwa Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania.

Shao, I. F. (2004). *Context for Gender Mainstreaming Internationally, Regionally and Nationally*. Paper Presented at a Gender Sensitization Workshop for UDSM Council Members, Zanzibar.

TUMA Research Manual First Edition, (2017): *A Revised Copy by Research Committee (FEHS) 2020*.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2015). Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchanguzi kuhusu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2015. Ilichukuliwa kutoka *https://www.udsm.ac.tz/web/index.php/centres/redet/taarifa-ya-tume-ya-taifa-ya-uchaguzi-kuhusu-uchaguzi-wa-rais,-wabunge-na-madiwani,-2015.*

Trochim, W. M. K. (2006). Introduction to Evaluation retrived on 30 October, 2020, from *http://www.Social research methods;net/kb/survey.php*.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

ISSN 2820-27275

Printed by Moshi Lutheran Printing Press
P.O Box 301 Moshi, Tanzania; email: moshilutheranpress@gmail.com